

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA NANE

Kikao cha Tatu – Tarehe 30 Januari, 2020

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae. Tunaendelea Waheshimiwa Wabungena Mkutano wetu wa Kumi na Nane, leo ni kikao cha tatu; Katibu

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

MHE. SHALLY R. RAYMOND – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Shughuli za Kamati hiyo katika kipindi cha Mwezi Januari, 2019 – Januari, 2020 pamoja na tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha nusu Mwaka, Julai – Disemba 2019.

ZAYNABU M. VULLU – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA MITAJI YA UMMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma kuhusu Shughuli zilizotekelezwa na Kamati hiyo kwa kipindi cha kuanzia Februari 2019 hadi Januari, 2020.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa. Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI KWA WAZIRI MKUU

SPIKA: Maswali kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu karibu. Kama ilivyoada, ni maswali ya kisera yasiyohitajia takwimu, na swali moja kwa moja badala ya kuanza kuzunguka ili Wabunge wengi zaidi waweze kupata nafasi ya kuuliza maswali.

Tunaanza na Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba Mbunge wa Buhigwe uliza swali lako tafadhali. *(Makofi)*

MHE. ALBERT O. NTABALIBA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa fursa hii niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali. Mheshimiwa Waziri Mkuu natambua na ninapongeza

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

juhudi za Serikali juu ya upatikanaji wa vitambulisho vya NIDA. Vilevile natambua na ninajua faida za vitambulisho vya NIDA kwa kutambua mtu mmoja mmoja kama Mtanzania na sababu za kiusalama. Hata hivyo kwa sasa hivi kumekuwa na changamoto kubwa ya upatikanaji wa namba hizo za NIDA kwenye vijiji na miji. Nini kauli ya Serikali kwasababu wananchi sasa wanapata mkanganyiko speedna upatikanaji nini kauli ya Serikali?

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Obama, Mheshimiwa Waziri Mkuu majibu tafadhali ya swali hilo.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Obama Mbunge wa Buhigwe kama ifuatavyo:-

Upo ukweli kwamba Watanzania wengi tulikuwa hatujawafikia kuwapa vitambulisho maarufu vya NIDA mpaka ngazi ya vijiji na kule vitongojini; jambo hili Serikali imelifanyia kazi. Kwanza tumeongeza idadi ya watumishi kwenye ngazi za halmashauri ili kuwezesha kufika mpaka kwenye vijiji na vitongoji na kufanya kazi hiyo.

Mbili, tumeongeza pia na mitambo ya kufanyia kazi ili baadaye tuweze kupata vitambulisho; na idadi hii ya watumishi hawa ambao tumeongeza nimpaka Makao Makuu, ili kuweza kuharakisha kutoa vile vitambulisho vyao.

Mheshimiwa Spika, tunachokifanya sasa, ili Watanzania waweze kupata huduma yeyote ile inayohitaji kitambulisho cha NIDA Serikali imeridhia kila yeyote anayetaka kitambulisho cha NIDA kwa mwananchi; na kama mwananchi atakuwa hajapata kitambulisho cha NIDA basi atumie namba aliyopewa ili kuweza kuhalalisha kupata huduma yeyote ile ambayo inahitaji kitambulisho huku akiwa hana kitambulisho. Hiyo ni njia ya kwanza ambayo tumeitumia kurahisisha kuwafikia Watanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini mbili, inawezekana pia namba hii ni ngumu kwa mwananchi huyo aliyeko kijiji kuipata. Tumetoa maelekezo kwa watendaji wetu wa NIDA walioko kule kwenye ngazi ya halmashauri kwamba sasa watoe orodha ya wale wote waliowaandikisha kwenye vituo vyao na namba zao ili angalau mwananchi aweze kufika pale kwenye kituo aone orodha na namba yake sasa imuwezeshe mwananchi huyu kupata huduma popote panapohitaji kitambulisho cha NIDA kwa kupeleka namba tu; hiyo ndiyo njia ambayo tumeirahisisha ili kuwafikia Watanzania wote mpaka vijijini na kuhakikisha kwamba sasa uzalishaji wa vitambulisho makao makuu kule Kibaha iende kwa haraka na vitambulisho vipolekwe mpaka vijijini kwa haraka ili kila Mtanzania aweze kupata vitambulisho.

Mheshimiwa Spika, lakini natambua kwenye eneo hili, naomba nizungumze jambo moja, kwamba yapo maeneo tumeongeza umakini mkubwa, na hasa maeneo ya mipakani, kwa lengo la kuzuia wananchi wa nchi jirani kujipatia kitambulisho cha NIDA nchini Tanzania halafu akafanya mambo yake huku ndani kupitia kitambulisho cha nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwahiyo mtaona kunaweza kuwa kuna ucheleweshaji huko kwenye miji iliyoko mipakani na nchi jirani za Tanzania. Kwasababu tunafanya zoezi hili kwa umakini kwa lengo la kutoa kitambulisho kwa Mtanzania tu. Na nitoe wito kwa Watanzania mtusaidie kuwatambua ambao siyo wakazi wa nchi wanaokuja kuchukua vitambulisho vyetu kwa lengo la kudhibiti hali ya ulinzi na usalama ndani ya nchi. Kwahiyo kama kunaweza kuwa kuna kuchelewa maeneo kadhaa hasa mipakani; natambua Mheshimiwa Mbunge unatoka Buhigwe. Buhigwe iko karibu na nchi ya Burundi, kwahiyo pale tumeongeza umakini sana pale ili tusiweze kutoa vitambulisho kwa ndugu zetu wa nchi jirani.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA:Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah, uliza swali lako.

MHE. MUNDE T. ABDALLAH: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuuliza swali kwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu Tanzania ni nchi ambayo inaendelea kwa kasi kubwa katika uchumi wa viwanda hususan Serikali ya Rais Joseph John Pombe Magufuli; ambayo imejikita sana kwenye uchumi wa viwanda mpaka ambapo muda huu tunaviwanda zaidi ya 3,700; si jambo dogo. Lakini maendeleo haya ya kasi kubwa ya uchumi yanabidi yaendane na maendeleo ya wananchi. Je Mheshimiwa Waziri Mkuu mnamkakati gani kama Serikali kuhakikisha maendeleo ya kasi kubwa ya uchumi wa viwanda na kuhakikisha maendeleo ya watu vinakwenda sambamba?

SPIKA:Majibu ya swali hiloMheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Munde Mbunge wa Mkoa wa Tabora kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Serikali yetu inayoongozwa na Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli imeelekeza kuboresha uchumi wake kupitia viwanda pia. Viwanda hivi baada ya kufanya *study* ya kuweza kuwafikia Watanzania na kuwapatia maendeleo; tunajua mchango wa viwanda popote palipo na kiwanda lazima kitumie mali ghafi na malighafi hizi ziko kwenye sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi, maliasili pia hata madini. Kwa hiyo panapokuwa na kiwanda kinachohitaji malighafi hiyo obvious malighafi hiyo na wale wote wanaozalisha malighafi hiyo watakuwa wameboreshewa uchumi wao kwasababu tayari wanauhakika wa soko pale kwenye kiwanda. Ule uhakika wa soko tayari tunapeleka tunaunganisha manufaa ya uwepo wa kiwanda na hali na maisha ya wananchi wanaopata huduma hiyo kwenye kiwanda hicho.

Lakini viwanda hivi navyo vinavyofaida nyingine nyingi ambazo pia tunaunganisha na maendeleo ya mtu mmoja mmoja. Leo mgogoro wetu wa kukosekana kwa ajira, Rais weru alikuwa na muono wa mbali sana. Viwanda hivi sasa vinaajiri Watanzania kwenye maeneo kilimo; na wote mnajua kwamba hata kwenye ajira tumeweka tumebana kidogo mianya ya watu wengi kutoka nje kuajiriwa badala yake tumefungua milango kuajiriwa kwa Watanzania wenyewe. Kwahiyo viwanda vingi vinaajiri Watanzania kwahiyo angalau tumepunguza mgogoro wa kutokuwepo kwa ajira.

Lakini mbili kwa uwepo wa viwanda hivi tunapata kodi, kodi hizi ndizo ambazo zinatuwzesha leo kujenga zahanati, kujenga shule, kujenga miundombinu ya barabara na maeneo mengine. Kwahiyo tunaufanya uchumi wa viwanda tunaupeleka pia kwa jamii. Hatujaishia hapo tu viwanda hivi sasa vinazalisha malighafi ambazo leo tunakuwa na uhakika nazo kwa uzalishaji wake na ubora wake, lakini pia kwa gharama nafuu na upatikanaji wa karibu kuliko kuagiza vitu kutoka nje zaidi. Kwahiyo tumetengeneza uwepo wa soko la ndani la uhakika ambako sasa uchumi huu tunaupeleka sasa kwa wananchi. Kwahiyo kufungamanisha kwa viwanda na uchumi wa mtu mmoja mmoja hasa kumejikita kwenye maeneo hayo, namna ambavyo viwanda vinaleta tija kwa uwepo wake na kwa wananchi walioko jirani na kwa Tanzania nzima. Tunaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda ili watanzania waweze kunufaika na uwepo wa viwanda hivyo.

Mheshimiwa Spika, nataka niwahakikishie Watanzania, tunaendelea kuhamasisha na kuita wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi tuendeleo kuwekeza kwenye viwanda ili tuboreshe pia uzalishaji na kupata masoko wa malighafi inayotakiwa viwandani. Ahsante sana.
(Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Ahsante sana, twende visiwani sasa Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, na vilevile nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ziara yake aliyoifanya Tanzania nzima bila kujali mvua, jua wala kula, nami ni shahidi upande wa kula; hasa kwa upande wa pili wa Muungano; Mheshimiwa nikupongeze kwa dhati kabisa, ni Waziri Mkuu wa Tanzania ikiwemo Zanzibar na kama kuna kitu kilichonivutia Mheshimiwa Waziri Mkuu ziara uliyoifanya katika ...

SPIKA: Swali lako Mheshimiwa Jaku.

MHE. JAKU HASHIM AYOUB: Mheshimiwa Spika, ahsante ziara uliyoifanya katika Kiwanda cha Sukari cha Mahonda, umeiona hali ile na ukatoa maagizo. Yale maagizo uliyotoa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni sawasawa na maagizo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuwa sukari ile inunuliwe pale, ikiisha ndipo waruhusiwe watu kuagiza nje yaani ni maagizo sawasawa uliyoyatoa wewe. Lakini kelele za mlango hazimkeri mwenye nyumba, wewe ndiyo mwenye nyumba zile kelele ulizozikuta pale zisikushughulisha soko kubwa la walaji liko Tanzania Bara.

Je, ni lini mtafikiria angalau ile bidhaa kama zinavyotoka hapa ni saruji ikiwemo Tanga cement, Twiga, Dangote, kiboko na mabati yanakwenda katika soko dogo la Zanzibar angalau nusu yake likaja katika soko lile...?

SPIKA: Ahsante sana, majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jaku, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nishukuru kwa kutambua jitihada kubwa tunazozifanya. Si mimi bali ni Serikali yetu; imeweka huo mpango na utaratibu wa kuwafikia wananchi popote walipo. Kwa hiyo ziara zangu ni utekelezaji wa mkakati wa Serikali wa kuwafikia wananchi kule waliko.

Mheshimiwa Spika, ni kweli nimefanya ziara kwenye Kiwanda cha Mahonda Mkoa wa Kaskazini Unguja; na nimepita ndani ya kiwanda nimeona, nimeenda mpaka Bohari tumekuta sukari nyingi bado imebaki. Kiwanda kile kinao uwezo wa kuzalisha tani 24,000 na sasa hivi kinazalisha tani 6,000. Mahitaji ya Unguja na Pemba ni tani 36,000. Hata hivyo nimeikuta sukari ghalani na bado mwekezaji wetu analalamika kwamba hana soko. Kwa kweli nililazimika kuwa mkali kidogo.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inahamasisha wawekezaji kuja kuwekeza hapa na tumewahakikishia kuwa na masoko na kuwalinda, lakini bado hatumpi masoko; na hatumpi masoko kwa sababu tunakaribisha sukari nyingi ya nje kuingia halafu ya ndani inabaki. Kwa kufanya hilo tutakuwa hatumtendei haki yule mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, ni vyema; umesema kwamba unahitaji soko pia na Bara, lakini palepale ilipo inapozalishwa sukari mahitaji ni tani 36,000, lakini hizo tani 6,000 hazijanunuliwa zimebaki bohari, mwekezaji anahangaika, anatafuta masoko, haiwezekani!

Mheshimiwa Spika, na mimi nilitumia lugha ile kwamba mpango huu si sahihi, mbovu kwa sababu kwanza tungehakikisha hizi tani 6,000 za ndani zinanunuliwa halafu uagize nyingine. Kama tani ni 36,000 ndiyo mahitaji ya eneo, kwanza tani 6,000 zingetoka; na wale waagizaji basi

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wangepewa masharti ya kwanza kuinunua sukari ya ndani halafu unawapa kibali cha kuweka *top up*. Sasa kuagiza sukari yote ya nje iwe inakuja ndani haiwezekani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, mimi kama Waziri Mkuu mwenye wajibu pia hata kwa chama changu kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi; mimi kwa pamoja na Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar ndio wenye jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Suala la viwanda liko kwenye Ilani ya Chama cha Mapinduzi na ninapaswa kwenda popote Tanzania kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, sina mipaka. Sasa leo ninapokuta mahali Ilani haitekelezeki lazima niwe mchungu na nitaendelea kuwa mchungu kwa kiasi hicho. (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Spika, lazima tuweke mpango wa kuwalinda wawekezaji wa ndani na kuwahakikishia masoko, na masoko tunayo. Pale naambiwa waagizaji wako watatu, kwa nini usiwape masharti angalau rahisi, ndio mpango mzuri. Waambie kwanza nunua tani 20,000 chukua tani 10,000 lete na mwingine, na mwingine, 6,000 tumezimaliza. Lakini unaagiza zote kutoka nje halafu huyu atauza wapi? Haiwezekani, haiwezekani. Halafu mtu anasema nimewachefua Wazanzibar; nimewachefua Wazanzibar au nimewachefua wanunuzi? (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Spika, kwenye hili naomba nilieleze zaidi kile Kiwanda pale Mahonda kinawanufaisha wale wananchi wa Kaskazini Unguja kwa sababu wenyewe wanalima miwa, na soko lao ni kile kiwanda. Ukichukua sukari ya nje kama hainunuliwi wale wananchi miwa wanayolima haiwezi kupata soko unawaumiza Wazanzibar. Kile kiwanda kiko pale kinaajiri watumishi 400, wanufaika ni wale walioko Kaskazini Unguja; lakini leo usipouza huyu hawezi kuajiri, hawezi kulipa mishahara kwa sababu sukari iko bohari, haiwezekani! Leo kile kiwanda kiko pale kinalipa kodi, kodi ndiyo ile ambayo imeniwezesha kwenda kuona Kituo cha Afya kule Bambi, kituo cha afya kule Kizimkazi nimeona maabara nzuri imejengwa yenye viwango pale Bwejuu, nimeenda pia Unguja, Kaskazini Pemba nimekuta VETA inajengwa nzuri kwa sababu ya fedha ya kodi ya viwanda! Haiwezekani! (Makofi/Vigelegele)

Mheshimiwa Spika, mimi naamini Watanzania walinielewa na Watanzania hawa hata wenzangu wa Zanzibar nilichosema ni sahihi. Hao wanaotamka kwamba wamechepuliwa ni wanunuzi, na wala wasio wazanzibari. Sera yetu ni moja ya kuwalinda Watanzania, na tutaendelea kufanya hilo; tutakuwa wakali pale ambapo mambo hayaendi. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, na mimi ni mlezi wa Mkoa wa Kaskazini, naungana nawe Mheshimiwa Waziri Mkuu katika majibu hayo. (Makofi)

Mheshimiwa Ruth Mollel uliza swali lako.

MHE. RUTH H. MOLLEL: Mheshimiwa Spika, ahsante kunipa nafasi ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika awamu ya nne na tano iliazishwa uboreshaji wa Serikali za Mitaa ambayo tuliita ugatuaji wa madaraka au tulikuwa tunaita *D by D*.

Mheshimiwa Spika, tangu wakati huo Serikali imeendelea kufanya kazi lakini ugatuaji wa madaraka haujaenda sawa sawa. Kwa mfano Serikali imechukuwa vyanzo vikubwa vya mapato vya Serikali za Mitaa; kodi ya majengo na kodi ya mabango. Je, hatua hii ambayo ilikuwa ituwezeshe Serikali za Mitaa kwa rasilimali na fedha inakinzana na dhana nzima ya ugatuaji wa madaraka?

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu Mheshimiwa Mollel, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tunazo Serikali za Mitaa zinayomajukumu yake na Serikali Kuu ambayo inawajibika pia hata kuihudumia hata Serikali ya Mitaa. Kuanzia mwaka 2014 uliousema na kufika sasa tumejifunza mambo mengi katika uendeshaji wa Serikali za Mitaa na Serikali Kuu, hasa katika utoaji wa huduma za jamii. Yapo maeneo yanahayo mafanikio, yapo maeneo yana udhaifu. Kwahiyo ni jukumu la Serikali kujiwekea taratibu wa kutibu udhaifu huu ili kuwafikia wananchi katika kuwapa huduma. Lakini bado wajibu wa kumuhudumia mwananchi kule tumewakabidhi Serikali za Mitaa ili wafanye kazi ile kwa ukaribu. *(Makofi)*

Sasa swali lako ni pale ambapo baadhi ya vyanzo tumepeleka Serikali Kuu kwa usimamizi bado Serikali Kuu inalo jukumu la kusimamia na hasa kwenye mapato. Serikali yetu tumeamua kudhibiti ukusanyaji wa mapato na mapato haya yarudi tena kwa wananchi, tunaporudisha kwa wananchi tunawapelekea hao hao Serikali ya Mitaa kwa mahitaji yao ili watekeleze hilo jambo, hatujawaondolea mamlaka ya kusema tunahitaji darasa, tunahitaji kituo cha afya, tunahitaji uboreshaji wa miundombinu; bado mamlaka ile tunayo.

Mheshimiwa Spika, na tumeongeza hata kuunda kwa *TARURA* ili isimamie miundombinu. Sasa hivi tunaenda kwenye maji isimamie utoaji wa maji. Pale ambapo kuna mahitaji Serikali za Mitaa iseme inahitaji shilingi ngapi kwa ajili ya nini, tunawapelekea. Ndiyo sababu leo tunaona huduma zinatekelezwa mpaka vijijini kwa sababu tunashirikiana na Serikali za Mitaa katika kuratibu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ule udhaifu wa usimamizi wa makusanyo, usimamizi na matumizi yake ambao ulikuwa umejitokeza sasa tunaendelea kuutibu; na ndiyo sababu unaona wakati wote tunapokwenda huko kwanza tunauliza ukusanyaji na kama makusanyo yoyote yameifadhiwa na matumizi yake, na pale ambapo matumizi yanakuwa si sahihi tunachukuwa hatua. Kwa hiyo tunakwenda tunafanya marekebisho kwa namna ya kutunza rasilimali za Watanzania zinazokusanywa kwenye maeneo haya lakini pia na matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mollel awe na amani kabisa kwamba tunafanya kazi kwa ushirikiano kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu kwa kuwapelekea rasilimali fedha, rasilimali watu ili ziweze kuhudumia Watanzania walioko kwenye Serikali za Mitaa huo ndio utaratibu tunaotoa. Lakini hatujaondoa huo wajibu wa kuwahudumia wale wananchi kupitia Serikali za Mitaa. Ahsante.

SPIKA: Ahsante, Mheshimiwa Leah Jeremiha Komanya, uliza swali lako tafadhali.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi kubwa katika sekta ya elimu na wananchi wameunga juhudi hizo kwa kuchangia ujenzi wa madarasa. Hata hivyo kuna maelfu ya wanafunzi waliofaulu kujiunga kidato cha kwanza hadi leo hawajaripoti shuleni kwaajili ya upungufu wa madarasa

Mheshimiwa Spika, nilitaka kujuwa ni nini kauli ya Serikali?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Waziri Mkuu tafadhali.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Komanya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sasa tunayo idadi nzuri na kubwa ya wanafunzi wanaofaulu darasa la saba kwenda Sekondari. Serikali msimamo wake ni kuwapeleka wanafunzi wote waliofaulu kwenda Sekondari kwa asilimia mia. Serikali imetoa maelekezo kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhakikisha kwanza unafanya sense kupitia mfumo wa elimu ambao unaweza kuutabiri halmashauri hii inaweza kutoa wanafunzi wangapi kwenda Sekondari na kujipanga katika kuboresha katika miundombinu tayari kwa kuwapokea vijana hawa.

Kazi hiyo inafanywa kila halmashauri kwa usimamizi wake na wanapofaulu tunataka wote waende waanze kidato cha kwanza kwa wakati. Hata mwezi wa Disemba nilitoa kauli nikiwa mkoani Lindi kwamba kila halmashauri ihakikishe wanafunzi wote wanaenda awamu moja badala ya kuwaweka awamu mbili kwa sababu awamu mbili wale awamu ya pili wanakosa baadhi ya *topics* za kusoma na kwahiyo *syllabus* hawawezi kwenda pamoja; na kwamba kila Halmshauri isimamie hilo. Kwahiyo, usimamizi huu ni lazima uzingatiwe

Mheshimiwa Spika, na tumewapa deadline kufikia tarehe 31 mwezi huu wa kwanza wanafunzi wote wawe wamekwenda shule. Kwahiyo tufanye subira mpaka tarehe 31 tupate taarifa, inawezekana pia kuna wasiwasi wa awali, kwamba wanafunzi wengi hawajaenda lakini kutokana na maelekezo tuliyoyatoa, na muda tuliowapa mpaka tarehe 31 unaweza ukawa umekamilika; kwahiyo baada ya tarehe 31 tutatoa taarifa na swali lako litapata majibu mazuri. Kwa sasa msimamo wa serikali ni kuwapeleka wanafunzi wetu wote wanaosajiliwa. Awe anakwenda chekechea, anaingia darasa la kwanza, anaingia kidato cha kwanza, anaingia kidato cha tano, wote lazima waingie darasani kwa wakati na waanze kusoma kadiri *syllabus* inavyoeleza. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Pascal Haonga.

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, uchaguzi wa Serikali za Mitaa, mchakato wa uchaguzi wa Serikali za Mitaa Mwaka 2019 uligubikwa na dosari nyingi sana, ikiwemo wagombea kutoka vyama vya upinzani kunyimwa fomu, ofisi kufungwa kwa muda wote, hivyo kusababisha baadhi ya wagombea, hasa wa upinzani kushindwa kupata fursa kuweza kugombea.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali haioni kwamba ni vema uchaguzi wa wa Serikali za Mitaa uweze kurudiwa sambamba na Uchaguzi mkuu utakaofanyika mwezi Oktoba mwaka huu?

SPIKA: Hili swali zuri kweli hili. Mheshimiwa Waziri Mkuu Majibu tafadhali kwa swali hilo. *(Kicheko)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haonga, Mbunge wa Mbozi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, chaguzi hizi zote zinasheria zake na kanuni zake; na hata kanuni za Serikali za Mitaa vyama vyote vya siasa vilishirikishwa katika kutengeneza kanuni zao. Moja kati ya kanuni hizo ni pale ambapo inatoa fursa kwa yeyote ambaye hajaridhika huko anakogombea, kwamba anaweza kukata rufaa, na atakapona rufaa hiyo kwenye ngazi inayofuata haikutendeka haki aende mahakamani. Kwa hiyo kulichukuwa hili kwa ujumla ujumla si sahihi sana kwasababu kila mmoja alipo alikuwa na mamlaka yake inayoratibu na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

anayo fursa ya kwenda kwenye mamlaka kukatia rufaa pale ambapo hajaridhika na utekelezaji wa jambo hilo. Vyama vyote vilishiriki kwenye hii kanuni ya kukata rufaa, kwa hiyo ni wajibu wa huyo mgombea kwenye eneo hilo kwenda kukata rufaa.

Mheshimiwa Spika, na kama kulikuwa na dosari kama ambavyo nimeeleza bado zilikuwa zinaweza kuelezwa huko huko kwenye ngazi hiyo, kwa hiyo, huna sababu ya kutengua uchaguzi wote wakati mgombea mwenye malalamiko ana fursa huko huko aliko kwa kukata rufaa na hatimaye hukumu itachukuliwa. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Casato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini uliza swali lako.

MHE. CASATO D. CHUMI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ili niweze kumuhuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali, katika siku za karibuni dunia imekumbana na majanga makubwa mawili; la kwanza ni ule ugonjwa ambao uko rafiki ya China unausababishwa na virus wa aina ya corona.

Mheshimiwa Spika, la pili ni baa la Nzige ambao tayari wameshafika katika baadhi ya nchi jirani na hasa za Afrika Mashariki. Nilikuwa napenda kufahamu, Serikali imejipangaje katika kukabiliana na kudhibiti masuala haya mawili ambayo kwa namna moja ama nyingine yasipodhibitiwa yanaweza yakaadhiri ukuaji wa maendeleo ya taifa letu na wananchi wetu na hasa ukizingatia kwamba kuna biashara kubwa kati ya nchi yetu na China?

Vilevile ukizingatia kwamba kupitia Jumuiya ya Afrika Mashariki wenzetu jirani wameshakubwa na baa la Nzige?

SPIKA: Majibu ya swali hilo. Mheshimiwa Waziri Mkuu tafadhali.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Chumi Mbunge wa Mafinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba nchini China kuna ugonjwa unaosababishwa na virusi vya corona ambao unapoteza maisha ya watu; na sasa tumeanza kuona hata nchi za jirani yake nazo pia zimepata maambukizi hayo. Lakini pia hili la pili la nzige tumepata taarifa kupitia mitandao na vyombo vya habari kwamba hapa nchi jirani ya Kenya mazao yao yanashambuliwa na hao nzige.

Mheshimiwa Spika, sasa tuanze na hili la corona, corona iliyopo nchini China, China ni nchi rafiki na Tanzania, Watanzania wengi wapo China, lakini pia wapo wachina walioko nchini Tanzania. Tunayo maingiliano mengi kati ya Tanzania na China. Wakati huu wa uongonjwa huu, kwanza tumewahakikishia Watanzania kwamba Tanzania haina tatizo hilo la corona; na jana Waziri wa afya pamoja na Naibu Waziri wa afya wametoa taarifa kwa Watanzania, na nimeona leo kwenye gazeti limetoka hili, sasa jukumu letu ni kuwa na taadhari tusije tukapata tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, sasa kwenye tahadhari Serikali imejipanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja tumeimarisha mawasiliano na Balozi yetu iliyoko China kujua hali huko China inaendeleaje; na Mheshimiwa Mbelwa Kairuki anafanya kazi hiyo ya kutupa mrejesho kila siku na hali iliyoko kule. Baalozi Mbelwa anaendelea kazi nzuri ya kuendelea kutoa elimu kwa Watanzania kwanza ametafuta madaktari wa Kitanzania ambao wamejifunza ugonjwa huo na kuendelea kuwaelimisha Watanzania walioko nchini China namna ya kujikinga.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, na balozi kule kwa Tanzania walioko China amewakanya watanzania wasiwe na mizunguko mingi sana kwa sababu ugonjwa huo maambukizi yake ni pale ambapo watu wanakutana. Hiyo moja.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumewataka Watanzania wale wanapohitaji labda kurudi Tanzania, na kwa sababu watatakiwa kusafiri kwenye ma treni, mabasi wafanye mawasiliano na Balozi juu ya namna nzuri ya kusafiri. Wasisafiri kwenda ubalozini Beijing ulipo Ubalozi na badala yake watumie mawasiliano ya kimtandao kupata ridhaa hiyo na kuambiwa hali ikoje ili wapate vibali vya kurudi.

Ndugu Watanzania tunatambua kuna wazazi wana watoto wetu wanasoma nchini China, na wengine wamesharudi likizo. Tunawasihi watoto hawa wasiende kwanza nchini China mpaka hapo tutakapopata taarifa za kidiplomasia.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mambo ya Nje Tanzania inaendelea kufanya mawasiliano na Balozi zote mbili, Balozi ya China Nchini Tanzania na Balozi Tanzania Nchini China kuona mwenendo wa ugonjwa huo. Pale ambapo Serikali itaridhika kwamba kule hali imepungua tutatoa tamko kwa Watanzania walioko likizo hapa kurudi nchini China kuendelea na masomo, na vinginevyo ikiendelea sana basi Serikali itatafuta utaratibu mwingine.

Mheshimiwa Spika, kwahiyo, nitowe wito kwa Watanzania kama ambavyo Wizara imetoa kwamba kila Mtanzania awe makini na wageni wanaoingia mpakani na hasa wale wote ambao tumewaweka mpakani kuhakiki wanaoingia nchini kupitia vifaa vyetu ambavyo vinaweza kutambua magonjwa mbalimbali kuvitumia vifaa hivyo kikamilifu ili kubaini hao ambao wana dalili ya magonjwa hayo ili kudhibiti kuingizwa ugonjwa huu wa corona hapa nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la nzige, kama ambavyo nimesema majirani zetu mazao yanaharibiwa. Nzige ni wadudu hatari sana, wakiingia hapa watamaliza mazao yetu. Tumechukuwa taadhari, Wizara yetu ya Kilimo inaendelea kuwasiliana na Wizara ya Kilimo nchini Kenya kuona mwenendo na ukuwaji wa tatizo hilo, na sisi huku tunajipanga kwa namna ambavyo tunaweza kushiriki kikamilifu; lakini Serikali yetu inashiriki pia kusaidia nchini Kenya kupoteza wadudu hao ili wasiongezeke tatizo hili likawa kubwa nchini Kenya lakini pia lisije likaamia huku nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, sasa bado nitowe wito kwa mikoa na wilaya na vijiji vilivyoko mpakani kuwa makini na hao wadudu nzige. Pale ambapo watawaona wakiingia watowe taarifa haraka sana kwenye mamlaka zao ili hatua kamili iweze kuchukuliwa.

Sisi tumejipanga kudhibiti hali hiyo na tutaendelea kudhibiti hali hiyo ili tusije tukapata tatizo hilo la kuwa na nzige hapa nchini kwetu. Ahsante sana.

SPIKA: Swali la mwisho kwa siku ya leo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu litatoka kwa Mheshimiwa Dkt. Stephen Kiruswa Lemomo.

MHE. DKT. STEPHEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa niweze kumuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu swali.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa kuwa Serikali yetu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Magufuli imejinasibu kuhamasisha ujenzi wa viwanda vikiwemo viwanda vya kuchakata nyama na mazao mengine yanayotokana na mifugo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wafugaji wanatengewa maeneo ya malisho na malisho hayo yanaendelezwa kwa kujenga na kukarabati mabwawa, kuchimba visima vya maji na kuwekewa miundombinu mingine muhimu ili kuboresha afya ya mifugo ili waweze kukidhi haja ya hivi viwanda kwa ajili ya ng'ombe hawa wanapokuwa wameongezewa thamani, wafugaji watapata bei yenye tija? Ahsante sana.

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri Mkuu, la wafugaji.

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Kiruswa Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli, kama ambavyo nimesema awali kwamba Serikali yetu imejikita katika kuhamasisha ujenzi wa viwanda kwa lengo la kukuza uchumi wetu; na nimeeleza vizuri sana mwanzo manufaa ya viwanda ikiwemo na kuendeleza sekta yenyewe. Kwa kiwanda cha nyama kuwepo kwake Wilayani Longido tuna uhakika wafugaji wetu watapata faida kubwa kwa kufuga kisasa, kwa kupata masoko ya uhakika lakini pia na sisi tutanufaika kwa kupata nyama iliyopitia kiwandani yenye ubora ambao na sisi tumeuona kwamba ni ubora uliohakikiwa na taasisi yetu.

Kwahiyo, uwepo wa kiwanda kile na mwekezaji huyo, Wizara yetu ya Mifugo na Uvuvi imeweka utaratibu mzuri sana sasa; kwamba wale wote waliowekeza viwanda tumewaunganisha na taasisi yetu ya NARCO kwa kuwapa maeneo yaliyotengwa kama ni maeneo ya malisho, kwa kuwapa eneo la kuhifadhia ng'ombe wao, kuwakuza ng'ombe wao na zile taratibu zote zile za mifugo ili ziweze kukamilika kabla hajaingia ndani ya kiwanda kwa lengo la kutoa nyama iliyo bora kwa ajili ya chakula kama ambavyo tumetaka iwe.

Kwa hiyo tumebaini kwamba ranchi zetu zote nchini au maeneo yote ya malisho nchini. Hawa tumewapa maeneo hayo kwanza wale wenye viwanda lakini pili wafugaji wakubwa na tatu tumewatambua pia na wafugaji wadogo ambao wana ng'ombe kuanzia 100 na kuendelea, ambao tumesema tusiruhusu kuwa na ng'ombe 100 vijijini kwa sababu kunakuwa na migogoro mingi ya mifugo kula mazao, mifugo kuharibu miundombinu mingine. Kwa hiyo tumewatengea maeneo kwenye hizo Rachi zetu au kwenye maeneo hayo ya malisho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa utaratibu huu tumetambua jitihada za wafugaji na kuboresha namna ya ufugaji wao na mahali pa kuuzia, kwa maana ya soko kwenye kiwanda. Mwekezaji naye sasa naona lengo la nchi la kumlinda mwekezaji wetu kwa kumpa maeneo ya kuhifadhia ng'ombe wake halafu awapeleke viwandani. Tunatarajia kuendelea kutenga maeneo mengi zaidi ya malisho na kutoa fursa nyingi zaidi kwa wafugaji wetu wa ngazi zote; wakubwa, wa kati na wadogo ili waendeshe shughuli zao za mifugo vizuri.

Mheshimiwa Spika, Waziri wetu pamoja na Naibu Waziri wake na Makatibu Wakuu wa Wizara hii wanafanya kazi hiyo kila siku, unawaona hata kwenye vyombo vya habari wakiendelea kuratibu maeneo haya ya malisho kwa lengo la kuboresha ufugaji nchini na pia kwa lengo la kukuza sekta ya nyama, kwa maana ya kuwa na viwanda vinavyotengeneza nyama hizi, zinazo-process nyama hizi kwa ajili ya chakula cha ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge aendeleo kuhamasisha na kuhakikishia wapiga kura wake kwamba Serikali yetu imejikita katika kuhifadhia na kulinda wafugaji wetu wote na kuhakikisha kwamba tunawatengeneza fursa za kupata pia na masoko yake. Ahsante sana. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri Mkuu ahsante sana, ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ahsante sana muda wa nusu saa umekwisha wa maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, nakushukuru sana kwa kuweza kuyajibu maswali yetu kwa ufasaha vizuri kabisa. Mheshimiwa Waziri Mkuu tunashukuru sana, ahsante sana. Sasa tunaendelea na maswali mengine. *(Makofi)*

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Tunaanza na Mheshimiwa Andrew Chenge, Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Na. 27

Ahadi ya Ujenzi wa Barabara za Mji wa Bariadi

MHE. ANDREW J. CHENGE aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi yake ya kujenga barabara za Mji wa Bariadi kwa Kiwango cha lami?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Mwita Mwikabe Waitara tafadhali. Karibu!

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mbunge wa Bariadi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutekeleza ahadi yake ya ujenzi wa barabara katika Mji wa Bariadi kwa kiwango cha lami kwa kujenga barabara zenye urefuwa kilometa 7.76 kwa kiwango cha lami, njia za waenda kwa miguu kilometa 9.4, mitaro ya maji ya mvua yenye urefu wa kilometa 10.11 na uwekaji wa taa 302 chini ya mradi wa uendelezaji miundombinu katika miji (*Urban Local Governments Strengthening Project-ULGSP*).

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya barabara na madaraja katika Mji wa Bariadi kwa kadri ya upatikanaji wa fedha. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Chenge.

MHE. ANDREW J. CHENGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa majibu yake mazuri. Napenda nithibitisha kabisa kwamba jibu lake ni sahihi na nimshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, alikuja Bariadi na kuzindua barabara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo nina swali moja tula nyongeza.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Spika, chini ya mradi huu halmashauri ya Mji wa Bariadi imenunua vifaa mbalimbali kwa kuendeleza maboresho hayo ikiwemo magari ya maji taka, grader na vifaa vingine. Vifaa hivi viko bandarini kwa muda mrefu sana; na hili siyo kwa Bariadi tu lakini kwa vifaa kama hivyo kwa miji mingine ambayo iko chini ya mradi huu ambao unafadhiliwa na *World Bank*.

Mheshimiwa Spika, napenda nifahamu suala la VAT kwa miradi inayotekelezwa na Serikali ambayo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alishalitolea maelekezo, ni lini sintofahamu hii kati ya TAMISEMI na Wizara ya Fedha itamalizika ili vifaa hivi vitoke bandarini viende vikafanye kazi iliyokusudiwa chini ya mradi huu? Naomba majibu.

SPIKA: Swali hili ni muhimu mno, sana kabisa, nadhani Wizara ya Fedha mnahitaji kusema kitu kuhusu jambo hili. Ni usumbufu mkubwa mno kwa Watanzania, Wizara ya Fedha nawatambua kumuona Naibu Waziri Fedha.

NAIBU WAZIRI WA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa fursa hii, na nimshukuru Mheshimiwa Andrew Chenge Mtemi kwa swali hili muhimu. Pia nimshukuru yeye kwa sababu ni mmoja wa wajumbe wa Kamati yetu ya Bajeti, Kamati inayofanya kazi kubwa katika kuishauri Serikali na kutoa maelekezo mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Mheshimiwa Rais alitoa maelekezo ni sahihi na tayari tulishaanza kuyafanyia kazi kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018, Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 na sasa tunaanza mchakato wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020 ambapo nina uhakika tulikofika sasa tutaweza kushughulikia tatizo hili la miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia tutaweza kuikamilisha katika mwaka huu wa fedha. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, ili tuendeleo naomba Mheshimiwa Mwenyekiti Najma aje aweze kuendelea.

Hapa Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Aliondoka Ukumbini)

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano, sasa ni zamu ya Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe, karibu.

Na. 28

Tatizo la Uchimbaji Mchanga na Uchafuzi – Dar es Salaam

MHE. HALIMA J. MDEE aliuliza:-

Jiji la Dar es Salaam linakabiliwa na tatizo sugu la uchimbaji mchanga na uchafu uliokithiri;

Je, Serikali ina mikakati gani ya muda mfupi na muda mrefu kukabiliana na kero hiyo sugu na hatarishi?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ridhaa yako naomba kwanza nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa George Simbachawene kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ndani, lakini pia Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Maziringira. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Maziringira, naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Halima James Mdee, Mbunge wa Kawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna changamoto kubwa ya uchimbaji wa mchanga Dar es Salaam. Aidha, yapo machimbo ya mchanga yaliyoruhusiwa kisheria na kupata vibali kutoka mamlaka husika kama Serikali za Mitaa (Halmashauri za Jiji na Manispaa), Ofisi za Mamlaka ya Mabonde na Wizara ya Madini. Hata hivyo, upo uchimbaji holela hususan katika maeneo ya mito na machimbo mengine ya mchanga ambayo si rasmi yanayoanzishwa na wananchi katika maeneo mbalimbali. Uchimbaji wa madini ya mchanga usio rasmi ni kosa kwa mujibu wa Kifungu 6 (1) cha Sheria ya Madini ya mwaka 2010 na marekebisho yake ya mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji huu huleta athari ikiwa ni pamoja na mmomonyoko wa kingo za mito, uharibifu wa maji na miundombinu, mwingiliano wa maji ya bahari katika nchi kavu (*sea water intrusion*), kubadilika kwa mkondo wa mto kutoka uelekeo wa asili, kuharibika kwa uimara wa mto (*channel instability*), uharibifu wa mimea ya asili ambayo husaidia kupunguza mmomonyoko na uharibifu wa mazalia ya viumbe hasa wakati kina cha maji kinapoongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na hili hatua zifuatazo zinachukuliwa:

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, kuelimisha wananchi kuhusu athari za uchimbaji holela wa mchanga na kuzuia uchimbaji holela. Aidha, mamlaka mbalimbali zikiwemo Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Maziringira, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dar es Salaam, Mamlaka za Mabonde na Tume ya Madini kupitia Ofisi ya Madini Mkoa wa Dar es Salaam zimekuwa zikifanya ukaguzi wa mara kwa mara na hatua stahiki kwa mujibu wa sheria huchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, Serikali inaandaa mkakati wa muda mrefu utakaotokana na Mapendekeo ya Kamati Maalum ya Wadau iliyoundwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kupendekeza hatua za kuchukuliwa ili kuwa na uchimbaji endelevu wa mchanga usiokiuka sheria za nchi; na kufanya tafiti na kuendeleza teknolojia za ujenzi zinazoweza kutumia mchanga kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchafuzi wa mazingira uliokithiri, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 Kifungu 139(1) imetoa mamlaka kwa Serikali za Mitaa kuzuia au kupunguza taka ngumu, taka vimiminika, gesi taka na taka zenye madhara. Serikali itaendelea kuelimisha wananchi na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria. Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia programu ya Elimu kwa Umma inatoa elimu kuhusu usimamizi na udhibiti wa taka kuanzia ngazi ya jamii, viongozi na wadau hasa katika eneo la urejelezaji wa taka ngumu. Natoa wito kwa Serikali za Mitaa kuwajibika kwa kuweka mipango endelevu na usimamizi wa taka kama ilivyobainishwa katika Kifungu 139(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima James Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anatoa majibu yake ametaja kama mamlaka nne hususan kwenye suala la mchanga. Ametaja Wizara

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Mazingira ambayo kuna NEMC, ametaja Wizara ya Nishati na Madini, ametaja halmashauri lakini vilevile kuna kitu kingine kinaitwa Bonde ama Pwani Ruvu Bonde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ya usimamizi wa mito yetu ni kutokana na ukweli kwamba si NEMC, si halmashauri, si Wizara ya Nishati na Madini ina mamlaka ya moja kwa moja ya ku-*deal* na masuala ya mchanga. Ni Pwani Ruvu Bonde ambayo ofisi zake ziko Morogoro ndiyo inaingia mikataba na watu wa kuchimba mchanga kwenye halmashauri zetu. Wananchi wetu wakipata mafuriko wanaenda halmashauri wakijua halmashauri inaweza ikawasaidia, wanajua NEMC inaweza ikawasaidia lakini ukweli ni kwamba Pwani Ruvu Bonde ndiyo inafanya kila kitu na kuchukua mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu kwa Serikali, kwa kuzingati hizo changamoto nilizozitunguza ni lini sasa mtabadilisha sheria zilizopo ili kuwe na mamlaka moja yenye usimamizi ili hili suala liweze kudhibitiwa vizuri? Swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, takataka za Dar es Salaam pamoja na maelezo yote mazuri na matamu uliyoyeleza ni ukweli kwamba Dar es Salaam yenye wakazi wasiopungua milioni tano, yenye majimbo kumi ya uchaguzi, yenye wilaya kubwa tano lina dampo moja tu ambalo liko Pugu Kinyamwezi; na dampo hilo liko katika hali mbaya sana. Sasa nilitaka Serikali ilieleze Bunge hili Tukufu ina mkakati gani wa kuhakikisha...

MHE. JUMA S. NKAMIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni maswali au anahutubia! (Kicheko)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima malizia swali lako, Mheshimiwa Halima malizia swali lako, Mheshimiwa Halima naomba umalizie swali lako.

MBUNGE FULANI: Tulia tujenge nchi wewe!

MWENYEKITI: Mheshimiwa Halima naomba umalizie.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Serikali katika majibu yake inipe majibu *serious*, kwamba ina mpango gani wa kujenga madampo mengine makubwa. Kama inashindwa kujenga katika kila jimbo basi *at least* kila wilaya iwe na dampo kubwa ili taka ziweze kwenda kutupwa kwa uharaka na kuzuia uchafu. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Azzan Zungu. (Makofi/Vigelele)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ni mara yangu ya kwanza nasimama kwenye upande wa Serikali, kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia wote viumbe vyake. Nimshukuru Mheshimiwa Rais kuwa na imani kubwa sana na mimi kuniweka kwenye wizara nyeti kama hii, lakini mafanikio yangu na mafanikio yetu wote ni kushirikiana, tufanye kazi kwa pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nitajibu swali namba mbili la Mheshimiwa Mbunge Halima Mdee. Ni kweli *crisis* ya taka katika Mkoa wa Dar es Salaam ni kubwa, si ndogo na Dar es Salaam inakuwa sasa hivi kwa asilimia kubwa sana. Kwa miaka miwili ijayo Dar es Salaam itakuwa na *population* siyo chini ya watu milioni nane mpaka tisa na dampo ni moja. Juzi mimi nimekwenda kwenye dampo, hali ya dampo ni mbaya lazima tukiri ni mbaya, miundombinu ni mibaya.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, hatua zimeshachukuliwa. Halmashauri ya Jiji imeshatoa fedha kujenga barabara ya lami katika eneo lote la dampo lakini baada ya hapo kuna mradi ambao unafadhiliwa na donors wa bilioni 75 fedha ambazozimeshakuja. Fedha hizi zimeshawekwa ili ziweze kuboresha dampo jipya la kisasa ambalo litaweza kubeba taka zote za Mkoa wa Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nim-assure Mheshimiwa Mbunge, Serikali iko kazini na Serikali iko makini kuhakikisha kuwa dampo hili linajengwa na fedha ziko tayari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu haya namwambia akae chini sasa. (Makofi/Kicheko)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri ahsante sana, kwa mara ya kwanza kujibu vizuri sana naona mpaka Mheshimiwa Halima mwenyewe ameridhika kabisa. Sasa nampa nafasi Mheshimiwa Naibu Waziri ajibu swali lake la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali la kwanza la Mheshimiwa Halima.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali dogo la kwanza la Mheshimiwa Halima Mdee. Kwanza nakubaliana naye, wanaotoa kibali na siyo cha kuchimba mchanga cha kusafisha mto ni Bonde. Ukishautoa ule mchanga kwenda nje maana yake Wizara ya Madini wanatoa kibali kingine kwa hiyo unapaswa kulipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Ofisi ya Makamu wa Rais kwa maana ya kupitia NEMC tunaowajibika sasa kusimamia athari ya mazingira na uhidhi wa maeneo hayo. Sasa nakubaliana naye kwamba umefika wakati lakini pia Ofisi ya Makamu wa Rais ilishaunda Kamati na kamati hii ilijumuisha wadau wote na imekuja na mapendekezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya mapendekezo ni kuwa sasa na mbadala wa mchanga, hasa kwenye maeneo ya ujenzi sasa hivi, kwenye kokoto ile vumbi ya kokoto ianze kutumika barabarani ili iweze kutumika badala ya mchanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, hata tunapojenga haya majengo yetu sasa tunaanza kutumia vyuma; na baada ya hapo kamati ile pia imependekeza iwepo sasa sheria maalumu na kuwe na bodi moja mbayo inaweza kusimamia zoezi hili. Kwa hiyo nakubaliana naye. N ashukuru.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo ana majibu ya ziada.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri mwenzangu wa Wizara ya Mazingira nipende tu kumtaarifu Mheshimiwa Halima Mdee, Mbunge kwamba hata sisi kwa upande wa Wizara ya Madini tunatoa leseni za uchimbaji wa mchanga tofauti na leseni nyingine. Leseni nyingine tunatoa miaka kumi ya uchimbaji wa madini mengine na leseni nyingine tunatoa kwa muda wa miaka saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leseni ya uchimbaji wa mchanga tunatoa kwa muda wa mwaka mmoja mmoja. Maana yake nini; ni kwamba kila tunapotoa leseni katika maeneo fulani basi tunaangalia vilevile na athari za mazingira kwa kushirikiana na Wizara ya Mazingira, na tunapoonna kwamba eneo hili halifai basi kwa mwaka unaofuata hatutaweza kutoa leseni hiyo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo tunatoa muda mfupi mfupi huku tuki- *monitor* mazingira yanavyokwenda katika maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunapotoa sisi leseni za uchimbaji tunategemea kabisa na mamlaka nyingine ikiwemo mamlaka za halmashauri na mamlaka nyingine ambazo zinalinda mabonde, tunashirikiana kwa pamoja katika kutoa vibali. Tunapokuwa tunaona kwamba eneo hili tunakubaliana kwamba mtu achimbe mchanga tunakuwa tumekubaliana kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapooona kwamba kuna athari inaweza kutokea katika uchimbaji wa mazingira, basi mamlaka ile nyingine tunashirikiana nazo kuhakikisha kwamba tunafuata maamuzi ambao wanaona na wao kwamba kuna athari au hakuna athari katika maeneo yale ya uchimbaji wa mchanga. Ahsante sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwako, Mbunge wa Kasulu Mjini.

Na. 29

Uhifadhi wa Vyanzo vya Maji Kasulu

MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO aliuliza:-

Katika nchi yetu na hasa Mkoa wa Kigoma kuna vyanzo vingi vya maji (*Water sources*) Jimbo la Kasulu peke yake kuna vyanzo vya uhakika zaidi ya 150.

(a) Je, kwa nini Serikali haiji na Mkakati wa kina wa uhifadhi wa vyanzo vya maji katika Wilaya ya Kasulu:-

(b) Jambo hili haliwezi kuachiwa Halmashauri zetu peke yake. Je, ni lini Serikali itakuja na mpango '*A Comprehensive Water Sources Protection Program*' ili vyanzo vya maji vilindwe na vitunzwe ili kukabiliana na uharibifu wa mazingira na kukabiliana na madhara ya tabianchi?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daniel Nicodemus Nsanzugwako, Mbunge wa Kasulu Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo mikakati mbalimbali ya kuhifadhi vyanzo vya maji nchini ikiwemo Wilaya ya Kasulu. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(i) Mkakati wa hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya ardhi, vyanzo vya maji nchini ulioandaliwa mwaka 2006 wenye hatua za muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu; na

(ii) Mkakati wa hatua za haraka za kuhifadhi mazingira ya bahari, maziwa, mabwawa na mito uliandaliwa mwaka 2008 kwa lengo la kuboresha mazingira ya bahari, maziwa, mabwawa na mito ili kuongeza kasi ya kulinda vyanzo vya maji kama vile mito ikiwa ni pamoja na kulinda na kuhifadhi bioanuai na rasilimali zake.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na UNEP inaandaa Mradi wa urejeshaji wa mifumo ya ikolojia pamoja na hifadhi ya bioanuai katika Bonde la Mto Malagarasi, Ruaha na Ziwa Rukwa. Mradi huu utatekelezwa katika ngazi za Mgazi, Uvinza, Buhoro, Msambala na Basunzu zilizopo katika Wilaya ya Uvinza, Kasulu na Kibondo Mkoani Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iko kazini na inashirikiana na wadau wengine katika suala la kulinda vyanzo vya maji, hii ikiwa ni pamoja na kuvitambua vyanzo vya maji na kuweka mipaka na kulinda eneo hilo kwa mujibu wa Sheria. Kazi hii inafanywa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Aidha, hatua mbalimbali za kisheria zinaendelea kuchukuliwa kwa waharibifu wa mazingira. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nsanzugwako swali la nyongeza kama lipo.

MHE. DANIEL N. NSANZUGWAKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusikiliza majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza lilikuwa ni mahususi kwa Kasulu Mjini ambapo timu ya wataalam wa NEMC na Wizara ya Maji wakiwa tisa walikuja kufanya survey pale mwaka 2018 na wakaandika ripoti nzuri sana, wakati huo alikuwa Waziri Makamba. Hiyo ripoti iko ofisini kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ile ripoti ifanyiwe kazi kwa sababu ilikuwa mahususi kwa ajili ya Mji wa Kasulu na Kasulu Vijijini ambako mito zaidi ya 50 ilibainika pale na moja ya chanjo kipo shambani kwangu, nami ndio nakilinda kwa gharama kubwa ili kisiharibike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni la Kitaifa zaidi. Nimekubaliana naye na sasa napenda nipate *time line*: Je, huo mradi wa urejeshaji wa ikolojia ya Mto Malagalasi unaanza lini kwa maana ya vijiji vya Buhoro, Busunzu, Msambala na Kabanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu amesema ni mradi wa Kitaifa, napenda kujua *time line* ya huo mradi wa kurejesha ikolojia ya Mto Malagarasi ambayo imeharibika sana.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Daniel Nsanzugwako kwa juhudi zake kubwa za kuhifadhi mazingira na ametupa ushirikiano wa kutosha tangu wataalam wamekuja na leo anaikumbuka ile taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba taarifa hiyo sasa nitakwenda kuisoma vizuri na nitakushirikisha kabla Bunge hili halijaisha, ni hatua gani ambazo tutaanza kuzichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na swali la pili, kwamba hatua gani mbadala na kwa wakati gani? Naomba pia kabla hatujamaliza shughuli zetu za Bunge leo, pia nitakupa taarifa hizi nikiwa nimeshawasiliana na wataalam kwamba wakati gani tunaweza kuanza kazi hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere Mbunge wa Bunda sasa aulize swali lake.

Na. 30

Ubadhirifu wa Mali ya Umma

MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuliza:-

Katika miaka ya hivi karibuni nchi yetu imekuwa na majina mengi katika Idara ya Ukaguzi toka Ofisi ya CAG kama vile Hati safi, Hati inayoridhisha na Hati chafu:-

(a) Je, Shirika au Halmashauri kupata hati safi ni ishara kwamba Shirika au Halmashauri husika halina ubadhirifu wa mali ya Umma kwa kuwa kuna kila dalili kuwa kutolewa kwa hati safi ni dalili ya wazi ya kuficha ubadhirifu katika baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma?

(b) Je, lini Serikali itafuta utaratibu huo ambao umekuwa kinga ya ubadhirifu wa mali ya Umma?

MWENYEKITI: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwita Boniphace Getere, Mbunge wa Bunda, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya Mwaka 2008 inampa mamlaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya kaguzi mbalimbali ambazo ni Ukaguzi wa Hesabu (*Financial Audits*), Ukaguzi wa Kiuchunguzi (*Forensic Audits*), Ukaguzi wa Ufanisi (*Performance Audits*) na Ukaguzi Maalum (*Special Audits*). Lengo Kuu la Ukaguzi wa Hesabu (*Financial Audits*) ni kutoa maoni kama Hesabu zinazokaguliwa zinaonyesha hali halisi ya mapato na matumizi ya Serikali kwa kuzingatia Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Taarifa za Fedha. Maoni haya hutolewa kwa njia ya hati za ukaguzi ambazo zimegawanyika katika makundi manne ambayo ni hati inayoridhisha; hati yenye shaka hati isiyoridhisha na hati mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hati inayoridhisha hutolewa wakati taarifa za fedha zilizowasilishwa na kukaguliwa zinapokuwa zimezingatia Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Hesabu katika Sekta ya Umma na Sheria na Kanuni za Fedha za Umma. Hati hii huonesha taarifa za fedha zinatoa taswira ya kweli na hali halisi ya mapato, matumizi, mali na madeni ya taasisi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya kuwa 'hati inayoridhisha' inatoa tafsiri ya kutokuwepo kwa kila aina ya ubadhirifu siyo sahihi kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, maoni ya ukaguzi yanatolewa kwa malengo maalum ya kuwafahamisha watumiaji wa taarifa za fedha kama taarifa hizo zinaonyesha ukweli na hali halisi ya hesabu za mizania (*financial positions*) kwa tarehe husika, taarifa za mapato na matumizi (*financial performance*) pamoja na taarifa ya mtiririko wa fedha (*cash flows*) kwa kipindi kilichokaguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, dhana ya ukaguzi wa hesabu inajikita katika masuala ambayo wakaguzi wanaamini kuwa ni mazito na yana athari kubwa kwenye taarifa za fedha

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

za taasisi husika. Hii ina maana kuwa, mambo ambayo hayana athari kwenye taarifa za fedha yanashughulikwa na mifumo ya udhibiti wa ndani ya taasisi husika.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa majibu haya ya sehemu (a), napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, utaratibu huu ndiyo unaotumika dunia nzima, hivyo Serikali haina mpango wa kufuta hati inayoridhisha yenye maoni ya kikaguzi wala kuingilia namna taaluma ya ukaguzi nchini inavyoendeshwa. Kutoa utaratibu mwingine itakuwa ni kukiuka Viwango vya Kimataifa vya Uandaaji wa Tarifa za Fedha katika Sekta ya Umma na pia Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi ambavyo Taifa na Serikali yetu imeviridhia vitumike.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwita Getere, kama una swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali ambayo yametolewa na Naibu Waziri, lakini mimi shida yangu ni moja tu. Mimi sio Mhasibu sana lakini ukitazama ukweli uliopo ni kwamba ukaguzi huu ambao ni wa Kimataifa unaonyesha nyaraka za kihesabu na vitabu vya kihesabu vinavyokaguliwa kama viko sawa, lakini havionyeshi matumizi ya ndani kama shirika limepata hati safi kwa maana kwamba halina ubadhirifu. Sasa je, Serikali inaonaje sasa, utaratibu wa Kimataifa uendelee lakini tuwe na utaratibu wa ndani ili kutambua ubadhirifu unaotokea kwenye mashirika yaliyo na hati safi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba kuna dhana ya ukaguzi ambapo wanaona kama kuna matatizo makubwa yanatokea kwenye athari za kihesabu; sasa haya matatizo makubwa na haya madogo anayoyataja sijayaona kwenye majibu yake; pengine angeweza kutusaidia kwamba haya matatizo makubwa ya kiathari za hesabu ni yapi kwenye shughuli za kimahesabu?

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nayajibu maswali yake yote mawili kwa sababu yote jibu lake ni moja. Zipo aina tofauti za kaguzi zinazofanyika ukiacha kaguzi za mahesabu kama nilivyosema ili kujibu maswali yake yote mawili kwamba ni matatizo gani makubwa na madogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kunapokuwa na matatizo hayo mengine ambayo yako nje ya taarifa za kihesabu, huwa kuna ukaguzi wa ufanisi (*performance audit*) ili kuweza kujiza Serikali juu ya namna bora ya kutumia rasilimali zake katika kubana matumizi; pia kuhimiza taasisi za Umma kuboresha utendaji wake wa kazi kufikia malengo kwa tija na kupata thamani halisi ya fedha.

Kwa hiyo, hapa tunakwenda kwenye miradi yenyewe kuangalia mchakato mzima wa mradi ulifanyikaje na mradi je, unajibu hali halisi ya thamani ya fedha kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna aina ya pili ya ukaguzi ambayo ni ukaguzi maalum (*special audit*). Ukaguzi huu maalum huombwa maalum na mtu *specific* au taasisi yenyewe ikiwa imegundua kuna matatizo hata kama taasisi yake ina hati inayoridhisha. Kwa hiyo, hii inakuwa na hadidu za rejea ambazo zimetolewa na mtu aliyeona kuna matatizo kwenye taasisi hiyo kwa hiyo inafanyika *special audit* ili kujibu hayo matatizo yaliyoonekana.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna ukaguzi wa kiuchunguzi (*forensic audit*). Huu ni ukaguzi wa kisayansi ambao nao unakuwa na hadidu za rejea, tunakwenda zaidi ya *special audit* kujua matatizo haya yamesababishwa na nini kwenye taasisi husika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tuendelee kuziamini ofisi zetu na hasa Ofisi ya Mkaguzi na Mdhhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa sababu wanafanya kazi zao kitaalamu zaidi.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango. Tunaendelea sasa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba Mbunge wa Busanda, sasa aulize swali lake.

Na. 31

Ujenzi wa Gati – Bukondo

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa Gati katika Kijiji cha Bukondo Halmashauri ya Wilaya ya Geita?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Bukwimba, Mbunge wa Busanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania ina mpango wa kufanya upembuzi yakinifu kwenye Maziwa yote Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa ili kutambua maeneo yanayofaa kujenga magati. Zabuni kwa ajili ya kumpata mtaalam mwelekezi wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu ilitangazwa na kupata kampuni ya *RINA* kutoka nchini Italia mwezi Desemba, 2018 kwa ajili ya kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kumpata mshauri mwelekezi huyo kumekuwa na mazungumzo ya maridhiano ya bei ya kufanya kazi ambayo yalikamilika mwezi Desemba, 2019. Kazi ya Upembuzi Yakinifu inatarajiwa kuanza mwezi Februari, 2020 na kukamilika ndani ya miezi 18. Hivyo, ujenzi wa gati katika eneo la Bukondo utategemea mapendekezo ya taarifa ya mshauri mwelekezi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, swali la nyongeza.

MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Gati hili la Bukondo siyo kwamba ni jipya, lipo, ila tu limeharibika kiasi kwamba meli zinapotua pale kwenye gati zinashindwa kutua vizuri, wananchi ni lazima wakanyage maji ndio wanaingia kwenye *ferry*. Kwa hiyo, siyo kwamba gati halipo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti za Serikali kila mwaka huwa naiona inawekwa kwenye lakini utekelezaji tu wa ujenzi sijaona ukifanyika. Napenda kujua sasa, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa lile gati kwa sababu tayari lipo? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa kuna barabara ambazo huwawezesha wananchi kufika kwenye gati hilo; barabara hizo nazo hazipitiki vizuri hasa katika kipindi hiki cha mvua; napenda kujua hatima ya hizi barabara. Kuna barabara ya kutokea Katoro - Inyara kwenda mpaka Bukondo; pia kuna barabara ya kutoka Nyarugusu kwenda Rwamgasa mpaka Katoro na nyingine ya kutokea Kahama ambayo tayari Serikali imeshaiweka kwenye bajeti ya kuweza kutengenezwa kwa kiwango cha lami; napenda kujua hizo barabara zitatengenezwa lini? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, katika majibu yangu ya awali nimeeleza kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari ina mpango wa kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kujenga magati kwenye maziwa yote makuu. Kwa kusema hivyo siyo kwamba hatujui kwamba kuna gati katika eneo hilo. Gati katika eneo hilo lipo na gati hilo mpaka sasa hivi linamilikiwa na Halmashauri pamoja na GGM.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu gati hilo kwamba linatakiwa kupata matengenezo na usimamizi maalum na ndiyo maana kwa ridhaa ya Bunge tulifanya marekebisho ya sheria kwenye Bunge lililopita kuhakikisha sasa kwamba Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari inaweza kumiliki bandari zote ambazo ziko kwenye maziwa makuu na eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu zinaendelea na upembuzi yakinifu unafanyika, siyo kwa eneo hilo peke yake, ni kwa maeneo yote nchi nzima; maeneo ya bahari pamoja na maziwa makuu. Tutakapokuwa tumekamilisha huo upembuzi yakinifu, basi tutaichukua na bandari hiyo tutairekebisha ili kuiweka miundombinu stahiki ya kuweza kuirekebisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili ameulizia kuhusu ujenzi wa kurekebisha barabara ambazo zinaingia kwenye eneo hilo la gati. Ni kweli katika mvua hizi zinazoendelea kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa miundombinu hasa ya barabara maeneo mbalimbali. Eneo hilo tunalifahamu na limeshatengewa katika zile shilingi bilioni tisa ambazo zimetengwa za dharura na lenyewe litazingatiwa kwa ajili ya kurekebisha.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Lijualikali, Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

MHE. PETER A. LIJUALIKALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kule kwenye Jimbo langu kuna ujenzi wa barabara ya Ifakara – Kidatu. Barabara hii ilizinduliwa na Mheshimiwa Rais mwaka 2018 na akatoa ahadi kwamba mpaka mwaka huu mwezi wa Nne itakuwa imeshakamilika. Barabara hii mpaka hivi sasa imekamilika kwa asilimia takribani tano tu na bado mwezi mmoja mradi uweze kufungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kauli ya Serikali, ni kwa nini barabara hii imechukua muda mrefu hivi na ni lini itakamilika ili adha ya watu wa Kilombero iweze kwisha?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara ya Kidatu - Ifakara ilianza kujengwa kwa kiwango cha lami na katika hatua za awali kumekuwa na kusuasua. Nami nimetembelea eneo hili, hata juzi RAS alitembelea eneo hili na kutoa maagizo makali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunafahamu changamoto zilizopo lakini hapo awali kulikuwa na changamoto ya masuala ya vifaa kwa maana ya zile *exemptions*. Tatizo hili lilishaisha na tumetoa maelekezo mkandarasi afanye kazi usiku na mchana ili kuweza kufidia muda ambao ulipotea wakati ule wa malumbano wa masuala ya *VAT Exemption*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wewe vuta subira, sisi tunaendelea kuisimamia kwa nguvu na utaona kwamba sasa kutakuwa na uhai mkubwa wa kuhakikisha barabara hii inajengwa na inakamilika na wananchi wanapata manufaa ya kuitumia barabara hii ikiwa katika kiwango cha lami. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Bonnah.

MHE. BONNAH L. KAMOLI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niulize, Serikali ina mpango gani kuhusiana na barabara za Mkoa wa Dar es Salaam hususan barabara ya Vingunguti - Liwiti ambapo kuna mradi mkubwa wa machinjio lakini barabara yake ni mbovu sana, ina mahandaki makubwa? Sasa Serikali ina mpango gani kuhusiana na hizo barabara? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, kama jana nilivyozungumza ni kwamba kati ya maeneo ambayo yamepata athari kubwa hasa kwa mvua za mwezi Oktoba na Novemba ni Mkoa wa Dar es Salaam. Nilisema kwamba katika hatua zile za awali, kama mkakati wa kunusuru hali ya uharibifu wa barabara katika Jiji ni pamoja na kupeleka fedha za dharura. Kwa hiyo, tulitumia takribani shilingi milioni 500 kurejeshwa maeneo ambayo yalikuwa yameharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mvua zinaendelea kunyesha, bado uharibifu unaendelea kutokea. Nasi kama Serikali tunajipanga na kila wakati tumetoa maelekezo kwa Mameneja wa Mikoa, waendeleo kutuletea hizo taarifa za uharibifu unaotokea ili tuendeleo kufanya uratibu kwa sababu suala la kurejeshwa miundombinu hasa kipindi hiki ambacho mvua zinaendelea kunyesha ni endelevu. Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge tuendeleo kushirikiana, watupe taarifa za maeneo ambayo yanaendelea kupata uharibifu na sisi tulivyojipanga tutaendeleo kuwahudumia wananchi katika maeneo haya ili kwanza waweze kupita, lakini mvua zikipungua tutakuja na mkakati wa kuona tunafanya maboresho makubwa.

MWENYEKITI: Haya, swali la mwisho la nyongeza Mheshimiwa Charles Tizeba.

MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Huko katika Ziwa Victoria kutokana na mvua nyingi zinazonyesha msimu huu, magati mengi yamemezwa na maji katika hili pamoja na gati alilolisema Mheshimiwa Bukwimba lakini Gati la Kisiwani Maisome na Gati la kule Bugorora Ukerewe na yenyewe yamezama, wananchi wanaingia kwenye vivuko kwa kuvua nguo. Tunaomba Serikali itupe kauli kwamba itashughulikia vipi kwa haraka magati haya ili wananchi wasiendeleo kupata aibu na usumbufu? *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ATASHASTA J. NDITIYE):

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimia Dkt. Charles Tizeba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunatambua kwamba kutokana na mvua hizi zilizonyesha magati mengi yamepata changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoweza kupitika vizuri baada ya kuwa yamejaa maji. Tumeendelea kufanya utafiti wa kina kwa kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari. Tukumbuke tu kwamba magati mengi ambayo yapo nchini bado yanamilikiwa na Halmashauri.

Kwa hiyo lazima kuwepo vikao vingi vya kukubaliana namna ya kuyachukua magati yale na kuyaendesha, kwa sababu sheria ilikuwa haijapitishwa na kwa kuwa sasa sheria imepitishwa ni lazima sasa tunakwenda hatua kwa hatua kuhakikisha kwamba yale magati yote ambayo yako chini ya kiwango yaliyokuwa yanamilikiwa na Halmashauri sehemu mbalimbali nchini yanarekebisha kwa kiwango ambacho kinakidhi *standard* za kuendeshwa na Mamlaka ya Bandari.

Kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba atuvumilie kidogo, tunakwenda kufanya utafiti wa kina na kuyarekebisha magati yote nchi nzima yaweze kupitika kwa kiwango na yaweze kuhudumia wananchi.

MWENYEKITI: Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 32

Hitaji la Huduma ya Mawasiliano Wilaya ya Simanjiro

MHE. ESTER A. MAHAWE aliuliza:-

Kata za Naberera, Kitwai, Lorbene, Loibosroit, Norakauwo na Komolo katika Wilaya ya Simanjiro hazina huduma ya mawasiliano ya simu:-

Je, ni lini sasa Serikali itapeleka minara ya simu ili wananchi hao waweze kupata huduma ya mawasiliano ya simu?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ATASHASTA J. NDITIYE)

alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa, Ester Alexander Mahawe, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya kufikisha huduma za mawasiliano nchi nzima. Kata ya Naberera, ilijumuishwa kwenye zabuni ya mwezi Agosti, 2017 na vijiji vitano vilipata mtoa huduma kampuni ya Vodacom ambayo tayari imefikisha huduma ya mawasiliano katika vijiji hivyo. Aidha, vijiji vingine vitatu katika Kata hiyo ya Naberera vilijumuishwa katika zabuni ya awamu ya tatu mwezi Disemba, 2018 na kupata mtoa huduma kampuni ya mawasiliano

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Tanzania TTCL ambayo inaendelea na utekelezaji wa mradi wa kufikisha mawasiliano katika vijiji hivyo. Hadi hapo ifikapo tarehe 30 Juni, 2020 tunategemea mradi utakuwa umekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Kata za Kitwai na Loibosroit zilijumuishwa kwenye zabuni ya awamu ya tatu na kupata watoa huduma kampuni ya *Halotel* kwa Kata ya Loibosroit na kampuni ya mawasiliano Tanzania kwa Kata ya Kitwai. Zoezi la kusaini mkataba lilifanyika tarehe 13 Desemba, 2018 na fedha za awali tayari zilikwishatolewa kwa watoa huduma ambapo kwa sasa wanaendelea na taratibu za ujenzi wa mnara ili kukamilisha mradi ifikapo Juni, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Kata ya Komolo iliingizwa kwenye zabuni ya awamu ya nne ya Julai, 2019, japokuwa haikufanikiwa kupata mtoa huduma hivyo tunategema itajumuishwa tena katika zabuni ya awamu ya tano. Aidha, Vijiji vya Kata za Lorbene na Norakauwo vyote kwa pamoja vitajumuishwa kwenye zabuni ya awamu ya tano ambayo itatangazwa katika mwaka wa fedha 2019/2020.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ester Mahawe.

MHE. ESTER A. MAHAWE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri na jitihada za Serikali, bado maeneo mengi ya Mkoa wa Manyara yana tatizo kubwa la mtandao. Ukiacha upatikanaji wa sauti, lakini bado kuna shida kubwa katika upatikanaji wa *internet*, kwa hiyo shughuli nyingi za Serikali zikiwemo hospitali, shule na ofisi mbalimbali zinashindwa kufanyika ipasavyo kutokana na ukosefu huo wa mtandao. Je, ni lini sasa Serikali itahakikisha *data* zinaweza kupatikana katika Mkoa wa Manyara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni stendi ya Mji wa Babati iliamia nje kidogo ya mji na tuna tatizo kubwa sana la mtandao katika stendi hiyo. Ni mtandao wa *tigo* peke yake ndiyo unaopatikana na kama tunavyofahamu shughuli zilizoko stendi ni nyingi na abiria ni wengi wanaotumia mitandao mbalimbali.

Je, ni lini Serikali itahakikisha kwamba mtandao unapatikana katika stendi ya Mji wa Babati na ni lini labda pia Waziri yuko tayari kuambatana na mimi kuona tatizo hili kubwa katika Mkoa mzima wa Manyara. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Ester Alexander Mahawe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Ester Mahawe kwa jinsi anavyofuatilia Mkoa wake mzima suala la upatikanaji wa mawasiliano. Ni kweli kwamba maeneo mengi ambayo Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote ulikuwa unatoa pesa kwa ajili ya kujenga minara ya mawasiliano, walikuwa wanapeleka minara ambayo ina-*supply* 2G ambayo inahudumia *voice* na *data* kwa maana ya *text* peke yake lakini *internet* hakuna. Kuanzia tenda iliyotangazwa na kusainiwa Desemba, 2018, tulizielekeza kampuni zote kwamba sasa hivi kuanzia 2019 minara yote itakayojengwa iwe na *access* ya 3G ili wananchi wa maeneo hayo waweze kutumia *data* na mpaka sasa hivi minara inayoendelea kujengwa ambayo tunategemea itakamilika Juni, 2020, mingi sana itakuwa na huduma ya *data* kwa maana ya 3G, 4G na kuendelea.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye swali lake la pili ni kweli kwamba stendi ya Babati ina mawasiliano ya tigo peke yake. Niyashauri makampuni mbalimbali yanayotoa huduma za mawasiliano nchini yachukue nafasi hii kuona fursa ya kuweka minara hiyo katika maeneo ya stendi ya mabati kwa sababu kuna mkusanyiko mkubwa wa watu, kuna uchumi mwingi, kwa hiyo wakiweka mawasiliano pale itasaidia sana kuhakikisha kwamba wananchi wa Babati kwenye stendi pale wanaweza kupata huduma ya mawasiliano kutoka kwenye makampuni mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa mimi niko tayari kuongozana na tutatembea na maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Manyara na Mheshimiwa Ester Mahawe kwa ruhusa yako. (Makofi)

MWENYEKITI: Naanza na Mheshimiwa Deo Ngalawa atafuatiwa na Mheshimiwa Kemi, Mheshimiwa Sophia na Mheshimiwa Selasini.

MHE. DEO F. NGALAWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kata ya Ibumi katika Jimbo la Ludewa ni kata pekee ambayo haina mawasiliano kabisa na bahati nzuri yupo mzabuni TTCL ameanza kujenga, lakini toka alipojenga ule mnara mpaka leo hii hatujui kinachoendelea. Naomba kauli ya Serikali sasa kujua ni lini wananchi wa Kata ya Ibumi watapata mawasiliano ya simu? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Ngalawa, Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kampuni ya mawasiliano Tanzania (TTCL) ilipewa zabuni ya kujenga mnara wa mawasiliano kwenye Kata ya Ibumi. Mpaka sasahivi ninavyoongea na Waheshimiwa Waunge, mnara huo ulikwishajengwa lakini bado haujawashwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulitokea tatizo la kiufundi katika kuwasha mnara huo, ambapo tatizo hilo sasa limerekebishwa na nimhakikishie Mbunge kwamba ndani ya siku 30, Mamlaka ya Mawasiliano pamoja na TTCL watashirikiana kuhakikisha kwamba changamoto hiyo iliyojitokeza inatatuliwa na watu wa Ibumi wataendelea kupata mawasiliano.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Kemi.

MHE. KEMILEMBE J. LWOTA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Katika Wilaya ya Kwimba, Kata za Bugando, Mkalalo na Mwabomba kumekuwa na tatizo kubwa sana la mawasiliano na ni la muda mrefu. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka mawasiliano kwenye Kata hizo za Wilaya ya Kwimba ili wananchi hao waweze kufaidika na mawasiliano ya nchi hiyo?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kemilembe, Mbunge wa Viti Maalum, Mwanza, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Kemilembe kwa jinsi anavyofuatilia masuala ya mawasiliano kwa Mkoa Mzima wa Mwanza

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambapo kwa kweli muda mwingi sana amekuwa akifuatilia maeneo mbalimbali ya Mkoa huo. Kuhusu Wilaya ya kwimba ni kweli Mheshimiwa Kemilembe alikuja akaniletea barua kuhusu kata ambazo alizitaja. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Kemilembe na Mbunge wa Kwimba kwamba tayari zabuni kuhusu kata alizozitungumza zimewekwa kwenye kitabu maalum ambapo anaweza akaja mezani kwangu kuangalia. Awamu ya tano tutahakikisha kata zote zilizobakia ambazo hazijapata mawasiliano zinapata mawasiliano.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sophia.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kama ilivyo katika Jimbo la Simanjiro vivyo hivyo Jimbo la Rungwe kuna shida ya mawasiliano hasa katika Kata za Ilima, Swaya, Bujera pamoja na Ikuti. Je, ni lini Serikali itasaidia wananchi wa maeneo haya waweze kupata mawasiliano mazuri hususan katika mitandao yote wana shida ya mawasiliano? Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

WAZIRI WA UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna maeneo katika Jimbo la Rungwe ambayo yana changamoto ya mawasiliano. Ni kweli pia kwamba hata Mbunge wa Jimbo la Rungwe, Mheshimiwa S. H. Amon amekwishafika ofisini lakini pia bahati nzuri ni Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu ambako ndiyo tunashughulikia masuala hayo, tumekwishaongea, amekwishaleta barua kwa maandishi na tayari zabuni ya Awamu ya Tano maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Sophia ambayo hata Mbunge anayafahamu yatajumuishwa kwa ajili ya kupelekewa mawasiliano. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini, halafu mwisho Mheshimiwa Nuru.

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Bunge la Kumi na hata Bunge hili nimekuwa nikiomba Serikali irekebishe tatizo la mwingiliano wa simu wa mitandao ya nchi jirani ya Kenya na Tanzania ambayo yanasumbua sana wananchi wangu katika Jimbo la Rombo kiasi kwamba wanajikuta wanatumia huduma za *roaming* na hivyo kuwa na gharama kubwa sana ya simu bila sababu yoyote. Nimekuwa nikipata ahadi nzuri sana kwa Mheshimiwa Naibu Waziri. Naomba kuuliza, ule mkakati ambao Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa ananiahidi na ameliahidi Bunge, unaendelea na umefikia wapi ili kutatua tatizo hili?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Selasini, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tumekuwa tukiwasiliana mara nyingi sana kuhusu mwingiliano wa mawasiliano kati ya nchi ya Kenya na nchi ya Tanzania kwa upande wa eneo la Rombo. Sio huyo tu, nimekuwa nikiwasiliana na Wabunge kutoka maeneo mbalimbali ambayo yako mipakani. Tunavyo vikao vya kikanda vinavyohusu masuala ya mawasiliano kwamba Mamlaka za Mawasiliano za nchi mbalimbali katika ukanda wa Afrika Mashariki na Kati huwa yanakutana mara nyingi kujadili masuala hayo ya mwingiliano. Pia kwenye mikutano ya Kimataifa ya ITU pia suala la mwingiliano wa mawasiliano huwa linajadiliwa mara nyingi sana.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Ni kweli kwamba mpaka sasa hivi Mheshimiwa Selasini atakuwa shahidi yangu kwamba upande wa *line* za *Voda* kuna marekebisho makubwa sana yanaendelea kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna changamoto moja kwamba wenzetu hawaweki minara kilometa tano *away from the border*, sisi tunaweka kilometa tano *away from the border*, hilo limeendelea kuongelewa na hivi mwezi wa Pili kuna kikao kingine kikubwa cha kufuatilia utekelezaji wa kampuni za simu kupeleka minara kilometa tano kutoka mpaka ulipo ili angalau mawasiliano yale yaweze kuwahusu watu wanaohusika na nchi tofauti. Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Selasini kwamba, tunaendelea na tukimaliza *Vodacom* pia tutakwenda na *tigo*, pia tutakwenda na *Airtel* ili kuhakikisha kwamba wanarekebisha hata zile *frequency* zao zisielekee nchi jirani ila ziwahudumie Watanzania.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Nuru.

MHE. NURU A. BAFADHILI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa katika Mtaa wa Kalimaji, Kata ya Moshono, katika Jiji la Arusha kuna tatizo la mawasiliano ya *tigo*, je, Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha mawasiliano hayo yanapatikana kwa vile wananchi wanayakosa hayo mawasiliano? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE): Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum na Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri tumekwishaongea sana na Mheshimiwa Nuru Bafadhili kuhusu suala hilo na bahati nzuri nimekwishamuonesha kwenye vitabu jinsi ambavyo maeneo aliyoyataja tulivyoyaweka na nimpungeze sana kwa jinsi alivyofuatilia maeneo yale mpaka tumeyaingiza kwenye tenda ya awamu ya tano. Nimhakikishie tu kwamba kuanzia mwezi wa Tatu tutatangaza tenda ili makampuni ya simu yaweze kuchukua kwa ajili ya kwenda kutekeleza miradi hiyo na wananchi wa maeneo yale waweze kupata mawasiliano. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Tunamalizia Wizara hii ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano kwa swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo.

Na. 33

Ujenzi wa Barabara ya Lushoto - Mlalo

MHE. RASHID A. SHANGAZI aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa barabara ya Lushoto – Mlalo kilomita 45 kwa kiwango cha lami?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, kama ifuatavyo:-

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Lushoto – Mlalo yenye urefu wa kilometa 41.93 ni sehemu ya barabara ya Mkoa ya Lushoto – Mlalo – Umba Junction yenye urefu wa kilometa 66.23 inayohudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, ilianza kujenga kwa kiwango cha lami kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Hadi kufikia Mwaka wa Fedha 2018/2019, jumla ya kilometa 8.6 zimeshakamilika kwa gharama ya Sh.5,263,802,375. Aidha, katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Serikali imeendelea kuitengea fedha barabara hii kwa ajili ya kuendelea na ujenzi. Sehemu iliyobaki yenye urefu wa kilometa 33 itaendelea kujengwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rashid Shangazi.

MHE. RASHID A. SHANGAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa Mlalo mwezi wa 12 baada ya zile mvua kubwa ambazo zimesababisha mafuriko na maporomoko makubwa sana kule na ameona barabara ile na hali ilivyo. Je, anatupa majibu gani ya haraka kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana na pia waongeze ujenzi angalau kwa kilometa 10 kila mwaka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; barabara ya kutoka Maramba kwenda Mnaro – Lunguza hadi Mnazi na yenyewe pia ni ni ya Wakala wa Barabara wa Mkoa. Halikadhalika, barabara ya kutoka Lukozi kwenda Mtae kupitia Manoro lakini pia kupitia Makose zote hizi ni barabara ambazo zinahudumiwa na Wakala wa Barabara wa Mkoa. Mpaka sasa hivi ninavyozungumza barabara hizi hazipitiki kwa maana kwamba wananchi wanapata, shida inabidi watumie usafiri wa bodaboda na kutembea kwa miguu. Serikali inatuhakikishia msaada gani wa haraka wa kuhakikisha kwamba barabara hizi zinapatika haraka inavyoweze kana? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza uniruhusu nitoe pole kwa Mheshimiwa Shangazi na wananchi wa Mlalo kwa sababu wakati ule wa mvua nyingi za mwezi wa kumi na mwezi wa kumi na moja tulipata maporomoko ya udongo ambayo pia yalisababisha vifo vya watu kama watano hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uniruhusu nimpongeze pia Mheshimiwa Mbunge, Mheshimiwa Shangazi kwa kweli ni mahiri kwa kushughulikia mambo na nafikiri wananchi wa Mlalo hawakufanya makosa kumchagua kwa sababu Mheshimiwa Shangazi utamuona anazungumzia juu ya barabara lakini sio barabara yake, amezungumza juu ya barabara ambazo zinaunganisha na maeneo mengine. Pia tumeona kwa umahiri wake hapa akishughulika na masuala ya michezo, wote tunafahamu. Mheshimiwa Shangazi pia ni *coordinator* mzuri kwenye upande wa chama, kwa hiyo, Mheshimiwa Shangazi nakupongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lako la barabara ya Mlalo, nafahamu kwamba kwenye mafuriko yaliyotokea hata eneo kubwa la uchumi kwenye eneo lako la umwagiliaji kule Mlalo ulipata shida na barabara haipitiki na ndio maana nilitembelea maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Shangazi kwamba kwa jinsi *nature* ilivyo, tulikubaliana na tumetoa maelekezo kwamba angalau tuongeze kidogo kwenye bajeti

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

zetu ndio mkakati wetu ili angalau maeneo yale yote yaliyo makorofi kama kilometa 10 hivi tuweze kuya-cover ili wananchi wasiendeleo kupata shida tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuhakikishie tunajitahidi kadri tutakavyoweza kupata nafasi kwenye bajeti yetu tupatazame eneo hili ili wananchi wa eneo hili la Mlalo waweze kupata huduma vizuri na hasa ukianza kule Mlalo kuelekea Lushoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, kama nilivyosema Mheshimiwa Shangazi anafuatilia kuona wananchi wa Mlalo wanaweza kusafiri kwa vizuri kabisa kuja huku Lushoto lakini wanaweza wakasafiri vizuri kabisa kwenda kule Malamba na Same kupitia kule Bondeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Shangazi nikuhakikishie kwa wananchi wako wa Malamba, Lunguza, Mnazi, Lukozi, Manolo na hadi kule Mtai kwa jinsi tulivyoona hali ilivyo na tumetoa maelekezo kwa Meneja wa TANROAD Mkoa wa Tanga kwamba tuweze kuweka fungu la kutosha kwa sababu hizi barabara angalau tuziboreshe ili madaraja yaweze kukaa vizuri, tuweke changarawe katika maeneo haya ili barabara ikae vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Shangazi vuta subira tu kwa sababu maeneo haya yote nimeyatembelea, nitakuwa na umakini mkubwa kuhakikisha kwamba wakati tunaangalia bajeti yetu basi wananchi wa maeneo haya wanapitika vizuri. Kwa sababu kisera lazima tuhakikishe wananchi kwanza wanapita halafu tuendeleo ku-deal na uboreshaji wa makalavati na madaraja ili wananchi hawa waweze kuwa supported kwenye hali ya uchumi katika eneo hili, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Haya naanza na Mheshimiwa Bulembo, halafu Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

MHE. ALHAJI ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kutokana na swali la msingi, barabara ya Korogwe – Magoma- Mashewa – Mtoni Mombo – Kibaoni – Kalahani – Maramba kwenda Tanga Mjini ina tatizo kama la Mlalo lakini barabara ile tatizo kubwa kuna makalavati madogo madogo ambayo mngelayafanyia haraka ili wananchi waweze kupita. Je, Wizara inatuamnia nini wale wananchi watoke kwenye kisiwa kilichopo sasa hivi? (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli maeneo haya Mheshimiwa Mbunge aliyoyataja yana changamoto, Mheshimiwa Bulembo nikuhakikishie kwamba nilivyofanya ziara maalum kuangalia maeneo ambayo yameathirika na mvua katika maeneo ya Mkoa wa Tanga nikianza kule Kilindi, nimekwenda Handeni lakini kwenye maeneo hayo umeyataja tumefanya ziara na Waheshimiwa Wabunge kwa hiyo nimeona. Na yale maeneo ambayo kimsingi yameharibiwa na yana nafasi ya kufanyiwa matengenezo kwa sababu yapo maeneo mengine ambayo bado maji yanapita kwa wingi sio rahisi kwa muda huu kufanya matengenezo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa maeneo hayo tulitoa maelekezo kwa maana kwamba TANROADS na TARURA washirikiane maeneo ambayo tuliyaona kwamba kwa haraka waweze kuweka makalavati na maeneo hayo mengi mengine ujenzi umekwishafanyika. Lakini kwa maeneo ambayo changamoto zake zinahitaji utatuzi wake kufanyika baada ya mvua kukoma, haya nayo tunayaweka kwenye utaratibu kama nilivyozungumza tumeshayatambua, tunayatengea fedha. Tunawahakikishia wananchi kwamba wanapita kwenye maeneo yale.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge uvute subira tumetambua maeneo yote, tutaendelea kuyashughulikia kulingana na changamoto na hali ilivyo kutokana na sehemu mahsusi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Rhoda Kunchela, atafuatia Mheshimiwa Mary Chatanda.

MHE. RHODA E. KUNCHELA: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya kutoka Tabora – Ipole – Koga – Inyonga kuelekea mpaka Mkoa wa Katavi kwa kipindi hiki cha mvua, barabara hii ni mbaya na haipitiki. Na wiki moja iliyopita daraja la Koga lilifungwa kwa hiyo ikasababisha wananchi wa Mkoa wa Katavi wakaanza kuzunguka kutoka Mpanda kuelekea Kigoma na kwenda mikoa mingine.

Je, Serikali hii ya Awamu ya Tano inajipangaje kuhakikisha inakamilisha ujenzi wa barabara hii wenye kilometa 359 ili wananchi hawa wa Mkoa wa Katavi waepukane na usumbufu na gharama ambazo wanazipata. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba ni muda mrefu fursa ya kutengeneza barabara ya lami kutoka Tabora kwenda Mpanda haikuwepo. Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba zipo kandarasi kubwa pale zinaendelea, mradi wa kilometa 103, kilometa 105 na kilometa 108 unafahamu na kwamba makandarasi waliopo hapo wana uwezo mkubwa hata kasi ya utengenezaji wa barabara upo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu ushoroba ule kwa maana ya ukanda ule tunautazama kwa macho mawili ndio maana tumeweza kuweka fedha nyingi. Nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa msukumo mkubwa, ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto za mvua hatuwezi kuzikwepa, Mheshimiwa Mbunge atakubaliana na mimi kwamba kwenye Mto Koga, ule mto ni mkubwa sana na tunapopata mvua nyingi, miaka mingi iliyopita tumekuwa na shida hiyo na hata hivyo tulikuwa tumetoa maelekezo kwa makandarasi kwamba wanavyoanza kufanya ujenzi waanze kushughulikia sehemu ambazo zina changamoto, ni kitu ambacho kinaendelea kufanyika lakini kwa sababu ya *nature* ya mvua kuwa nyingi, tulilazimika kuifunga ile barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge mkakati mkubwa wa kuunganisha Mkoa wa Katavi na mikoa mingine unafanyika kwa Serikali ya Awamu ya Tano unafahamu kwamba ipo barabara ile ukitoka Mpanda kwenda kule Malagarasi ujenzi unaendelea na unafahamu tumeshaunganisha vizuri na Rukwa na unafahamu upo mpango wa kujenga barabara kutoka maeneo ya Stalike kwenda Kizi kule unafahamu.

Kwa hiyo, niseme katika Mkoa wa Katavi miradi mikubwa sana ipo kuhakikisha kwamba mkoa huu unaunganishwa na mikoa mingine kama ilivyofanyika kwenye mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge wakati huu wa mvua tuvumiliane na tuendeleo kumuomba Mungu atupe mvua zenye heri ili adha kubwa ambayo wananchi wanaipata tuweze kuondokana nayo, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mary Chantanda, Mheshimiwa Richard Ndassa.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza Mji wa Korogwe upo bondeni, mvua zote ambazo zinanyesha kuanzia vuli

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hadi sasa masika zimeendelea kuathiri sana miundombinu iliyopo kwenye mji ule. Na mara nyingi nikiiomba Serikali kwamba kama inawezekana ni vizuri tukatengewa fedha za kutosha ili tuweze kujenga mifereji ambayo itasaidia kupunguza kasi ya uharibifu wa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, sasa mtakuwa tayari angalau kuweza kuwa mnatutengea fedha ziweze kujenga mifereji wakati tukiendelea kusubiri barabara za lami ambazo Serikali imeendelea kutupa angalau kwa kidogo kidogo ili kupunguza hata hiyo gharama ambayo kila mwaka mnatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara za changarawe, nashukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Naibu Waziri wa Ujenzi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA): Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Chatanda kwa kufuatilia mambo ya Mji wa Korogwe. Na ninafahamu Mheshimiwa Chatanda utakubaliana na mimi, zipo barabara za lami ambazo zimejengwa pale mjini ni matokeo ya ufuatiliaji wako, kwa hiyo nakupongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kudhibiti maji ya mvua kwenye barabara zetu, tunafahamu pia kwamba maji yasipodhibitiwa ni adui mkubwa wa barabara; kwa hiyo, maji yasipodhibitiwa unakuta barabara zetu hizi zinazojengwa zinaharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge tumeshatoa maelekezo kwamba wenzetu upande wa *TARURA*, *TANROADS* lakini na wenzetu upande wa halmashauri zetu watu wa mipango miji na afya tushirikiane kuona kwamba tunakuja kuwa na mipango mizuri ya kuhakikisha kwamba maji ya mvua tunaya-control vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu muda mwingi nimekuwepo Tanga na niseme kwamba kati ya mikoa ambayo mwaka huu imeshambuliwa sana na maji ya mvua, kati ya mikoa hiyo Mkoa wa Tanga. Na tumetoa maelekezo pia kwa wenzetu upande wa *TANROADS* kwamba katika katika bajeti hii inayokuja, mikoa ambayo tunaiona imekuwa na *nature* ya uharibifu mkubwa wakati wa mvua tuitazame kwa macho mawili ikiwemo Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Chatanda uvute subira, mimi na wewe tutakuwa bega kwa bega kuhakikisha mipango inakuwa mizuri ya kuwa na ubora wa miundombinu katika Mji wa Korogwe. Lakini pia kuhakikisha kwamba angalau tunapata *allocation* nzuri kwa sababu kibajeti hali sio nzuri lakini tutahakikisha tunaweka vipaumbele kwenye maeneo ambayo tumeona yamekuwa na shida. Kwa hiyo, vuta subira, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ndassa, halafu Mheshimiwa Aisharose.

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi lilikuwa linazungumzia ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Mheshimiwa Waziri ningependa kujua sasa kwa sababu tunayo barabara yetu ya kutoka Isandula inayopita Mkalama na kwenda Ngudu mpaka Hungumalo. Ningependa kujua sasa ni lini barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami ili kuchachua maendeleo na uchumi katika Mji wa Ngudu.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara yangu imeshakamilisha usanifu wa awali na upembuzi yakinifu wa barabara hii muhimu ambayo Mheshimiwa Mbunge anaitaja. Barabara hii inapita kwenye Majimbo matatu kama alivyozungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuhakikishie Mheshimiwa Ndassa baada ya kukamilisha zoezi hili ambalo barabara hii ina urefu wa kama kilometa 60 hivi na kidogo ambayo inaanzia kule Isandula, inakuja Ngudu, Nyaminama inapita Mabuki hadi kule Hungumalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa vile tumeshamaliza zoezi la usanifu na kutambua gharama za barabara hii, tunajipanga tukipata fedha nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa eneo lako hili kwamba tutaanza ujenzi wa barabara ya lami. Tunajua inapita katika maeneo ambayo ina uchumi mkubwa, ahsante sana.

MWENYEKITI: Tunamalizia na Mheshimiwa Aisharose.

MHE. AISHAROSE N. MATEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona, mvua zinazoendelea kunyesha nchini kote zimeleta madhara makubwa Mkoani kwangu Singida na kusababisha barabara inayoanzia Mjini Singida – Ninyuhe hadi Iyumbu yenye urefu wa kilomita 115 madaraja kukatika na kusitisha shughuli zote za kiuchumi kwa wananchi wa Jimbo la Singida Magharibi. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami na kurekebisha miundombinu ya barabara hii, nakushukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu majibu ya swali hilo kwa ufupi.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara hii ambayo inapita maeneo ya Ngungila inakwenda kule Iyumbu ni barabara ambayo imepita kwenye bonde kubwa ambalo wananchi wa maeneo haya wanategemea sana uzalishaji wa mpunga. Kwa hiyo, tunafahamu kama Serikali lakini niseme hatua kubwa ambazo tumezichukua kazi iliyokuwa inaendelea ni pamoja na kujenga madaraja na makalavati katika eneo hili la Ngungila ili wananchi waweze kupita pamoja na kujaza vifusi kufanya barabara iwe juu katika eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunatambua umuhimu wa barabara hii na tumeona uharibifu uliotokea kutokana na mvua. Lakini namuomba anikubalie kwamba hatua ya kwanza ni ya kuboresha barabara hii ili wananchi waweze kupita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile hatua ya kujenga kwa barabara hii kwa kiwango cha lami itafanyika baadaye lakini Mheshimiwa Mbunge unafahamu barabara hii itaunganishwa na barabara ile ya kutoka Sabasaba inapita Sepuka – Ndago inaenda kutoka Kizaga. Kwa maana hiyo tutakuwa tumeipunguza sana barabara hii kwa kiu yako ya kujenga barabara kiwango cha lami tutaizingatia baada ya barabara hii niliyoitaja kuwa imekamilishwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana, tunamalizia sasa tunaingia Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Akina Mama Wanaojifungua Wakiwa Gerezani

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI aliuliza:-

Wapo akina mama wanaojifungua wakiwa gerezani na kuendelea kutumikia adhabu zao huku wakiwa na watoto wachanga:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwapumzisha kama miezi sita bila kufanya kazi ili wapate nguvu kwanza?

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alfredina Apolinary Kahigi, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba wapo wafungwa wanawake wanaoingia na ujauzito gerezani na kujifungua wakiwa bado wanatumikia adhabu zao. Serikali kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Jeshi la Magereza inatambua umuhimu wa kumpatia huduma stahiki pamoja na kutofanya kazi ngumu kwa mama mjamzito na aliyejifungua akiwa gerezani, ili aweze kumnyonyesha na kumhudumia mwanae inavyostahili mfano, kupelekwa kliniki, kupewa maziwa kwa ajili ya mwanae, chakula cha ziada na kutengwa na wenzie kwa kipindi kisichopungua miezi mitatu ili aweze kujihudumia vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma za wafungwa hawa zimeainishwa vizuri katika Kanuni za Kudumu za Uendeshaji wa Jeshi la Magereza kifungu Na. 728 - 729 Toleo Na. 4 la mwaka 2003.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Alfredina Kahigi, swali la nyongeza.

MHE. ALFREDINA A. KAHIGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi kwa mara nyingine tena. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri kama yanatekelezwa lakini nina maswali yangu mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikibainika mwanamke aliyefungwa gerezani akachukua mimba, je, ni hatua gani za kisheria atakazochukuliwa? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; iwapo mwanamke huyo aliyefungwa amehukumiwa kufungwa miaka 10 na zaidi, je, yule mtoto ambaye amejifungulia humo gerezani atakaa nae mpaka kifungo chake kiishe? Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Kahigi kwa maswali mafupi ya Kibunge, Mheshimiwa Naibu Waziri karibu kwa majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ameuliza ikibainika atachukua mimba lakini moja kwa moja nilivyomuelewa ni kwamba anakusudia atachukulia mimba nje ya gereza kwa sababu hakuna uwezekano wa kuchukua mimba akiwa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

gerezani. Na kama akiwa amechukua mimba akiwa nje ya gereza utaratibu ndio kama ambavyo nimezungumza katika jibu langu la msingi kwamba atajifungua, atakapokuwa amejifungua atapewa utaratibu maalum kwa mujibu wa sheria ambayo nimeinukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swala ni kwamba je, akishakujifungua ambalo ni swali lake la pili. Akishajifungua na amefungwa muda mrefu, nini hatma ya yule mtoto? Jibu ni kwamba mtoto yule atakapofikia umri wa kumaliza kunyonya, maafisa Ustawi wa Jamii wanakwenda katika magereza kwa ajili ya kuzungumza na yule mama ili mtoto yule aweze kupata fursa ya kupata malezi nje ya gereza aidha kwa jamaa zake ama kwa watu au taasisi zozote ambazo zimekuwa zikihudumia watoto ikiwa hana jamaa. Huo ndio utaratibu wa kawaida ambao tupo nao kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi ambacho wapo magerezani watoto wale wanahudumiwa vizuri kwa kadri ambavyo sheria inazungumza ikiwemo hata kuweza kuwapatia huduma ya elimu za awali katika shule zilizopo karibu na magereza.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

MHE. ASHA ABDULLAH JUMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kwa kuwa hali ya maumbile ya mwanadamu, hasa mwanamke yanapelekea kujifungua au kupata watoto: Je, Serikali inachukua hatua gani kudhibiti utungwaji mimba ndani ya Magereza ili kupunguza shida ambazo watoto hao watapata katika kulelewa katika mazingira ambayo siyo rafiki kama Magereza; kwa kuwa bado inasemekana kwamba kuna mchanganyiko wa wanawake na wanaume na wanapata access ya kukutana? Sasa Mheshimiwa Waziri atuambie atadhibiti vipi utungwaji mimba?

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Asha Abdullah Juma. Mheshimiwa Naibu Waziri swali hilo linakuja kwa namna yake nyingine tena.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza wakati najibu swali la msingi kuhusiana na uwezekano wa mwanamke kupata mimba ndani ya Magereza. Nimezungumza hivyo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba Magereza yametenganishwa, hakuna mchanganyiko kati ya Magereza upande wa wanawake na wanaume; hata Askari ambao wanahudumia wafungwa na mahabusu wa kike basi wanakuwa ni Askari wa kike. Kwa hiyo, mara nyingi tunapozungumzia upataji mimba wa Magereza inakuwa ni kwa wafungwa ama mahabusu ambao wameingia tayari Magerezani ikiwa mimba zimeshaanza kutungwa.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Kama hilo linafanyika, basi tunashukuru sana na tunaamini hayo mambo yatakuwa hayapatikani tena huko Magerezani.

Tunaendelea na Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 35

Mkakati wa Kupunguza Mahabusu Nchini

MHE. SABREENA H. SUNGURA aliuliza:-

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Je, Serikali ina mkakati gani wa kupunguza mahabusu katika Magereza na Vituo vya Polisi nchini?

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiki kirefu Serikali kupitia vyombo vyake vya haki jinai nchini imekuwa ikifanya juhudi mahususi kupunguza idadi ya mahabusu katika Magereza yote hapa nchini. Kupitia mikakati mbalimbali idadi ya mahabusu imekuwa ikipungua mara kwa mara na bado juhudi zinaendelea za kuhakikisha Magereza yetu yanahifadhi wahalifu kulingana na uwezo wake kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya mikakati inayotumika kutatua tatizo la mahabusu Magerezani ni pamoja na Vikao vya Kamati za Kusukuma Kesi (*Case Flow Management Committee*), Idara ya Mahakama kuisitiza matumizi ya Sheria ya Dhamana kwa makosa yanayodhaminika, uundwaji wa kikosi kazi cha haki jinai kupitia makosa mbalimbali (*Criminal Justice System Task Force*) pamoja na mikakati mingine inayotokana na Idara ya Mahakama.

MWENYEKITI: Mheshimiwa James Mbatia.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: He!

MBUNGE FULANI: Mwenye swali hajauliza.

MWENYEKITI: Mwenye swali kwanza.

MHE. SABREENA H. SUNGURA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Moja, kwa kuwa wananchi wengi sana wa Tanzania ambao wamekuwa wakipelekwa mahabusu, *whether* wana kesi za kujibu ama hawana, ama ni kesi zinazopata udhamini, wamekuwa wakiingia mahabusu bure, lakini kutoka ni hela; napenda kuuliza: Je, Serikali imewahi kufanya utafiti kwamba suala hili linatokea na ni hatua gani wanachukua? Kwa sababu siyo suala la kisheria kwamba mtu akiingia mahabusu kutoka lazima atoe hela ndiyo atolewe. Ni suala la *practice*, sisi tuliopo mitaani tunajua kwamba mtu anapelekwa mahabusu lakini siku ya kutoka wengi wao wanakuwa wanachajwa. Je, Serikali inachukua hatua gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa kumekuna wimbi kubwa la kesi, hususan za uhujumu uchumi na utakatishaji fedha kwa vijana hasa vijana hawa kama akina Tito, Kabendera na wengine wengi ambao hatuwajui, wamekuwa wakikaa mahabusu kwa muda mrefu na kesi zao zikiendelea huko; inawezekana siku ya siku wakaja kukutwa na hatia ama wasikutwe na hatia; lakini kwa kuwa tulipitisha sheria hapa Bungeni ya *pre-bargaining* ambayo inamtaka mshtakiwa ama wakili wake ama mwendesha mashtaka kuomba mahakamani waweze kupata ili kupunguza ukubwa wa adhabu, kupunguza muda wa adhabu lakini kuondoa baadhi ya kesi; pia Mheshimiwa Rais kupitia maombi maalum ya barua alikuwa akiwahi kutoa msamaha; sasa Bunge halioni ni wakati muafaka sasa tuje tufanye mabadiliko ya Sheria ya Uhujumu Uchumi ili kuweka *flexibility* kwa Majaji na Mahakimu ambao wamekuwa wakiendesha kesi hizi na wenyewe waweze kuangalia ukubwa wa kosa na kuweza kutoa dhamana? (*Makofi*)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu Bunge tumetunga sheria, tumewafunga mikono kwamba hawawezi kutoa dhamana kwa makosa ya uhujumu uchumi. Hata hivyo, mtu anaweza akahujumu uchumi ama kufanya utakatishaji fedha kwa 20,000/=, mwingine shilingi bilioni moja, wote wananyimwa dhamana kitu ambacho kinasababisha mlundikano wa kesi.

Je, Bunge sasa halioni ni wakati muafaka wa kuleta mabadiliko ya sheria hii ili vijana ambao hawana hatia na wanateseka huko Magerezani waweze kupunguza idadi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo mawili.

NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza anazungumzia kwamba kuna kauli ambayo inatapakaa katika jamii kwamba unaingia mahabusu bure na unatoka kwa pesa. Siwezi nikapingana na kauli hii kwa sababu mbali ya kazi kubwa na nzuri ambayo Askari wetu wamekuwa wakiifanya ya kusimamia usalama wa nchi hii na ndiyo maana nchi yetu iko salama, lakini tunakiri kwamba wako baadhi ya Askari ambao wamekuwa wakikiuka maadili na ndio hao ambao pengine wanatuhumiwa na mambo kama ambayo amezungumza Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba pale ambapo tunabaini Askari yeyote anayekiuka maadili yake kwa kufanya utaratibu kama ambao ameuzeleza wa kuwatoza mahabusu fedha ama kuwabambikia ama kuwaonea, tumekuwa tukichukua hatua. Wapo Askari kadhaa ambao wamechukuliwa hatua mbalimbali kila mwaka ingawa ni wachache mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la mabadiliko ya sheria, nadhani ni mamlaka ya Bunge hili kutunga sheria na kubadilisha pale ambapo inaona inafaa. Naye ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kanuni anazifahamu. Kama kuna utaratibu ambao Mheshimiwa Mbunge anadhani kuna haja ya kuleta hoja binafsi ama utaratibu mwingine ambao ataona unafaa, basi ni juu ya Mbunge yeyote kutumia haki yake ya Kikatiba na kikanuni.

MWENYEKITI: Mheshimiwa James Mbatia.

MHE. JAMES F. MBATIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Suala hili la hadhi ya mahabusu wetu ni suala nyeti na pana; na kwa kuwa sisi wote humu ndani tunayo nafasi ya kufanya marekebisho katika sheria hizi ili haki ya aina yoyote ya mahabusu iweze ikatendeka; na tumemsikia Jaji Mkuu akisema kwamba pamoja na kuwepo kwa wingi wa mahabusu ni kutokana na kutokufanyika kwa upelelezi na kuukamilisha ndiyo mtu aweze kupeleleka Mahakamani:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuiuliza Serikali, au Serikali kama imesikia kilio cha Jaji Mkuu na ushauri wao, nasi ni Wabunge na tukitegemea tunayo nafasi ya kuweza kufanya mabadiliko ya sheria hizi sasa, maana huwezi kujua kesho, wote hapa ni wafungwa watarajiwa; iwe kwamba, kama ni miezi mitatu upelelezi haujakamilika, basi mfungwa au mahabusu aachiwe au vinginevyo kwa busara itakavyoelekeza sheria hii sasa ifanyiwe marekebisho mahabusu waweze kupata haja na haki zao za kimsingi.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Simbachawene majibu ya swali hilo. *(Makofi)*

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi wa rehema kubwa na ndogo anazotujalia sote hata kufika siku hii ya leo. Vile vile nimshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbatia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hadi sasa jitihada hizi zinazofanyika kwa njia hizi tatu ambazo Mheshimiwa Naibu Waziri amejibu kwenye jibu la msingi ni maelekezo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alipotembelea Magereza likiwepo Gereza la Butimba na akatoa maelekezo kwamba hali ilivyo, Magereza yamezidiwa na mahabusu ndio wengi zaidi na ndiyo maana hatua zinaendelea kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, DPP amekuwa akifanya jitihada za kutembelea Magereza na kuongea na wafungwa. Pia nasi kama Wizara tumekuwa tukifanya hivyo na ninaamini kabisa kila baada ya muda tutakuwa tunapunguza baadhi ya mahabusu ambao wana kesi ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua kubwa zinafanyika, nami nadhani iko haja ya jitihada hizi zinazofanyika tukawa tunaleta taarifa hapa kwenye Kamati au kwa njia yoyote ambayo mtaona inafaa kwa sababu ni kweli jitihada zinafanyika. Isipokuwa mchakato wake kama mnavyofahamu, zipo haki za wafungwa, zipo haki za mahabusu na zipo pia haki za waliotendewa makosa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, usilichukulie jambo hili kama ni jepesi. Lazima lichujwe, liangaliwe na upo utaratibu wa kisheria wa kufanya mambo haya. Kwa hiyo, pia tusikimbilie kushabikia tu haki za hawa waliotenda makosa. Ni kweli wanazo, lakini zipo haki pia za waliotendewa makosa. Kwa hiyo jambo hili linahitaji tuli-balance vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa jibu hilo watakubaliana nami kwamba jitihada hizi kwa kweli ni kubwa na zimetokana na maagizo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kwa maelezo au majibu hayo ya ziada. Tunamalizia Wizara yetu ya mwisho, Wizara ya Maji. Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Tabora Kaskazini, sasa aulize swali lake.

Na. 36

Mradi wa Maji Kutoka Ziwa Victoria

MHE. ALMAS A. MAIGE aliuliza:-

Serikali inatekeleza mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria na kuyapeleka Mkoa wa Tabora katika Miji ya Igunga, Nzega, Manispaa ya Tabora, Sikonge, Isikizya na Urambo:-

(a) Je, ni vijiji gani vya Mashariki vya Jimbo la Tabora Kaskazini – Uyui vitapatiwa maji kutokana na mradi huo?

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(b) Kwa vile ni idadi ndogo tu ya vijiji kati ya 82 vya Jimbo la Tabora Kaskazini ndiyo vitapatiwa maji na mradi huo: Je, Serikali ina mpango gani wa kuvipata maji vijiji vyote katika Jimbo la Tabora Kaskazini?

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Almas Athuman Maige, Mbunge wa Jimbo la Tabora Kaskazini lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatekeleza mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenye Miji ya Tabora, Igunga na Nzega pamoja na vijiji zaidi ya 102 vilivyopo umbali wa kilomita 12 kila upande kutoka bomba kuu. Vijiji vilivyopo Jimbo la Tabora Kaskazini katika mradi huu ni 26 ambavyo ni Igoko, Isikizya, Ikonolo, Mswa, Itobola, Isenegenzya, Majengo, Ikongolo, Kanyenye, Kiwembe na Kalemela,

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imeanza kutekeleza miradi katika miji 28 kupitia mkopo wa Dola za Marekani milioni 500 kutoka Benki ya *Exim* ya India. Mradi huo utapeleka maji katika Miji ya Sikonge, Urambo, Kaliua na baadhi ya maeneo ya Wilaya ya Uyuji kwa kutoa maji Ziwa Victoria. Mpaka sasa vijiji vilivyotambuliwa wakati wa usanifu wa kupeleka maji Sikonge, Urambo na Kaliua ni 14 ambavyo ni Kasisi B, Ilalongulu, Mpenge, Isenga, Ngokolo, Ulimakafu, Mabama, Tumaini, Maswanyaa, Chali Ndonoo, Itinka, Tulieni na Utemini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kwa miradi yote miwili itahudumia jumla ya vijiji 40 vya Jimbo la Tabora Kaskazini. Serikali itaendelea kutenga na kutoa fedha ili kuhakikisha vijiji vyote vilivyobaki vinapata huduma ya maji.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

MHE. ALMAS A. MAIGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuuliza maswali yangu mawili ya nyongeza, naomba nitoe kwa dhati kabisa shukrani kubwa kwa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa miradi mingi aliyoweka katika Jimbo langu. Naomba niitaje hapa kwa niaba ya Bunge ili lielewe miradi gani ipo Jimboni kwangu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria ambao ni sehemu ya shilingi bilioni 600; Kituo cha Afya cha Upuge, shilingi milioni 850; Hospitali ya ngazi ya Wilaya Isikizye shilingi bilioni mbili; Kituo cha VETA kinachojengwa Isikizye, sasa ni shilingi bilioni tano; Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Magharibi mabilioni na umeme wa REA wa vijiji 18 mabilioni ya shilingi. Naomba salamu hizi na pongezi zimfikie Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Je Serikali ina mpango gani kupeleka maji vile vijiji 42 vilivyobakia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili: Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka wataalam wa maji ili kuchunguza vyanzo vya maji katika vijiji vya Kata za Ufuluma, Shitage, Nsimbo, Bukumbi, Makazi na Igulungu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri aliyekuja kufuatilia mradi huko kwetu, nasi tumemwekea binti aende akaoe. Karibu sana Mheshimiwa Aweso. *(Kicheko)*

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya maswali hayo.

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, lakini nashukuru kwa zawadi aliyonipa. Nataka nimhakikishie mimi beberu, siyo jogoo la pasaka bwana, nipo tayari. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kama Serikali ambacho nataka kusema ni kwamba tumejipanga vizuri katika kuhakikisha tunaondoa kabisa tatizo la maji katika Mkoa wa Tabora. Tuna mradi mkubwa zaidi ya shilingi bilioni 600. Pamoja na hayo, kutokana na mapenzi makubwa na mahaba ya Mkoa wa Tabora, tumeshapeleka shilingi 8,345,000,000/= katika kuhakikisha tunaendelea kutatua tatizo la maji na fedha hizi tutatekeleza kwa kutumia wataalam wetu wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Wizara ya Maji tupo tayari kupeleka wataalam kufanya usanifu kwa vijiji ambavyo havijapata maji ili viendelee kupata huduma hii muhimu sana ya maji. Ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha. Kwa hiyo, huu ni muda wa matangazo. Naomba nianze kuwatangaza wageni waliopo Bungeni asubuhi hii. Kwanza wageni waliopo Jukwaa la Mheshimiwa Spika. Tuna wageni 25 wa Mheshimiwa Spika ambao ni Kwaya ya Nuru kutoka Kanisa la KKKT Mlima Kola Dayosisi ya Morogoro wakiongozwa na Afande Mwashibanda Shibanda. Karibuni sana wanakwaya wetu kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika, karibuni katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Naibu Spika ambao ni wasanii kutoka Jiji la Dar es Salaam; Ndugu Judith Wambura *(Lady Jay Dee)*, Ndugu Martin Kadinda na Ndugu Deogratius Samanis. Karibuni sana wageni wetu ambao mpo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge. Tuna wageni 10 wa Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge, Kiongozi wa Upinzani Bungeni ambao ni kutoka Taasisi ya TWARIKA, Tanzania wakiongozwa na Msemaji Mkuu wa Taasisi hiyo, Sheikh Haruna Lotha. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Freeman Mbowe katika Bunge letu. *(Makofi)*

Mwingine ni wa Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mbunge na Waziri wa Fedha na Mipango, ambaye ni Katibu Mkuu wa Taasisi ya *The Islamic Foundation*, Ndugu Musa Buluki. Karibu sana Katibu Mkuu ambaye pia ni kaka yetu huyo, kaka yake au ni mdogo wake Mheshimiwa Dkt. Ashatu. Basi karibu sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Subara Mgalu, Mbunge na Naibu Waziri wa Nishati ambao ni Katibu wa CWT Mkoa wa Mtwara, Ndugu Susan Shasha na Ndugu Dhahabu Christopher. Karibuni wageni wetu. Sijawaona hapo jukwaani.

Tuna wageni tisa wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, Mbunge, ambao ni wapiga kura wake kutoka Hanang wakiongozwa na Mheshimiwa Diwani Matata Bongo. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu katika Bunge letu.

Pia tuna wageni watatu wa Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mbunge, ambao ni viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mwanga wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Mheshimiwa Theresia Msuya ambaye ameongozana na Diwani wa Kata ya

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Kigonigoni, Mheshimiwa Jeremiah Shayo na Afisa Elimu wa Wilaya Ndugu Mariana Mgonja. Karibuni sana wageni wa Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe. *(Makofi)*

Pia tuna mgeni wa Mheshimiwa Ritta Kabati, ambaye ni dereva mwanamke wa mitambo ya Jiji la Dodoma, Ndugu Esther Nyinge. Karibu sana dereva wetu mwanamke wa mitambo ya Jiji la Dodoma. *(Makofi)*

Wengine ni wageni nane wa Mheshimiwa Stanslaus Mabula ambao ni wafanyakazi kutoka *Wasafi Media* Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Hellen Kazimoto lakini pia na Zembwela Chumvi, mtangazaji wa *Wasafi TV*, ambaye pia huyu ni kaka yake Mheshimiwa Awezo. Karibuni sana watangazaji wetu kutoka *Wasafi Media* Jijini Dar es Salaam katika Bunge letu.

Kuna wageni wengine waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo kuna mgeni kutoka Jijini Dodoma ambaye amekuja kutembelea Bunge kujifunza jinsi inavyofanya kazi, ndugu Ramadhani Omar, karibu sana kwa mafunzo katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tuna wanafunzi 200 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Mkufunzi wao Dkt. Mnata Resani, karibuni sana wanafunzi wa kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma kwa ajili ya mafunzo katika Bunge letu, naamini mmepata vizuri na mnaendelea kujifunza. *(Makofi)*

Pia tuna wanafunzi 100 na Walimu sita kutoka Shule ya Msingi St.Monica ya Jijini Arusha, karibuni sana wanafunzi wetu, mmependeza sana na sare zenu hizo, karibuni sana katika Bunge letu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge pia kuna tangazo hapa la uzinduzi wa mpango mkakati wa kikundi cha Wabunge Vinara wa Lishe leo tarehe 30 Januari 2020/ Wajumbe wote wa kikundi cha Wabunge Vinara wa Lishe wanatangaziwa kwamba kutakuwa na hafla ya uzinduzi wa mpango mkakati wa kikundi cha Wabunge Vinara wa Lishe leo tarehe 30 Januari 2020 katika ukumbi wa Msekwa kuanzia saa saba, mara baada ya kuahirishwa kwa kikao cha Bunge, Wajumbe wote mnaombwa mhudurie katika kikao hicho, Katibu tuendeleo.

Katibu!

NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA KAMATI

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI HIYO KATIKA KIPINDI CHA MWEZI FEBRUARI, 2019 HADI JANUARI, 2020

NA

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA KUHUSU SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI HIYO KATIKA KIPINDI CHA MWEZI FEBRUARI, 2019 HADI JANUARI, 2020

MWENYEKITI: Haya tunaanza na hoja za Kamati, tunamkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti ili aweze kuwasilisha taarifa ya Kamati, karibu Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. MASHIMBA M. NDAKI - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya mwaka kuhusu utekelezaji wa shughuli za Kamati ya Bajeti katika kipindi cha mwezi Januari, 2019 hadi mwezi Januari, 2020. Kwa vile taarifa hii ni ndefu kidogo nitaomba kwamba iingizwe katika kumbukumbu zako za Bunge yote kwa ujumla wake kwa sababu kuna sehemu ambazo sitazisoma hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii pia inatoa tathimini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu mwaka kuanzia Julai hadi Desemba, 2019 na mwelekeo hadi Juni, 2020. Kamati ya Bajeti ilitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti, Sura ya 439 ya mwaka 2015, Kanuni za Bunge, Toleo la 2016 fasili ya 9 ya Nyongeza ya Nane, Sheria ya Fedha na Sheria nyingine, taratibu na miongozo mbalimbali iliyopo inahusiana na masuala ya fedha, uchumi, kodi na bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza shughuli hizo Kamati ilikutana na Serikali, Taasisi, Mashirika na Sekta Binafsi pamoja na wadau mbalimbali ili kuwasikiliza pamoja na kupokea taarifa na maoni mbalimbali ambayo Kamati ilitumia wakati ikitekeleza majukumu yake na hatimaye kutoa maoni na ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu 13. Sasa nitaanza utekelezaji wa shughuli za Kamati. Zifuatazo ni kazi zilizotekelezwa na Kamati ya Bajeti katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari, 2019 hadi mwezi Januari, 2020.

- (1) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2018/2019;
- (2) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2018/2019;
- (3) Kutathimini na kuchambua makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2019/2020 yatokanayo na vyanzo vya kodi na vyanzo vingine visivy vya kodi;
- (4) Kupitia na kujadili kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha mwaka 2020/2021;
- (5) Kupitia na kujadili utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/20;
- (6) Kuchambua na kushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2019 (*The Finance Act*) 2019.
- (7) Kujadili na kuidhinisha Bajeti ya Mifuko ya Mahakama, Bunge na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi;
- (8) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2019/2020;
- (9) Kupitia na kujadili kuhusu Mwongozo wa kutayarisha mpango wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021;
- (10) Kujadili na kuidhinisha bajeti ya Wizara wa Fedha na Mipango pamoja na Mafungu yaliyo chini yake;

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(11) Kushiriki mafunzo mbalimbali yenye lengo la kuwaongezea Wajumbe wa Kamati uwezo wa kutekeleza majukumu yao;

(12) Kukutana na wadau mbalimbali wa masuala ya kodi na kujadili changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sheria mbalimbali za kodi na zisizo za kikodi zinazoathiri Sekta Binafsi;

(13) Kufanya utafiti na uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato na kutoa mapendekezo kuhusu hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti;

(14) Kutoa ushauri wa ujumla kuhusu bajeti ya Serikali kwa Bunge na Kamati za Kudumu za Bunge;

(15) Kuchambua hoja zilizojitokeza kwenye Kamati za Bunge za kisekta wakati wa kujadili bajeti za Wizara kwa mwaka 2017/2018 kwa ajili ya kuishauri Serikali;

(16) Kuchambua taarifa za utekelezaji na utendaji kutoka kwenye Wizara inayosimamiwa na Kamati pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo;

(17) Kuchambua taarifa ya utendaji kazi ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2018/2019;

(18) Kufanya ziara nchini Uganda na Rwanda ili kujifunza kuhusu mfumo wa *account jumufu (TSA)*; na

(19) Kufanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo na Taasisi ninazozisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatoa shukrani kwanza kwa Mheshimiwa Spika, pia Kwa Mheshimiwa Naibu Spika, kwako pia Mwenyekiti, pili kwa Serikali na wadau wote kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Kamati kukamilisha shughuli zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie tathimini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa 2018/2019. Tathimini ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali inakwenda sambamba na kuangalia mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi jumla, kwa muhtasari mwenendo wa viashiria hivyo vya ukuaji wa uchumi vimethaminiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza pato la Taifa; takwimu za Serikali zinaonyesha uchumi wa Taifa ulikuwa kwa asilimia 6.8 katika mwaka wa 2018. Sekta zilizochangia kwa kiasi kikubwa kwa ukuaji huo ni sanaa na burudani asilimia 13.7, ujenzi asilimia 12.9, Uchukuzi na Uhifadhi wa mizigo asilimia 11.8, pamoja na Habari na Mawasiliano asilimia 9.1. Sekta ya Kilimo pamoja na kuwa na mchango mkubwa wa takribani asilimia 27 kwenye pato la Taifa ukuaji wake ulikuwa ni asilimia 4.3. Hivyo bado kuna haja ya Serikali kuondoa vikwazo vinavyosababisha Sekta ya Kilimo kutokua kwa kasi pamoja na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili Sekta Binafsi iwe na mchango mkubwa katika ukuaji wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, mfumuko wa bei; Kamati inaipongeza Serikali kwa kupunguza mfumuko wa bei kutoka asilimia 5.3 mwaka 2017 hadi asilimia 3.5 mwaka 2018. Kiwango hicho kimefikiwa kutokana na upatikanaji wa chakula cha kutosha nchini, hivyo ni wazi kwamba wakulima wa nchi ndiyo kwa kiasi kikubwa wamesaidia katika kupunguza mfumuko wa bei. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuhakikisha (*NFRA*) inakuwa na mtaji wa kutosha na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

inatekeleza jukumu lake la msingi la kuhifadhi chakula ili kulinda mfumuko wa bei. Kuna jedwali hapo tumelionesha Waheshimiwa Wabunge wanaweza wakaona, niende kipengele kingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa thamani ya shilingi; takwimu zinaonesha kuwa kwa kipindi cha Julai hadi Novemba, 2018 dola ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa Sh.2,276, ikilinganishwa na Sh.2,235 katika kipindi cha Julai hadi Novemba, 2017. Hii inaonesha shilingi ilipungua thamani dhidi ya dola kwa asilimia 1.8. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza sera zenye mlengo wa kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje na hasa viwanda vinavyozalisha bidhaa ambazo zinaagizwa nje kwa wingi. Sera hizo zitasaidia kupunguza nakisi ya urari wa biashara na hivyo kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni na hivyo kuongeza thamani ya shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la Taifa; deni la Serikali liliongezeka kutoka shilingi bilioni 49728.03 Machi, 2017 hadi kufikia shilingi bilioni 50,772.27 mwaka 2018, sawa na ongezeko la asilimia 2.1, kiasi kikubwa cha deni la Serikali linamilikiwa na wakopeshaji kutoka nje. Kamati inatambua kuwa ongezeko la deni linatokana na mahitaji ya kugharamia miradi ya maendeleo. Hata hivyo ni vema Serikali ikahakikisha inazingatia matakwa ya Sheria ya Mikopo, Misaada na dhamana ya Serikali, Sura ya 165 na vigezo vya Kimataifa ili kuhakikisha deni linaendelea kuwa himilivu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kipengele kingine utekeleza wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2018/2019 na mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2019/2020. Kwa mujibu wa kanuni ya 94 Bunge lilijadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2019/2020 uliowasilishwa Bungeni na Waziri wa Fedha na Mpango. Kamati ilipata fursa ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa mwaka 2018/2019, kuchambua na baadaye kutoa maoni na mapendekezo kuhusu mpango wa mwaka 2019/2020 kupitia taarifa ya Kamati iliyowasilisha Bungeni. Bunge lilitoa maoni na mapendekezo na hatimaye Mpango huo uliidhinishwa. Baadhi ya masuala yaliyobainishwa katika tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2018/2019 yako kwenye taarifa yetu na Waheshimiwa Wabunge wanawaweza wakayaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini ya Kamati kwamba Serikali itazingatia ushauri uliotolewa na Kamati ili mapendekezo yaliyobainishwa yatekelezwe katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kipengele kingine Muswada wa Sheria ya fedha wa mwaka 2019 yaani (*The Finance Bill 2019*). Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, Kamati iliwasilisha Bungeni taarifa yake ya maoni na ushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya fedha wa mwaka 2019 na hatimaye Bunge lako Tukufu liliidhinisha Muswada huu kuwa Sheria ambayo ilianza kutumika tarehe Mosi Julai, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia na kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2019 shughuli hii ilifanyika kwa kupitia kifungu kwa kifungu pamoja na kupokea maoni kutoka kwa wadau. Baada ya kujiridhisha na maudhui yake Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Serikali na kupendekeza marekebisho pale ilipobidi. Sheria zilizofanyiwa marekebisho katika Muswada huo ni Sheria (10) kama ambavyo tumeziorodhesha hapo, utekelezaji wa Sheria hizi umefafanuliwa kwa kina kwenye uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 kwa kipindi cha nusu mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo wa kutayarisha mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021. Mwezi Novemba, 2019 Serikali iliwasilisha Bungeni Mpango wa Maendeleo wa Taifa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

pamoja na Mwongozo wa maandalizi ya mpango wa bajeti kwa mwaka 2020/2021 kama Sheria ya Bajeti inavyoelekeza. Kamati ya Bajeti ilipitia na kujadiliana na Serikali kuhusu Mwongozo wa maandalizi ya mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021 pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Taifa. Kimsingi Mwongozo huu umeendelea, umeelekeza masuala ya msingi ya kuzingatiwa katika uandaaji wa Mpango na Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sura ya Bajeti kwa mwaka 2020/2021 inaonesha kuwa Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya shilingi trilioni 34.36 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 3.78 ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka 2019 ambayo ilikuwa na trilioni 33.12, mapato ya ndani yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 23.46 ikiwa ni sawa na asilimia 68.3 ya Bajeti. Kati ya fedha hizo mapato ya kodi ni shilingi trilioni 19.76, mapato yasiyo ya kodi ni shilingi trilioni 2.89 na mapato ya halmashauri shilingi bilioni 803.76. Aidha, Serikali inatarajia kupata kiasi cha shilingi trilioni 5.212 zikiwa ni misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na kuziba nakisi ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja Mwongozo wa kutayarisha Mpango wa Bajeti ya Serikali mwaka 2020/2021. Pamoja na mapitio hayo Kamati iliishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu mpango huo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza, lilikuwa ni ukusanyaji wa mapato kwa mfumo wa GEPG. Kamati iliishauri Serikali ihakikishe kila halmashauri zinakusanya mapato yake kwa njia ya mfumo wa Serikali wa kielekitroniki wa ukusanyaji wa mapato yaani GEPG. Hatua hii ni muhimu ili kuhakikisha kwamba uwiano wa ukusanyaji wa mapato ufikie walau asilimia 18 ya pato la Taifa kwa lengo la kuziba nakisi ya Bajeti na kutekeleza miradi ya maendeleo yenye tija kwa Taifa. Kwa sasa uwiano wa ukusanyaji wa mapato ya asilimia 11.5 ya pato la Taifa. Aidha, nguvu kubwa ielekezwe katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kupitia vyanzo vipya vya kodi na visivyo vya kikodi pamoja na kuimarisha ushirikiano wa Kijumuiya na wa Kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha pili, ni taarifa ya utekelezaji na vipaumbele; Kamati ilipendekeza pia Mpango wa Maendeleo uainishe hatua za utekelezaji wa vipaumbele kama vilivyoainisha kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano ikizingatiwa kuwa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2020/2021 ni mpango wa mwisho kwa mpango wetu ule wa miaka mitano. Hali hii itatoa taswira ya mwelekeo na ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hivyo kusaidia kufanya tathmini bora ya utekelezaji kwa kipindi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo; mafanikio ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2020/2021, yanategemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa rasilimali fedha. Kamati iliishauri Serikali kuainisha namna ambavyo itavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, kushiriki katika utekelezaji wa mpango pamoja na kuhamasisha Sekta Binafsi, kushirikiana na Sekta ya Umma katika kugharamia na kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kufungua soko la mitaji, Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kufungua zaidi soko la mitaji ili kwanza kuvutia mitaji kutoka nje na kupunguza athari za Serikali kukopa katika soko dogo la fedha la ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na utekelezaji wa mwongozo wa ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo; Kamati iliishauri Serikali kuendelea kutekeleza mwongozo wa ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo (*Development Cooperation Framework-DCF*) ili kukuza mahusiano ya kimaendeleo na hivyo kusaidia

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

upatikanaji wa fedha kutoka kwa wahisani wa kibajeti. Hatua za awali za utekelezaji wa mwongozo huo zimeonesha mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hoja za Kamati za Bunge za Kisekta; katika Bunge la Bejeti la Mwaka 2019, Kamati ilipokea jumla ya hoja 26 zilizowasilishwa mbele yake. Kati ya hoja hizo, hoja 18 zilihusu bakaa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mafungu mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2018/2019, hoja 9 zilihusu nyongeza ya fedha kwa ajili ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu mbalimbali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 na hoja 3 zilihusu mapendekezo kuhusu Sera, Sheria na mabadiliko ya kikodi na hivyo hazikuwa na athari ya Kibajeti moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti ilikamilisha jukumu hili kwa kukutana na Kamati ya Uongozi pamoja na Serikali kwa lengo la kufanya mashauriano kuhusu hoja husika. Katika kikao hicho, Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu hoja husika na matokeo ya mashauriano hayo yaliwasilishwa Bungeni kupitia Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hoja zilizofanyiwa Kazi na Serikali zilikuwa tatu zilizofanyiwa kazi na hoja ambazo Serikali iliahidi kuzifanyia kazi zilikuwa mbili. Ni mategemeo ya Kamati kuwa Serikali imeendelea kuzifanyiakazi hoja hizo kama ambavyo iliahidi katika vikao vyake pamoja na Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tuangalie utekelezaji wa Sheria ya fedha ya Mwaka 2019 kwa kipindi cha nusu Mwaka 2019/2020; katika mwaka wa fedha 2019/2020 Bunge lilifanya marekebisho katika Sheria mbalimbali zilizokuwa na lengo la kuongeza mapato ya Serikali, kupanua wigo wa mapato, kuimarisha usimamizi wa mapato na matumizi pamoja na kuchochea ukuaji wa viwanda Nchini. Marekebisho hayo yalitarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 453,754.3. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019 makusanyo halisi kutokana na hatua hizo yalifikia shilingi milioni 167,961 ikiwa ni ufanisi wa asilimia 40.9 ya lengo la kukusanya shilingi milioni 410,377.2 kwa kipindi hicho. Ufanisi mdogo umesababishwa na kukosekana kwa mapato yaliyotarajiwa hasa kutokana na kutekeleza *tax amnesty* ambayo Kamati na Bunge lako walipitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipitia, ilichambua na kujadili taarifa ya utekelezaji wa Sheria ya fedha ya Mwaka 2019 katika kipindi cha nusu mwaka 2019/2020. Katika uchambuzi wa utekelezaji wa sheria hizi Kamati imebaini masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148 (*The Value Added Tax Cap. 148*); marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani yalilenga kusamehe kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye makasha yenye majokofu yanayotumika kwenye Kilimo cha Kisasa cha mboga mboga, vifaa vya kukaushia nafaka, vilainishi vya ndege, tiketi za ndege, vipeperushi, kalenda, shajara, karatasi zenye nembo na sare za wafanyakazi zilizowekwa nembo ya Shirika husika la ndege. Lengo lilikuwa ni kupunguza gharama za uzalishaji na kuboresha kilimo cha kisasa nchini pamoja na kuiwezesha nchi kuingia mikataba mbalimbali za huduma za usafiri wa anga (*Bilateral Air Service Agreements*). Vilevile, Serikali ilifuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani uliokuwa unatolewa kwenye taulo za kike kwa kuwa haukuwezesha kupatikana kwa bidhaa hiyo muhimu kwa bei nafuu kwa walengwa na badala yake unawanufaisha wafanyabiashara badala ya walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2019, Misamaha ya kodi ya Ongezeko la Thamani iliyotolewa kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 ilikuwa shilingi milioni 754.2 ikiwa ni sawa na asilimia 91.6 ya lengo la nusu mwaka na asilimia 45.8 ya lengo la

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mwaka la kukusanya shilingi milioni 1,646.7. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuchukua hatua sanjari ambazo zinaonekana kero kwa wananchi katika sekta ya kilimo ili kuikwamua sekta hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147; marekebisho yaliyofanyika kwenye sheria ya ushuru wa bidhaa yalilenga kutoza asilimia 10 kwenye bidhaa mbalimbali kama mabomba, vifaa vya plastiki vya ujenzi, nywele za bandia pamoja na kupunguza Ushuru wa Bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa kutokana na usindikaji wa matunda yanayozalishwa hapa Nchini kwa kiwango kinachozidi asilimia 75. Marekebisho hayo yalitarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 3,987.5 lakini marekebisho haya yalipunguza mapato kwa shilingi milioni 1,004.3, ikiwa ni ufanisi wa asilimia hasi 25.2. Kwa kuwa hatua hii ilikuwa na nia njema ya kulinda viwanda vya ndani lengo linaweza kuwa limefikwa lakini si kwa upande wa mapato yaliyokuwa yanatarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332; marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 yalilenga kuanzisha mfumo mpya wa kutoza kodi kwenye mauzo ghafi yasiyozidi shilingi milioni nne kwa wafanyabiashara waliopo kwenye mpango wa *presumptive tax system* na kupunguza kiwango cha chini cha kodi kutoka shilingi laki 150,000 kwa mwaka hadi shilingi 100,000. Marekebisho haya yaliongeza mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 14,778,000.8 ikilinganishwa na lengo la kuongeza mapato kwa shilingi milioni 17,596,000.3 kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba sawa na ufanisi wa asilimia 84.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yam Mwaka 2004; marekebisho yaliyofanywa kwenye viwango vya pamoja vya Ushuru wa Forodha na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyokuwa na lengo la kulinda viwanda vya ndani ya jumuiya na kuchochea uzalishaji viwandani pamoja na kukuza ajira yameonyesha matokeo mazuri. Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2019, marekebisho hayo yaliongeza mapato ya Serikali kwa shilingi milioni 15,490,000.4, ikilinganishwa na lengo la mwaka la shilingi milioni 31,074,000 sawa na ufanisi wa asilimia 49.9 kwa mwaka. Kwa mwenendo huu ni dhahiri Serikali itaweza kufikia lengo zima la mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 238; Serikali kupitia Bunge ilifanya marekebisho kwenye Sheria ya usimamizi wa kodi ya Mwaka 2015. Moja ya marekebisho haya yalilenga kuongeza muda wa ziada wa miezi sita hadi Desemba 2019 kwa walipakodi waliokubaliwa kulipa kodi wanazodaiwa kwa utaratibu maalum wa kusamehe malimbikizo ya riba na adhabu kwa asilimia 100 kwa kufanya marekebisho ya Kifungu cha 70(2) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015. Lengo la hatua hii ni kutoa ahueni kwa walipakodi waliokuwa na malimbikizo makubwa yanayoathiri biashara zao na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Marekebisho haya yalitarajiwa kuongeza mapato kwa Shilingi milioni 367 kwa muda wa ziada wa miezi sita hadi Desemba 2019. Makusanyo halisi kutokana na hatua hii hadi Desemba 2019 ni shilingi milioni 126,074 sawa na asilimia 34.3 ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168; Sheria ya Usalama Barabarani ilifanyiwa marekebisho yakiwa na pamoja na kuongeza ada ya leseni ya udereva na kuongeza muda wa matumizi kutoka miaka mitatu hadi mitano. Marekebisho haya yalikuwenda pamoja na kuongeza ada ya kadi ya usajili wa vyombo vyote vya moto. Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2019 makusanyo halisi kutokana na marekebisho haya yalifikia Shilingi milioni 13,376,000.3, ikilinganishwa na lengo la mwaka la shilingi milioni 18,147,000

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa kipindi hicho, ambayo ni sawa na ufanisi wa asilimia 147.4 ya lengo la nusu mwaka na asilimia 73.4 ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia ilifanya marekebisho mengine madogo madogo katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na sheria nyingine ili kuondoa urasimu na Sheria hizo ni miongoni mwa Sheria ambazo zilikuja kufanyiwa kazi na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende sasa kwenye utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa kipindi cha nusu mwaka kwa Mwaka wa fedha 2019/2020 na muelekeo hadi Juni 2020; katika mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali ilipanga kukusanya na Kutumia jumla ya Shilingi bilioni 33,105.4. Kati ya fedha hizo jumla ya Shilingi bilioni 20,856.8 zilitarajiwa kutumika kwa matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 12,248.6 kwa matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Desemba mwaka 2019 Serikali ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi bilioni 15,857.2 kutokana na vyanzo vya ndani sawa na asilimia 96.2 ya makadirio ya nusu mwaka na asilimia 47 ya mapato yote yaliyokusudiwa katika Mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi wa kina na kubaini kwamba kwa mwenendo huu ni wazi kwamba hadi mwisho wa Mwaka wa Fedha 2019/2020 Serikali inaweza kutekeleza Bajeti kwa asilimia kati 80 hadi 90. Hatua hii ni kubwa na sisi katika Kamati tuliipongeza sana Serikali na tuliona inastahili pongezi kwa sbaabu ni hatua iliyofikiwa kubwa sana kwa kweli na sidhani kama tulishawahi kufika kiwango hiki kwa kipindi hiki cha Bunge lako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mwenendo wa makusanyo ya mapato; Kama inavyoonyesha katika jedwali Namba tatu ambalo liko hapo juu Waheshimiwa Wabunge wanaweza kuliona, mwenendo unaonyesha kwamba Serikali imeweza kuvuka lengo la kukusanya zaidi ya asilimia 50 kwa mapato yatanayo na Misaada ya Kisekta asilimia 110, Mikopo ya masharti ya Kibiashara asilimia 157, Mikopo ya ndani yaani *Roll over* asilimia 55.1. Hata hivyo, kwa upande wa mapato ya kodi Serikali imeweza kukusanya asilimia 95.2 ya lengo la nusu mwaka na Serikali za Mitaa zimeweza kukusanya asilimia 92.8 ya lengo la nusu mwaka. Mwenendo huu unaonyesha kwamba ni wazi kwamba Serikali inaweza kukusanya kati ya asilimia 80 kama nilivyosema hadi 90 ya makusanyo yote kwa mwaka huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mwenendo wa matumizi; katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2019 Serikali imetoa ridhaa ya matumizi yenye jumla ya Shilingi bilioni 15,316.6 sawa na asilimia 91.2 ya lengo. Kamati ilifanya uchambuzi wa matumizi hayo na kubaini masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida; hadi kufikia mwezi Desemba Mwaka 2019 Serikali ilikuwa imetumia jumla ya shilingi bilioni 10,524.6 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na asilimia 68.7 ya mapato yote yaliyokusanywa muda huo na asilimia 50.4 ya matumizi yote ya kawaida ya Shilingi bilioni 20,856,549. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Serikali imepeleka fedha za matumizi ya kawaida kwa zaidi ya asilimia 80 kwa mafungu yote isipokuwa tu kwa Fungu Na. 7 la Msajili wa Hazina ambalo limepokea asilimia 16 tu ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kamati imeendelea kuishauri Serikali kutokana na umuhimu wa fungu hili na mafanikio makubwa yaliyopatikana kwenye ukusanyaji wa gawio na mchango wa asilimia 15 ni muhimu sasa fungu hili lipatiwe fedha za kutosha kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi wa Hazina

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya maendeleo; katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 Serikali ilipanga kutumia jumla ya Shilingi bilioni 12,248,602 katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Desemba jumla ya Shilingi bilioni 3,767.2 sawa na asilimia 61.6 ya

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

lengo la nusu mwaka shilingi bilioni 6,111.6 na asilimia 30.7 ya Bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge. Hivyo ni wazi kwamba hadi kufikia mwisho wa Mwaka wa Fedha 2019/2020 kuna uwezekano mkubwa wa Serikali kutekeleza Bajeti ya Maendeleo kati ya asilimia 60 hadi 70. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zote za maendeleo zinapelekwa kama zilivyoidhinishwa na Bunge. Vilevile, kamati inasisitiza ulipaji wa kodi kwa hiari ili kupata fedha za kutosha na za uhakika za kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ugharamiaji wa Deni la Taifa; hadi kufikia mwezi Desemba 2019 jumla ya Shilingi...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kengele ya pili naomba uende kwenye hitimisho.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru. Naomba taarifa hii kwa sbabau ni ndefu basi iingizwe katika Kumbukumbu zako za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekee kwenye maoni na mapendekezo; baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Serikali pamoja na utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Kamati ina maoni na mapendekezo ya ujumla yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa Sheria ya mawasiliano na kielektroniki; marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya EPOCA Mwaka 2017, yalielekeza kampuni zote za simu kujiorodhesha kwenye soko la hisa na kuuza asilimia 25 ya hisa zake kwa umma na hatimaye kampuni hizo kuorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es salaam. Kamati inaendelea kusisitiza Kampuni za simu ambazo bado hazijaorodheshwa kwenye soko la Hisa la Dar es Salaam waweze kufanya hivyo ili Watanzania waweze kushiriki katika uwekezaji kwenye sekta ya mawasiliano kama Sheria inavyotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya ngozi; wakati wa kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2019 Kamati ilipokea Taarifa kutoka kwa wafanyabiashara wa ngozi kuhusu mlundikano wa ngozi katika maghala uliosababishwa na viwango vya ushuru wa mauzo nje yaani *export levy* ya asilimia 10 kwa ngozi zilizosindikwa hadi hatua ya *Wet blue* na asilimia 80 kwa ngozi ghafi, viwango ambavyo vilipelekea ngozi kukosa soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya tafiti yaliyofanywa na Serikali yalionyesha pia bado kuna mlundikano. Aidha, taarifa ya tafiti haikuweza kubainisha endapo viwango vya tozo vya ushuru wa mauzo nje ya Nchi kama vinaathiri biashara hiyo na hivyo kusababisha mlundikano. Hivyo basi, Kamati inaiagiza Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Mifugo na Uvuvi washirikiane na Wizara ya Fedha na Mipango kufanyia utafiti viwango hivyo vya ushuru na kuangalia ni namna gani vinaweza kuja na mikakati ya kusaidia na kuinua sekta hiyo ambayo ina manufaa makubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, minara ya mawasiliano kwa Shirika la TTCL; Kamati ilipotebembela kampuni ya simu ya TTCL ilibaini kwamba kampuni hiyo ina changamoto kubwa ya minara ya mawasiliano ambapo hivi sasa TTCL ina jumla ya minara 485 tu kati ya minara 14,000 iliyopo hapa nchini. Aidha, kati ya minara hiyo ya TTCL, minara 207 tu ndiyo inamilikiwa na Shirika na iliyobaki Shirika linapanga kutoka kwa watoa huduma wengine kama Vodacom, Halotel, Helios Towers na wengine. Kimsingi, idadi hiyo ya minara ni michache kwa Shirika kufikia lengo la kutoa huduma Nchi nzima. Umiliki mdogo wa minara kwa shirika la umma una athari za kiulinzi na usalama kutokana na kazi muhimu zinazoendeshwa na Shirika. Hivyo basi, ili kuondokana na changamoto hii, Kamati inashauri Serikali kuiwezesha kifedha TTCL kulingana na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mpango wake wa miaka mitano ili kuboresha miundombinu ya Shirika na hivyo kuwa na ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele kingine ni Kukosekana kwa Vifaa vya kupakua na kupakia mizigo Bandari ya Dar es salaam; Kamati imebaini kuna ukosefu wa vitendea kazi kama vile *cranes* na *conveyor belts* kwa Bandari ya Dar es salaam kwa ajili ya kushusha mizigo na kupakia na hivyo kurefusha muda wa kushusha na kupakia mizigo. Kamati inapendekeza maboresho yanayoendelea katika Bandari ya Dar es Salaam yaendeleo sanjari na upatikanaji wa vitendea kazi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala jingine ni changamoto ya utekelezaji wa mradi wa uboreshaji wa Miji; Kamati ya Bajeti katika uchambuzi wake imebaini kwamba kuna mikwamo katika utekelezaji wa Miradi ya Benki ya Dunia kwa baadhi ya Halmashauri za Miji. Mkwamo huu unatokana na Serikali kudai kodi ya ongezeko la thamani katika utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuleta kwa hati ya dharura mabadiliko ya Sheria ya VAT ili Bunge lako Tukufu liweze kufanya mabadiliko yatakayonusuru utekelezaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa uwasilishaji wa mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria; hii siyo mara ya kwanza kwa Kamati yako kuishauri Serikali kuidhinisha Bunge juu ya mapendekezo yake yaliyopelekwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki kabla hayajapitishwa. Ushauri huu unatokana na ukweli kwamba utaratibu wa kuyafanyia mabadiliko endapo Bunge halitaridhia ni mrefu na unachukua muda. Hivyo, Kamati inaendelea kupendekeza mabadiliko hayo yawe yanawasilishwa Kamati ya Bajeti kwa niaba ya Bunge ili kamati itoe maoni yake kabla hayajapelekwa katika Jumuiya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ya biashara na uwekezaji; Kamati inaishauri Serikali kujielekeze katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ili kuvutia sekta binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati inashauri Serikali ijielekeze katika kuondoa vikwazo vinavyozuia maendeleo ya viwanda Nchini hasa vikwazo vya ushindani usio sawa baina ya viwanda vya ndani dhidi ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya nje, ufinyu wa mitaji ya fedha, gharama kubwa za uzalishaji, miundombinu duni ya uzalishaji, mlolongo na taratibu kuwa mrefu, sheria kubadilika mara kwa mara na uwepo wa uhusiano hafifu kati ya sekta ya viwanda na sekta nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa viwango vya riba na mfumuko wa bei; Kamati ya Bajeti katika nyakati tofauti tofauti inaitaarifu Serikali kuhusu viwango vya riba katika sekta ya Benki kuwa vya juu kuliko uhalisia. Mfano; hadi kufikia Novemba 2019 viwango vya riba vilikuwa asilimia 16.87 ili hali mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.8. Ieleweke wazi kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya mfumuko wa bei na viwango vya riba haitarajwi kiuchumi viwango vya riba vizidi mfumuko wa bei kwa zaidi ya mara mbili. Hivyo, kamati inaishauri Serikali kuangalia gharama za uendeshaji wa Mabenki ili kuhakikisha viwango vya riba vinaendana na mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya kodi ya majengo kwa Halmashauri zote katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019 yalikuwa shilingi bilioni 6.7 sawa na asilimia 61.7 ya lengo la shilingi bilioni 10.8 katika kipindi hicho. Kodi ya majengo haikufikia lengo kutokana na walipakodi wengi kupendekeza kulipa kodi na tozo katika tarehe za mwisho wa mwaka. Kutokana na changamoto hiyo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kujumuisha makusanyo ya kodi ya majengo katika ankara za maji au umeme. Hatua hii itasaidia ukusanyaji wa kodi hiyo kila mwezi kwa gharama ndogo na kuondoa usumbufu kwa wananchi kutaka kulipa kodi hiyo kila mwisho wa mwaka.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimisha kwa kukushukuru kwanza wewe mwenyewe, Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika kwa miongozo yenu ambayo mmekuwa mkiipatia Kamati na hivyo kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pia napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Mbunge na Waziri wa Fedha na Mipango na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, Mbunge na Naibu Waziri kwa ushirikiano wao ambao wamekuwa wakitoa kwa Kamati katika kipindi chote cha vikao vya Kamati. Nawashukuru pia wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii ambao kwa kweli mchango wao ni mkubwa sana kwenye Kamati hii. Wako makini na ni mahiri sana katika kuchangia na kufanikisha shughuli za Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Ndugu Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati katika kipindi chote. Pamoja naye napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA MWAKA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KATIKA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI, 2019 HADI MWEZI JANUARI, 2020 PAMOJA NA TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA JULAI - DESEMBA 2019 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(Imetolewa chini ya Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016)

1.0. UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka kuhusu Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Bajeti katika kipindi cha mwezi Januari 2019 hadi mwezi Januari 2020.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii pia inatoatathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya katika kipindi cha nusu Mwaka kuanzia Julai hadi Desemba 2019 na mwelekeo hadi Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilitokeleza majukumu yake kwa kuzingatia kifungu cha 9(1) cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 Mwaka 2015, Kanuni za Bunge Toleo la 2016 Fasili ya 9 ya Nyongeza ya Nane, Sheria ya Fedha, Sheria nyingine, taratibu na miongozo mbalimbali iliyopo inayohusiana na masuala ya fedha, uchumi, kodi na bajeti. Katika kutekeleza shughuli hizo, Kamati ilikutana na Serikali, Taasisi, Mashirika na Sekta binafsi pamoja na wadau mbalimbali ili kuwasiliza pamoja na kupokea Taarifa na maoni mbalimbali ambayo Kamati ilitumia wakati ikitekeleza majukumu yake na hatimaye kutoa maoni na ushauri kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kumi na tatu (13). Sehemu ya kwanza ni Utangulizi, sehemu ya pili ni utekelezaji wa shughuli za Kamati, sehemu ya tatu ni tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/19, sehemu ya nne ni Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2018/19 na Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2019/2020, sehemu ya tano inahusu Muswada Wa Sheria

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Fedha wa Mwaka 2019 (The Finance Bill, 2019), sehemu ya sita inahusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2019/2020, sehemu ya saba imeainisha hoja za Kamati za Bunge za kisekta, sehemu ya nane inahusu Utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 kwa kipindi cha nusu mwaka 2019/2020, sehemu ya tisa niUtekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2019/2020 na mwelekeo hadi Juni, 2020, sehemu ya kumi inabainisha Ziara mbalimbali za Kamati, Sehemu ya kumi na moja ni Mafunzo ambayo Kamati ilipewa, Sehemu ya Kumi na mbili nimaoni na mapendekezo ya ujumla na sehemu ya kumi na tatu ni Hitimisho.

2.0. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI

Mheshimiwa Spika, zifuatazo ni kazi zilizotekelezwa na Kamati ya Bajeti katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari 2019 hadimwezi Januari 2020: -

- a) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2018/2019;
- b) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha Mwaka 2018/2019;
- c) Kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha Mwaka 2019/2020 yatoanayo na vyanzo vya kodi na vyanzo vingine visivyo vya kodi;
- d) Kupitia na kujadili kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha Mwaka 2020/2021;
- e) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na mafungu yaliyo chini yake kwa mwaka wa fedha 2018/2019; pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020;
- f) Kuchambua na kushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2019(The Finance Act, 2019);
- g) Kujadili na kuidhinisha Bajeti ya Mifuko ya Mahakama, Bunge na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi
- h) Kupitia na kujadili utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2019/2020;
- i) Kupitia na kujadili kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/2021;
- j) Kujadili na kuidhinisha Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mafungu yaliyo chini yake;
- k) Kushiriki mafunzo mbalimbali yenye lengo la kuwaongezea wajumbe wa Kamati uwezo wa kutekeleza majukumu yake;
- l) Kukutana na wadau mbalimbali wa masuala ya kodi na kujadili changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika utekelezaji wa sheria mbalimbali za kodi na sizizo za kikodi zinazoathiri sekta binafsi

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- m) Kufanya utafiti na uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato na kutoa mapendekezo kuhusu hatua za kupunguza utegemezi wa kibajeti;
- n) Kutoa ushauri wa jumla kuhusu Bajeti ya Serikali kwa Bunge na Kamati za Kudumu za Bunge;
- o) Kuchambua hoja zilizojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta wakati wa kujadili Bajeti za Wizara kwa mwaka 2017/2018 kwa ajili ya kuishauri Serikali;
- p) Kuchambua Taarifa za utekelezaji na utendaji kutoka kwenye Wizara inayosimamiwa na Kamati pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo;
- q) Kuchambua Taarifa ya utendaji kazi ya Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha 2018/19;
- r) Kufanya ziara nchini Uganda na Rwanda kujiifunza kuhusu mfumo wa Akaunti Jumuifu (TSA); na
- s) Kufanya ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na Taasisi inazozisimamia.

Mheshimiwa Spika, Kamati inatoa shukrani kwanza kwako wewe Binafsi na Pili kwa Serikali na wadau wote kwa ushirikiano wao ulioweza kukamilika kwa shughuli hizo.

3.0. TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2018/2019

Mheshimiwa Spika, tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali inakwenda sambamba na kuangalia mwenendo wa viashiria mbalimbali vya uchumi jumla. Kwa muhtasari mwenendo wa viashiria hivyo vya ukuaji wa uchumi vimetathminiwa kama ifuatavyo: -

3.1. Pato la Taifa

Mheshimiwa Spika, takwimu za Serikali zinaonesha uchumi wa Taifa ulikua kwa **asilimia 6.8** katika mwaka 2018. Sekta zilizochangia kwa kiasi kikubwa kwa ukuaji huo ni Sanaa na burudani **asilimia 13.7**, ujenzi **asilimia 12.9**, uchukuzi na uhifadhi wa mizigo **asilimia 11.8** pamoja na habari na mawasiliano **asilimia 9.1**. Sekta ya kilimo pamoja na kuwa na mchango mkubwa wa takribani **asilimia 27** kwenye pato la taifa ukuaji wake ni **asilimia 4.3** tu. Hivyo bado kuna haja ya Serikali kuondoa vikwazo vinavyosababisha sekta ya kilimo kutokukua kwa kasi pamoja na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili sekta binafsi iwe na mchango mkubwa katika ukuaji wa pato la Taifa.

3.2. Mfumuko wa Bei

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kupunguza mfumuko wa bei kutoka **asilimia 5.3** mwaka 2017 hadi **asilimia 3.5** mwaka 2018. Kiwango hicho kimefikwa kutokana na upatikanaji wa chakula cha kutosha nchini. Hivyo ni wazi kwamba wakulima wa nchi hii ndiyo kwa kiasi kikubwa wanasaidia katika kupunguza mfumuko wa bei. Kamati ya inaishauri Serikali kuendelea kuhakikisha NFRA inakuwa na mtaji wa kutosha na inatekeleza jukumu lake la msingi la kuhifadhi chakula ili kulinda mfumuko wa bei.

Jedwali Na. 1. Mwenendo wa Mfumuko wa bei na Fahirisi

Na	Mwaka	2014	2015	2016	2017	2018
1.	Mfumuko wa Bei	6.1%	5.6%	5.2%	5.3%	3.5%
2.	Fahirisi ya Bei	92.7	97.9	102.9	108.4	112.2

Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu

3.3. Mwenendo wa Thamani ya Shilingi

Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa kwa kipindi cha Julai hadi Novemba 2018, Dola ya Marekani imebadilishwa kwa wastani wa **Shilingi 2,276** ilikilinganishwa na **Shilingi 2,235** katika kipindi cha Julai hadi Novemba 2017. Hii inaonesha Shilingi ilipungua thamani dhidi ya Dola kwa **asilimia 1.8**. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza Sera zenye mlengo wa kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje na hasa viwanda vinavyozalisha bidhaa ambazo zinaagizwa nje kwa wingi. Sera hizo zitasaidia kupunguza nakisi ya urari wa biashara na hivyo kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni na hivyo kuongeza thamani ya Shilingi.

3.4. Deni la Taifa.

Mheshimiwa Spika, Deni la Serikali liliongezeka kutoka **Shilingi bilioni 49,728.03** machi 2017 hadi kufikia **Shilingi bilioni 50,772.27 mwaka 2018** sawa na ongezeko la **asilimia 2.1**. Kiasi kikubwa cha deni la Serikali linamilikiwa na wakopeshaji kutoka nje. Kamatiinatambua kuwa ongezeko la deni linatokana na mahitaji ya kugharamia miradi ya maendeleo. Hata hivyo, ni vema Serikali ikahakikisha inazingatia matakwa ya Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana ya Serikali Sura ya 165na vigezo vya kimatatifa ili kuhakikisha deni linaendelea kuwa himilivu.

4.0. UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2018/19 NA MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 2019/2020

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 94 Bunge lilijadili mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2019/2020 uliowasilishwa Bungeni na Waziri wa Fedha na Mipango. Kamati ilipata fursa ya kufanya tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa tatu wa Maendeleo wa Mwaka 2018/2019, kuchambua na baadaye kutoa maoni na mapendekezo kuhusu Mpango wa mwaka 2019/2020, kupitia Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni. Bunge lilitoa maoni na mapendekezo na hatimaye Mpango huo kuidhinishwa. Baadhi ya masuala yaliyobainishwa katika tathmini ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2018/19 ni kama ifuatavyo: -

- i. Uwepo wa changamoto katika upatikanaji wa mapato ya ndani na ya nje kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo;
- ii. Baadhi ya miradi ya kielelezo ya muda mrefu kutokutekelezwa kwa wakati. Mfano Mradi wa Makaa ya mawe, chuma, vanadium na Titanium wa Liganga na Mchuchuma, Mradi wa Kiwanda cha Matairi cha *General tyre*, Kurasini Logistic Centre pamoja na Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi;
- iii. Serikali kuchelewa kufanya tathmini ya utekelezaji wa mpango wa Miaka 5 na mwaka mmoja ili kuweza kubaini changamoto ambazo zitajenga msingi wa kuandaa mpango wa maendeleo wa awamu ya 3 katika kipindi cha Miaka mitano. Aidha, changamoto hii inatokana na Serikali kutumia utekelezaji wa nusu mwaka wa mpango wa kila mwaka unaotekelezwa kwa kipindi

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

husika kupanga mpango wa mwaka unaofuata kwa kipindi kijacho cha fedhahivyo kushindwa kufanya tathmini ya utekelezaji kwa kipindi chote cha utekelezaji wa mpango husika.

iv. Kuendelea kuwepo kwa ukwepaji wa kodi ikiwa ni pamoja na biashara ya magendo katika mwambao wa bahari pamoja na mipaka yetu; na

v. Uwekezaji usioridhisha katika sekta ya kilimo na utafutaji wa masoko kwa mazao ya kilimo ya biashara na chakula.

Mheshimiwa spika, ni matumaini ya Kamati kwamba Serikali itazingatia ushauri uliotolewa na Kamati ili mapendekezo yaliyobainishwa yatekelezwe katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2020.

5.0. MUSWADA WA SHERIA YA FEDHA WA MWAKA 2019 (THE FINANCE BILL, 2019).

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86 (5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016 Kamati iliwasilisha Bungeni taarifa yake ya maoni na ushauri kuhusu Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019 (The Finance Bill, 2018) na hatimaye Bunge lako Tukufu liliidhinisha Muswada huo kuwa Sheria ambayo ilianza kutumika tarehe 1 Julai, 2019.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia na kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2019. Shughuli hii ilifanyika kwa kupitia kifungu kwa kifungupamoja na kupokea maoni kutoka kwa wadau. Baada ya kujiridhisha na maudhui yake, Kamati ilifanya majadiliano ya kina na Serikali na kupendekeza marekebisho pale ilipobidi. Sheria zilizofanyiwa marekebisho katika Muswada huo ni Sheria Kumi (10) ambazo ni:-

i. Sheria ya Huduma za Viwanja vya Ndege Sura ya 365 (*The Airport Service Charge Act*) na Sheria ya Huduma za Bandari Sura ya 264 (*The Port Service Charge Act*);

ii. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura ya 147 (*The Excise (Management and Tariff Act)*);

iii. Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya Mwaka 2004;

iv. Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 (*The Income Tax Act*);

v. Sheria ya Usalama wa Barabarani Sura ya 148 (*The Road Traffic Act*);

vi. Sheria ya Viwango Sura 130 (*The Standards Act*);

vii. Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Sura 219 (*Tanzania Food, Drugs, and cosmetics act*);

viii. Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 238 (*Tax Administration Act*); na

ix. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura ya 148 (*Value Added Tax*).

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Sheria hizi umefafanuliwa kwa kina kwenye uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2019 kwa kipindi cha nusu mwaka.

6.0. MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA PAMOJA NA MWONGOZO WA KUTAYARISHA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, mwezi Novemba, 2019 Serikali iliwasilisha Bungeni Mpango wa Maendeleo wa Taifa pamoja na Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021

kama Sheria ya Bajeti inavyoelekeza. Kamati ya Bajeti ilipitia na kujadiliana na Serikali kuhusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021 pamoja na Mapendekezo ya Mpango wa Mapendekezo wa Taifa. Kimsingi Mwongozo huu umeelekeza masuala ya msingi ya kuzingatiwa katika uandaaji wa Mpango na Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Sura ya Bajeti kwa mwaka 2020/2021 inaonyesha kuwa, Serikali inatarajia kukusanya na kutumia jumla ya **shilingi trilioni 34.36** ikiwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 3.78** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2019/20 ya **shilingi trilioni 33.12**. Mapato ya ndani yanatarajia kuwa **shilingi trilioni 23.46** ikiwa ni sawa na **asilimia 68.3** ya bajeti. Kati ya fedha hizo mapato ya kodi ni **shilingi trilioni 19.76**, mapato yasiyo ya kodi **shilingi trilioni 2.89** na mapato ya Halmashauri **shilingi bilioni 803.76**. Aidha, Serikali inatarajia kupata kiasi cha **shilingi trilioni 5.212** zikiwa ni misaada na mikopo nafuu kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na kuziba nakisi ya bajeti.

6.1. Maoni ya Kamati kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Pamoja na Mwongozo wa Kutayarisha Mpango na Bajeti Ya Serikali kwa Mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mapitio hayo, Kamati iliishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu Mpango huo kama ifuatavyo: -

6.1.1. Ukusanyaji wa Mapato kwa Mfumo wa (GepG)

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali ihakikishe kila halmashauri zinakusanya mapato yake kwa njia ya Mfumo wa Serikali wa kieletroniki wa ukusanyaji wa mapato (GePG). Hatua hii ni muhimu ili kuhakikisha kwamba uwiano wa ukusanyaji wa mapato ufikie walau **asilimia 18** ya Pato la Taifa kwa lengo la kuziba nakisi ya bajeti na kutekeleza miradi ya maendeleo yenye tija kwa taifa. Kwa sasa uwiano wa ukusanyaji wa mapato ni **asilimia 11.5** ya Pato la Taifa. Aidha, nguvu kubwa ielekezwe katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kupitia vyanzo vipya vya kodi na visivyo vya kikodi pamoja na kuimarisha ushirikiano wa kijumuiya na kikanda.

6.1.2. Taarifa ya Utekelezaji wa Vipambebe.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipendekeza pia Mpango wa Maendeleo uainishe hatua za utekelezaji wa vipambebe kama vilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka 5 ikizingatiwa kuwa Mpango wa Maendeleo wa 2020/2021 ni Mpango wa mwisho wa Miaka 5. Hali hii itatoa taswira ya mwelekeo na ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo na hivyo kusaidia kufanya tathmini bora ya utekelezaji kwa kipindi husika.

6.1.3. Upatikanaji wa Rasilimali fedha kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mafanikio ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/21 yanategemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa rasilimali fedha. Kamati iliishauri Serikali kuanisha namna ambavyo itavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi (FDI) kushiriki katika utekelezaji wa mpango pamoja na kuhamasisha Sekta Binafsi kushirikiana na Sekta ya Umma katika kugharamia na kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati kwa maendeleo ya nchi.

6.1.4. Kufungua Soko la Mitaji (Liberization of Capital Market)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kufungua zaidi Soko la Mitaji (Liberization of Capital Market) ili kwanza kuvutia mitaji kutoka nje na kupunguza athari za Serikali kukopa katika soko dogo la fedha la ndani.

6.1.5. Utekelezaji wa Mwongozo wa Ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati iliishauri Serikali kuendelea kutekeleza Mwongozo wa Ushirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo (*Development Cooperation Framework-DCF*) ili kukuza mahusiano ya kimaendeleo na hivyo kusaidia upatikanaji wa fedha kutoka kwa wahisani wa kibajeti. Hatua za awali za utekelezaji wa mwongozo huo zimeonyesha mafanikio.

7.0. HOJA ZA KAMATI ZA BUNGE ZA KISEKTA

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Bajeti la mwaka 2019, Kamati ilipokea jumla ya hoja 26 zilizowasilishwa mbele yake. Kati ya hoja hizo, hoja 14 zilihusu bakaa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mafungu mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2018/19, Hoja 9 zilihusu nyongeza ya fedha kwa ajili ya makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2019/20 na hoja 3 zilihusu mapendekezo kuhusu sera, sheria na mabadiliko ya kikodi na hivyo hazikuwa na athari ya kibajeti moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilikamilisha jukumu hili kwa kukutana na Kamati ya Uongozi pamoja na Serikali kwa lengo la kufanya mashauriano kuhusu hoja husika. Katika kikao hicho, Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu hoja husika na matokeo ya mashauriano hayo yaliwasilishwa Bungeni kupitia Taarifa ya Kamati.

7.1. Hoja zilizofanyiwa Kazi na Serikali

Mheshimiwa Spika, baada ya majadiliano Baina ya Kamati ya Uongozi, Kamati ya Bajeti na Serikali hoja zilizofanyiwa kazi na Serikali ni kama ifuatavyo: -

i. Hoja zilizohusu bakaa ya fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/19, Serikali iliweza kutoa fedha kwa baadhi ya mafungu kulingana na fedha zilivyokuwa zinapatikana. Baadhi ya mafungu hayo ni pamoja na Fungu 52-Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambapo Serikali ilitoa **shilingi bilioni 30.2** kwa ajili ya ununuziwa vifaa tiba na Fungu 44 & Fungu 60- Wizara ya Viwanda na Biasharailiyopewa **shilingi bilioni 5.2** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

ii. Hoja za madeni ya Bohari ya Dawa (MSD), madai ya marejesho ya kodi ya ongezeko la thamani (VAT Refunds) na madeni ya Waalimu, Serikali iliahidi kuwa madeni hayo yatalipwa kadiri uhakiki wa madeni hayo utakavyokuwa unakamilika; na

iii. Kuhusu ya ujenzi wa majengo ya Ubalozzi ambayo imekua hoja ya muda mrefu, Serikali ilishaanza kazi za awali katika Ubalozzi wa Tanzania nchini Oman. Aidha, Serikali iliahidi kuwa ujenzi wa majengo ya Ubalozzi kwa nchi nyingine utaendelea kutengewa fedha kwa miaka ijayo.

7.2. Hoja ambazo Serikali iliahidi kuzifanyia kazi

Mheshimiwa Spika, Hoja nyingine ambazo zilihataji muda ili Serikali iweze kuzifanyia kazi na kutoa mrejesho au utekelezaji ni kama zifuatazo: -

i. Serikali iliahidi kuangalia uwezekano wa kuongeza fedha kwa mafungu mbalimbali mara baada ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka wa fedha fedha 2019/20;

ii. Kuhusu hoja za kisera na sheria, Serikali ilipokea hoja hizo na kuahidi kuzifanyia kazi kupitia utaratibu wa maamuzi wa Serikali. Baadhi ya hoja hizo ni pamoja na utozwaji wa kodi ya makampuni kwa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA);

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo ya Kamati kuwa Serikali imeendelea kuzifanyia kazi hoja hizo kama ilivyoahidi.

8.0. UTEKELEZAJI WA SHERIA YA FEDHA YA MWAKA 2019 KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2019/20 Bunge lilifanya marekebisho katika sheria mbalimbali zilizokuwa na lengo la kuongeza mapato ya Serikali, kupanua wigo wa mapato, kuimarisha usimamizi wa mapato na matumizi pamoja na kuchochea ukuaji wa viwanda nchini. Marekebisho hayo yalitarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **shilingi milioni 453,754.3**. Katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019 makusanyo halisi kutokana na hatua hizo yalifikia **shilingi milioni 167,961** ikiwa ni ufanisi wa **asilimia 40.9** ya lengo la kukusanya **shilingi milioni 410,377.2** kwa kipindi hicho. Ufanisi mdogo umesababishwa na kukosekana kwa mapato yaliyotarajiwa kupatikana kwa kutekeleza **tax amnesty**.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipitia, ilichambua na kujadili Taarifa ya utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2019 katika kipindi cha nusu mwaka 2019/20. Katika uchambuzi wa utekelezaji wa sheria hizi Kamati imebaini masuala yafuatayo: -

8.1. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148 (The Value Added Tax Cap 148)

Mheshimiwa Spika, marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani yalilenga kusamehe kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) kwenye makasha yenye majokofu yanayotumika kwenye Kilimo cha Kisasa cha mboga mboga (horticulture), vifaa vya kukaushia nafaka (Grain Drying Equipment), vilainishi vya ndege, tiketi za ndege, vipeperushi, kalenda, shajara, karatasi zenye nembo na sare za wafanyakazi zilizowekwa nembo ya Shirika husika la ndege. Lengo likiwa ni kupunguza gharama za uzalishaji na kuboresha kilimo cha kisasa nchini pamoja na kuiwezesha nchi kuingia mikataba mbalimbali za huduma za usafiri wa anga (Bilateral Air Service Agreements). Vilevile, Serikali ilifuta msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani uliokuwa unatolewa kwenye taulo za kike kwa kuwa haukuwezesha kupatikana kwa bidhaa hiyo muhimu kwa bei nafuu kwa walengwa na badala yake unawanufaisha wafanyabiashara badala ya walengwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2019, Misamaha ya kodi ya Ongezeko la Thamani iliyotolewa kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 ilikuwa **shilingi milioni 754.2** ikiwa ni sawa na **asilimia 91.6** ya lengo la nusu mwaka na **asilimia 45.8** ya lengo la mwaka la kukusanya **shilingi milioni 1,646.7**. Kamati inashauri Serikali kuendelea kuchukua hatua sanjari ambazo zinaonekana kero kwa wananchi katika sekta ya kilimo ili kuikwamua sekta hii muhimu.

8.2. Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147

Mheshimiwa Spika, marekebisho yaliyofanyika kwenye sheria ya ushuru wa bidhaa yalilenga kutoza **asilimia 10** kwenye bidhaa mbalimbali kama mabomba na vifaa vya plastiki vya ujenzi; nywele za bandia pamoja na kupunguza Ushuru wa Bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa kutokana na usindikaji wa matunda yanayozalishwa hapa nchini kwa kiwango kinachozidi **asilimia 75**. Marekebisho hayo yalitarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa **shilingi milioni 3,987.5** lakini marekebisho hayo yalipunguza mapato kwa **shilingi milioni 1,004.3**, ikiwa ni ufanisi wa **asilimia -25.2**. Kwa kuwa hatua hii ilikuwa na nia njema ya kulinda viwanda vya ndani lengo linaweza kuwa limefikiwa lakini si kwa upande wa mapato yaliyokuwa yanatarajiwa.

8.3. Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332

Mheshimiwa Spika, marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 yaliyolenga kuanzisha mfumo mpya wa kutoza kodi kwenye mauzo ghafi yasiyozidi shilingi **milioni nne (4,000,000/=)** kwa wafanyabiashara waliopo kwenye mpango wa *Pre sumptive tax system* na kupunguza kiwango cha chini cha kodi kutoka shilingi laki moja na nusu **(150,000/=)** kwa mwaka hadi **shilingi laki moja (100,000/=)**. Marekebisho haya yaliongeza mapato ya Serikali kwa **shilingi milioni 14,778.8** ikilinganishwa na lengo la kuongeza mapato kwa **shilingimilioni 17,596.3** kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2019, sawa na ufanisi wa **asilimia 84**.

8.4. Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yam waka 2004.

Mheshimiwa Spika, marekebisho yaliyofanyika kwenye viwango vya pamoja vya Ushuru wa Forodha na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yaliyokuwa na lengo la kulinda viwanda vya ndani ya jumuiya na kuchochea uzalishaji viwandani pamoja na kukuza ajira yameonyesha matokeo mazuri. Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2019, marekebisho hayo yaliongeza mapato ya Serikali kwa **shilingi milioni 15,490.4**, ikilinganishwa na lengo la mwaka la **shilingi milioni 31,074**, sawa na ufanisi wa **asilimia 49.9**. Kwa mwenendo huu ni dhahiri Serikali itaweza kufikia lengo zima la mwaka.

8.5. Sheria ya Usimamizi wa Kodi Sura 238.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bunge ilifanya marekebisho kwenye Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya Mwaka 2015. Moja ya marekebisho haya yalilenga kuongeza muda wa ziada wa miezi sita (6) hadi Desemba 2019 kwa walipakodi waliokubaliwa kulipa kodi wanazodaiwa kwa utaratibu maalumu wa kusamehe malimbikizo ya riba na adhabu (*Tax Amnesty on Interest and Penalties*) kwa **asilimia 100** kwa kufanya marekebisho ya Kifungu cha 70 (2) cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015. Lengo la hatua hii ni kutoa ahueni kwa walipakodi waliokuwa na malimbikizo makubwa yanayoathiri biashara zao na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Marekebisho haya yalitarajiwa kuongeza mapato kwa **Shilingi milioni 367,000** kwa muda wa ziada wa miezi sita hadi Desemba 2019. Makusanyo halisi kutokana na hatua hii hadi Desemba 2019 ni **shilingi milioni 126,074.0**, sawa na **asilimia 34.3** ya lengo.

8.6. Sheria ya Usalama Barabarani Sura 168

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Usalama Barabarani ilifanyiwa marekebisho yakiwa na pamoja na kuongeza ada ya leseni ya udereva na kuongeza muda wa matumizi kutoka miaka mitatu hadi mitano. Marekebisho haya yalikuwenda pamoja na kuongeza ada ya kadi ya usajili wa vyombo vyote vya moto. Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Desemba 2019 makusanyo halisi kutokana na marekebisho haya yalifikia **Shilingi milioni 13,376.3**, ikilinganishwa na lengo la mwaka la **shilingi milioni 18,147** kwa kipindi hicho, ambayo ni sawa na ufanisi wa **asilimia 147.4** ya lengo la nusu mwaka na **asilimia 73.4** ya lengo la mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia ilifanya marekebisho mengine madogo madogo katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na sheria nyingine ili kuondoa urasimu, kuboresha mazingira ya ufanyaji biashara na uwekezaji, yakiwemo ya kufuta jumla ya tozo 54 zilizokuwa zikitozwa na Wizarambalimbali, Idara na Taasisi zinazojitegemea. Hatua hii ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa kuboresha mfumo wa uhibitaji wa biashara (*Blue Print for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment*). Vile vile hatua hii ililenga kuondoa muingiliano wa majukumu ya kiutendaji yaliyokuwa yakitekelezwa na Wizara, Idara na Taasisi zinazojitegemea.

9.0. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KATIKA KIPINDI CHA NUSU YA KWANZA YA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 NA MWELEKEO HADI JUNI 2020.

Mheshimiwa Spika, Katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali ilipanga kukusanya na Kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 33,105.4**. Kati ya fedha hizo jumla ya **Shilingi bilioni 20,856.8** zilitarajiwa kutumika kwa matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 12,248.6** kwa matumizi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Desemba mwaka 2019 Serikali ilikuwa imekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 15,857.2** kutokana na vyanzo vya ndani sawa na **asilimia 96.2** ya makadirio ya nusu mwakana **asilimia 47** ya mapato yote yaliyokusudiwa katika mwaka wa fedha 2019/20.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imefanya uchambuzi wa kina na kubaini kwamba kwa mwenendo huu ni wazi kwamba hadi mwisho wa mwaka wa fedha 2019/20 Serikali inaweza kutekeleza Bajeti kwa asilimia kati 80 hadi 90. Hatua hii ni kubwa na inastahili pongezi kwa vyombo vyote vinavyosimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

Jedwali Na. 2. Sura ya Bajeti na Utekelezaji kwa mwaka 2019/20 (Bilioni)

Na	Chanzo	Bajeti (2019/20)	Lengo nusu mwaka	Utekelezaji	Asilimia % ya Bajeti
1.	Mapato ya Kodi	19,100,932.3	9,550,466	9,100,502.3	95.29
2.	Mapato ya Halmashauri	765,483	382,742	355,400	92.86
3.	Mapato yasiyo ya kodi	3,178,912.8	1,589,456	688,605.7	43.32
4.	Misaada na Mikopo kutoka nje	272,813	136,407	136,407	100
5.	Mikopo ya ndani	1,499,774	749,887	667,100	88.96
6.	Mikopo ya ndani roll over	3,460,218	1,730,109	1,905,400	110.13
7.	Mikopo ya masharti ya kibiashara	2,316,404	1,158,202	1,822,100	157.32
8.	Miradi ya nje	2,510,863	1,255,432	1,318,046	104.99
9.	Jumla	33,105,409.7	16,552,700	15,857,154	95.76

Chanzo: Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti Nusu mwaka MOF

9.1. Uchambuzi wa Mwenendo wa Makusanyo ya Mapato

Mheshimiwa Spika, Kama inavyoonyesha katika jedwali Namba 3 hapo juu mwenendo unaonyesha kwamba Serikali imeweza kuvuka lengo la kukusanya zaidi ya **asilimia 50** kwa mapato yatokanayo na Misaada ya Kisekta **asilimia 110**, Mikopo ya masharti ya Kibiashara **asilimia 157**, Mikopo ya ndani (Roll over) **asilimia 55.1**. Hata hivyo, kwa upande wa mapato ya kodi Serikali imeweza kukusanya **asilimia 95.2** ya lengo la nusu mwaka na Serikali za Mitaa imeweza kukusanya **asilimia 92.8** ya lengo la mwaka. Mwenendo huu unaonyesha kwamba ni wazi kwamba Serikali inaweza kukusanya kati ya **asilimia 80** hadi **90** ya mapato iliyokusudia kukusanya katika mwaka wa fedha 2018/19. Hatua hii ni ya kupongezwa.

9.2. Uchambuzi wa Mwenendo wa Matumizi

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2019 Serikali iimetoa ridhaa ya matumizi yenye jumla ya **Shilingi bilioni 15,316.6** sawa na **asilimia 91.2** ya lengo. Kamati ilifanya uchambuzi wa matumizi hayo na kubaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

9.2.1. Matumizi ya Kawaida

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Desemba mwaka 2019 Serikali ilikuwa imetumia jumla ya **shilingi bilioni 10,524.6** kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na **asilimia 68.7** ya mapato yote yaliyokusanywa muda huo na **asilimia 50.4** ya matumizi yote ya kawaida ya **Shilingi bilioni 20,856,549**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba Serikali imepeleka fedha za matumizi ya kawaida kwa zaidi ya **asilimia 80** kwa mafungu yote isipokuwa tu kwa Fungu namba 7 la Msajili wa Hazina ambalo limepokea **asilimia 16** tu ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutokana na umuhimu wa fungu hili na mafanikio makubwa yaliyopatikana kwenye ukusanyaji wa gawio na mchango wa **asilimia 15** ni muhimu sasa lipatiwe fedha za kutosha kwa ajili ya kuimarisha utendaji kazi wake.

9.2.2. Matumizi ya Maendeleo

Mheshimiwa Spika Katika mwaka wa fedha 2019/20 Serikali ilipanga kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 12,248,602** katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia mwezi Desemba jumla ya **Shilingi bilioni 3,767.2** sawa na **asilimia 61.6** ya lengo la nusu mwaka **shilingi bilioni 6,111.6** na **asilimia 30.7** ya Bajeti yote iliyoidhinishwa na Bunge. Hivyo ni wazi kwamba hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha 2019/20 kuna uwezekano mkubwa wa Serikali kutekeleza Bajeti ya Maendeleo kwa kati ya **asilimia 60** hadi **70**. Kamati inaishari Serikali kuhakikisha kwamba fedha zote za maendeleo zinapelekwa kama zilivyo idhinishwa na Bunge. Vilevile, kamati inasisitiza ulipaji wa kodi kwa hiari ili kupata fedha za kutosha na za uhakika za kutekeleza miradi ya maendeleo.

9.2.3. Ugharamiaji wa Deni la Taifa

Mheshimiwa Spika, Hadi kufikia mwezi Desemba 2019 jumla ya **Shilingibilioni 3,813.6** sawa na **asilimia 32** ya mapato yote ya Serikali katika kipindi cha nusu mwaka zilitumika kugharamia Deni la Serikali. Kati ya fedha hizo **shilingi bilioni 455.7** zilitumika kulipa deni la Serikali ambalo ankara za malipo hazijapokelewa. Hali hii inaonyesha kwamba ni lazima tuendeele kupanua wigo wa ukusanyaji wa mapato ili tuwe na deni ambalo halitasababisha matatizo katika uchumi kwa siku zijazo na vizazi vijavyo.

10.0. ZIARA YA KAMATI KUTEMBELEA TAASISI, IDARA NA MAMLAKA ZILIZOCHINI YA WIZARA

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari 2019 hadi Januari, 2020 katika nyakati tofauti Kamati ilifanya ziara katika mikoa ya Arusha na Dar es salaam. Ziara hizo zilikuwa na lengo la: -

i. kukagua shughuli zinazotekelezwa na Taasisi zinazosimamiwa na Kamati;

ii. kukagua utekelezaji wa Mifumo mbalimbali ya kikodi iliyoidhinishwa na Bunge wakati wa kupitisha Muswada wa Sheria wa Fedha 2018 iliyokuwa na lengo la kuhuisha mapato ya Serikali na jinsi unayofanya kazi katika viwanda ambavyo tayari vimeanza kutumia mifumo hiyo;

iii. kukagua utekelezaji wa Mfumo wa kuhuisha fedha zote nchini na jinsi unavyotekelezwa katika ngazi tofauti tofauti za Serikali;

iv. kutembelea na kukagua shughuli za viwanda vya kimkakati mjini Arusha; pamoja na

v. kukagua utekelezaji wa hatua mbalimbali za maendeleo zinazochukuliwa na Serikali kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali na kuchochea uchumi wa nchi.

10.1. Masuala Muhimu yaliyojitekeleza

Mheshimiwa Spika, kwa muhtasari naomba niwasilishe masuala muhimu yaliyobainika wakati wa ziara ya kamati Kutembelea Soko la hisa (DSE), Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR), Mamlaka ya

Bandari (TPA), Shirika la Simu la Tanzania (TTCL), Jengo jipya la Abiria la Uwanja wa Taifa wa Julius Nyerere (JNIA terminal III), Kiwanda cha TANALEC pamoja na Benki Kuu. Masuala ya Msingi yaliyojitokeza ni kama ifuatavyo: -

10.1.1 Mwenendo wa Soko la Hisa la Dar es salaam (DSE)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilibaini kushuka kwa mwenendo wa biashara katika Soko la Hisa la Dar es salaam (DSE) pamoja mtaji wa soko la DSE uliotokana na kushuka kwa thamani pamoja na mauzo ya hisa za makampuni ya nje na ndani yaliyoorodheshwa kwenye Soko. Aidha, sababu kuu iliochangia kushuka kwa mauzo ya hisa ilitokana mfuko mpya wa hifadhi ya jamii kutoshiriki katika soko kwa miezi 15.

10.1.2 Kuchelewa kuanza kwa Soko la bidhaa (Tanzania Merchantile Exchange)

Mheshimiwa Spika, Kuchelewakuanza kazi kwa Soko la TMX, Kamati inaona umuhimu wa kuanza kwa soko hili hasa ikizingatiwa kuwa uchumi wa Tanzania kwa kiasi kikubwa unategemea kilimo. Kamati ilibaini kuwa pamoja na Soko kuwa tayari kuanza mauzo ya mazao bado kuna haja ya Serikali kuwekeza rasilimali fedha za kutosha pamoja na rasilimali watu ambao ni wabobezi katika tasnia hii. Kamati iliishauri Serikali kuhakikisha kwamba soko hili linaanza kufanya kazi kikamilifu kwa faida ya Taifa.

10.1.3 Uwekezaji wa Serikali kwenye Mashirika ya Umma

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba pamoja nakuwa Serikali imefanya uwekezaji mkubwa kwenye baadhi ya mashirika ya umma kupitia miradi ya kimkakati iliyopo chini ya mashirika hayo, bado uwekezaji huo hauonekani kwenye mali za mashirika hayo. Baadhi ya miradi hiyo ni kama vile Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano chini ya TTCL na mradi wa bomba la gesi kuja Dar es salaam ulioko chini ya TPDC. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa mali hizo zinaingizwa kwenye umiliki wa Mashirika husika ili kuondokana na changamoto ya mitaji kwa mashirika hayo na hivyo kuyawezesha mashirika hayo kuweza kukopa katika taasisi za kifedha kwa kutumia thamani ya mali za mashirika.

10.1.4 Faida ya uwekezaji wa Serikali

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuwekeza kwa kiasi kikubwa katika Mashirika ya Umma na Taasisi mbalimbali. Aidha, Kamati inaona Serikali bado haijafaidika kwa kiasi kikubwa kutokana na uwekezaji unaofanyika kwenye baadhi ya Mashirika na Taasisi za Umma. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa thamani ya gawio inayotokana na uwekezaji wake uendane na thamani ya mtaji uliyowekezwa katika Taasisi na Mashirika ya Umma ili uwekezaji huo uongeze mapato zaidi kwa Serikali.

10.1.5 Kuhuisha Mfumo wa Usimamizi wa Forodha

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imebaini kwamba kuna tofauti ya mfumo unaotumiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania inatumia mfumo wa TANCIS wakati nchi jirani zinazohudumiwa na bandari ya DSM bado wanatumia mfumo wa ASCUDA+++ hivyo kupelekea mifumo kutokusomana na kusababisha ucheleweshaji wa mizigo hasa mipakani. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba mfumo wetu wa TANCIS unaunganishwa na mifumo ya nchi jirani ili kuharakisha biashara ya mizigo mipakani.

10.1.6 Akaunti Jumuiifu ya Fedha (TSA)

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembela Benki Kuu ya Tanzania tawi la Arusha na Ofisi ya Halmshauri ya Jiji la Arusha ilikujionea utekelezaji wa Mfumo wa Akaunti Jumuiifu wa TSA. Mfumo ulilalamikiwa na changamoto moja kubwa ya kutokuwepo kwa mtandao (network) wa uhakika ambapo mtandao unakuwa unakata kabisa kiasi cha kupelekea malipo kutofanyika kwa wakati. Changamoto hiyo ilibainika kusababishwa na udogo wa *bandwidth* kwa kuwa Servers za mifumo yote zinasimamiwa na kuhifadhiwa katika ofisi za TAMISEMI - Dodoma na hivyo kupelekea kulemewa. Kufuatia hili, Kamati ilielekeza Wizara ya Fedha pamoja na TAMISEMI

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kukaa pamoja na kuona ni jinsi gani wanaweza kutatua changamoto hii na kuimarisha mtandao ili kuwezesha mfumo huu kufanya kazi kwa ufanisi zaidi. Aidha, ilipendekezwa servers hizo ziwepo kikanda kwa ajili ya kuleta ufanisi zaidi.

11.0. MAFUNZO KWA KAMATI

Mheshimiwa Spika, katika kipindi husika ilipata fursa ya kupata mafunzo mbalimbali yaliyolenga kuwajengea uwezo. Ofisi ya Bunge kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango na Taasisi zake ziliratibu mafunzo hayo pamoja na mafunzo yanayoratibiwa na programu za Miradi ya LSP II na PFMRP. Mafunzo hayo yaliwasaidia Wajumbe wa Kamati katika kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kusimamia Bajeti ya Serikali na hatimaye kuweza kushauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, mafunzo hayo yalikuwa ni pamoja na:-

i. Mwongozo wa Uchambuzi wa Bajeti na namna Serikali inavyokokotoa makisio ya ukuaji wa uchumi nchini;

ii. Kupitishwa katika kanuni za Usimamizi wa Sekta Ndogo ya Fedha;

iii. Kupitishwa katika mfumo wa ukadiriaji wa masuala mbalimbali ya uchumi Jumla (Financial Programing);

iv. Usimamizi wa Mashirika ya Umma;

v. Mfumo wa uondoshwaji wa mizigo bandarini – TANCIS;

vi. Kupitishwa katika Sheria mbalimbali zikiwemo Sheria ya Kodi ya Mapato, Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Sura 147 (The Excise (Management and Tariff) Act, Cap 147), Sheria ya Umoja wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (East African Community Customs Management Act, 2004) na Protokali ya Umoja wa Forodha ya Afrika Mashariki (*The East African Customs Union Protocol, 2004*).

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilipata fursa ya kutembela nchi za Uganda na Rwanda ambapo ilikwenda kujifunza namna nchi hizo zinaendesha Mfumo wa Akaunti Jumuiya baada ya kuanza kutumika nchini.

12.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA JUMLA

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Serikali pamoja na utekelezaji wa majukumu ya Kamati, Kamati ina maoni na mapendekezo ya ujumla yafuatayo:-

12.1. Utekelezaji wa Sheria ya Mawasiliano na Kielektroniki (EPOCA).

Mheshimiwa Spika, Marekebisho yaliyofanyika kwenye Sheria ya EPOCA mwaka 2017, yalielekeza kampuni zote za simu kujiorodhesha kwenye soko la hisa na kuuza **asilimia ishirini na tano (25%)** ya hisa zake kwa umma na hatimaye kampuni hizo kuorodheshwa kwenye soko la hisa la Dar es salaam. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa kati ya kampuni zote za simu ni kampuni ya Vodacom tu ambayo imeweza kuingia kwenye soko. Pamoja na kuwa Vodacom wameingia sokoni sio hisa zote ambazo zimeweza kununuliwa na inalamikiwa kutoa gawio dogo lakini pia kushuka kwa thamani ya hisa za kampuni hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kampuni za simu ambazo bado hazijaorodheshwa kwenye soko la Hisa la Dar es salaam waweze kufanya hivyo ili Watanzania waweze kushiriki katika uwekezaji kwenye sekta ya mawasiliani kama sheria inavyotoka.

12.2. Sekta ya Ngozi

Mheshimiwa Spika, wakati wa kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 Kamati ilipokea Taarifa kutoka kwa wafanyabiashara wa ngozi kuhusu kuhusu mlundikano wa ngozi katika maghala uliosababishwa na viwango vya ushuru wa mauzo nje yaani export levy ya **asilimia 10** kwa ngozi zilizosindikwa hadi hatua ya wet blue na **asilimia 80** kwa ngozi ghafi, viwango ambavyo vilipelekea ngozi kukosa soko. Hivyo, Serikali iliahidi kulifanyia utafiti suala hilo na kuwasilisha Taarifa kwenye Kamati.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ya tafiti uliofanywa na Serikali yalibaini kuwepo na mlundikano wa ngozi katika maghala ambayo yalifanywa utafiti katika mikoa ya Dar es salaam, Pwani, Mwanza na Kilimanjaro. Aidha, taarifa ya tafiti haikuweza kubainisha endapo viwango vya tozo vya ushuru wa mauzo nje ya nchi kama vinaathiri biashara hiyo na hivyo kusababisha mlundikano. Hivyo basi, Kamati inaiagiza Wizara ya Viwanda na Biashara na Wizara ya Mifugo na Uvuvi wakishirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango kufanyia utafiti viwango hivyo vya ushuru na kuangalia ni namna gani zinaweza kuja na mikakati ya kusaidia na kuinua sekta hiyo ambayo ina manufaa makubwa ya kimapato kwenye uchumi wa nchi.

12.3. Minara ya Mawasiliano kwa Shirika la TTCL.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipotebembela kampuni ya simu ya TTCL ilibaini kwamba kampuni hiyo ina changamoto kubwa ya minara ya mawasiliano ambapo hivi sasa TTCL ina jumla ya **minara 485** tu kati ya **minara 14,000** iliyopo nchini. Aidha, kati ya minara hiyo ya TTCL, **minara 207** tu ndiyo inamilikiwa na Shirika na iliyobaki Shirika linapanga katika minara ya watoa huduma wengine wakiwemo kampuni ya *Helios Towers*, Airtel, Vodacom na Halotel. Kimsingi, idadi hiyo ya minara ni michache kwa Shirika kufikia lengo la kutoa huduma nchi nzima. Umiliki mdogo wa minara kwa shirika la umma una athari za kiulinzi na usalama kutokana na kazi muhimu zinazoendeshwa na Shirika. Hivyo basi, ili kuondokana na changamoto hii, Kamati inashauri Serikali kuiwezesha kifedha TTCL kulingana na mpango wake wa miaka 5 ili kuboresha miundombinu ya Shirika na hivyo kuwa shindani.

12.4. Kukosekanakwa Vifaa vya kupakua na kupakia mizigo Bandarini

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuna ukosefu wa vitendea kazi kama vile *cranes* na *conveyor belts* kwa Bandari ya Dar es salaam kwa ajili ya kushusha mizigo na kupakia na hivyo kurefusha muda wa kushusha na kupakia mizigo. Kamati inapendekeza maboresho yanayoendelea katika Bandari ya Dar es salaam yaende sanjari na upatikanaji wa vitendea kazi hivyo muhimu.

12.5. Changamoto ya Utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Miji na Majiji kutokana na Kodi ya Ongezeko la Thamani.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti katika uchambuzi wake imebaini kwamba kuna mikwamo katika utekelezaji wa Miradi ya Benki ya Dunia kwa baadhi ya Halmashauri za Miji. Mkwamo huo unatokana na Serikali kudai kodi ya ongezeko la thamani katika utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuleta kwa hati ya dharura mabadiliko ya Sheria ya VAT ili Bunge lako Tukufu liweze kufanya mabadiliko yatakayonusuru utekelezaji wa miradi hiyo.

12.6. Utaratibu wa uwasilishaji wa mapendekezo ya Mabadiliko ya Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, hii sio mara ya kwanza kwa kamati yako kuishauri Serikali kulishirikisha bunge juu ya mapendekezo yake yanayopelekwa katika jumuiya ya Afrika mashariki kabla hayajapitishwa. Ushauri huu unatokana na ukweli kwamba utaratibu wa kuyafanyia mabadiliko endapo Bunge halitaridhia ni mrefu na unachukua muda. Hivyo, Kamati inapendekeza mabadiliko hayo yawe yanawasilishwa Kamati ya Bajeti kwa niaba ya bunge ili kamati itoe maoni yake kabla hayajapelekwa katika jumuiya.

12.7. Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kujielekeze katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ili kuvutia Sekta binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Njia zinazoweza kutumika ni pamoja na kutoa udhamini kwa wakopaji wadogo (credit guarantee schemes) pamoja na kuongeza matumizi ya mikopo inayojidhamini yenyewe (lease finance) ili kuisaidia sekta hiyo kushiriki kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali ijielekeze katika kuondoa vikwazo vinavyozuia maendeleo ya viwanda nchini hasa vikwazo vya ushindani usio sawa baina ya viwanda vya ndani dhidi ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya nje, ufinyu wa mitaji ya kifedha, gharama kubwa za uzalishaji, uwepo wa miundombinu duni ya uzalishaji, mlolongo wa taratibu kuwa mrefu, sheria kubadilika mara kwa mara na uwepo wa uhusiano hafifu kati ya sekta ya viwanda na sekta nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali ikajielekeze katika kutatua vikwazo hivi pamoja na kuwa na mkakati maalumu wa kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa viwandani.

12.8. Mwenendo wa Viwango vya riba na Mfumuko wa Bei

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti katika nyakati tofauti tofauti imeitaarifu Serikali kuhusu viwango vya riba katika sekta ya benki kuwa vya juu kuliko uhalisia. Mfano hadi kufikia Novemba 2019 viwango vya riba vilikuwa **asilimia 16.87** ilihali mfumuko wa bei ulikuwa kwa **asilimia 3.8**. Ileweke wazi kwamba kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya mfumuko wa bei na viwango vya riba haitarajiwi kiuchumi viwango vya riba vizidi mfumuko wa bei kwa zaidi ya marambili. Hivyo, kamati inaishauri Serikali kuangalia gharama za uendeshaji wa mabanki ili kuhakikisha viwango vya riba vinaendana na mfumuko wa bei.

12.9. Ukusanyaji wa Kodi ya Majengo

Mheshimiwa Spika, makusanyo ya kodi ya majengo kwa Halmashauri zote katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2019, yalikuwa **shilingi bilioni 6.7** sawa na **asilimia 61.7** ya lengo la **bilioni 10.8** katika kipindi hicho. Kodi ya majengo haikufikia lengo kutokana na walipakodi wengi kupendelea kulipa kodi na tozo katika tarehe za mwisho wa mwaka (mwezi Juni). Kutokana na changamoto hiyo, Kamati inashauri Serikali kuangalia uwezekano wa kujumuisha makusanyo ya kodi ya majengo katika ankara za maji au umeme. Hatua hii itasaidia ukusanyaji wa kodi hiyo kila mwezi kwa gharama ndogo na kuondoa usumbufu kwa wananchi kutaka kulipa kodi hiyo kila mwisho wa mwaka.

13.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru kwanza wewe Mheshimiwa Spika pamoja na Naibu Spika kwa miongozo yenu ambayo mmekuwa mkiipatia Kamati na hivyo kuwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Pili, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip I. Mpango, Mb Waziri wa Fedha na Mipango na Dkt. Ashatu Kijaji, Mb Naibu Waziri kwa ushirikiano wao ambao wamekuwa wakitoa kwa Kamati katika kipindi chote cha vikao vya Kamati. Nawashukuru pia wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango ambao walishirikiana na Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii kwaumahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kutekeleza shughuli za Kamati. Aidha, nawapongeza kwa michango yao, maoni na ushauri ambayo imesaidia katika kuhakikisha kuwa Kamati inasimamia Serikali ipasavyo. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifauatavyo: -

1. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb – Makamu Mwenyekiti

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

2. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
3. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
4. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
5. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
6. Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb
7. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb
8. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb
9. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
10. Mhe. Hasna Sudi Katunda Mwilima, Mb
11. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
12. Mhe. Balozi Adadi Mohamed Rajab, Mb
13. Mhe. Abdallah Majurah Bulembo, Mb
14. Mhe. Prof. Anna Kajumulo Tibaijuka, Mb
15. Mhe. Stephen Julius Masele, Mb
16. Mhe. Ali Hassan Omar, Mb
17. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
18. Mhe. Dkt. Dalaly Peter Kafumu, Mb
19. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
20. Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb
21. Mhe. Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala, Mb
22. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb
23. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb
24. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
25. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb
26. Mhe. Suleiman Ahmed Saddiq, Mb

Mheshimiwa Spika, mwisho napenda kutumia fursa hii kumshukuru Ndg. Stephen Kagaigai, Katibu wa Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati katika kipindi chote. Pamoja na yeye, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati ya Bajeti kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu sasa lipokee na kujadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

Mashimba M. Ndaki, Mb
M/MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA BAJETI
30 Januari, 2020

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mashimba Ndaki. Hoja imeungwa mkono kwa taarifa hiyo nzuri ambayo imechambua mambo mengi. Sasa namkaribisha Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili aweze kuja kutoa taarifa ya mwaka ya shughuli. Mheshimiwa Raphael Chegeni, karibu.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI – MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa muda, naomba taarifa yote ya Kamati iingizwe kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (*PIC*) kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020 na kuliomba Bunge lako Tukufu kuipokea na kuijadili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma imetekeleza majukumu yake ya kufuatilia uwekezaji katika Mashirika na Taasisi za Umma na Kampuni ambayo Serikali ina hisa kwa mujibu wa Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa uwekezaji wa mitaji ya Umma ni jukumu la msingi la Kamati hii. Utekelezaji wa jukumu hili ni katika kuhakikisha kunakuwa na jicho la Bunge katika kuangalia uwekezaji wa mitaji ya Umma. Jumla ya thamani ya uwekezaji wa Serikali katika Taasisi 266 za ndani ya nchi na nje ya nchi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ulifikia shilingi trilioni 59.64.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa jumla uliofanywa na Serikali kwa Taasisi zinazotakiwa kutoa gawiwo na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni shilingi trilioni 11.72 na kufanya faida ya shilingi trilioni 1.05. Katika faida iliyopatikana Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 683.23 na kiasi kingine cha shilingi bilioni 370.59 ilitokana na tozo mbalimbali zilizopelekwa moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Juni 30, 2019 Serikali imefanya uwekezaji wa shilingi bilioni 681.38 katika mashirika 10 yaliyo nje ya nchi kama inavyoonekana katika taarifa ya Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa taarifa zilizowasilishwa na Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma ili kubaini iwapo dhima ya Serikali kuwekeza katika Taasisi hizo inatimizwa. Kamati ilifanya uchambuzi na kubaini mambo yafuatayo:-

(i) Gharama kubwa za uendeshaji wa mashirika na Taasisi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya dhumuni la Serikali la kufanya uwekezaji ni kukusanya mapato yasiyo ya kodi kwa njia ya faida na gawio na michango katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, dhumuni hilo halitekelezwi kwenye baadhi ya Taasisi za Umma kutokana na taasisi hizo kuwa na gharama kubwa za uendeshaji kinyume na Sheria ya Fedha Na. 16 ya mwaka 2015. Matumizi makubwa hasa yasiyoendana na jukumu la msingi yanasababisha taasisi hizo kukosa faida na kushindwa kutoa gawio Serikalini.

(ii) Miradi kutokamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Taasisi za Umma zimekumbwa na tatizo kubwa la kushindwa kukamilisha miradi yake kwa wakati uliopangwa hali inayochelewesha kupatikana kwa faida inayotokana na uwekezaji katika miradi hiyo na kukosekana kwa ufanisi na tija ya utekelezaji wa miradi hiyo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

(iii) Kupungua kwa mitaji katika Taasisi za Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua dhamira njema ya Serikali ya kuwekeza katika Taasisi zake kwa kuzipatia mitaji na namna mbalimbali. Kamati inaishauri Serikali kutumia dhamira hiyo njema kwa taasisi nyingine za Umma kama Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) kwa kutaja baadhi ili taasisi hizo ziweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuzalisha mapato ya kutosha kwa ajili ya Taifa letu. Kukosekana kwa mitaji kunasababisha ongezeko la matumizi ya shirika lisiloendana na mapato, shirika kushindwa kulipa madeni yake na kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati.

(iv) Kuongezeka kwa Madeni (*Payables and Receivables*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji mzuri wa Taasisi za Umma unapimwa pia kwa uwezo wa Taasisi hiyo kukusanya madeni inayodai (*receivables*) na kulipa madeni inayodaiwa (*payables*). Kutokufanya vizuri kwa kigezo hicho kunaweza kuondoa ufanisi wa kiutendaji. Katika uchambuzi wetu Kamati imebaini kuwa Taasisi nyingi zimekuwa na tatizo la kukosa mbinu mbadala na mikakati madhubuti ya kukusanya madeni (*receivables*) ili kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kuwa na mlundikano wa madeni kutokana na kutolipa madeni inayodaiwa (*payables*).

(v) Kukosekana kwa ufanisi katika kampuni za ubia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuongeza mapato katika Taasisi za Umma kuna baadhi ya Taasisi za Umma zimepewa kibali cha kufanya uwekezaji kwa ubia na kampuni nyingine ambazo siyo za Umma. Kamati ilipata nafasi ya kuchambua taarifa ya *TR* kuhusu ufanisi wa mitaji na hisa za shirika la Utangazaji *TBC* katika uwekezaji wake na urushaji wa matangazo kidigitali katika kampuni ya *STAR Media Limited*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imebaini utendaji usioridhisha; naomba nirudie, Kamati imebaini utendaji usioridhisha wa kampuni ya *STAR Media Tanzania Limited* kwa kuwa imekuwa ikipata hasara tangu kuanzishwa kwake mwaka 2009. Kampuni ilitarajiwa kuanza kuzalisha faida na kutoa gawio Serikalini kwa wana hisa wake ifikapo mwaka 2014. Hata hivyo, taarifa ya fedha ya mwaka 2014 inaonesha hasara ya dola milioni 8.6, wakati mwaka 2013 hasara ilikuwa dola za Kimarekani milioni 626.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya taarifa ya fedha za Kampuni ya Ubia kwa mwaka 2014 kuonesha hasara kubwa badala ya faida ilivyotarajiwa, uongozi wa *TBC* ulimtaka *CAG* kufanya ukaguzi maalum kwa hesabu za *STAR Media Tanzania Limited*. Kutokana na ukaguzi huo *CAG* aligundua maeneo 34 yenye matatizo katika utendaji wa kazi wa kampuni ya *STAR Media Tanzania Limited*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wote ulioainishwa katika *report* ya *CAG* kuhusu utendaji usioridhisha na Kampuni ya Ubia, ni kielelezo tosha kuwa Serikali ina jukumu la kuingilia kati ili kupata suluhu ya jambo hilo kwa haraka iwezekanavyo.

(vi) Sheria za Taasisi kupitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi wa taarifa za uwekezaji za Taasisi za Umma, Kamati imebaini kuwa zipo taasisi zina miradi na shughuli nyingi zenye fursa kubwa ya kuchangia katika uchumi wa Taifa na ustawi wa nchi. Hata hivyo, taasisi hizo zinashindwa kutekeleza majukumu yao kulingana na mazingira ya sasa ya kibiashara katika sheria zilizoanzishwa na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

taasisi hizo kuwa ni za muda mrefu sana na taasisi kukosa nguvu za kisheria katika kutekeleza majukumu yake.

(vii) Kukosekana kwa miundombinu muhimu katika maeneo ya miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Umma zimekuwa zikitekeleza majukumu mbalimbali kutokana na dhumuni la kuanzisha taasisi hizo. zipo baadhi ya Taasisi za Umma ambazo jukumu lake ni kuwekeza katika ujenzi wa miradi mbalimbali kama nyumba za makazi na biashara. Uwekezaji huo unaendana sambamba na ujenzi wa miundombinu wezeshi katika maeneo ya miradi kama maji, umeme na barabara. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya kukosekana kwa miundombinu hiyo muhimu katika maeneo ya miradi hali iliyosababisha kuognezeka gharama za miradi na athari hiyo unakutana nayo katika mnunuzi wa mwisho.

(viii) Watendaji wa Taasisi kukoa Mamlaka kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utendaji wa shughuli za kila siku za Taasisi mara nyingi maamuzi sahihi hufanywa na mtu mwenye mamlaka kamili. Utekezaji wa majukumu ya Taasisi za Umma wenye ufanisi na weledi kwa kiasi kikubwa unategemea uwepo wa watumishi wenye mamlaka kamili ya kutekeleza majukumu hayo. Hata hivyo, kumekuwa na watumishi na baadhi ya Taasisi ambazo wamekuwa wakikaimu katika nafasi walizonazo zaidi ya miezi 30.

(ix) Serikali kuchelewa kulipa madeni kwa Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na desturi kwa Serikali na Taasisi zake kutokulipa madeni yanayotokana na kupata huduma kutoka kwa taasisi nyingine za Serikali hali inayopunguza mapato ya Taasisi zinazotoa huduma hiyo.

(x) Uwekezaji wa Serikali katika kampuni ambazo ina umiliki wa asilimia 50 na pungufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee na kwa niaba Kamati naomba kutoa shukurani za dhati kwako kwa kuona umuhimu wa Kamati hii kukutana na ku-share na taasisi ambazo Mheshimiwa Spika aliona umuhimu wake na Serikali ambayo imeridhia suala hilo ilikuwa na umiliki wa hisa chache (*minority shares*). Lengo la kukutana na taasisi hizi ilikuwa ni kupokea taarifa za uwekezaji unaofanywa na Serikali pamoja na changamoto zinazokabiliana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa inayokabiliana nayo ni ucheleweshaji wa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT refund*), kuathirika kwa soko la wazalishaji wa bidhaa nchini, taasisi kutolipa madeni yake (*overdue payments*), changamoto za kisheria, baadhi ya taasisi kujiendesha kwa hasara na kuchelewa kwa upanuzi ya miradi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, PIC ni Kamati mpya katika Bunge la Kumi na Moja na ni jicho la Bunge katika kuangalia uwekezaji wa mitaji ya Umma. Aidha, taarifa hii ni ya mwisho kuwasilishwa katika Bunge lako la Kumi na Moja. Saa hizi ni saa 11.00 jioni, kwa hiyo, ndiyo taarifa ya mwisho hii. Katika utekezaji wa majukumu yake tangu kuundwa kwa Kamati hii, changamoto nyingi za kiutendaji katika Taasisi za Umma zilibainika na mafanikio mbalimbali yamepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya changamoto zilizobainika ambazo kwa kiasi kikubwa zimefanyiwa kazi na Serikali ni pamoja na utoaji wa gawiwo na uchangiaji katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Upungufu wa mitaji, utegemezi mkuu wa ruzuku ya Serikali, kuchelewa kwa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uteuzi wa Bodi za Wakurugenzi, matumizi makubwa yasiyohusiana na uwekezaji, uwekezaji usiokuwa na tija, Serikali kutolipa madeni yake, utendaji wa taasisi usioridhisha, mikataba isiyokuwa na tija na Taasisi za Umma kutomtambua Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutoa mfano, Kamati ilisitiza Serikali kusimamia Taasisi zake na kuhakikisha zinatoa gawio Serikalini pamoja na michango yote. Mafanikio ya ufuatiliaji huo yameonekana ambapo katika mwaka wa fedha 2018/2019, Serikali ilipokea gawiwo na michango katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa jumla ya shilingi trilioni 1.05, ukilinganisha na gawiwo la shilingi bilioni 422.96 iliyopo katika mwaka wa fedha 2015//2016, sawa na ongezeko la asilimia 149, yaani ndani ya miaka minne tumepata mafanikio haya. Aidha, mafanikio haya na shukrani nyingi ziende kwa Bunge lako Tukufu kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi ya kipekee, Kamati inapenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kuhakikisha kuwa kunakuwa na usimamizi bora katika Taasisi na mashirika ya Umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika utoaji wa gawiwo pamoja na uchangiaji katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Kamati inampongeza sana Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Dkt. Philipo Mpango na timu yake yote akiwemo Katibu Mkuu, Bwana Doto James pamoja na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa kuwa msaada mkubwa sana kwa Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati inamshukuru kwa kufanya maamuzi Mheshimiwa Rais ya kuteua Wakuu wa Taasisi pamoja na Wenyeviti wa Bodi kwa wakati. Aidha, Kamati inazipongeza taasisi zote zilizotoa gawiwo na michango kwa Mfuko Mkuu wa Serikali kwa wakati. Kuna waliotoa kwa wakati na wengine kwa kulazimishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kumpongeza Msajili wa Hazina, hii ni pasipo shaka, Ndugu Athumani Mbutuka na wafanyakazi wote wa Ofisi yake kwa kusikia kilio cha Kamati cha muda mrefu cha kukosekana kwa Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina. Kwa mara ya kwanza naliambia Bunge lako Tukufu kwamba historia imeandikwa kwa Msajili wa Hazina kuandika taarifa ya mwaka na kuiwasilisha kwa Kamati. Pongezi nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati iliwasilisha taarifa yake ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kuanzia Februari, 2018 hadi 2019 mbele ya Bunge lako Tukufu. Taarifa hiyo ilijumuisha maoni na mapendekezo ya Kamati ambayo yalikuwa na maazimio ya Bunge na kwenda kufanyiwa kazi na Serikali kuongeza tija na ufanisi katika Taasisi za Umma. Aidha, Kamati imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa maazimio 12 yaliyotolewa kwa kupitia kwa *Treasury Registrar (TR)*, ambaye ndiye Msimamizi Mkuu wa Taasisi za Umma kwa niaba ya Serikali. Hata hivyo, kati ya maazimio hayo, ni maazimio saba tu ndiyo yamefanyiwa kazi na maazimio matano yaliyotolewa na Bunge hayajatekelezwa kikamilifu na Serikali kama ilivyoainishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maoni ya jumla ya Kamati yaliyotokana na uchambuzi wa mitaji ya Umma naomba kutoa mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

(i) Gharama Kubwa za Uendeshaji.

KWA KUWA, baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yamebainika kuwa na gharama kubwa za uendeshaji kinyume na Sheria ya Fedha Na. 16 ya 2015 Kifungu cha 46 (10) (a)(1);

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

NA KWA KUWA, Uwepo wa gharama hizo kubwa zinazifanya taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu, sambamba na kushindwa kutoa gawio au kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali;

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina ihakikishe Taasisi na Mashirika yote ya Umma yanazingatia matakwa ya Sheria ya Fedha Na. 16 ya 2015 pamoja na Miongozo yote inayotolewa na Msajili wa Hazina. Aidha, sheria hii ipitiwe kwa kuweka kipengele kitakachoitaka Bodi na Menejimenti kuachia madaraka. Naomba nirudie; aidha, sheria hii ipitiwe kwa kuweka kipengele kitakachoitaka Bodi na Menejimenti kuachia madaraka, endapo watakwenda kinyume na matakwa ya sheria hii.

(ii) Miradi Kutokamilika kwa Wakati.

KWA KUWA, baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yamekuwa yakitekeleza miradi mingi ya uwekezaji kwa muda mrefu na miradi hiyo kutokamilika kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali kama ufinyu wa mtaji, mikataba isiyokuwa na tija na kukosekana kwa utawala bora katika utekelezaji wa miradi hiyo;

NA KWA KUWA, kushindwa kukamilika kwa miradi hiyo kunaongeza gharama za miradi na kukosekana kwa tija ya uanzishwaji wa miradi hiyo;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuhakikisha changamoto zote zilizopo katika miradi yote zinaondolewa haraka iwezekanavyo na miradi yote iliyosimama inakamilishwa ili tija ya uwekezaji huo ipatikane na waliosababisha hasara wawajibishwe.

(iii) Kupungua kwa Mtaji katika Taasisi za Umma.

KWA KUWA, baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yamekuwa na changamoto kubwa kiutendaji inayosababishwa na kukosekana kwa mtaji likiwemo Shirika la Madini la Taifa (STAMICO);

NA KWA KUWA, kukosekana kwa mtaji kumesababisha ongezeko la matumizi ya shirika yasiyoendana na mapato, Shirika kushindwa kulipa madeni yake na kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kulifufua shirika hili kwa kuondoa changamoto zote zilizopo kwa kuliongezea mtaji, kukamilisha uhamisho wa umiliki ili kulipa shirika uhalali wa kumiliki na kusimamia miradi iliyokabidhiwa na kuliondolea shirika madeni makubwa yaliyorithiwa. Aidha, Serikali ipeleke mtaji kwa Taasisi zote za Umma zinazostahili na zenye changamoto kama hiyo, mojawapo ni *Air Tanzania*.

(iv) Kuongezeka kwa Madeni.

KWA KUWA, taasisi nyingi zimekosa ufanisi katika kigezo cha madeni ya kudai na kudaiwa, kwa kuwa na tatizo la kukosa mbinu mbadala na mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa madeni (*receivables*) pamoja na kuwa na malimbikizo ya madeni (*payables*);

NA KWA KUWA, kutofanya vizuri kwa kigezo hicho kunazorotesha utendaji wa Taasisi na Mashirika hayo na kupunguza mapato ya Serikali;

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuandaa miongozo maalum kwa Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika itakayoainisha madhara yatakayopatikana kutokana na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kushindwa kubuni mikakati madhubuti ya ukusanyaji na ulipaji wa madeni na itakayowajibisha watendaji watakaokiuka miongozo hiyo.

(v) Kukosekana kwa Ufanisi katika Kampuni za Ubia.

KWA KUWA, Kampuni ya Ubia ya *Star Media Tanzania Ltd* imebainika kuwa na upungufu mkubwa na zaidi katika utendaji kama Kampuni ya Ubia kupata hasara mfululizo, mtaji wa Kampuni ya Ubia kupungua, uwezo mdogo wa kampuni kulipa madeni pamoja na Mbia Mwenza, *Star Communication Technologies Company Ltd* kugoma kutekeleza hoja zilizotolewa na CAG;

NA KWA KUWA, kutorekebishwa kwa upungufu huo kwa muda mrefu kumesababisha Kampuni ya *Star Media Tanzania Ltd* kushindwa kutoa gawio kwa wanahisa wake akiwemo Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC);

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali, ihakikishe inafanyia kazi hoja zote zilizotolewa na CAG ikiwa ni pamoja na kusimamia kwa ukaribu na kuondoa upungufu wote uliopo pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria watu wote waliochangia utendaji mbovu wa Kampuni ya *Star Media Tanzania Ltd* na kuona kama kuna haja ya kuendelea na ubia huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, Sheria za Taasisi kupitwa na wakati:-

KWA KUWA, kumekuwa na baadhi ya taasisi na mashirika ya umma ambayo sheria zake zimepitwa na wakati.

NA KWA KUWA, ni muda mrefu sana na nyingine kukosa nguvu ya kisheria kutekeleza majukumu yake.

NA KWA KUWA, uwepo wa sheria zilizopitwa na wakati zinasababisha taasisi na mashirika hayo kushindwa kutekeleza majukumu yake kulingana na mazingira ya sasa ya kiushindani na ya kibiashara.

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuwa, ilete Bungeni mapendekezo ya mabadiliko ya sheria; kwa mfano TAWA na Shirika la Masoko ya Kariakoo, kwa hiyo, sheria zote zinazopitwa na wakati, ili taasisi na mashirika ya umma yatekeleze majukumu yake kwa ufanisi na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, kukosekana kwa Miundombinu Muhimu Katika Maeneo ya Miradi:-

KWA KUWA, maeneo mengi ya miradi ya nyumba inayotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) na Kampuni ya *watumishi Housing* yamekosa miundombinu ya maji, umeme na barabara.

NA KWA KUWA, kukosekana kwa miundombinu hiyo muhimu kumesababisha ongezeko kubwa la gharama za uwekezaji kwa taasisi zinazohusika na miradi hiyo, hasa nyumba za gharama nafuu na kuhamisha mzigo huo wa gharama kwa mnunuzi wa mwisho.

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kushughulikia masuala yote ya kisera kuhusu upelekaji wa miundombinu muhimu kufanyika kabla ya mradi kuanza, ili kuleta unafuu wa bei za nyumba kwa mlaji na mwisho kupunguza mzigo wa gharama kwa taasisi zinazohusika na miradi hiyo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Vilevile kuwe na makubaliano na mipango ya pamoja juu ya ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme na barabara katika maeneo ya mradi kabla ya kuanza kwa mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, Watendaji wa Taasisi Kukosa Mamlaka Kamili:-

KWA KUWA, kumekuwa na tabia kwa Bodi za Wakurugenzi na Taasisi za Mashirika ya Umma kuwaacha watendaji wao wakikaimu nafasi walizonazo kwa muda mrefu bila kuwathibitisha au kutafuta mtu mwingine wa kujaza nafasi hizo na kuwafanya watumishi hao kutokuwa na mamlaka kamili.

NA KWA KUWA, kutokana na mamlaka kamili kutokuwa na mamlaka kamili katika nafasi zao kunachangia utendaji kazi usioridhisha, kutojamini katika utoaji wa maamuzi na muda mwingine kufanya maamuzi yasiyo sahihi na kupunguza morali ya kazi.

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kupitia Bodi za Wakurugenzi za Taasisi na Mashirika machache yenye changamoto hiyo kuhakikisha watumishi wao ambao wanakaimu na wana uwezo mkubwa na wenye sifa stahiki na weledi katika utendaji kazi wao wanathibitishwa katika nafasi zao, ili waweze kuwa na mamlaka kamili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, Taasisi za Serikali Kutolipa Madeni yake kwa wakati:-

KWA KUWA Serikali na taasisi zake imekuwa na desturi ya kutolipa madeni yake yanayotokana na kupata huduma kutoka katika taasisi nyingine za Serikali na kunakuwa na mlundikano wa madeni hayo yasiyolipika.

NA KWA KUWA, tatizo hilo limekuwa likichangia kushindwa utekelezaji wa miradi ya taasisi zinazodai kutokana na kukosekana kwa fedha za kutosha za kuendesha miradi hiyo.

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kupitia Msajili wa Hazina kuendelea kuzikutanisha taasisi zilizobaki zinazodaiwa na kusimamia ili kuhakikisha madeni yote yanalipwa na kila taasisi inapata inachostahili shughuli za msingi za taasisi hizo ziweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, kumshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu makini uliowezesha kuwasilisha taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, Kamati imeweza kutekeleza majukumu yake kutokana na maelekezo ya Kiti chako, ikiwa ni pamoja na ushauri wa msaada kipindi chote cha kutekeleza majukumu ya shughuli za Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora katika taasisi na mashirika ya umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika utoaji wa magawio na mchango Serikalini.

Vilevile napenda kumshukuru Msajili wa Hazina, Ndugu Athuman Selemani Mbutuka, kwa ushirikiano wake wa dhati alioutoa kwa Kamati kwa kushauri namna bora ya kuzifanya taasisi za mashirika ya umma kuwa na ufanisi katika utendaji na uelekezaji wake kwa kuleta tija kwa Taifa. Aidha, ili kukamilisha dhima ya Serikali kufanya uwekezaji katika mitaji ya umma.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ambao wamekuwa wakishirikiana kwa karibu na Kamati katika kuhakikisha tunakuwa na usimamizi madhubuti wa taasisi na mashirika ya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Kamati hii imebahatika ina ma-Ester watano kati ya ma-Ester sita katika Bunge lako, ni faraja kwa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya Kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Majina yote yameorodheshwa katika taarifa hii naomba yasomeke yalivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru vilevile Katibu wa Bunge, Ndugu yetu Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano wa hali ya juu alioutoa ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri stahiki na kuiwezesha Kamati kutimiza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati. Shukrani kwa Idara ya Kamati ya Bunge kwa kuratibu vema shughuli za Kamati chini ya Mkurugenzi Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati; kwa kweli, wamefanya kazi kubwa sana Ndugu Amina Salum na Ndugu Elieka Saanya na msaidizi wa Kamati Delabose Pauline Mavunde.

Pia, tunawashukuru watumishi kutoka Ofisi ya Mshauri wa Mambo ya Sheria ya Bunge, Ndugu Seraphine Tamba na Ndugu Matamus Fungo pamoja na Idara yote ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa ushirikiano wao mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ni matokeo ya uchambuzi wa kina kuhusu uwekezaji wa mitaji ya umma uliofanywa na taasisi na mashirika ya umma. Maoni na mapendekezo yanatokana na uchambuzi uliofanywa na kamati ni kwa lengo la kuishauri Serikali katika eneo la uwekezaji wa mitaji ya umma, ili uwekezaji huo ulete tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma Kuhusu Uchambuzi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma na Kujadili, ikiwa ni pamoja na Maoni na Mapendekezo, ili hatimaye Serikali iifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA (PIC) KWA KIPINDI CHA KUENZIA FEBRUARI, 2019 HADI JANUARI, 2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

(Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016)

SEHEMU YA KWANZA

MAELEZO YA JUMLA

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya mwaka ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020 na kuliomba Bunge lako Tukufu kuipokea na kujadili.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma imetekeleza majukumu yake ya kufuatilia uwekezaji katika Mashirika na Taasisi za Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa.

1.1 Majukumu ya Kamati

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ina majukumu yafuatayo: -

a) Kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na Sheria na miongozo mujarabu ya biashara; na

b) Kuchambua na kujadili Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina na Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa.

Mheshimiwa Spika, Katika kutekeleza majukumu yake ya kikanuni, Kamati pia imefanya kazi zake kwa kuzingatia miongozo mingine kama ifuatayo: -

i) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

ii) Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011;

iii) Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001;

iv) Sheria ya Msajili wa Hazina Sura ya 370;

v) Sheria ya Mashirika ya Umma ya Mwaka 1992; na

vi) Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015

1.2 Shughuli zilizotekelezwa

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka mmoja kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa njia ya kufanya vikao kwa kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Taasisi na Mashirika ya Umma kuhusu uwekezaji unaotekelezwa na Taasisi hizo. Aidha, Kamati imefanya ziara katika baadhi ya Taasisi za Umma ili kujiridhisha iwapo uwekezaji unaofanywa na Taasisi hizo una tija. Vile vile, Kamati ilipatiwa semina za mafunzo kuhusu namna bora ya utekelezaji wa majukumu ya Kamati na mambo ya kuzingatia katika uchambuzi na ukaguzi wa miradi ya uwekezaji wa mitaji ya Umma. Ufafanuzi kuhusu shughuli hizo ni kama ifuatavyo: -

a) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ilipokea, ilichambua na ilijadili Taarifa za Msajili wa Hazina kuhusu

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya umma yapatayo Kumi na Nane (18). Orodha ya Taasisi hizo ni kama ifuatavyo: -

- i) Shirika la Masoko ya Kariakoo (KMC);
- ii) Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF);
- iii) Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Tanga (Tanga Uwasa);
- iv) Shirika la Nyumbu;
- v) Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF);
- vi) Shirika la Nyumba la Taifa (NHC);
- vii) Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA);
- viii) Shirika la Bima la Taifa (NIC);
- ix) Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC);
- x) Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA);
- xi) Wakala wa barabara Tanzania (TANROADS);
- xii) Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT);
- xiii) Kampuni ya Watumishi Housing (WHC);
- xiv) Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC);
- xv) Mamlaka ya Wanyama Pori Tanzania (TAWA);
- xvi) Shirika la Madini la Taifa (STAMICO);
- xvii) Mamlaka Majisafi na Usafi wa Mazingira Mbeya (Mbeya Uwasa);
- xviii) Benki Kuu ya Tanzania (BOT);

Pamoja na jukumu hilo la kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma, Kamati pia ilipata fursa ya kupokea Taarifa ya Uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Kampuni ambazo ina umiliki wa Hisa Asilimia Hamsini na Pungufu.

Mheshimiwa Spika, Kwa namna ya kipekee Kamati inakushukuru kwa kuridhia maombi yetu na kutoa kibali ili Kamati iweze kuangalia ufanisi wa uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Taasisi na Makampuni ambayo ina umiliki wa Hisa wa Asilimia Hamsini na Pungufu. Orodha ya Makampuni ambayo yalifika mbele ya kamati ni kama ifuatavyo:-

- i) Kiwanda cha Sukari cha Kilombero;
- ii) Kiwanda cha Mabati cha Aluminium Africa (ALAF);

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

- iii) Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA);
- iv) Benki ya NMB;
- v) Chinese Tanzania Joint Shipping Company Ltd;
- vi) Airtel Tanzania Ltd; na
- vii) Tazama Pipelines Ltd

b) Ziara za Ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwezi Machi, 2019, Kamati ilifanya ziara za ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji inayotekelezwa na Taasisi na Mashirika ya umma yaliyopo katika Jiji la Dar es Salaam. Mantiki ya ukaguzi ni kuiwezesha Kamati kufanya tathmini ya ufanisi na tija ya uwekezaji unaofanywa na Taasisi hizo. Taasisi zilizotembelewa na kukaguliwa ni: -

- i) Shirika la Uzalishaji Mali JKT (SUMA JKT)
- ii) Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC)
- iii) Shirika la Ugavi wa Umeme (TANESCO)
- iv) Shirika la Reli Tanzania (TRC)
- v) Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL)
- vi) Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA)
- vii) Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA)

Aidha, miradi iliyotembelewa na Ufafanuzi wake inaonekana katika Kiambatisho Na. 01 cha Taarifa hii.

1.3 Muhtasari wa dosari zilizobainika katika uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maelezo ya kina kuhusu matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za uwekezaji wa mitaji ya Umma, naomba kulidokeza Bunge lako tukufu kwa muhtasari dosari kuu zilizobainika katika utaratibu wa uwekezaji wa mitaji ya Umma. Dosari hizo ni: -

- i) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kuwa na gharama kubwa za uendeshaji na kukiuka Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 Kifungu cha 46 (10) (A)(1) inayokataza kufanya matumizi yanayozidi Asilimia 60 ya mapato ghafi hali inayosababisha taasisi hizo kutobakiwa na ziada;
- ii) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma kukosa mtaji wa uendeshaji hali inayosababisha Taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi;
- iii) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kukosa watendaji wenye mamlaka kamili kwa kuwa watendaji hao wamekuwa wakikaimu nafasi zao kwa muda mrefu;
- iv) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yamekuwa na malimbikizo makubwa ya madeni kwa sababu ya kutolipa madeni hayo kwa wakati;

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

v) Baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yameshindwa kukamilisha miradi yake kwa wakati na kusababisha kuongezeka kwa gharama za miradi hiyo na kuiletea hasara Serikali.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA NA MATOKEO YAKE

2.1 Maelezo ya Jumla kuhusu uchambuzi wa Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina kuhusu uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Juni, 2019

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ni jukumu la msingi la Kamati hii kwa mujibu wa Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Utekelezaji wa Jukumu hilo ni katika kuhakikisha kunakuwa na jicho la Bunge katika kuangalia Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Ibara 63 (2), imelipa Bunge mamlaka ya kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika masuala mbalimbali kwa niaba ya wananchi. Kwa upande wa usimamizi wa Mitaji ya Umma, madaraka hayo yamekasimiwa kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma.

Mheshimiwa Spika, Ufuatiliaji wa uwekezaji wa Mitaji ya Umma umekuwa ukifanyika kwa njia mbalimbali zikiwemo uchambuzi wa Taarifa za Uwekezaji na ziara za ukaguzi wa Miradi ya Uwekezaji. Katika kipindi cha Januari, 2019 hadi Januari, 2020, uchambuzi wa Taarifa za uwekezaji uliofanywa na Kamati ulibainisha kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni 2019, Serikali ilifanya Uwekezaji katika jumla ya Taasisi, Mashirika ya Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa Mia Mbili Sitini na Sita (266) za ndani ya nchi na Taasisi Kumi (10) za nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya uwekezaji wa ndani katika jumla ya Taasisi na Mashirika **229** ambapo ina umiliki wa Hisa Asilimia 100 na Taasisi **37** ambapo ina umiliki wa Hisa pungufu ya Asilimia 100 na kufanya jumla ya Taasisi na Mashirika **266**. Jumla ya thamani ya uwekezaji wa Serikali katika Taasisi na Mashirika hayo kwa mwaka wa fedha 2018/19 ulifikia **Shilingi 59,642,392,933,444.70**

Mchanganuo wa umiliki unaoneshwa katika Jedwali Namba 1.


Jedwali Na. 1 Umiliki wa Hisa za Serikali

NA	KIASI CHA UMILIKI KATIKA ASILIMIA (%)	IDADI YA TAASISI
1.	100	229
2.	50+	1
3.	50	4
4.	Pungufu ya 50	32
5.	JUMLA	266

Chanzo: Taarifa ya TR 2018/2019

Picha halisi ya mchanganuo uliopo kwenye Jedwali Na. 01 inaonekana kupitia Chatu Duara Na. 01 ya Taarifa hii.

Chati Duara Na. 01: Picha halisi ya Mchanganuo wa umiliki wa Serikali katika Taasisi, Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa.



Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Msajili wa Hazina imebainisha kuwa, mpaka kufikia tarehe 30 Juni, 2019, Serikali imefanya uwekezaji wa jumla ya **Shilingi 58,869,917,771,206.40** katika jumla ya Taasisi na Mashirika 230 ambayo Serikali ina umiliki wa kuanzia Asilimia 51 mpaka 100. Vile vile, Serikali imewekeza jumla ya **Shilingi 772,475,162,238.27** katika Makampuni 36 ambayo umiliki wake wa hisa ni Asilimia 50 na pungufu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina ina jukumu la kukusanya mapato yasiyo ya kodi kutoka katika vyanzo mbalimbali kama Gawio kutoka katika Mashirika ya Umma na kampuni ambazo Serikali ina umiliki wa hisa chini ya Asilimia 51, Michango ya Asilimia 15 ya mapato ghafi kutoka katika Mashirika ya Umma yaliyoainishwa katika gazeti la Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Fedha, Asilimia 28 ya Mfuko wa kusimamia Mawasiliano ya simu (TTMS), Asilimia 70 ya ziada kutoka katika Mashirika ya Umma na rejesho la Riba na Mikopo iliyotolewa na Serikali kwa Mashirika na Taasisi za Umma.

Hata hivyo, baadhi ya Taasisi hususan za Elimu, Mifuko ya Hifadhi ya jamii, Afya, Kilimo na Utafiti hazitowi Gawio wala Mchango wa Asilimia 15 katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa muktadha huo, Serikali haipimi manufaa ya uwekezaji wake katika Taasisi hizo kwa kuangalia fedha taslimu zinazopatikana, na badala yake hupima manufaa yake kwa kuangalia huduma mbalimbali zinazotolewa na Taasisi hizo kwa jamii.

Kamati imeangalia na kuchambua thamani ya uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Taasisi na Mashirika ya Umma, pamoja na faida iliyopatikana ya uwekezaji huo (Return on Investment)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kulingana na mchanganuo wa makundi makuu matatu ya Taasisi na Mashirika ya Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa uliofanywa na Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, Kundi la kwanza ni Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo yanamilikiwa na Serikali kwa asilimia 100, yanafanya biashara na yanatakiwa kutoa gawio ambapo, hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2019, Serikali iliwekeza jumla ya **Shilingi 9,550,839,042,127/=** na kupata faida ya **Shilingi 688,834,076,897/=** kutokana na uwekezaji huo. Rejesho la Uwekezaji (Return on Investment) huo ni sawa na **Asilimia 7.21**.

Kundi la Pili ni Taasisi zisizofanya biashara na Mamlaka za Udhhibiti. Aidha, Taasisi hizi zinamilikiwa na Serikali kwa Asilimia 100 na zinatakiwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo, hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2019, Serikali iliwekeza jumla ya **Shilingi 1,474,022,643,084/=** na kupata faida ya **Shilingi 117,521,657,270/=**. Faida iliyopatikana kutokana na uwekezaji huo (Return on Investment) ni sawa na **Asilimia 7.97**.

Kwa ujumla, hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2019, uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo ina umiliki wa hisa Asilimia 100 na ambayo yanatakiwa kutoa gawio pamoja na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi 11,024,861,685,212/=** na faida iliyopatikana kutokana na uwekezaji huo ni **Shilingi 806,355,734,167/=** sawa rejesho (Return on Investment) la **Asilimia 7.31**.

Mheshimiwa Spika, kundi la tatu ni uwekezaji wa Serikali katika Taasisi ambazo ina umiliki wa hisa Asilimia 50 na pungufu. Kimsingi Taasisi hizi zinatakiwa kutoa gawio kwa Serikali kulingana na kiwango cha uwekezaji wa Serikali katika Taasisi hizo. Hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2019, Serikali iliwekeza jumla ya **Shilingi 696,302,589,025/=** na kupata faida (gawio) ya **Shilingi 46,226,706,531/=** sawa na **Asilimia 6.64** (Return on Investment).

Uwekezaji wa Jumla uliofanywa na Serikali kwa Taasisi zinazomilikiwa kwa asilimia 100 na zile zenye hisa asilimia 50 na pungufu na zinazotakiwa kutoa gawio na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni jumla ya **Shilingi 11,721,164,274,237/=** na kupata faida ya **Shilingi 1,053,816,218,154/=**. Kiasi cha faida kilichoingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ni **Shilingi Trilioni 1.05** ambapo kati ya hizo, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 683.23** na kiasi kingine cha **Shilingi Bilioni 370.59** iliyotokana na tozo ambayo haikupitia kwa Msajili wa Hazina ilipelekwa moja kwa moja katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina na kubaini kuwa, katika mapato yasiyo ya kodi yanayokusanywa na Serikali, Gawio linachangia asilimia kubwa ikilinganishwa na vyanzo vingine. Hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2019, Jumla ya **Shilingi Trilioni 1.05** zilikusanywa kutoka katika vyanzo mbalimbali. Aidha, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikusanya jumla ya **Shilingi Bilioni 683.23** ambapo, makusanyo yaliyotokana na Gawio yalikuwa ni **Shilingi Bilioni 402.66 (58.93%)**; Michango ya Asilimia 15 ya Mapato Ghafi ya Mashirika **Shilingi Bilioni 148.16 (21.69%)**; ziada na mapato mengineyo **Shilingi Bilioni 114.51 (16.76)**, Marejesho ya Mtambo wa TTMS **Shilingi Bilioni 16.61 (2.43%)**; na Marejesho ya Mikopo na Riba **Shilingi Bilioni 1.29 (0.19%)**. Ni wazi kuwa Gawio limechangia Asilimia kubwa (58.93) ya mapato yote ikifuatiwa na Michango ya asilimia 15 ya Mapato Ghafi ya Mashirika. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuchukua hatua za makusudi ili kuboresha chanzo hiki muhimu cha mapato. Mchanganuo wa ulipaji wa Gawio na Mchango katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa Taasisi, Mashirika ya Umma na Makampuni ambayo Serikali ina hisa unaonekana katika Kiambatisho Namba 2 cha Taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali pia imefanya uwekezaji katika Mashirika yaliyo nje ya Nchi. Uchambuzi wa Taarifa ya Msajili wa Hazina umeonesha kuwa, hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2019, thamani ya uwekezaji uliofanywa na Serikali katika Mashirika Kumi (10) yaliyopo nje ya Nchi

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

umefikia jumla ya **Shilingi 681,387,087,130.29**. Orodha ya Taasisi hizo pamoja na umiliki wa Serikali unaonekana katika jedwali Namba 2.


Jedwali Namba 2

NA.	JINA LA TAASISI	UMILIKI WA SERIKALI
1.	African Development Bank (ADB)	0.76%
2.	Shelter Afrique	0.52%
3.	East African Development Bank (EADB)	24.98%
4.	International Bank for Reconstruction and Development (IBRD)	0.06%
5.	International Development Association (IDA)	0.26%
6.	International Finance Corporation (IFC)	0.04%
7.	Multilateral Investment Guarantee Agency (MIGA)	0.22%
8.	PTA BANK (now Eastern and Southern African Trade and Development Bank (TDB))	8.36%
9.	African Reinsurance Corporation (Africa Re)	0.80%
10.	African Trade Insurance Agency (ATI)	8.37%

Chanzo: Taarifa ya TR 2018/19


Mheshimiwa Spika, Uwekezaji wa Serikali katika Taasisi na Mashirika ya Umma umeongezeka kwa **Asilimia 8** kutoka **Shilingi 55,178,297,752,577.60** katika mwaka wa fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2018 hadi kufikia **Shilingi 59,642,392,933,444.70** katika mwaka wa fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2019. Aidha, Uwekezaji huo umefanyika kwa Taasisi 260 ambazo zimeandaa Taarifa za hesabu. Ongezeko la uwekezaji uliofanywa na Serikali umetokana na Sehemu kubwa ya Taasisi na Mashirika ya Umma kuwasilisha Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa zinazotoa sura ya thamani halisi ya hisa na mitaji kwa sasa, Kuongezeka kwa hisa za baadhi ya Taasisi za kibiashara na mitaji ya baadhi ya Taasisi zisizo za kibiashara na ongezeko kubwa la fedha za hisa linalotokana na tathmini mpya ya hisa na mtaji. Uwekezaji wa Serikali umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka kwa wastani wa Asilimia 26. Mwenendo wa ukuaji wa uwekezaji kwa miaka Mitano umeoneshwa katika Chatii Namba 1.

Mwenendo wa Ukuaji wa Uwekezaji wa Serikali



Aidha, mwenendo wa ukuaji wa uwekezaji wa mitaji na faida kwa miaka Minne umeoneshwa katika Mchoro (Graph) Namba 1.

Mchoro (Graph) Na. 01: Sura ya ongezeko la thamani ya uwekezaji na faida kwa mwaka 2015/16, 2016/17, 2017/18 na 2018/19



2.2 Uchambuzi wa Uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Uwekezaji katika Mashirika na Taasisi za Umma ni uwekezaji au utumiaji wa rasilimali za Umma katika kujenga Miundombinu ya Msingi (Physical Infrastructure) kama vile Miundombinu ya Usafirishaji, Nishati, Maji, Umwagiliaji, Afya, Elimu n.k. ambapo ukamilikaji wake hugeuka kuwa Mtaji wa Serikali kwa Shirika au Taasisi itakayosimamia na kuendeleza Miundombinu hiyo. Hata hivyo, Kwa mujibu wa Kifungu (2) cha Sheria ya Msajili wa Hazina Sura 370; Uwekezaji katika Mashirika ya Umma umetafsiriwa kuwa ni Mtaji wa Serikali katika Mashirika kwa njia ya Hisa, Mikopo, Fedha Taslim, Hati Fungani na Majengo yaliyowekwa moja kwa moja katika Shirika, Kampuni au Taasisi ya Umma.

Aidha, dhima ya Serikali kuwekeza katika Mashirika ya Umma ni kukuza Uchumi wa Nchi kwa madhumuni ya Kupata mapato kwa njia ya faida/gawio, kusogeza na kutoa huduma kwa urahisi kwa jamii na kuchochea maendeleo ya sekta mbalimbali za uchumi, kudhibiti utoaji wa huduma na kulinda maslahi ya jamii (Wazalishaji na Watumiaji) na kutengeneza ajira kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Taarifa zilizowasilishwa za Taasisi na Mashirika ya Umma ili kubaini iwapo dhima ya Serikali kuwekeza katika Taasisi na Mashirika hayo inatimizwa ikiwa ni pamoja na kuangalia ufanisi na tija ya uwekezaji unaofanywa na Taasisi hizo. Katika uchambuzi wake, Kamati ilitumia njia zifuatazo:-

i) Kupitia Taarifa za Uwekezaji na Utendaji wa Mashirika na Taasisi za umma zinazofanya uwekezaji wa mitaji ya Umma;

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ii) Kupitia Sheria zilizoanzisha Taasisi na Mashirika ya Umma ili kujiridhisha iwapo uwekezaji umezingatia Taratibu, Sheria na Miongozo mujarabu ya biashara;

iii) Kupokea, kuchambua na kujadili Taarifa za Msajili wa Hazina kuhusu uchambuzi wa utendaji na uwekezaji wa Taasisi na Mashirika ya Umma ili kupokea maoni ya Msimamizi wa Taasisi na Mashirika yanayofanya uwekezaji wa mitaji ya umma; na

iv) Kufanya mahojiano na Wenyeviti wa Bodi na Menejimenti za Taasisi na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, kwa kutumia njia hizo, Kamati ilifuatilia uwekezaji huo wa mitaji ya umma kwa kufanya uchambuzi na kubaini mambo makuu yafuatayo: -

i) Gharama kubwa za Uendeshaji;

ii) Miradi kutokamilika kwa Wakati

iii) Kupungua kwa Mtaji katika Taasisi za umma

iv) Kuongezeka kwa madeni (Payables and Receivables)

v) Kukosekana kwa ufanisi katika Kampuni za Ubia

vi) Sheria za Taasisi Kupitwa na Wakati

vii) Kukosekana kwa Miundombinu muhimu katika Maeneo ya Miradi

viii) Watendaji wa Taasisi kukosa Mamlaka Kamili

ix) Taasisi za Serikali kutolipa Madeni yake

x) Uwekezaji wa Serikali katika Kampuni ambazo ina Umiliki wa Hisa Asilimia Hamsini na Pungufu

xi) Mafanikio ya Kamati

2.2.1 Gharama Kubwa za Uendeshaji

Mheshimiwa Spika, moja ya dhumuni la Serikali la kufanya uwekezaji ni kukusanya mapato yasiyo ya kodi kwa njia ya faida na gawio. Hata hivyo, dhumuni hilo linashindwa kutekelezwa na baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kutokana na Taasisi hizo kuwa na gharama kubwa za uendeshaji kinyume na Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 Kifungu cha 46 (10) (A)(1). Matumizi makubwa hasa yasiyoendana na jukumu la msingi yanasababisha Taasisi hizo kukosa faida na kushindwa kutoa gawio na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Mfano wa Taasisi zilizobainika kuwa na matumizi makubwa ni NSSF, NHC, AICC na NIC.

Kamati imechambua kwa kina Taarifa ya Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) na kubaini uwepo wa matumizi makubwa yasiyoendana na majukumu ya msingi ya Shirika. Katika kipindi cha mwaka 2017/18, kiasi cha **Shilingi Bilioni 148** sawa na **Asilimia 26.9** ya matumizi yote kilitumika katika gharama za uendeshaji. Kati ya kiasi hicho, kiasi cha **Shilingi Bilioni 136.78** sawa na **Asilimia 19.75** ya michango yote ya wanachama kwa mwaka kilitumika kwa ajili ya shughuli za kiutawala. Kiasi hiki ni kikubwa ikilinganishwa na ukomo wa **Asilimia 10** kama inavyoelekezwa na iliyokuwa Mdhambi na msimamizi wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (SSRA).

Vile vile, uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) umebainisha kuwa, mapato ya Shirika yamekuwa yakiongezeka au kupungua sambamba na matumizi ya Shirika.

Hali hiyo inapunguza kiwango cha faida ya Shirika. Shirika linatakiwa kupunguza matumizi kwa kuwa iwapo matumizi yatakuwa makubwa ikilinganishwa na mapato yanaweza kuhatarisha uendeleu wa Shirika. Katika mwaka wa fedha 2016/17, mapato ya Shirika yalikuwa ni **Shilingi Bilioni 154.225** wakati matumizi yakiwa ni **Shilingi Bilioni 122.693**. Aidha mapato ya Shirika kwa mwaka wa fedha 2016/17 yalipungua na kufikia **Shilingi Bilioni 116.076** wakati matumizi yakiwa ni **Shilingi Bilioni 83.214**. Uwiano wa matumizi kwa mapato kwa mwaka 2017/18 ni 1:0.82, ikimaanisha kuwa katika kila **Shilingi 1000** inayopatikana inatumika **Shilingi 820** hali inayopunguza faida ya Shirika.

Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha kimebainika pia kuwa na matumizi makubwa ambapo, baada ya uchambuzi wa kina, Kamati ilibaini ongezeko katika gharama za uendeshaji ambapo, katika mwaka 2016/17 gharama za uendeshaji zilikuwa ni **Shilingi Bilioni 13.4** na kuongezeka hadi kufikia **Shilingi Bilioni 14.3** mwaka 2017/18. Ongezeko la gharama za uendeshaji linaenda sambasamba na kushuka kwa mapato ambapo katika mwaka 2015/16 Taasisi ilipata hasara ya **Shilingi Milioni 469**. Mwenendo wa utendaji wa taasisi unaonesha kuwa, AICC imekua ikitumia mapato yake ghafi kwa **Asilimia 93** hadi **Asilimia 103** ikimaanisha kukosekana kwa ufanisi wa kigezo cha Asilimia 50 kilichoweka na Msajili wa Hazina pamoja na kukiuka matakwa ya Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015.

Pamoja na mambo mengine, Kamati pia ilifanya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Shirika la Bima la Taifa (NIC) na kubaini kuwa, matumizi ya Shirika (bila mishahara) kwa mwaka 2018/19 ni **Asilimia 59.3** ya mapato ghafi ambapo, mapato yalikuwa ni **Shilingi 42,095,000,000/=** ikilinganishwa na matumizi ya **Shilingi 33,537,000,000/=**. Kiwango hiko kimezidi kigezo cha ufanisi kilichowekwa na Msajili wa Hazina cha Asilimia 50. Hata hivyo, kama Shirika litaendelea kuongeza matumizi hayo, litakiuka matakwa ya Kifungu cha 46 (1) (A) cha Sheria ya Fedha Na. 16 ya mwaka 2015 inayoelekeza Mashirika kuwa na matumizi ya uendeshaji yasiyozidi asilimia 60

Kamati inaitaka Serikali kuendelea kuweka mkazo kwa Taasisi zake zote ili kuhakikisha matumizi ya uendeshaji hayazidi Asilimia 60 ya mapato ghafi ili Taasisi hizo ziweze kutengeneza faida sambasamba na kuongeza kiasi cha gawio kitakachokwenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

2.2.2 Miradi kutokamilika kwa Wakati

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Taasisi za Umma zimekumbwa na tatizo kubwa la kushindwa kukamilisha miradi yake kwa wakati uliopangwa hali inayocheleweshwa kupatikana kwa faida inayotokana na uwekezaji katika miradi hiyo na kukosekana kwa ufanisi na tija ya utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati imebaini mapungufu hayo ilipochambua Taarifa za Uwekezaji wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Kwa upande wa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii, Kamati imebaini kuwa, Miradi yote inayotekelezwa na Shirika ilianzishwa kati ya mwaka 2012 hadi 2014. Hata hivyo, utekelezaji wake haujakamilika kwa wakati kwa mujibu wa mikataba iliyoingwiwa kati ya Shirika na wabia wengine. Kuchelewa huko kumepelekea kujitokeza kwa changamoto za kimkataba ikiwemo baadhi ya wakandarasi kushindwa kumudu kuendelea na utekelezaji wa mkataba.

Mheshimiwa Spika, katika mradi wa ujenzi ya barabara ya kuunganisha daraja la Nyerere na ile ya feri – kibada, matatizo kadhaa yamejitokeza ikiwemo mkandarasi kutokamilisha mradi kwa wakati. Mradi ulianza tarehe 26 Aprili, 2017 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 25 Novemba, 2017. Hata hivyo, mpaka NSSF inakutana na Kamati pamoja na mkandarasi kuongezewa muda kwa awamu mbili mradi bado haujakamilika na malipo yaliyofanyika mpaka sasa ni **Shilingi Bilioni 13.07**. Tatizo kubwa lililopo ni mkandarasi kudai malipo ya kazi yaliyo nje ya mkataba bila idhini ya Shirika ambapo, madai yake yamefikia **Shilingi Bilioni 36** wakati Mkataba ni wa **Shilingi Bilioni 21.4**. Miradi mingine ya NSSF iliyosimama na kushindwa kukamilika kwa wakati ni Mradi wa

Holiday Inn (Azania Building) ambao ulianza Mwezi Novemba, 2013 na ulitegemewa kukamilika Mwezi Novemba, 2017 Pamoja na Mradi wa Mji wa Kisasa wa Dege (Eco Village) ambao ulitakiwa kukamilika ndani ya Miaka Minne kuanzia Mwezi Januari, 2014 hadi Mwezi Disemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Nyumba la Taifa ni Shirika la kimkakati katika kuhakikisha linafanya biashara pamoja na kutoa huduma ya nyumba za bei nafuu kwa wananchi wa Tanzania. Shirika hili limekuwa na mwenendo usioridhisha kutokana na miradi mingi inayotekelezwa kushindwa kukamilika kwa wakati. Kamati imebaini tatizo hili ambapo, kusua kwa miradi hiyo kunaliingizia Shirika gharama kwa kuwa lilishaingia mikataba na wakandarasi wanaotekeleza miradi hiyo. Uchambuzi umebainisha kwamba, utekelezaji wa Mradi wa 711 uliopo Kawe, Mradi wa Morroco square, Mradi wa Rejent Estate umesimama kwa muda mrefu sasa hali ambayo haitoi picha nzuri kwa utendaji wa Shirika.

Serikali inatakiwa kuhakikisha changamoto zote zilizopo katika miradi hiyo zinaondolewa haraka iwezekanavyo na miradi yote iliyosimama inakamilishwa ili tija ya uwekezaji huo ipatikane.

2.2.3 Kupungua kwa Mtaji katika Taasisi za Umma

Mheshimiwa Spika, kamati inatambua dhamira njema ya Serikali ya kuwekeza katika Taasisi zake kwa kuzipatia Mtaji kwa kutoa Fedha katika mfuko Mkuu wa Serikali, kubadilisha deni kuwa mtaji na ufadhili wa miradi mbalimbali ambapo Serikali hutoa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati kama ufungaji wa rada za kuongoza ndege, ununuzi wa ndege na ujenzi wa reli ya kiwango cha kimataifa (SGR) na baadae kuhamisha miradi hiyo kwenye Taasisi na Mashirika baada ya kukamilika. Kamati inaishauri Serikali kutumia Dhamira hiyo njema kwa Taasisi nyingine za Umma kama Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kwa kutaja baadhi ili kuziwezesha Taasisi hizo kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kuzalisha mapato ya kutosha kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa limekumbwa na changamoto kubwa ya kiutendaji inayosababishwa na kukosekana kwa mtaji. Kukosekana kwa mtaji kumesababisha ongezeko la matumizi ya Shirika lisiloendana na mapato, Shirika kushindwa kulipa madeni yake na Shirika kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati.

Uchambuzi wa Taarifa za kifedha za Shirika umebainisha kuwa, Mtaji wa Shirika umekuwa ukipungua mwaka hadi mwaka ambapo, mwaka 2015/16, 2016/17 na 2017/18 mtaji wa Shirika ulikuwa ni **Shilingi 49,484,530,878.00**, **38,423,563,000.00** na **33,369,201,000.00** mtawalia. Kupungua kwa mtaji ni kiashiria kibaya kwa uendeleu wa Shirika kwakuwa shirika limekabidhiwa miradi mingi mikubwa na ya kimkakati ambayo utekelezaji wake utafanikiwa ikiwa Shirika litakuwa na mtaji wa kutosha. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuongeza mtaji katika Shirika hili muhimu ili liweze kujiendesha kwa ufanisi Zaidi.

Kutokana na kupungua kwa Mtaji mwaka hadi mwaka, kumekuwa na ongezeko la matumizi ya Shirika yasiyoendana na mapato. Matumizi ya Shirika yamekuwa yakiongezeka kutoka **Shilingi Bilioni 9.05** mwaka 2016/17 hadi kufikia **Shilingi Bilioni 10.16** mwaka 2017/18 sawa na ongezeko la **Asilimia 12**. Ukuaji wa gharama za uendeshaji hauendani na ukuaji wa mapato ya Shirika ambapo, mapato ya Shirika yalishuka kutoka **Shilingi Bilioni 6.33** mwaka 2016/17 hadi kufikia **Shilingi Bilioni 2.01** mwaka 2017/18 sawa na pungufu ya **Asilimia 48**.

Katika kipindi cha miaka mitatu kiwango cha gharama kwa mapato kimekuwa kikubwa ambapo ni kati ya 101% na 206% ikiwa ni wastani wa 134%. Hali hii inadhihirisha kuwa utendaji

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wa Shirika hauzalishi mapato ya kutosheleza ambapo Shirika limekuwa likitumia wastani wa **Asilimia 134** ya mapato yake ghafi kwa ajili ya gharama za uendeshaji.

Athari nyingine ya kukosekana kwa Mtaji katika Shirika la Madini la Taifa ni Shirika kushindwa kulipa madeni yake. Katika uchambuzi wake, Kamati pia imepima uwezo wa Shirika kwa kuangalia kigezo cha ukwasi na endapo Shirika lina uwezo wa kulipa madeni yake. Imebainika kuwa, wakati mali za muda mfupi za Shirika zikiendelea kupungua, kiwango cha madeni ya muda mfupi kimekuwa kikiongezeka. Uwiano unaohitajika ni wa 2:1 lakini uwiano wa sasa wa Shirika katika kipindi cha miaka mitatu ni kati ya 0.091:1 na 1.26:1. Ikimaanisha kuwa, kwa kila Shilingi moja inayopatikana inatumika yote kulipa madeni. Endapo uwezo wa Shirika kulipa madeni yake utaendelea kupungua, Shirika litashindwa kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu yake ya msingi.

Pamoja na hayo, tatizo kubwa linalolikabili Shirika la Madini la Taifa ni kushindwa kutekeleza miradi yake. Shirika limepewa jukumu la kutekeleza miradi mbalimbali kama mradi wa Dhahabu wa Stamigold Biharamuro, Mradi wa ubia wa Tanzaniteone, Mradi wa Makaa ya mawe Kiwira, Mradi wa Dhahabu wa Buckreef, Mradi wa Dhahabu wa buhemba, Mradi wa ununuzi wa Madini ya Bati na Mradi wa utafiti wa madini katika leseni zinazomilikiwa na Shirika. Miradi hiyo ni muhimu sana lakini imeshindwa kutekelezeka kwa ukamilifu wake kutokana na kukumbwa na changamoto mbalimbali pamoja na Shirika kukosa mtaji, Shirika kukosa uhalali wa kumiliki na kusimamia baadhi ya miradi kutokana na kutokamilika kwa uhamisho wa umiliki, Shirika kurithi madeni mengi kutoka katika miradi hiyo hali inayozorotesha utekelezaji wa miradi hiyo muhimu. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuondoa changamoto zilizobainika katika Shirika hili muhimu kama ilivyofanya katika Taasisi nyingine kama Kampuni ya Ndege Tanzania na nyinginezo ili uwekezaji wa Shirika uwe ni wenye ufanisi wa hali ya juu.

2.2.4 Kuongezeka kwa Madeni (Payables and Receivables)

Mheshimiwa Spika, uendeshaji mzuri wa Taasisi na Mashirika ya umma unapimwa pia kwa uwezo wa Taasisi hiyo kukusanya madeni inayodai (receivables) na kulipa madeni inayodaiwa (payables). Kutofanya vizuri kwa kigezo hiko kwa kiasi kikubwa kunaweza kuondoa ufanisi wa kiutendaji. Katika uchambuzi wa Taarifa za Taasisi za umma zilizowasilishwa mbele ya Kamati imebainika kuwa, Taasisi nyingi zimekuwa na tatizo la kukosa mbinu mbadala na mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa madeni (receivables) ili kuongeza mapato ya Serikali pamoja na kuwa na mlundikano wa madeni kutokana na kutolipa madeni inayodaiwa. Madeni hayo yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka hali inayozorotesha utendaji wa Taasisi na Mashirika hayo. Mfano wa baadhi ya Taasisi zilizobainika kushindwa kulipa na kukusanya madeni yake ni KMC, NHC na TCAA.

Kamati ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Shirika la Masoko Kariakoo (KMC) na kubaini ongezeko la madeni ya kudai na kudaiwa. Katika eneo la madeni ya kudai (receivables), madeni yameongezeka kwa **Asilimia 36.2** kutoka **Shilingi Milioni 376.1** Mwaka wa fedha 2016/17 hadi kufikia **Shilingi Milioni 512.3** mwaka wa fedha 2017/18. Ongezeko la madeni hayo limetokana na kuongezeka kwa madeni ya biashara (trade receivables) kwa Asilimia 31.1 kutoka **Shilingi Milioni 362.8** mwaka 2016/17 hadi kufikia **Shilingi Milioni 475.8** mwaka 2017/18. Vile vile, madeni ya Shirika (payables) yamekuwa yakiongezeka kutokana na Shirika kushindwa kulipa madeni yake ambapo, madeni hayo yameongezeka kwa **Asilimia 17.4** kutoka **Shilingi Milioni 756.1** katika mwaka wa fedha 2016/17 hadi kufikia **Shilingi Milioni 888.5** mwaka wa fedha 2017/18.

Vile vile, uchambuzi wa Taarifa ya utendaji na uwekezaji wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) umebainisha kuwa, kumekuwa na changamoto ya kuongezeka kwa madeni ya kudai (receivables) kwa asilimia Tisa kutoka **Shilingi Bilioni 27.604** Mwaka wa Fedha 2016/17 hadi

Shilingi bilioni 30.134 Mwaka wa Fedha 2017/18. Ukuaji wa madeni hayo unaathiri ukwasi wa Taasisi. Aidha, Shirika limekuwa likidaiwa kutoka kwa watoa huduma mbalimbali. Madeni hayo yanatokana na kodi (deferred tax) na mikopo (Borrowings). Pamoja na kwamba madeni ya Shirika yamepungua kwa asilimia 9 kwa mwaka wa fedha 2017/18 ikilinganishwa na mwaka 2016/17, Shirika linatakiwa kuboresha ulipaji wake wa madeni ili kufikia uwiano elekezi wa 2:1 badala ya uwiano uliopo sasa wa 1.62:1

Changamoto ya kuongezeka kwa madeni imejitokeza pia katika Mamlaka ya Usimamizi wa Anga Tanzania (TCAA) ambapo, kwa kipindi cha miaka mitatu kumekuwa na kiasi kikubwa cha fedha ambazo Mamlaka haikuweza kukusanya mapato yake licha ya kuwa imetoa huduma. Katika mwaka wa fedha 2015/16 kiasi cha **Shilingi Bilioni 10.170** sawa na **Asilimia 18** ya mapato yote yaliyopaswa kukusanywa na Mamlaka hakikukusanywa; Mwaka 2016/17 kiasi cha **Shilingi Bilioni 14.928** sawa na **Asilimia 23** na mwaka 2017/18 kiasi cha **Shilingi Bilioni 19.777** sawa na **Asilimia 27** hakikukusanywa. Kwa upande mwingine, TCAA imekuwa ikidaiwa (trade payables) fedha nyingi ambapo, kwa mwaka wa fedha 2017/18 TCAA ilifunga hesabu zake ikiwa na madeni ya **Shilingi Bilioni 7.847** ikiwa ni ongezeko la **asilimia 36** ikilinganishwa na deni la **Shilingi Bilioni 4.966** la mwaka 2016/17.

Kamati imeendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha Taasisi zake zote zinalipa madeni yake pamoja na kubuni mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa mapato ili kuongeza mapato ya Taasisi hizo na kuweza kujiendesha kwa ufanisi.

2.2.5 Kukosekana kwa Ufanisi katika Kampuni za Ubia

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza mapato katika Taasisi na Mshirika ya Umma, kuna baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yamepewa kibali cha kufanya uwekezaji kwa ubia na Kampuni nyingine ambazo si za Umma. Katika eneo hili, Kamati ilipata nafasi ya kuchambua Taarifa ya Msajili wa Hazina kuhusu ufanisi wa mitaji na hisa za Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) katika uwekezaji wake katika urushaji wa matangazo kidijitali katika Kampuni ya Star Media Tanzania Ltd. Katika uchambuzi uliofanywa na Kamati, imebainika kuwa, utendaji wa Kampuni ya ubia hauna tija kwa Mbia mwenza TBC na Taifa kwa ujumla.

Kampuni ya Star Media Tanzania Ltd ni Kampuni ya ubia kati ya Shirika la Utangazaji Tanzania lenye umiliki wa **Asilimia 35** na Kampuni ya Star Communications Network Technology Co. Ltd ya Nchini China yenye umiliki wa **Asilimia 65**. Uchambuzi wa kina wa Taarifa zilizowasilishwa mbele ya Kamati na Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kuhusu uwekezaji wake katika Kampuni ya Star Media Tanzania Ltd umebainisha mapungufu mbalimbali ambayo kimsingi yanatakiwa kufanyiwa kazi na Serikali kwa haraka zaidi ili Taifa linufaike na uwekezaji huo. Mapungufu yaliyobainika ni kama Kampuni ya Ubia kupata hasara mfululizo, Mtaji wa kampuni ya Ubia kupungua, Uwezo mdogo wa kampuni kulipa madeni.

Mheshimiwa Spika, baada ya uchambuzi wa Taarifa ya TBC, Kamati imebaini utendaji usioridhisha wa Kampuni ya Star Media Tanzania Ltd kwa kuwa imekuwa ikipata hasara tangu kuanzishwa kwake Mwaka 2009. Hadi kufikia Tarehe 31 Desemba, 2018, Kampuni ilipata hasara ya kiasi cha **Dola za Kimarekani 3,743,803**. Kupatikana kwa hasara hiyo ya kila mwaka kumesababisha Kampuni kushindwa kulipa gawio kwa wanahisa wake. Aidha, Kampuni ya Ubia ilishindwa kutekeleza Mpango wa Biashara (Business Plan 2009 – 2014) ambao ulionesha kuwa Kampuni ingeanza kuzalisha faida na kutoa gawio kwa wanahisa wake ifikapo Mwaka 2014. Hata hivyo, Taarifa ya fedha ya Mwaka 2014 ilionesha hasara ya **Dola za Kimarekani Milioni 8,631,316** wakati Mwaka 2013 hasara ilikuwa **Dola za Kimarekani Milioni 626,080**.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Baada ya taarifa za fedha za Kampuni ya Ubia kwa Mwaka 2014 kuonesha hasara kubwa badala ya faida kama ilivyotarajiwa, Uongozi wa Shirika la Utangazaji Tanzania ulimtaka Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalumu katika Hesabu za Star Media Tanzania Ltd. Mwezi Septemba, 2016 hadi Mwezi Novemba, 2017, CAG alikamilisha ukaguzi wa hesabu za Mwaka 2013 na 2014 pekee.

Aidha CAG alishindwa kukagua hesabu za Mwaka 2015 kutokana na kutopewa nyaraka. Kutokana na Ukaguzi huo, CAG aligundua **maeneo 34** yenye matatizo katika utendaji wa Kampuni ya Star Media Tanzania Ltd yakiwemo masuala ya kukiuka taratibu za fedha, Utawala Bora, kughushi nyaraka, ajira, uchukuaji wa mikopo pasipo kufuata taratibu na kutofuata taratibu za utunzaji wa daffari la mali za Kampuni. CAG aliagiza maeneo yote yaliyobainika kuwa na mapungufu yafanyiwe kazi kwa haraka ili kuondoa matatizo hayo lakini Menejimenti ya kampuni ya Ubia imeonesha kutokuwa na nia ya kutekeleza Mapendekezo ya CAG na Maazimio ya makubaliano katika MOU.

Vile vile, kutokana na utendaji usioridhisha wa kampuni ya star Media Tanzania Ltd, hadi kufikia Tarehe 1 Desemba, 2018, mtaji wa kampuni umepungua hadi kufikia **mtaji hasi** (negative equity) wa **Dola za Kimarekani Milioni 51.989** ikilinganishwa na mtaji wa **Dola za Kimarekani Milioni 238** uliowekezwa Mwaka 2009 wakati wa kuanzishwa kwa Kampuni hiyo.

Kamati pia imeangalia uwezo wa Kampuni ya ubia kulipa madeni yake. Uchambuzi umeonesha kuwa, kampuni haiwezi kulipa madeni yake kutokana na kuwa na madeni mengi ya muda mfupi ikilinganishwa na mali za muda mfupi. Hali hii imesababishwa na utendaji usioridhisha wa kampuni hiyo ya Ubia. Hata hivyo, pamoja na matatizo yote yaliyowasilishwa na Shirika la Utangazaji Tanzania kuhusu uwekezaji wake katika Kampuni ya ubia, Kamati haikupata fursa ya kukutana na mbia mwenza ambaye ni Kampuni ya Star Communications Network Technology Co. Ltd ili kwa pamoja kuangalia namna bora ya kuondoa changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Mapungufu yote yalioainishwa katika ripoti ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu utendaji usioridhisha wa Kampuni ya ubia ni **kielelezo tosha kuwa Serikali** ina jukumu la kuingilia kati ili kupata suluhu la jambo hilo kwa haraka iwezekanavyo ili kulinda maslahi ya TBC na Taifa kwa ujumla. Vile vile, Serikali ifuatilie kwa ukaribu mwenendo wa Kampuni zote za Ubia ambazo umiliki wake unahusisha Taasisi za Umma kwa ajili ya kudhibiti wawekezaji ambao hawatendi haki kwa wabia wenza hasa wenye hisa chache.

2.2.6 Sheria za Taasisi Kupitwa na Wakati

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wa Taarifa za uwekezaji za Taasisi na Mashirika ya Umma, kamati imebani kuwa zipo Taasisi zina miradi na shughuli nyingi zenye fursa kubwa ya kuchangia katika uchumi na ustawi wa Taifa. Hata hivyo, Taasisi na Mashirika hayo yanashindwa kutekeleza majukumu yao kulingana na mazingira ya sasa ya kibiashara kutokana na Sheria zilizoanzisha Taasisi hizo kuwa ni za muda mrefu sana au Taasisi kukosa nguvu ya kisheria katika utekelezaji wa majukumu yake. Mfano wa baadhi ya Taasisi hizo ni Shirika la Masoko ya Kariakoo na Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA).

Katika kutekeleza majukumu yake ya kikanuni, kamati ilikutana na Shirika la Masoko ya Kariakoo na kubaini changamoto hiyo ya Sheria ambapo, Shirika lilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Shirika la Masoko ya kariakoo Na. 36 ya mwaka 1974 (The kariakoo Market Corporation Act, 1974). Aidha, mwaka 1985 Sheria ilifanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Kariakoo Market Corporation (Amendment) Act, 1985 ambapo umiliki wa Shirika uligawanywa kwa asilimia 51 (Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam) na Asilimia 49 zilibaki Serikali Kuu. Sheria ya Shirika la

Masoko ya kariakoo ni ya muda mrefu sana hivyo kusababisha Shirika kushindwa kujikita kwenye biashara kulingana na mazingira ya kibiashara ya sasa.

Changamoto ya Sheria imejitokeza pia kwa Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania. Taarifa ya Mamlaka imeeleza kuwa, katika utekelezaji wa shughuli zake, inakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa Sheria mahususi inayosimamia utekelezaji wa shughuli za Mamlaka ili iwe ni Mamlaka inayojitegemea na kuwa na nguvu ya Kiutendaji. Hali ilivyo sasa, TAWA imeanzishwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori ambapo, Kifungu cha 8 cha Sheria ya Wanyamapori kinamtaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya Wanyamapori kuanzisha Mamlaka inayojitegemea kwa ajili ya kusimamia shughuli za Wanyamapori. Majukumu yaliyopewa TAWA ni makubwa na nyeti hivyo kuna kila sababu ya Taasisi hii kuwa na Sheria mahususi na hivyo kuwa na nguvu ya kutekeleza majukumu yake.

Serikali inatakiwa kuliangalia suala hili kwa mapana yake na kuhakikisha Taasisi na Mashirika yote ambayo Sheria zake zimepitwa na wakati zinafanyiwa marekebisho ili Taasisi hizo ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ukamilifu.

2.2.7 Kukosekana kwa Miundombinu muhimu katika Maeneo ya Miradi

Mheshimiwa Spika, Taasisi na Mashirika ya Umma yamekuwa yakitekeleza majukumu mbalimbali kutokana na dhumuni la uanzishwaji wa Taasisi hizo. Zipo baadhi ya Taasisi za Umma ambazo jukumu lake ni kuwekeza katika ujenzi wa miradi mbalimbali kama nyumba za makazi na biashara. Uwekezaji huo unaendana sambamba na ujenzi wa miundombinu wezeshi katika maeneo ya miradi kama maji, umeme na barabara. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto ya kukosekana kwa miundombinu hiyo muhimu katika maeneo ya miradi inayotekelezwa na baadhi ya Taasisi kama NHC na Watumishi Housing.

Changamoto kubwa inayosababisha miradi mingi hasa ile ya nyumba za gharama nafuu inayotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa kuwa na gharama kubwa ni kukosekana kwa miundombinu muhimu katika maeneo ya mradi. Shirika limekuwa likilazimika kuweka miundombinu ya barabara, umeme na maji hali inayoongeza gharama za uzalishaji na athari hiyo anakutana nayo mnunuzi wa mwisho. Aidha, ununuzi wa ardhi kwa gharama za juu kwa kiasi kikubwa umekuwa ukichangia katika ongezeko la gharama za mradi.

Changamoto hiyo imebainika pia katika Kampuni ya Watumishi Housing (WHC) ambapo, gharama za nyumba zinazouzwa na WHC zimekuwa haziendani na hali ya sasa ya soko hali inayosababisha nyumba hizo kushindwa kuuzika.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kushughulikia masuala yote ya kisera kuhusu upelekaji wa miundombinu muhimu kufanyika kabla ya miradi kuanza ili kuleta unafuu wa bei za nyumba kwa mlaji wa mwisho na kupunguza mzigo wa gharama kwa Taasisi zinazohusika na miradi hiyo. Vile vile, Taasisi zinazohusika na ujenzi wa nyumba zifanye kazi kwa karibu na Mamlaka za Serikali zinazohusika na miundombinu ya Maji, Umeme na Barabara ili Mamlaka hizo zifanye uratibu wa miundombinu hiyo katika maeneo ya miradi badala ya kufanywa na Shirika la Nyumba na Kampuni ya Watumishi Housing kama ilivyo sasa.

2.2.8 Watendaji wa Taasisi kukosa Mamlaka Kamili

Mheshimiwa Spika, katika utendaji wa shughuli za kila siku za Taasisi za umma, mara nyingi maamuzi sahihi hufanywa na mtu mwenye mamlaka kamili. Utekelezaji wa majukumu ya Taasisi na Mashirika ya umma wenye ufanisi na weledi kwa kiasi kikubwa unategemea uwepo wa watumishi wenye mamlaka kamili ya kutekeleza majukumu hayo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mtumishi kutokuwa na mamlaka kamili katika nafasi yake kunachangia utendaji kazi usioridhisha, kutojamini katika utoaji wa maamuzi na muda mwingine kufanya maamuzi yasiyo sahihi na kupunguza morali ya kazi. Kwa muktadha huo, kamati inashauri Serikali kupitia Bodi za Wakurugenzi za Taasisi zote zenye changamoto hii kuhakikisha watumishi ambao wanakaimu na wana uwezo mkubwa, sifa stahiki na weledi katika utendaji kazi wao wanathibitishwa katika nafasi zao ili waweze kuwa na mamlaka kamili badala ya kuwaacha wakikaimu kwa muda mrefu kama ilivyobainika katika Mamlaka ya Usafiri wa anga Tanzania (TCAA) na Wakala wa barabara Tanzania (TANROADS).

Baada ya uwasilishaji wa Taarifa ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania, Kamati imebaini uwepo wa watumishi wengi ambao wanakaimu nafasi walizonazo. Mara zote Kamati imekuwa ikitoa maelekezo kwa Bodi za Wakurugenzi kuondoa tatizo hilo. Tatizo hilo pia limejitokeza katika Wakala wa barabara Tanzania ambapo, kumekuwa na baadhi ya Mameneja wanaokaimu kwa Zaidi ya miezi 30. Hali hiyo haileti afya kwa utendaji wa Taasisi.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa, baadhi ya Taasisi za Umma zimekuwa zikitumia kigezo cha Miundo ya Taasisi hizo kutokamilika kama sababu ya kukosekana kwa watumishi wenye mamlaka kamili. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mapitio ya miundo ya Taasisi ambayo ipo katika mchakato kwa haraka zaidi ili kuondoa tatizo lililopo. Aidha katika nafasi ambazo hazina mtendaji mwenye mamlaka kamili kwa sababu yoyote ile, Uongozi wa Taasisi za Umma uhakikishe unawakaimisha watendaji wenye uwezo na weledi ambapo ndani ya muda wa kisheria mtendaji huyo athibitishwe na kama hakidhi vigezo atolewe na kuwekwa mwenye vigezo stahiki.

2.2.9 Serikali kuchelewa kulipa madeni kwa Taasisi zake

Mheshimiwa Spika, imekuwa ni desturi kwa Serikali na Taasisi zake kutolipa madeni yanayotokana na kupata huduma kutoka katika Taasisi nyingine ya Serikali. Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na Ofisi ya Msajili wa Hazina za kuzikutanisha Taasisi na Mashirika ya Umma yanayodaiana kiasi kikubwa cha fedha kwa lengo la kuhamasisha makubaliano ya kulipa madeni hayo, bado kuna Taasisi ambazo zinadaiwa fedha nyingi na Taasisi nyingine za Umma.

Kamati imekuwa ikiishauri Serikali mara kwa mara kuhakikisha Taasisi zake zinalipa madeni yake baada ya kupata huduma kutoka Taasisi nyingine ili kuongeza ukwasi wa Taasisi hizo zilizotoa huduma. Mlundikano wa madeni kwa muda mrefu unasababisha madeni hayo kutolipika na Taasisi zinazodai kushindwa kutekeleza miradi yake ya uwekezaji kutokana na kukosekana kwa fedha. Mfano wa Taasisi ambazo zimekuwa zikidai fedha nyingi kutoka katika Taasisi nyingine za Umma ni Mbeya Uwasa na AICC

Mheshimiwa Spika, Kamati imefanya uchambuzi wa Taarifa ya Kituo cha Mikutano cha Kimataifa Arusha (AICC) na kubaini changamoto kubwa ya wateja wao kushindwa kulipa madeni yao yanayotokana na kupata huduma mbalimbali kama za mikutano, pango la nyumba na ofisi na huduma za afya. Tatizo hilo kwa kiasi fulani linapunguza mapato ya Taasisi na kukwamisha baadhi ya shughuli za Taasisi kutokana na kukosekana kwa fedha. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018, malimbikizo ya madeni ya wateja mbalimbali waliopata huduma AICC ni **Shilingi Bilioni 6.7** ambapo kati ya hizo, **Shilingi Bilioni 3.6 (54%)** ni madeni ya Wizara na Taasisi za Serikali zilizopata huduma za mikutano, kodi ya pango la ofisi na nyumba na huduma za afya.

Kamati pia imebaini tatizo kubwa la kutolipwa madeni yake (Ankara za maji) kutoka katika Taasisi za Serikali ambazo zimekuwa zikipatiwa huduma na Mamlaka ya majisafi na Usafi wa Mazingira Jijini Mbeya (Mbeya uwasa). Uchambuzi umebainisha kuwa, hadi kufikia Juni, 2019, madeni ya wateja yalifikia jumla ya **Shilingi Bilioni 1.5** ambapo, wadaiwa sugu wa Mamlaka ni

pamoja na Jeshi la Polisi **Milioni 640**, Jeshi la Magereza Mkoa **Milioni 598**, Chuo cha Magereza **Milioni 209**, Mkurugenzi wa Jiji **Milioni 131** na JWTZ **Milioni 30.7**.

Kamati inaishauri Serikali kupitia kwa Msajili wa Hazina kuendelea kuzikutanisha Taasisi zote zinazodaiana ili kwa pamoja waweze kuondoa changamoto hizo na kuhakikisha madeni hayo yanalipwa kwakuwa kiasi cha fedha kinachodaiwa ni kikubwa hali inayopunguza mapato ya Taasisi na kusababisha Taasisi zishindwe kutekeleza miradi yake.

2.2.10 Uwekezaji wa Serikali katika Kampuni ambazo ina Umiliki wa Asilimia Hamsini na Pungufu

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee na kwa niaba ya Kamati, naomba kutoa shukrani za dhati kwako kwa kuona umuhimu wa Kamati hii kukutana na kushauriana na Taasisi ambazo Serikali ina umiliki wa hisa chache (Minority Share). Lengo la kukutana na Taasisi hizi ni kupokea Taarifa za uwekezaji ambao unafanywa na Serikali pamoja na changamoto wanazokabiliana nazo.

Jambo hili limekuwa la manufaa sana kwa Kamati kwa kuwa imepata wasaaa wa kuzifahamu kwa karibu Taasisi hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kukutana na Taasisi hizi, Kamati imebaini kuwa zinakumbana na changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji kupatiwa ufumbuzi ili kuongeza ufanisi katika uwekezaji. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo: -

i) Uchelewashaji wa Kurejesha Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT Refund)

Mheshimiwa Spika, hii ni moja ya changamoto kubwa ambayo Kamati imekutana nayo kwa Makampuni na Taasisi binafsi ambazo zimekidhi vigezo vya kurejeshewa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT Refund). Mamlaka ya mapato Tanzania (TRA) imekuwa hairejeshi kwa wakati malipo hayo, jambo ambalo linaathiri mtiririko wa fedha (Cash flows) wa Makampuni husika hali inayopunguza ufanisi. Mfano wa Kampuni zinazoidai Mamlaka ya Mapato Tanzania ni pamoja na Kampuni ya Mabati ya Aluminium Africa (ALAF) ambayo inaidai zaidi ya **Shilingi Bilioni 15** za Kitanzania.

ii) Kuathirika kwa Soko la Wazalishaji wa Bidhaa Nchini

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sasa kumekuwa na kilio cha wazalishaji wa bidhaa nchini kuharibiwa soko na uingizwaji kwa wingi wa bidhaa ambazo kwanza zinapatikana nchini, lakini pia bidhaa hizo hazina ubora (substandards) au zimezalishwa kwa ruzuku huko zitokako. Aidha, mwigo (counterfeits) wa bidhaa za Makampuni unaofanywa na wahalifu unaathiri soko kwa kiasi kikubwa jambo ambalo, hupelekea bidhaa zinazozalishwa nchini kukosa ushindani sokoni. Mfano wa Taasisi ambazo zimekumbwa na hali hii ni pamoja na Kampuni ya Mabati ya Aluminium Africa (ALAF) na Kampuni ya Sukari ya Kilombero.

Mheshimiwa Spika, uwepo wa mabati yasiyokidhi viwango na yale bandia umeathiri kwa kiasi kikubwa utendaji wa Kampuni ya ALAF ambayo inamilikiwa na Serikali kwa Asilimia 23.4. Vile vile, Kiwanda cha Sukari kilombero (ambacho Serikali ina umiliki wa hisa Asilimia 25) pamoja na viwanda vingine katika tasnia hii, vimekuwa wahanga kutokana na sukari iliyozalishwa kwa Ruzuku, isiyokuwa na viwango na sukari bandia kuingizwa nchini. Kamati inaishauri serikali kupitia mamlaka zinazohusika, kuhakikisha inadhibiti uhalifu huo ili kuwezesha makampuni yetu kushindana kwenye uwanja ulio sawa.

iii) Taasisi kutolipwa madeni yake (Overdue payments)

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwa kuna Taasisi ambazo ufanisi wake umeshuka kutokana na kutolipwa madeni yake kwa wakati. Hali hii imejitokeza zaidi kwenye Taasisi

zinazofanya biashara na Serikali kupitia Mashirika yake. Hali hii inaathiri kwa kiwango kikubwa mtiririko wa fedha katika Kampuni na Mashirika ambayo yanafanya biashara. Mfano wa Taasisi zinazoidai Serikali ni TAZARA na ALAF. Kampuni ya Mabati ya Aluminium Africa (ALAF) inaidai Wakala wa Ujenzi (TBA) kiasi cha **Shilingi Bilioni 3.94** kwa biashara iliyofanyika Mwaka 2017.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali kupitia Msajili wa Hazina kuweka utaratibu wa kuzihimiza Taasisi za Serikali ambazo zinadaiwa kulipa madeni yake ili kuziwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuleta mchango kwenye uchumi kama ilivyokusudiwa.

iv) Changamoto za Kisheria

Mheshimiwa Spika, Kamati pia imebaini kuwa Sheria nyingi zilizoanzisha Makampuni ni aidha zimepitwa na wakati au zinakinzana katika hatua fulani za utekelezaji wa majukumu katika uwekezaji. Hali hii inapunguza ufanisi kwani utekelezaji wa baadhi ya majukumu unakuwa mgumu. Mfano wa Taasisi ambazo zina changamoto za Kisheria ni Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ambayo ina Sheria ya muda mrefu na hivyo kuonekana kupitwa na wakati na kuhitaji maboresho ili kuendana na mazingira ya sasa.

Kamati inaishauri Serikali kupitia Mamlaka husika, kuhakikisha kuwa mchakato wa kufanya maboresho ya Sheria za Taasisi zote zinazohitaji maboresho unaharakishwa ili kuondoa vikwazo vinavyosababishwa na mapungufu ya kisheria na kuongeza ufanisi katika uwekezaji.

v) Baadhi ya Taasisi Kujiendesha kwa Hasara

Mheshimiwa Spika, Kamati ilikutana na Taasisi kadhaa ambazo zinajiendesha kwa hasara. Hali hii imechangiwa na sababu mbalimbali zikiwemo za Upungufu wa mitaji, Uchakavu wa vitendea kazi, kutokuwa na vitendea kazi vya kutosha, upungufu wa wataalamu, madeni makubwa na ya muda mrefu. Mfano wa Kampuni zenye tatizo hili ni TAZARA na Airtel.

Mheshimiwa Spika, moja ya Taasisi ambazo zinajiendesha kwa hasara ni Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) ambayo inajiendesha kwa hasara kwa miaka mitatu mfululizo yaani kuanzia Mwaka 2015/2016 hadi mwaka 2017/2018. Hali hii imesababishwa kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa gharama za uendeshaji (operational costs) ambapo gharama za uendeshaji zinazidi mapato ya TAZARA. Mapato ya TAZARA yameendelea kushuka kutokana na kushuka kwa ufanisi wa reli, miundombinu chakavu, upungufu wa mtaji, madeni (payables) makubwa ya hadi **Shilingi Bilioni 225** na inadai (receivables) Taasisi mbalimbali kiasi cha **Shilingi Bilioni 7.3**. Hali hii imefanya Shirika kushindwa kujiendesha na hivyo kusababisha hasara kwa muda mrefu sasa.

Mheshimiwa Spika, tangu Serikali ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuingia madarakani, ufuatiliaji wa Taasisi ambazo Serikali ina hisa chache umeimarishwa kwa kiwango kikubwa, ikiwa ni pamoja na kufuatilia uendeshwaji wake (performance) kupitia Mikataba ya ubia (shareholders' agreements), Mikataba ya huduma za kimenejimenti na kuimarisha Bodi za Wakurugenzi kwa kuteua wakurugenzi wapya wenye weledi na ujuzi stahiki (relevant skills). Hadi kufikia Juni, 2019 Serikali ilikuwa imeteua wakurugenzi wa Bodi wapya 31 katika Kampuni ambazo Serikali ina hisa chache.

Hali hii imedhihirika kwa kuangalia Taarifa ya fedha ya Kampuni ya simu ya Airtel ambayo kwa miaka mingi imekuwa ikiendesha kwa hasara. Tathmini ya miaka mitatu iliyopita imeonesha kwamba, Shirika limetoka kutengeneza hasara ya **Shilingi Bilioni 109** Mwaka 2017 hadi kufikia hasara ya **Shilingi Bilioni 36.81** Mwaka 2018 kwa hesabu zilizokaguliwa ikiwa hasara imepungua kwa **Asilimia 199%**.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa, Kampuni hii imebadilika kabisa kutoka kutengeneza hasara mpaka kutengeneza faida ya **Shilingi Bilioni 22.7**, kufikia Mwaka 2019 kwa hesabu ambazo hazijakaguliwa (unaudited financials).

Mheshimiwa Spika, Matokeo haya yameonesha kuwa, kuna ufanisi katika juhudi za Serikali za kufuatilia kwa ukaribu utendaji wa Taasisi ambazo Serikali ina hisa chache. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali kutumia njia hiyo hiyo kufuatilia kwa karibu Taasisi zote ambazo zinajiendesha kwa hasara na zile ambazo hazijaonesha tija katika uwekezaji wake ili kubadilisha kabisa dhana ya *'business as usual'* na badala yake zibadilike na kuleta matokeo chanya ya uwekezaji ili kuiunga mkono Serikali ya Awamu ya Tano ambayo inaamini katika kuipeleka Tanzania kwenye uchumi wa kati kupitia Viwanda.

vi) Upanuzi wa Miradi ya Uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Kamati imekutana na Taasisi ambazo zina uhitaji mkubwa wa kupanua miradi yake ili kukidhi mahitaji ya soko na kuongeza tija kwa wanahisa na jamii inayozitunguka.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Sukari ya Kilombero (KSC) ambayo Serikali ina **hisa 25%**, inalenga kupanua kiwanda ili kuongeza uwezo wa uzalishaji na tija.

Gharama za mradi huu ni **Shilingi Bilioni 495** za ki Tanzania. Upanuzi wa kiwanda umekuja baada ya kuonekana kuna uhitaji mkubwa wa sukari nchini ambapo soko la ndani halijawahi kujitoshesha. Mradi ukifanikiwa kukamilika utakuwa wa manufaa makubwa kwa wananchi wanaozunguka maeneo ya kiwanda ambao ni wakulima wadogo (out growers) wanaotegemea kuuza zao la muwa kwenye kiwanda hiki.

Mheshimiwa Spika, wakulima watakaonufaika na mradi huu wanategemewa kufika **wakulima 14,000 hadi 16,000** ifikapo 2027/2028. Idadi hii ni mara mbili ya idadi ya sasa ya **wakulima 8,000** ambapo inatarajiwa kuwa, pato lao litaongezeka toka **shilingi bilioni 63** hadi **shilingi bilioni 300** ifikapo 2028. Aidha, mradi huu ukikamilika utapunguza kwa kiasi kikubwa uingizwaji wa sukari nchini na kuokoa fedha za kigeni kiasi cha **Shilingi bilioni 170** ambazo zingetumika kuingiza sukari nchini. Mchango wa Kampuni kwenye uchumi unategemewa kuongezeka kutoka **Shilingi bilioni 340** hadi **Shilingi bilioni 750** kwa mwaka iwapo upanuzi huu utafanyika.

Mheshimiwa Spika, Kamati baada ya kupitia taarifa hii, inashawishika kuishauri Serikali ambayo ni mwanahisa kuchukua hatua za makusudi za kufanya tathmini ya mradi huu na iwapo itajiridhisha na tija itakayopatikana, iruhusu upanuzi na utekelezaji wa mradi huu kuanza mara moja kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto nyingi zinazozikabili Taasisi hizi, bado kuna Taasisi ambazo zimefanya vizuri kwa maana ya kukua kwa kiwango cha kuridhisha na hata kuweza kutoa gawio kwa wanahisa. Katika kundi la Taasisi ambazo Serikali ina hisa chache, na ambazo Kamati imekutana nazo, Kampuni zifuatazo zimeweza kutoa gawio kwa Serikali: - Kampuni ya Mabati ya Aluminium Africa (ALAF), Benki ya NMB, Kiwanda cha Sukari Kilombero (KSC), Kampuni ya Simu ya Airtel na Bomba la Mafuta la TAZAMA. Kamati inatoa rai kwa Taasisi nyingine kujiwekea mikakati ya kimageuzi (Turn Around Strategy) ili kuzihuisha Taasisi hizo na kuongeza tija katika uwekezaji.

2.2.11 Mafanikio ya Kamati

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ni Kamati mpya katika Bunge la Kumi na moja. Hata hivyo, Kamati hii ni jicho la Bunge katika kuangalia

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa mujibu wa Kanuni ya 12 ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016. Aidha, Taarifa hii ni ya mwisho kuwasilishwa katika Bunge lako Tukufu la Kumi na Moja.

Hivyo basi, napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kuipa nafasi Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kuleta tija kwa Taifa. Vile vile, Naishukuru Serikali kupitia Msajili wa Hazina kwa kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hii kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa manufaa ya Taifa kwa ujumla.

Katika utekezaji wa majukumu yake tangu kuundwa kwa Kamati hii, changamoto nyingi za kiutendaji zilibainika na mafanikio mbalimbali yamepatikana. Baadhi ya changamoto zilizobainika wakati kamati hii inaanza kukutana na Taasisi na Mashirika ya Umma Januari, 2016 ambazo kwa kiasi kikubwa zimefanywa kazi na Serikali ni kama ifuatavyo:-

a. Utoaji wa Gawio na Uchangiaji katika Mfuko Mkuu wa Serikali

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuundwa kwa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya umma, Taasisi na Mashirika mengi ya Umma yalikuwa hayaoni umuhimu wa kulipa gawio kwa wanahisa wake pamoja na kuchangia Asilimia 15 ya mapato ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali licha ya kuwa ni takwa la kisheria. Hali hiyo iliikosesha Serikali mapato mengi. Hata hivyo, Kamati ilisimamia kikamilifu suala hilo na kuzitaka Taasisi zote zinazotakiwa kutoa gawio na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali kutekeleza jukumu hilo. Kufuatia juhudi hizo, katika mwaka wa fedha 2018/19 Serikali ilipokea gawio la **Shilingi 1,053,816,218,154** ikilinganishwa na gawio la **Shilingi 422,968,027,083.68** lililipokelewa katika mwaka wa fedha 2015/2016 sawa na Ongezeko la **Asilimia 149** ndani ya Miaka Minne.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaunga mkono maelekezo ya Mheshimiwa Raisi Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ya kuzitaka Taasisi zote kuhakikisha zinatoa gawio Serikalini na kwa Uongozi wa Taasisi ambao utashindwa kutekeleza maelekezo hayo kuachia madaraka waliyonayo. Kwa maelekezo hayo, Kamati inaona ni muda sasa wa Serikali kutunga Sheria na Kanuni zitakazo walazimisha Viongozi wote wa Taasisi kulipa gawio Serikalini na endapo zitashindwa kutekeleza takwa hilo, Sheria ichukue mkondo wake.

b. Upungufu wa Mtaji

Mheshimiwa Spika, katika utendaji wake, Kamati ilikutana na changamoto ya baadhi ya Taasisi za Umma kuwa na upungufu wa mtaji wa uendeshaji hali iliyosababishwa na Serikali kushindwa kutekeleza wajibu wake wa kupeleka mtaji kama ilivyoahidi wakati wa uanzishwa wa Taasisi hizo. Kukosekana kwa mtaji kulisababisha Taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa ufanisi na kutoleta tija inayotarajiwa. Kamati iliitaka Serikali kupeleka mtaji katika Taasisi hizo na pendekezo hilo kwa kiasi fulani lilitokelezwa kwa Serikali kupeleka mtaji katika baadhi ya Taasisi hivyo Kamati inasisitiza pendekezo hilo litekelezwe kwa ukamilifu wake.

c. Utegemezi Mkubwa wa Ruzuku ya Serikali

Mheshimiwa Spika, huko nyuma, Taasisi nyingi za Umma zilikuwa hazina mbinu mbada ya kutafuta mapato na badala yake zilikuwa zikisubiri kuletewa Ruzuku ya Serikali hali iliyokuwa ikiongeza mzigo Serikalini na kusababisha miradi mikubwa ya kimkakati na ya kitaifa kushindwa kutekeleza kutokana na fedha nyingi kupeleka katika Taasisi za Umma kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kamati haikuridhishwa na suala hilo hivyo, ilizitaka Taasisi zote za Umma kutumia vyema rasilimali walizonazo na kubuni mikakati madhubuti ya utafutaji wa mapato bila ya kuathiri majukumu ya msingi ya Taasisi hizo. Kutokana na pendekezo hilo, Serikali kupitia Msajili wa Hazina imekuwa ikifuatilia utendaji wa Taasisi hizo kwa kuidhinisha nyaraka mbalimbali kama mpango mkakati na kuhakikisha Taasisi zote zinajiendesha bila ya kutegemea Ruzuku ya Serikali.

d. Kuchelewa kwa uteuzi wa Bodi za wakurugenzi

Mheshimiwa Spika, wakati Kamati hii inaanza kutekeleza majukumu yake Mwaka 2016, ilikutana na Taasisi nyingi ambazo hazikuwa na Bodi za Wakurugenzi. Taasisi nyingi zilikuwa zikikaa muda mrefu hadi kufikia Miaka Miwili bila ya Bodi za Wakurugenzi hali iliyosababisha Taasisi hizo kuwa na utendaji usioridhisha kutokana na kutokuwa na msimamizi kwa niaba ya Serikali na kukosekana kwa chombo cha kufanya maamuzi. Baada ya Kamati kulitilia mkazo suala hili, Serikali imefanya uteuzi wa Bodi nyingi za Wakurugezi. Vile vile, Ofisi ya Msajili wa Hazina imekuwa ikihifadhi Taarifa za uteuzi wa Bodi na taarifa muhimu kuhusu Wajumbe wa Bodi pamoja na kuzikumbusha Wizara mama kuhusu uteuzi wa Bodi mpya Miezi Sita kabla ya Bodi iliyopo kumaliza muda wake.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumshukuru na kumpongeza Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kufanya uteuzi wa Wenyeviti wa Bodi mbalimbali na kuhakikisha Taasisi za Umma zinakuwa na usimamizi madhubuti ambapo hali ilivyo sasa, Taasisi na Mashirika 176 yana Bodi za Wakurugenzi zilizo hai wakati Mashirika 56 Bodi zake za Wakurugenzi zimemaliza muda wake na taratibu za uteuzi zinaendelea. Kamati inaendelea kushauri uteuzi wa Bodi ufanyike kwa wakati.

e. Matumizi Makubwa Yasiyohusiana na Uwekezaji

Mheshimiwa Spika, Taasisi nyingi zilikuwa zikikiuka matakwa ya Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 Kifungu cha 46 (10) (A)(1) kilichokuwa kikizitaka Taasisi za umma kudhibiti matumizi yake ya gharama za uendeshaji na kutozidi Asilimia 60 ya mapato ghafi. Ilikuwa ni desturi ya Taasisi za Umma kutumia mapato yote yanayopatikana na kutobakiwa na ziada au kupata nakisi. Uwiano wa mapato na matumizi haukuwa ni wa kuridhisha kwakuwa Taasisi zilikuwa na kiasi kikubwa cha matumizi ikilinganishwa na mapato. Kamati haikuridhishwa na mwenendo huo kwakuwa Serikali ilikuwa ikipoteza mapato mengi katika eneo hilo kwakuwa Taasisi hizo zilikuwa zikishindwa kutengeneza faida na kutoa gawio Serikalini. Hali ilivyo sasa, Taasisi nyingi zinazingatia takwa hilo la kisheria na kwa baadhi ambazo bado zina matumizi makubwa imeendelea kuisisitiza Serikali kuzichukulia hatua za kisheria.

f. Uwekezaji Usio na Tija

Mheshimiwa Spika, Kamati pia ilibaini baadhi ya Taasisi zilizokuwa zikifanya uwekezaji usio na tija. Kwa kuwa Taasisi nyingi za Umma zilikuwa zikifanya uwekezaji wake bila ya kumshirikisha Msajili wa Hazina, changamoto nyingi zilikuwa zikijitokeza wakati wa uendeshaji wa miradi. Taasisi zilikuwa zikianza kufanya uwekezaji bila ya kufanya upembuzi yakinifu (feasibility study) wa kutosha na kuangalia gharama halisi za mradi, muda utakaotumika kukamilisha mradi, faida itakayopatikana kutokana na mradi huo na muda utakaotumika kurejesha faida. Changamoto hiyo kwa kiasi kikubwa imeondolewa na uwekezaji wowote unaofanyika na Taasisi za Umma unazingatia miongozo ya Msajili wa Hazina.

g. Serikali kutolipa madeni yake

Mheshimiwa Spika, Serikali kutolipa madeni yake kwa Taasisi zake lilikuwa ni tatizo sugu. Ilikuwa ni kawaida kwa Taasisi moja ya Umma kupata huduma kutoka katika Taasisi nyingine ya Umma bila ya kulipia huduma hiyo na bila ya kuchukuliwa hatua yoyote. Kamati ililionga suala hilo na kumtaka Msajili wa Hazina kufuatilia kwa karibu na kuondoa tatizo hilo. Agizo hilo linaendelea kutekelezwa ambapo, Serikali kupitia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani (IAG) imekuwa ikifanya uhakiki wa madeni ambayo inadaiwa katika Taasisi za Umma kwa lengo la kuthibitisha uhalali wake na kulipwa.

Vile vile, Ofisi ya Msajili wa Hazina imeanzisha utaratibu wa kukutanisha Taasisi za Umma zinazodaiana kiasi kikubwa cha fedha kwa lengo la kuhamasisha makubaliano ya kulipa. Zoezi

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hilo limefanikiwa ambapo, TPDC inailipa Benki ya Maendeleo TIB **Shilingi Bilioni 5** kila mwezi. Mfano mwingine ni Tanesco inailipa Benki ya Maendeleo ya TIB kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.2** kila wiki. Utaratibu huu unaendelea kwa Taasisi zote za Umma.

h. Utendaji wa Taasisi usioridhisha

Mheshimiwa Spika, Taasisi nyingi zilikuwa zikishindwa kufikia malengo yake kwa kiwango kilichotarajiwa kwa kuwa katika Mikataba ya utendaji kazi ya viongozi wa Mashirika, hapakuainishwa kipimo cha utendaji kazi na muda wa utekelezaji wa miradi (Performance Based Contract). Hali hii ilisababisha miradi ya Taasisi hizo kutokamilika kwa wakati na kutoleta tija iliyotarajiwa.

Kamati ilitoa maelekezo kwa Serikali namna ya kutatua changamoto hii na hali ilivyo sasa, Ofisi ya Msajili wa Hazina imekuwa ikiingia Mikataba ya Utendaji Kazi na Taasisi na Mashirika ya Umma. Lengo la Mikataba ya Utendaji Kazi ni kuhakikisha kuwa kila Taasisi ya Umma inaweka vipaumbele vya utendaji kazi na kuvitekeleza kwa ufanisi katika kila mwaka wa fedha na kuainisha vigezo vya kiutendaji vitakavyotumika kupima utendaji kazi. Vigezo vinavyotumika katika tathmini ya utendaji kazi vimegawanyika katika Makundi manne (4) ambayo ni Usimamizi wa Rasilimali watu, Huduma kwa Wananchi na Wateja wa Taasisi, Utawala Bora na usimamizi na udhibiti wa mapato.

Hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2019, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilikuwa imeingia Mkataba wa Utendaji na Taasisi na Mashirika ya Umma 124 ikilinganishwa na Taasisi 24 ambazo ziliingia Mkataba Mwaka wa fedha wa 2015/16 wakati Mfumo wa Mikataba ya Utendaji Kazi unaanzishwa rasmi.

i. Mikataba Isiyo na Tija

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Taasisi za Umma ambazo zilikutana na Kamati zilibainika kuingia mikataba isiyo na tija ya uwekezaji iliyokuwa ikilingiza Taifa katika hasara kubwa. Baada ya Kamati kuliona suala hilo, iliishauri Serikali kupitia mikataba yote ambayo Taasisi za Umma imeingia na wawekezaji kutoka nje ya nchi na kuangalia namna bora ya kufanya marekebisho ya vipengele hasi vya mkataba au kuvunja mikataba hivyo. Tatizo hili linafanyiwa kazi kwa ukaribu na Serikali inahakikisha Taasisi za Umma haziingii tena mikataba ambayo hailinufaishi Taifa.

j. Taasisi za Umma kutomtambua Msajili wa Hazina

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yalikuwa hayamtambui Msajili wa Hazina kama msimamizi wa mali za Umma kwa niaba ya Serikali. Taasisi hizo zilikuwa hazipeleki nyaraka muhimu kama Bajeti ya Taasisi, Mpango Mkakati, Mpango wa Biashara, Sera ya uwekezaji na Taarifa nyingine muhimu kwa ajili ya kufanyiwa mapitio na kupata kibali cha Msajili wa Hazina. Hali hiyo ilisababisha Taasisi hizo kujiendesha bila ya miongozo muhimu na kusababisha utendaji usio na tija. Kamati ilizitaka Taasisi zote za Umma kuhakikisha zinafuata miongozo yote inayotolewa na Msajili wa Hazina na kutofanya matumizi na Uwekezaji wa aina yoyote bila ya kupata idhini ya Msajili wa Hazina. Agizo hili la Kamati limetekelezwa kwa ukamilifu wake na sasa Taasisi zote zinamshirikisha Msajili wa Hazina katika hatua zote za utendaji.


Mheshimiwa spika, Kamati imeshuhudia masuala mbalimbali yaliyotolewa na kufanyiwa kazi na Serikali na kuleta matokeo chanya hasa katika ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi. Ongezeko la mapato katika Taasisi na Mashirika ya Umma limechangiwa na marekebisho makubwa yaliyoyafanyika katika Taasisi na Mashirika ya hayo. Uchambuzi wa ulinganisho kati ya Mashirika ya Umma (SOEs) na Kampuni ambazo Serikali inamiliki Hisa chini ya Asilimia 51 (MIs) kwa fedha zinazokusanywa na Msajili wa Hazina unaonesha kuwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019, Taasisi

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

za Umma (SOEs) na Kampuni ambazo Serikali ina hisa chache (MIs) zilifanikiwa kupata rejesho la mtaji (ROI) la **Asilimia 7.21** na **Asilimia 6.64**, mtawalia.

Mwenendo wa uchambuzi kwa miaka mitano iliyopita unaonesha kwamba rejesho la mtaji kwa Taasisi za Umma (SOEs) limekuwa likiongezeka kutoka mwaka hadi mwaka, wakati rejesho la mtaji kwa Taasisi ambazo Serikali ina hisa chache (MIs) limekuwa likipanda na kushuka kama inavyoonekana katika Kielelezo hapo chini

Mwenendo wa Rejesho la Mtaji kwa SOEs and MIs, 2014/15-2018/19



Chanzo: Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina 2018/2019

Mheshimiwa Spika, Kamati inajivunia mafanikio yanayopatikana katika Taasisi na Mashirika ya umma kwa kuwa kumekuwa na utekelezaji mkubwa wa jukumu lake la kikanuni la kuchambua na kubaini iwapo utekelezaji wa miradi ya uwekezaji wa umma una tija, ufanisi na kuwa umezingatia Taratibu, Sheria na Miongozo Mujarabu ya Biashara. Mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa Mapato yasiyo ya Kodi kutoka katika Mashirika na Taasisi za Umma mpaka sasa yamechangia jumla ya **Shilingi Trilioni 1.05**. Aidha, mafanikio haya na shukrani hizi ziende kwa Bunge lako Tukufu kwa usimamizi mzuri wa shughuli za Serikali. Kamati inaamini makusanyo hayo yataendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kwa manufaa mapana ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda kumpongeza Msajili wa Hazina Ndg. Athumani Mbuttuka na wafanyakazi wote wa Ofisi yake kwa kusikia kilio cha Kamati cha muda mrefu cha kukosekana kwa Taarifa ya Mwaka ya Msajili wa Hazina, ambayo **kwa mara ya Kwanza katika historia tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina sasa imetoka**. Kamati inajivunia kupatikana kwa Taarifa hii kwa kuwa suala hili limekuwa likipigiwa kelele na Kamati kwa miaka iliyopita tangu kuanzishwa kwake bila mafaniko.

2.3 Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma iliwasilisha Taarifa yake ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kuanzia Februari, 2018 hadi Januari, 2019 mbele ya Bunge lako Tukufu. Taarifa hiyo ilijumuisha Maoni na Mapendekezo ya Kamati ambayo yalikuwa ni Maazimio ya Bunge na kutakiwa kufanyiwa kazi na Serikali ili kuongeza tija na ufanisi katika Taasisi na Mashirika ya Umma. Aidha, Kamati imekuwa ikifuatilia utekelezaji wa Maazimio **Kumi na Mbili**

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

yaliyotolewa kupitia kwa Msajili wa Hazina ambaye ndiye Msimamizi Mkuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma kwa niaba ya Serikali.

Hata hivyo, kati ya Maazimio hayo, ni Maazimio **Saba** pekee ndiyo yaliyofanyiwa kazi na Maazimio **Matano** yaliyotolewa na Bunge hayajatekelezwa kikamilifu na Serikali hali inayosababisha Utendaji na Uwekezaji wa baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma kutokuwa na ufanisi na tija. Hoja ambazo utekelezaji wake haujakamilika kikamilifu ni kama ifuatavyo:-

i) Bunge liliazimia kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina ihakikishe Taasisi na Mashirika yote ya Umma yanaandaa nyaraka zote muhimu zinazotakiwa katika uendeshaji wa Taasisi na kuhakikisha nyaraka hizo zinatumika kikamilifu. Ofisi ya Msajili wa Hazina imekuwa ikifanya ufuatiliaji ili kuhakikisha Mashirika yote yanaandaa nyaraka hizo lakini bado kuna baadhi ya Taasisi za umma ambazo zimeandaa Mpango Mkakati ambao hautekelezeki na hauoneshi dira ya Taasisi hizo.

ii) Bunge liliazimia Serikali kupeleka Mtaji wa kutosha kwa Taasisi na Mashirika ya Umma kama ilivyoahidi wakati wa uanzishwaji wa Taasisi hizo na kama fedha hizo zilivyoidhinishwa na Bunge. Pamoja na Serikali kuwekeza kwa kutoa fedha na kujenga miradi mbalimbali inayomilikiwa na Taasisi za Umma, bado kuna baadhi ya Taasisi za Umma zilizoanzishwa kimkakati ambazo hazina mtaji wa kutosha hali inayosababisha Taasisi hizo kushindwa kutekeleza miradi yake na kuzalisha mapato ya kutosha. Shirika la Madini la Taifa (Stamico) limekuwa na Tatizo la Mtaji kwa muda mrefu licha ya Kamati kulipigia kelele suala hili ili kuboresha utendaji wa Taasisi hiyo. Hivyo kamati inaitaka Serikali kutekeleza azimio hilo kwa ukamilifu wake.

iii) Azimio lingine ambalo halijafanyiwa kazi kikamilifu ni matumizi makubwa ambayo hayaendani na uwekezaji. Bunge liliazimia Serikali izichukulie hatua Taasisi zote zinazokiuka matakwa ya Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 ili Taasisi hizo ziweze kupunguza matumizi na kutengeneza faida. Licha ya takwa la kisheria lililopo, bado kuna baadhi ya Taasisi chache ambazo matumizi yake ambayo hayaendani na uwekezaji yanazidi Asilimia 60 ya mapato ghafi.

iv) Azimio la Bunge la kuitaka Serikali kuleta Bungeni mapendelezo ya kuzifanyia marekebisho Sheria zote za Taasisi ambazo zimepitwa na wakati ili kuziwezesha Taasisi hizo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi kwenye mazingira ya sasa yenye ushindani mkubwa wa kibiashara bado halijafanyiwa kazi kikamilifu kwa baadhi ya Taasisi kama Mamlaka ya Wanyamapori Tanzania (TAWA) na Shirika la Masoko ya Kariakoo ambayo Sheria zake haziendani na wakati wa sasa hali inayosababisha utendaji usio na tija.

v) Kamati ilieleza changamoto zinazopatikana kutokana na Serikali kutolipa madeni yake hali inayopunguza mapato ya Taasisi zinazotoa huduma. Kutokana na hoja hiyo, Bunge liliazimia kuwa, Serikali pamoja na Taasisi zake ilipe madeni yote yanayotokana na kupata huduma kutoka katika Taasisi nyingine ili Taasisi hizo ziweze kutumia fedha hizo kujiendesha na kutekeleza miradi mbalimbai ya uwekezaji. Hata hivyo, bado Azimio hilo halijafanyiwa kazi kikamilifu na Serikali na Taasisi zake kwakuwa bado kuna Taasisi chache ambazo ni wadaiwa sugu na hawaoneshi jitihada za kulipa madeni wanayodaiwa licha ya kupatiwa huduma.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

3.1 Maoni

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa kina uliofanywa na Kamati ulijikita zaidi katika kuhakikisha dhima ya Serikali kufanya uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa inatekelezwa kikamilifu na Serikali inapata faida kutokana na uwekezaji uliofanyika katika Taasisi na Mashirika yake. Kutokana na uchambuzi wa Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, Kamati inapenda kutoa maoni ya jumla kama ifuatavyo:-

Kamati ya uwekezaji wa Mitaji ya Umma imeshuhudia hatua mbalimbali za mageuzi ya kiutendaji zinazochukuliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa Taasisi na Mashirika ya Umma. Mageuzi hayo yamesababisha mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kutoka katika Mashirika na Taasisi za Umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa ambapo, hadi kufikia Tarehe 30 Juni, 2019, Mfuko Mkuu wa Serikali ulikusanya jumla ya **Shilingi Trilioni 1.05**.

Usimamizi bora wa Taasisi na Mashirika ya Umma umechangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa Taasisi na Mashirika yanayotoa Michango na Gawio Serikalini. Mwenendo wa mapato yanayokusanywa katika Mfuko Mkuu wa Serikali umekuwa ni wa kuridhisha ambapo, katika mwaka wa fedha 2018/19 mapato yanayotokana na gawio na michango ya Taasisi na Mashirika ya Umma na Kampuni ambazo Serikali ina hisa ni jumla ya **Shilingi 1,053,816,218,154** ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi 422,968,027,083.68** kilichokusanywa katika mwaka wa fedha 2015/16

Mheshimiwa Spika, Kiu ya Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ilikuwa ni kuhakikisha kunakuwa na ufanisi na tija katika fedha za umma zilizowekezwa na Serikali. Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Msajili wa Hazina na Serikali kwa ujumla kwa kuzisimamia Taasisi na Mashirika ya Umma kwa ufanisi na matunda ya usimamizi huo yanaonekana. Aidha, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuendelea na usimamizi huo ili utekeleaji wa Bajeti ya Serikali usitegemee zaidi kodi na badala yake uchangiwe kwa kiasi kikubwa na mapato yasiyo ya kodi.

Ongezeko la mapato yasiyo ya kodi linategemea kwa kiasi kikubwa na baadhi ya mambo yanayofanywa na Msajili wa Hazina kama kuangalia Utawala bora katika Taasisi, kuhakikisha Taasisi zinaongeza ufanisi katika utendaji na kupunguza gharama za uendeshaji, kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mara kwa mara na kuingia mikataba ya utendaji kazi baina ya Serikali na Wenyeviti wa Bodi na Menejimenti za Taasisi.

Kwa muktadha huo, Kamati inaendelea kushauri na kuisisitiza Serikali kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi wa hali ya juu na kubainisha maeneo yote yenye changamoto za kiutendaji ili ziweze kufanyiwa kazi na Serikali haraka iwezekanavyo. Kwa kufanya hivyo, Taasisi na Mashirika ya Umma yatatekeleza majukumu yake kikamilifu na kuipatia fedha Serikali ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa manufaa ya Nchi yetu.

3.2 Mapendekezo

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maoni ya jumla ya Kamati yaliyotokana na uchambuzi wa Mitaji ya Umma, naomba kutoa mapendekezo ya kamati kama ifuatavyo:-

3.2.1 Gharama Kubwa za Uendeshaji

KWA KUWA, baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yamebainika kuwa na gharama kubwa za uendeshaji kinyume na Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 Kifungu cha 46 (10) (A)(1),

NA KWA KUWA, Uwepo wa gharama hizo kubwa zinazifanya Taasisi hizo kushindwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu sambamba na kushindwa kutoa gawio au kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina ihakikishe Taasisi na Mashirika yote ya Umma yanazingatia matakwa ya Sheria ya Fedha Na 16 ya 2015 Kifungu cha 46 (10) (A)(1) pamoja na Miongozo yote inayotolewa na Msajili wa Hazina. Aidha, Sheria hii ipitiwe kwa kuweka kipengele kitakachoitaka Bodi na Menejimenti kuachia madara endapo watakwenda kinyume na matakwa ya Sheria.

3.2.2 Miradi Kutokamilika kwa Wakati

KWA KUWA, baadhi ya Taasisi na Mashirika ya umma yamekuwa yakitekeleza miradi mingi ya Uwekezaji kwa muda mrefu na miradi hiyo kutokamilika kwa wakati kutokana na sababu mbalimbali kama ufinyu wa mtaji, mikataba isiyo na tija na kukosekana kwa utawala bora katika utekelezaji wa miradi hiyo,

NA KWA KUWA, Kushindwa kukamilika kwa miradi hiyo kunaongeza gharama za miradi na kukosekana kwa tija ya uanzishwaji wa miradi hiyo,

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuhakikisha changamoto zote zilizopo katika miradi yote zinaondolewa haraka iwezekanavyo na miradi yote iliyosimama inakamilishwa ili tija ya uwekezaji huo ipatikane na watakaosababisha hasara wawajibishwe.

3.2.3 Kupungua kwa Mtaji katika Taasisi za Umma

KWA KUWA, baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma yamekumbwa na changamoto kubwa ya kiutendaji inayosababishwa na kukosekana kwa mtaji likiwemo Shirika la Madini la taifa (STAMICO),

NA KWA KUWA, Kukosekana kwa mtaji kumesababisha ongezeko la matumizi ya Shirika yasiyoendana na mapato, Shirika kushindwa kulipa madeni yake na Shirika kushindwa kutekeleza miradi mbalimbali ya kimkakati,

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kulifufua Shirika hili kwa kuondoa changamoto zote zilizopo kwa kulingezea mtaji, kukamilisha uhamisho wa umiliki ili kulipa Shirika uhalali wa kumiliki na kuisimamia miradi iliyokabidhiwa na kuliondolea Shirika madeni makubwa yaliyorithiwa. Aidha, Serikali ipeleke mtaji kwa Taasisi zote za Umma zinazostahili na zenye changamoto hiyo.

3.2.4 Kuongezeka kwa Madeni

KWA KUWA, Taasisi nyingi zimekosa ufanisi katika kigezo cha madeni ya kudai na kudaiwa kwakuwa na tatizo la kukosa mbinu mbadala na mikakati madhubuti ya ukusanyaji wa madeni (receivables) pamoja na kuwa na malimbikizo ya madeni (payables),

NA KWA KUWA, kutofanya vizuri kwa kigezo hicho kunazorotesha utendaji wa Taasisi na Mashirika hayo na kupunguza mapato ya Serikali,

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kuandaa miongozo maalumu kwa Watendaji Wakuu wa Taasisi na Mashirika itakayoainisha madhara yatakayopatikana kutokana na kushindwa kubuni mikakati madhubuti ya ukusanyaji na ulipaji wa madeni na itakayowawajibisha watendaji watakaokiuka miongozo hiyo.

3.2.5 Kukosekana kwa Ufanisi katika Kampuni za Ubia

KWA KUWA, Kampuni ya Ubia ya Star Media Tanzania Ltd imebainika kuwa na mapungufu makubwa na mengi ya kiutendaji kama Kampuni ya Ubia kupata hasara mfululizo, Mtaji wa kampuni ya Ubia kupungua, Uwezo mdogo wa kampuni kulipa madeni pamoja na Mbia Mwenza Star Communication Technologies Co. Ltd kugoma kutekeleza hoja zilizotoewa na CAG,

NA KWA KUWA, Kutorekebisha kwa mapungufu hayo kwa muda mrefu kumesababisha Kampuni ya Star Media Tanzania Ltd kushindwa kutoa gawio kwa wanahisa wake akiwemo Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC),

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kuwa Serikali ihakikishe inafanyia kazi hoja zote zilizotolewa na CAG ikiwa ni pamoja na kusimamia kwa ukaribu na kuondoa mapungufu yote yaliyopo pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria watu wote waliochangia utendaji mbovu wa Kampuni ya Star Media Tanzania Ltd na kuona kama kuna haja ya kuendelea na ubia huo.

3.2.6 Sheria za Taasisi kupitwa na Wakati

KWA KUWA, kumekuwa na baadhi ya Taasisi na Mashirika ya Umma ambayo Sheria zake zimepitwa na Wakati kwakuwa ni za muda mrefu sana na nyingine kukosa nguvu ya Kisheria kutekeleza majukumu yake,

NA KWA KUWA, uwepo wa Sheria zilizopitwa na wakati unazisababishia Taasisi na Mashirika hayo kushindwa kutekeleza majukumu yake kulingana na mazingira ya sasa ya kiushindani na ya kibiashara,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kuwa Serikali ilete Bungeni mapendekezo ya mabadiliko ya Sheria za TAWA na Shirika la Masoko ya kariakoo pamoja na Sheria zote zilizopitwa na wakati ili Taasisi na Mashirika ya Umma yatekeleze majukumu yake kwa ufanisi na tija.

3.2.7 Kukosekana kwa Miundombinu Muhimu katika Maeneo ya Miradi

KWA KUWA, Maeneo mengi ya miradi ya nyumba inayotekelezwa na Shirika la Nyumba la Taifa na kampuni ya Watumishi Housing yamekosa miundombinu muhimu ya maji, umeme na barabara,

NA KWA KUWA, Kukosekana kwa miundombinu hiyo muhimu kumesababisha ongezeko kubwa la gharama za uwekezaji kwa Taasisi zinazohusika na miradi hiyo hasa ya nyumba za gharama nafuu na kuhamisha mzigo huo wa gharama kwa mnunuzi wa mwisho,

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kushughulikia masuala yote ya kisera kuhusu upelekaji wa miundombinu muhimu kufanyika kabla ya miradi kuanza ili kuleta unafuu wa bei za nyumba kwa mlaji wa mwisho na kupunguza mzigo wa gharama kwa Taasisi zinazohusika na miradi hiyo.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Vile vile, kuwe na makubaliano na mipango ya pamoja juu ya ujenzi wa miundombinu ya maji, umeme na barabara katika maeneo ya mradi kabla ya kuanza kwa mradi husika.

3.2.8 Watendaji wa Taasisi kukosa Mamlaka Kamili

KWA KUWA, imekuwa tabia kwa Bodi za Wakurugenzi za Taasisi na Mashirika ya Umma kuwaacha Watendaji wao wakikaimu nafasi walizonazo kwa muda mrefu bila ya kuwathibitisha au kutafuta mtu mwingine wa kujaza nafasi hizo na kuwafanya watumishi hao kutokuwa na mamlaka kamili,

NA KWA KUWA, kutokuwa na mamlaka kamili katika nafasi zao kunachangia utendaji kazi usioridhisha, kutojamini katika utoaji wa maamuzi na muda mwingine kufanya maamuzi yasiyo sahihi na kupunguza morali ya kazi,

KWA HIYO BASI, Bunge linaishauri Serikali kupitia Bodi za Wakurugenzi za Taasisi na Mashirika machache yenye changamoto hiyo kuhakikisha watumishi ambao wanakaimu na wana uwezo mkubwa, sifa stahiki na weledi katika utendaji kazi wao wanathibitishwa katika nafasi zao ili waweze kuwa na mamlaka kamili.

3.2.9 Taasisi za Serikali kutolipa madeni yake

KWA KUWA, Serikali na Taasisi zake imekuwa na desturi ya kutolipa madeni yanayotokana na kupata huduma kutoka katika Taasisi nyingine ya Serikali na kuwa na mlundikano wa madeni yasiyolipika,

NA KWA KUWA, tatizo hilo limekuwa likichangia kushindwa kutekelezeka kwa miradi ya Taasisi zinazodai kutokana na kukosekana kwa fedha za kutosha za kuendeshea miradi hiyo,

KWA HIYO BASI, Bunge linashauri kuwa Serikali kupitia Msajili wa Hazina kuendelea kuzikutanisha Taasisi zilizobaki zinazodaiana na kuzisimamia ili kuhakikisha madeni yote yanalipwa na kila Taasisi inapata inachostahili ili shughuli za msingi za Taasisi hizo ziweze kutekelezeka.

SEHEMU YA NNE

4.0 HITIMISHO

4.1 Shukrani

Mheshimiwa Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa uongozi wenu makini ulioniwezesha kuwasilisha Taarifa hii hapa Bungeni. Aidha, Kamati imeweza kutekeleza majukumu yake kutokana na maelekezo ya kiti chako ikiwa ni pamoja na ushauri na msaada kwa kipindi chote cha utekelezaji wa shughuli za Kamati.

Kwa namna ya pekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuhakikisha kunakuwa na usimamizi bora katika Taasisi na Mashirika ya Umma na kuweka msukumo wa hali ya juu katika utoaji wa Gawio Serikalini.

Vile vile, napenda kumshukuru Msajili wa Hazina Ndugu Athumani S. Mbutuka kwa ushirikiano wake wa dhati aliutoa kwa Kamati kwa kushauri namna bora ya kuzifanya Taasisi na Mashirika

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ya Umma kuwa na ufanisi katika utendaji na uwekezaji wake na kuleta tija kwa Taifa ili kukamilisha dhima ya Serikali kufanya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Aidha, napenda kuwashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Msajili wa Hazina ambao wamekuwa wakishirikiana kwa karibu na Kamati katika kuhakikisha kunakuwa na usimamizi madhubuti wa Taasisi na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika kuboresha mijadala, maoni na mapendekezo ya kamati na kunipa heshima ya kuiwasilisha Taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Zaynab Matitu Vulu, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Amina Idd Mabrouk, Mb – Mjumbe
4. Mhe. Atupele Fredy Mwakibete, Mb – Mjumbe
5. Mhe. Charles John Mwijage, Mb – Mjumbe
6. Mhe. Daimu Iddi Mpakate, Mb – Mjumbe
7. Mhe. Desderius John Mipata, Mb – Mjumbe
8. Mhe. Edwin Mgante Sannda, Mb – Mjumbe
9. Mhe. Esther Alexander Mahawe – Mjumbe
10. Mhe. Esther Amos Bulaya, Mb – Mjumbe
11. Mhe. Esther Michael Mmasi, Mb – Mjumbe
12. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb – Mjumbe
13. Mhe. Godfrey William Mgimwa, Mb – Mjumbe
14. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Juma Othman Hija, Mb – Mjumbe
16. Mhe. Lolesia Jeremia Bukwimba – Mjumbe
17. Mhe. Maftah Abdallah Nachuma, Mb - Mjumbe
18. Mhe. Muhammed Amour Muhammed, Mb - Mjumbe
19. Mhe. Othman Omar Haji, Mb - Mjumbe
20. Mhe. Qambalo Willy Qulwi, Mb – Mjumbe
21. Mhe. Richard Philip Mbogo, Mb - Mjumbe
22. Mhe. Sonia Jumaa Magogo, Mb - Mjumbe
23. Mhe. Vuma Hole Augustine, Mb - Mjumbe

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano wa hali ya juu alioutoa ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri stahiki na kuiwezesha kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu na kwa wakati. Shukran kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu vema shughuli za Kamati chini ya Kaimu Mkurugenzi Ndugu Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati Ndugu Amina Salumu na Ndugu Elieka Saanya na Msaidizi wa Kamati Ndugu Pauline Mavunde. Pia tunawashukuru Watumishi kutoka Ofisi ya Mshauri wa Mambo ya Sheria wa Bunge Ndugu Seraphine Tamba na Ndugu Matamus Fungo pamoja na Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge kwa ushirikiano wao mzuri.

4.2 Hoja

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii ni matokea ya uchambuzi wa kina kuhusu Uwekezaji wa Mitaji ya Umma unaofanywa na Taasisi na Mashirika ya Umma, maoni na mapendekezo yanayotokana na uchambuzi uliofanywa na Kamati ni kwa lengo la kuishauri Serikali katika eneo la Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili uwekezaji huo ulete tija kwa Taifa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Naomba kutoa hoja kwamba Bunge sasa liipokee Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, kuhusu uchambuzi wa uwekezaji wa Mitaji ya Umma, na kuijadili ikiwa na Maoni na Mapendekezo ili hatimaye Serikali iyafanyie kazi.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja.

Mhe. Dkt. Raphael Masunga Chegeni, Mb

**MWENYEKITI
KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA
UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA**

30 Januari, 2020

MHE. ZAYNABU M. VULLU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Raphael Chegeni, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (*PIC*). Naona hoja imeungwa mkono vizuri sana na sasa Waheshimiwa Wabunge tuanze moja kwa moja na uchangiaji wa jumla kwa taarifa zote mbili.

Naomba tuanze na Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi na baadaye Mheshimiwa Augustine Ole na Mheshimiwa Mbaraka Dau ajiandae. Karibu sana Mheshimiwa Dkt. Sware.

MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Nitajikita katika maeneo manne na nitachangia ripoti kutoka Kamati ya Bajeti ambayo mimi pia ni Mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza nataka niligusia ni juu ya Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148 (*Value Added Tax*). Naishauri Serikali ilianganalie suala hili kwa sababu, kwa hali tuliyonayo sasa Serikali inapopata mikopo mfano kutoka *World Bank* ile mikopo inakuwa *taxed*. Sasa mkopo unautozaje kodi, hususan vile vifaa ambavyo vinatumika kama *capital* inayoenda kutekeleza ile miradi, kwa hiyo, unachukua mkopo, mkopo tena unaukata kodi. Naomba Serikali ianganalie hili jambo upya, japokuwa kuna baadhi ya maeneo tumeyafanyia marekebisho kwenye sheria iliyopita. Kwenye sheria iliyopita tulifanyia kwenye baadhi ya maeneo, lakini kwa ujumla wake naomba sheria hii ianganaliwe upya *Value Added Tax especially* katika mikopo tunayoichukua kutoka *World Bank* ili kutekeleza miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ninalotaka nigusie ni suala la ambalo lina ukakasi kidogo nalo ni katika uchumi wetu, ukuaji wa uchumi. Kumekuwa na sintofahamu kwamba, ukiangalia uchumi wa watu au *purchasing power* kwenye *field* tunasema uchumi hauko vizuri, lakini tukija kwenye *paper work* na taarifa za Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango tunahakikishiwa kwamba, tupo vizuri. Kuna baadhi kweli ya sekta zinafanya vizuri kiuchumi nazo zimetubeba, mfano ni sekta ya madini na ujenzi na sekta hizi zimeweza kufanya vizuri kwa kuwa Serikali imewezeza, ime-*feed in funds* kwenye hizi Wizara husika na imefanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa kwa nini Serikali isiangalie kwamba, kumbe ukiiwezesha sekta inaweza ikatutoa kama ilivyofanya kwenye madini na ujenzi, basi hivyo hivyo ifanye kwenye sekta ambayo ni *very sensitive* katika uchumi wetu kwa sababu *majority* ya Watanzania tuko kwenye sekta ya kilimo. Kilimo chenyewe uvuvi au ufugaji au kwenye *forestry*, basi Serikali ianganalie hivyo, ili kututoa kwenye huu mkwamo wa kiuchumi katika *level* ya watu mmoja-mmoja na *purchasing power* kwa sababu huku chini hatuko vizuri, lakini ukiliangalia hilo

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

katika *micro economy level* tunaona kwa ujumla wake iko vizuri, lakini *majority* ya Watanzania tunalia njaa ndio hali ilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu naomba niligusie ni kuhusu Shirika la Taifa la Mawasiliano (*TTCL*). Suala hili tumeweza kulijadili kwa kina katika Kamati yetu ya Bajeti na hali tumeiona kwamba, shirika hili lina uwezo wa kufanya vizuri na kutukwamua katika hali ya uchumi tulionao kutuwezesha kama shirika la mawasiliano namba moja litawezeshwa. Hili pia, sio suala tu la kukuza uchumi bali pia ni hali ya *security* ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hali liliyonayo sasa hivi shirika hili linamiliki minara 207 tu kati ya minara 14,000 ambayo inamilikiwa na sekta nyingine binafsi. Kwa hiyo, shirika hili likiwezesha kama wataenda kwenye teknolojia *advanced* zaidi kama tuta-*invest* zaidi labda ni *satellite level* au kununuliwa *telephone towers* au watawekeza kwenye mambo ya mawasiliano kwa ujumla wake au *internet* basi shirika hili linaweza kutoka, lakini kwa hali iliyopo sasa hivi shirika hili linasuasua na ni vigumu kwake ku-*compete* na mashirika mengine kwenye masuala ya mawasiliano na pia tuna-*risk* nchi yetu kwenye masuala ya *security*, kwa sababu huyo anayemiliki mawasiliano kwa ujumla wake ni muwekezaji kutoka nje, akiamua kuzima mitambo tunaweza tukapata hali ambayo si shwari katika nchi. Kwa hiyo, naomba Shirika la Mawasiliano liangaliwe kwa jicho la ziada kwenye masuala sio tu kukuza uchumi *potential* yake ila pia katika *security* ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ambalo naomba niligusie kutoka katika taarifa yetu ya Kamati na naomba nisisitizie kwa Serikali walichukulie jambo hili kwa unyeti wake nalo ni hali ya mfumuko wa bei. Japokuwa hali ya mfumuko wa bei imekuwa ikishuka mfano ukilinganisha mfumuko wa bei umeshuka kutoka 5.5% mwaka 2017 mpaka 3.5% mwaka 2018, lakini hali hii ya mfumuko wa bei inaweza ikabadilika kwa hali tunayoi-*experience* sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasena hivi? Namba moja, hali ya chakula iko hatarishi kwa sababu ya hali ya hewa tunayoiona. Ni mikoa mingi sana sasa hivi ina-*experience* hali ya mafuriko sio tu ambayo inaondosha uchumi wa wananchi katika mashamba au makazi yao, hii pia wale ambao wamefanikiwa kulima mazao tayari sasa hivi yana hali mbaya kwa sababu ya mvua zinazoendelea kunyesha na majira ambayo hayatabiriki; hilo ni katika Mikoa ya Kigoma, Tanga, Dar-es-Salaam, Iringa, Lindi na kadhalika, kwa hiyo, kuna hali mbaya ya viashiria vya kutokuwa na chakula nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia pia kwa sababu, tuna taasisi yetu ya *NFRA* na Bodi ya Nafaka ya Mazao Mchanganyiko hatukuwapandishia bajeti, hatukuwawezesha kibajeti. *NFRA last time 2019/2020*, hatukuwaongezea bajeti na kazi yao hawa vyombo hivi vya *NFRA* ni kuhakikisha usalama wa chakula nchini, usalama wa chakula nchini ndio usalama wa nchi wenyewe. Tumetoka kuuza mazao yetu nje na sasa tunawa-*task* tena *NFRA* kufanya biashara ilhali chombo hiki kazi yake mahususi ni kuhakikisha usalama wa chakula nchini kwa kununua chakula. Kwa hiyo, naiomba Serikali kupitia maoni yetu ya Kamati ya Bajeti ilichukulie suala hili kwa ukubwa wake na unyeti wake, *NFRA*, Bodi ya Mazao ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko yaangaliwe kwa jicho la kipekee, ilhali tuhakikishe *security* ya nchi yetu kwa kupitia chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kine ambacho ni kitu ambacho tunakiona na tuna-*experience* ni hali ya haya majanga yanayotokea aidha ni kwa sababu ya haya mabadiliko ya hali ya tabia-nchi au pia ni miundombinu yetu wenyewe tumeiharibu basi, mvua zinazonyesha zinakuwa zinaharibu miundombinu na kuharibu kile ambacho ni *sources* za *income* sisi kama wananchi. Kwa bahati mbaya bajeti iliyopita tuliyoipitisha hatukumpatia Mheshimiwa Waziri Mkuu fedha yoyote katika Mfuko wa Maafa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui tutafanyaje Mheshimiwa Waziri husika wa Fedha na Mipango tuna dalili mbalimbali za viashiria vya milipuko ya magonjwa, tuna viashiria mbalimbali vya hali ya wadudu wanaoenda kuharibu mazao, sasa tuko kwenye *in between* tutatokajetokaje. Tunajisifia mfumuko wa bei ndio uko vizuri na unashuka, lakini viashiria vyote vinaonesha kwamba, tunakoenda tutakuwa tuna hali mbaya sana.

Kwa hiyo, naomba sana kwenye haya mambo manne Wizara husika naomba ichukulie kwa umakini wake kwa sababu, ni maeneo ambayo ni nyeti sana kama Taifa letu na kuweza kutukwamua katika hali ya uchumi tuliyonayo. Nashukuru sana kwa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi kwa ushauri mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Augustine Vuma na baadaye Mheshimiwa Mbaraka Dau ajiandae.

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa uhai huu. Kwanza niseme kwamba, naona fahari kubwa sana kuwa Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma. Kamati ambayo kwa kushirikiana na Serikali imefanya mambo makubwa, ime-*improve* vitu vingi sana kwenye mashirika ya umma. Pia nimpongeze Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kuwasilisha vizuri taarifa yetu na nimpongeze pia kwa namna ambavyo anaendelea kuendesha Kamati hii kwa weledi mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza nipende kumpongeza Mheshimiwa Rais yeye mwenyewe kwa kuamua kushirikiana na Mawaziri kuhakikisha kwamba, anasimamia mashirika ya umma kwa ukaribu mkubwa, lakini na weledi wa hali ya juu sana. Usimamizi huu na umakini ambao Rais ameonesha umeleta mafanikio makubwa sana kwenye mashirika ya umma, ziko chagamoto ndiyo, lakini mafanikio ni makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano taarifa imeonesha hapa na imesema kwamba, Shirika kama TANESCO kwa zaidi ya miaka 20 shirika limekuwa linapata hasara zaidi ya miaka 20 wanatengeneza hasara tupu. Na wamekuwa wanatumia fedha za umma kwa ajili ya kujiendesha, yaani wamekuwa wanapokea ruzuku, lakini kwa mara ya kwanza imetoka kwenye shirika linalotengeneza hasara na kuanza kutoa gawio, limetoa zaidi ya bilioni 1.4 mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama haitoshi Shirika la Madini la STAMICO. Hili nalo tangu lmeanzishwa mwaka 1970 halijawahi kutoa gawio lolote Serikalini, lakini chini ya jembe Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli sasa STAMICO imetoa gawio la shilingi bilioni moja. Kama hiyo haitoshi tumeona uundwaji wa kampuni ya *Twiga Minerals*, hii sasa ndio baba lao, shirika ambalo limeenda kufanya mabadiliko makubwa sana. Tumeibiwa sana, tumenyonywa sana na vijana wote wa nchi hii, wasomi, wazee, hata ambao hawajasoma kila mtu alikuwa anajua kwamba, nchi hii ilikuwa inaibiwa kwenye upande wa madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunapata mwanga mweupe kwamba, kwa mara ya kwanza imeundwa kampuni ambayo tutakuwa tunagawana *fifty fifty* yaani 50 wao 50 sisi, jambo ambalo ni maajabu kabisa kwenye nchi yetu kwa hiyo, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. Wabezaji watakuwepo tu watabeza, acha wabeze, lakini Watanzania wenye akili timamu wanaona na wanaona kazi kubwa ambayo anaifanya na wako pamoja na yeye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri kwenye mambo machache. Jambo la kwanza nataka kama alivyosema Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwepo na mabadiliko ya sheria ili tuweze haya mambo ambayo Rais mheshimiwa Dkt. Magufuli anayafanya kwenye mashirika

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mbalimbali yaweze kuwa sheria. Kwa sababu, leo yuko Rais Magufuli na leo amesema, kesho akinyamaza asiposema au kesho akitoka, tuna uhakika gani kama atakayekuja naye atakuja kusema kama alivyosema Mheshimiwa Dkt. Magufuli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wakati anapokea mwaka jana gawio, Mheshimiwa Rais akasema mashirika yote ya umma ambayo hayajatoa gawio leo, akawapa siku 30 nadhani ilikuwa, siku 60, akasema ambao hawajatoa gawio basi bodi za mashirika hayo zimejifuta rasmi. Baada ya kutoa kauli ile ziliongezeka bilioni 20 zaidi, hizi bilioni 20, Mheshimiwa Waziri, Mama Ndalichako anajua, ndizo fedha ambazo zinzenda kutumika kugharamia elimu bila malipo nadhani kwa mwezi ni bilioni 19. Yaani kauli moja tu ya Rais imeenda kugharamikia elimu mwezi mzima nchi nzima. Kwa hiyo, haya mambo tuyafanye sasa kuwa ni sheria kwamba, tufanye mabadiliko ya sheria, sheria isitamke tu kwamba, mashirika yalete gawio, lakini bodi ambazo zitashindwa kuongoza mashirika kuleta gawio ziwe zimejivunja kwa mujibu wa sheria, iwe sheria kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wale ambao watafanya matumizi ambayo hatuyaelewi kwa sababu, matumizi nayo yamekuwa *regulated* na sheria. Kama wataenda kinyume na sheria kwa sababu yako makampuni mengi na mashirika mengi ambayo wanatumia hela hovy hovy tu, sasa lazima tuweke kisheria hii kwamba, wakienda nje ya mfumo wa sheria bodi zenyewe zijivunje na kama haitoshi hata kwenye uwekezaji usio na tija, tumeona NSSF, watu wanaenda kujenga majumba porini huko ambayo hayauziki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tuseme haya tuyaweke kwenye sheria kwa sababu, hawa watu najua wanaenda kufanya uwekezaji mbovu wana akili, kwa nini nyumba zao wanajenga mjini, lakini uwekezaji wanaenda kupeleka maporini? Wanajua, washapiga *percent* zao halafu wanafanya vitu vya hovy. Sasa lazima Sheria itamke kwamba itoe kwamba mtu anapofanya uwekezaji ambao hauna tija ambao kwa wazi wazi unaonekana kabisa kwamba huu ni utapeli, na zenyewe wawajibishwe, Bodi kuvunjwa na kuchukuliwa hatua za Kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Msajili wa Hazina TR, kwanza nimpongeze Msajili wa Hazina Bwana Mbutuka amekuwa ni msaada mkubwa sana kwenye Kamati yetu, ametuongoza vizuri sana na kwa sababu amepewa jukumu la kusimamia Mashirika zaidi ya 200 kwenye nchi hii, mimi nadhani anapaswa kuongezewa raslimali watu lakini pia na raslimali fedha, mashirika zaidi ya 200 ya nchi hii huyu Msajili wa Hazina ndiye anayeangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika 256 kwa hiyo lazima aongewe fedha sisi tunajua kazi ambayo anaifanya kule tunajua kwa hiyo aongezewe pesa na raslimali watu ili aende kuyasimamia vizuri mashirika haya ninaamini akiongezewa fedha na raslimali watu tutajua mengi zaidi kwenye Mashirika huko tukishirikiana na Kamati yetu ambayo iko chini ya Jemedari Mheshimiwa Chegeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba suala la sukari, tumekutana na watu wa Kilombero tukaenda mpaka Kiwandani kwao kutembelea. Suala la sukari nchi hii bado kuna jambo la ziada na nimuombe Mheshimiwa Rais, jambo hili aliingilie kati mwenyewe, ukweli ni kwamba nchi hii ya Tanzania ina ardhi kubwa sana ya kuweza kuzalisha miwa ya kutosha, lakini ukweli ni kwamba tunayo nafasi kubwa sana ya kuongeza uzalishaji wa sukari kinachotakiwa hapa ni utashi tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji wapo, kama tukipunguza *bureaucracy* kwenye Uwekezaji lakini pia kukatoka msukumo mkubwa wako watu wengi ambao wanaweza wakawekeza kwenye sukari na tukapata sukari ya kutosha kwenye nchi hii. *(Makofi)*

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo tu-*burn importation of sugar*, kuagiza sukari nje ya nchi ndiyo kunaleta sukari isiyo na viwango, sukari ya bei ndogo ambayo inakuja kuathiri uzalishaji wa sukari nchini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nimekuwa naona kwenye maduka wanauza, juzi nimeshangaa kweli, kwenye maduka tunauziwa sukari hii nyeupe hii, kwa ajili ya matumizi, juzi wamekuja wataalamu wanatuambia sukari nyeupe ni sukari ya viwandani, siyo nzuri kwa afya mtu kuunga kwenye chai, lakini tunakula sisi, na wengine wanakula wakidhani sukari nyeupe ndiyo sukari tamu, ndiyo sukari ya *premium* kumbe wanakula uchafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hayo yote kama tunakuwa tuna uzalishaji mkubwa wa sukari kwenye nchi yetu maana yake tunaweza kupunguza uingizaji wa sukari isiyo na viwango lakini pia tunaamini tutakuwa tunalinda Viwanda vyetu katika nchi, na tutaongeza uchumi kimsingi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ninalisema kwa uchungu mkubwa kwa sababu ninaamini tunao uwezo wa kuzalisha sukari kwa kiwango ambacho Taifa hili linahitaji na wakati mwingine mpaka tukafanya *exportation* kwa sababu ardhi tunayo, Wawekezaji wapo, kinachotakiwa ni utashi na kuweka mazingira mazuri ya Uwekezaji ili watu waje kulima na kuzalisha sukari. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kabisa ni kuhusu hawa watu ambao wanakaimu Ofisi, ooohh! muda umeisha nadhani...

MBUNGE FULANI: Bado! Bado! bado.

MWENYEKITI: Malizia sentensi yako ya mwisho....

MHE. AUGUSTINE V. HOLLE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, Makaimu hawa ufanisi wao wa kufanya kazi ni mdogo kwa sababu mtu anapokuwa anakaimu nafasi yake *confidence* ya kufanya kazi inakuwa ni ndogo sana. Kwa hiyo, Mashirika mengi yana watu ambao wana Kaimu tunaomba Mamlaka ili jambo kama tumeweza kuchomoa Wafanyakazi hewa tukafanya hiyo, hili linashindikana vipi kwenye Mashirika haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye uchunguzi mzuri wa ambao wanafaa wapewe nafasi zao na ambao hawafai basi waondolewe wapewe watu wengine ili kuondoa suala la kukaimu kuongeza ufanisi kwenye Mashirika ya Umma. Nakushukuru sana naunga mkono hoja. Ahsante. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Vuma, tunaendelea na Mheshimiwa Mbaraka Dau.

MHE. MBARAKA K. DAU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema hii ya uhai na pumzi na leo tumeweza kukutana hapa kuweza kujadili masuala mbalimbali yanayohusu nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru kwa namna ya kipekee sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Jemedari Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalazimika kuyasema haya mapema kwa sababu kwa namna ya kipekee sisi wananchi tunaotokea Mafia Kisiwani tumepata Ghati la Nyamisati ambalo limeshakamilika na Serikali hivi sasa inakamilisha Kivuko kwa ajili ya wananchi wa Mafia

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ambacho kitakuwa tayari nadhani kama siyo mwezi ujao basi utakuwa ni mwezi wa tatu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo niye kwenye mada husika, nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati zote mbili kwa namna ambavyo wamewasilisha taarifa zao hapa za mwaka. Nitajadili zote kwa pamoja, Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma pamoja na Kamati ambayo pia ninaihudumu Kamati ya Bajeti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati ya Bajeti inasema TRA wamefanya vizuri sana katika ukusanyaji wa mapato na tunawapongeza sana na uwepo wa Kamishna Jenerari Mpya pale naamini umekuwa ni chachu wa kila siku tunayoiona TRA inavunja rekodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefika sasa mpaka trilioni 1.5 kwa kweli ni mafanikio makubwa sana. Nasahihishwa hapa trilioni 1.9 ni mafanikio makubwa sana kwa kweli na tunawashukuru sana tunampongeza sana Kamishna Jenerari na tunaamini kwamba wataendelea kuvunje rekodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini taarifa inasema mapato yanayotokana na vyanzo ambavyo si vya kikodi hayajafanya vizuri sana. Sasa eneo hilo nafikiri ipo haja ya kuhakikishwa kwamba tuna *improve*, mwaka jana hapa tulipitisha Sheria hapa kuhusu masuala ya Bandari kwa sababu maeneo ambayo vyanzo vingi sana maeneo ambayo kule mapato yanakopotea sana ni kwenye hizi zinaitwa bandari bubu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tulipitisha Sheria hapa ambayo tumempa Mamlaka Waziri Mwenye dhamana ya masuala ya Bandari aweze kurasimisha Bandari ambazo anaona inafaa. Sasa nafikiri labda kama wenyewe wapo hapa watakapokuja na wao kuchangia watuambie watu wa Bandari, wanaohusika na dhamana ya Bandari, hivi mpaka sasa wamerasimisha Bandari ngapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano sisi tunaotoka kule kwetu kule Bandari zimekuwa nyingi sana na mapato ndiko yanakovuja vuja kule ili twende vizuri, lakini eneo jingine ni eneo ambalo ya mapato ambayo pia si ya kodi, mwaka jana na mwaka huu pia nilizungumza hapa kuhusu namna gani sasa kwa sababu tunaiona TRA inaweza kukusanya kwa asilimia nyingi sana na wako vizuri, lakini sasa inaonekana kwamba tunamkamua yule ng'ombe sasa anakaribia kumaliza maziwa yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ipo haja ya kuongeza *tax base* na kuangalia maeneo mengine ambapo Serikali sasa inaweza ikapata mapato ambayo pia mengine wala si mapato ya Kikodi na tulizungumza hapa mwaka jana na ninashukuru sana nimemuona Waziri Mwenye dhamana ya Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba yapo maeneo ambayo Serikali ikiwekeza kwa mfano kwenye uvuvi wa Bahari Kuu, kwenye Uvuvi wa Bahari kuu, bado hatujafanya vizuri sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imebahatika kuwa na Mawaziri ambao ni *very aggressive* na mimi ninawashukuru na ninawapongeza sana, wanafanya kazi nzuri sana. Lakini tunahitaji tuongeze nguvu zaidi kwa sababu mapato haya ambayo ninaamini tunayakosa kule kwenye uvuvi wa Bahari Kuu ni mapato makubwa sana. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeiangalia taarifa hii, pia tulitenga na fedha kwa ajili ya ujenzi wa Bandari ya Uvuvi sijui tunakwenda vipi? Na nimeona pia kwamba Serikali ina Mpango wa kununua meli yake yenyewe ya Uvuvi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nitoe angalizo kidogo hapa, isije ikawa ile hadithi ya Kuku na yai, kipi kianze, unaweza ukawa na Bandari ya Uvuvi pamoja ukanunua na Meli lakini kinachotakiwa kuanza hapa tuanze kwanza na ujenzi Bandari halafu meli ije, kwa sababu tutakuwa tunanunua kutokana na gharama kubwa za ununuzi wa Meli hizi za Uvuvi ambayo gharama zake ni kubwa naona. Serikali tungewekeza kwanza kwenye Miundombinu ya Kibandari ambayo *multiply effect* yake ni kubwa sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu wananchi kutakuwa na Viwanda mule vya kuchakata mazao mbalimbali ya samaki, ambayo yatafanya biashara ya minofu kama ile ambayo iliyokuwa ina-boom miaka ile ya 90 kule Mwanza na sisi tukaweza kuitumia Bahari Kuu yetu iweze kutu-feed na minofu ya samaki aina ya *tuner* ambao wanapatikana zaidi sana katika Pwani yetu hii ya Tanzania. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nashauri na Mheshimiwa Waziri unanisikia ni vizuri sana tukaharakisha mchakato ule wa kuwa na Bandari na Uvuvi tukishakuwa na Bandari ya Uvuvi baadaye meli, hata meli za wageni sasa tukazikaribisha zikaja alimradi kwamba wanapovuna mazao yetu kule Bahari Kuu wasiende nayo nje yarudi ndani ili yaweze kutoa ajira pamoja na mapato mengine zaidi ya Kiserikali ambayo yatasaidia katika kuboresha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala tulilizungumza kwenye Kamati suala la namna gani TRA inaweza ikakusanya Kodi ya Majengo, Kodi ya Majengo ni ushauri ambao ulitolewa na sikuiona kwenye taarifa lakini naomba niusisitize hapo, kwamba Kamati ilishauri katika mjadala badala ya kuanza kuhangaika na Wafanyakazi wa TRA wakaingia mitaani kwa wingi kwenda kufuata nyumba hadi nyumba. Inawezekana *workforce* hiyo tukawa hatuna na moja ya *principle* nzuri za ukusanyaji wa kodi, lazima Kodi iwe *convenient*, lazima kodi iwe *economical* huwezi ukatumia gharama nyingi sana kukusanya Kodi ambayo mwisho wake ile Kodi inakuwa ni ndogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, likaja wazo na naomba sana wenzetu wa Wizara ya Fedha na Mipango waliangalie pamoja na TRA likaja wazo kwamba hii kodi ya majengo kwa nini isiingizwe katika bili ya luku? Bili ya luku halafu ikawa *spread* kwa muda wa miezi kumi na mbili ili mtu anaponunua luku basi anakuwa ameshalipa Kodi yake ya Majengo, lakini na kubwa zaidi ni kwa sababu sasa hivi umeme umesambaa karibu nchi nzima, na kwa taarifa tulizo nazo kutoka kwa Wizara husika ni kwamba mpaka kufikia Juni mwakani 2021 tutakuwa tumefikia vijiji vyote. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi ninaamini kwa kutumia utaratibu huu Serikali inaweza ikakusanya Kodi yake ya Majengo TRA bila ya bughudha bila ya kukimbizana na watu, au kuongeza *workforce* kubwa zaidi kuanza kuingia ingia kwenye *address* mbalimbali najua kuna changamoto. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengine ya kibiashara labda nyumba moja inaweza ikawa na fremu za maduka labda thelathini, arobaini na kila fremu ina mashine yake ya luku lakini haya ni mambo ambayo *administratively* wanaweza wakaripoti baadaye wataalam au Watendaji wa TRA wakaenda maeneo kama hayo waka-*harmonize* hayo mambo na Serikali ikaweza ikanufaika zaidi na mapato. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine tumeona ufanisi mzuri wa ile *ETS* ile *stamp* ya Kodi kwenye bidhaa ilivyoanza inafanya vizuri na kwa kuwa taarifa zinaonekana kwamba tunakwenda vizuri, nilikuwa nashauri tu na Mheshimiwa Mwenyekiti wangu wa Bajeti ambaye ndiye mtoa hoja kama mtaona inafaa basi twende kuishauri Serikali sasa twende ku-extend zaidi bidhaa za aina nyingi zaidi ziingie kwenye utaratibu huu wa *ETS* kwa sababu umeonekana kwamba ni wenye manufaa makubwa sana na unaleta mapato mengi ya Kiserikali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza nizungumzie jambo moja dogo kuhusiana na *TRA*, *TRA* wanatoa *certificate* kwa hizi Taasisi *NGO's* ambazo zinakuwa wanapata kama *exemption* ya kulipa kodi, na kule kwetu sisi tuna shida kidogo, tuna shida, kuna wawekezaji wamewekeza pale wanataka kuja kutupatia sisi kitu kinachoitwa *CSR* ile *Cooperate and Social Responsibility* kwa ajili ya kurudisha kwa jamii ya Mafia. Lakini hawa Wawekezaji wanatuambia kwamba wataipatia Halmashauri ya Mafia msaada wa bilioni mbili, lakini ule msaada wa bilioni mbili ukija ukiuchanganua na ninaamini wenzangu wa *TAMISEMI*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukija ukiuchanganua ni kwamba ni mafunzo, ni semina ni tiketi za ndege za Wawezeshaji kutoka Ulaya kulala katika *five star hotel* na mambo mengine, lakini kinachokwenda kwa wananchi wa Mafia wenyewe ni *almost* sifuri kwa sababu wanakuja wao na *ma-translators* wao kwa ajili ya kutafsiri kwa watoto eti wanasema wanawafundisha namna ya ujasiriamali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo limetuletea matatizo sana na Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Waziri Jafo kama upo nililileta kwako na ukasema kwamba utachukua hatua, kuna tatizo pale tunarundikiwa jambo, tunaambiwa *CSR* ya bilion mbili lakini ukweli hasa hakuna kitu kule *on the ground* na hii nimelisema hapa kwa makusudi, nimelisema hapa kwa makusudi kwa sababu lina *tax implication* kwa ajili ya *TRA* tuangalie Taasisi hizi sasa ambazo zinakuja kwa wananchi wetu na inaweza likaja likawa swali kwamba inakuwaje kwamba hayo mambo si mgeweza tu kuyamaliza huko kwenye Baraza lako la Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye uendeshaji wa haya mambo kuna kitu kinaitwa *technical no how* na kuna kitu kinaitwa *technical no who*, sasa kwenye *technical no how*, nimejaribu kujenga hoja sana ili jambo liishe kule lakini wenzangu wamenizidi kwenye kitu kinaitwa *technical no who*, na ninaamini Waziri Mwenye dhamana wa hiyo unanielewa nina maana gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Mbaraka Dau kwa kukamilisha uchangiaji kwa asubuhi hii mpaka mchana huu. Waheshimiwa Wabunge nawashukuru kwa kuwajibika vizuri toka asubuhi hadi mchana huu.

Kabla sijasitisha shughuli za Bunge naomba niwataje Wachangiaji hawa wataanza kuchangia hapo jioni, tutaanza na Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Sonia Magogo, Mheshimiwa Charles Mwijage na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab. Baada ya kuwataja hao, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 kamili Jioni.

(Saa 07.00 Mchana, Bunge lilisitishwa hadi Saa 11:00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa tukae.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu na tutaanza na Mheshimiwa Sonia Magogo na baadaye Mheshimiwa Mheshimiwa Halima James Mdee ajiandae.

HOJA ZA KAMATI

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI HIYO KATIKA KIPINDI CHA MWEZI FEBRUARI, 2019 HADI JANUARI, 2020

NA

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI WA MITAJI YA UMMA KUHUSU SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI HIYO KATIKA KIPINDI CHA MWEZI FEBRUARI, 2019 HADI JANUARI, 2020

(Majadiliano Yanaendelea)

MHE. SONIA J. MAGOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu. Kabla sijaanza kuchangia nianze kwa kuwapongeza Wenjeviti wetu wa Kamati kwa wasilisho zuri. Nijielekeze sasa moja kwa moja kwenye kuchangia kwenye Kamati ya Uwekezaji ambayo ndiyo Kamati niliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua dhamira kuuu ya Serikali kuwekeza katika mashirika ya umma ni pamoja na kukuza uchumi wa nchi, kuchochea maendeleo ya sekta mbalimbali na kutengeneza ajira kwa wananchi. Pamoja na haya yote, tumekuwa tukushuhudia Serikali ikiwekeza fedha zake kwenye baadhi ya mashirika, lakini mashirika haya miaka yote yamekuwa yakizalisha hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sioni sababu ya kwa nini Serikali iendelee kuchoma pesa zake kwenye mashirika haya ambayo hayana tija. Kwa sababu Serikali imekuwa ikitoa mitaji yake kulingana na mahitaji ya mashirika yale, lakini unakuta mashirika mengine yanafanya vizuri sana na mashirikia mengine yanashindwa hata kutoa gawio kwa Serikali. Kwa hiyo badala kuendelea kuyaangalia haya mashirika ambayo yamekuwa yakizalisha hasara kila mwaka ningeshauri Serikali iangalie kwa upande wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitolea mfano wa Mkoa wangu wa Tanga, Mkoa wa Tanga tumejaliwa kuwa na viwanda vingi sana, lakini vile viwanda sasa hivi vimegeuka kuwa magofu, mfano tulikuwa na Kiwanda cha Chuma, Kiwanda cha Mbolea, Kiwanda cha Mkonge, Matunda na Chai. Hivi viwanda vyote sasa hivi havifanyi kazi. Iwapo serikali itaviangalia hivi viwanda na kuviwezesha nina imani vinaweza kuleta tija katika mapato na vilevile kuongeza ajira kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine nigusie mashirika yenyewe ambayo Serikali inaweka mitaji yake. Hizi taasisi unakuta zenyewe kwa zenyewe zinasababishana kurudurishana nyuma na kuweka ugumu katika utendaji. Hii ni kwa sababu utakuta taasisi moja inaihudumia taasisi nyingine kwa mkopo, lakini imekuwa ni ngumu sana zile taasisi kurejesha ile mikopo kwa wakati, hivyo kufanya ugumu katika utendaji wa hizi taasisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuchukulie mfano mashirika ya hifadhi ya jamii, haya mashirika sehemu yake kubwa ya uendeshaji yanategemea michango ya wanachama ya kila mwezi. Unakuta michango ile ya wanachama inakatwa vizuri kwenye mishahara wa mwanachama, lakini haipelekwi kwa wakati ama haipelekwi kabisa sehemu husika. Hii hupelekea Mifuko yetu

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

hii ya Hifadhi ya Jamii kufanya kazi katika mazingira magumu sana. Hivyo, niombe Serikali ingalie ni namna gani inaweza kusaidia haya mashirika ambayo yamekuwa yakitoa huduma na mwisho wa siku hayapati mrejesho wa fedha ili yaweze na yenyewe kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo ningezumzia suala la ubunifu; unakuta mashirika yetu haya yana fursa nyingi sana ambazo wanaweza kuzitumia na kupata kipato ambacho kingewasaidia kujiendesha wakati wanasubiri ruzuku za Serikali. Kwa kushindwa kutumia ubunifu wao wanakaa muda mrefu bila kutekeleza majukumu yao, kwa sababu ya kukosa ruzuku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio hilo tu hata kwenye kujitangaza, sisi wenyewe kama Wajumbe wa Kamati tulikuwa tunakwenda maeneo mengine tunashangaa. Tunakuta bidhaa ambazo ni nzuri sana lakini sisi wenyewe hatufahamu kama zile bidhaa zinategenzwa mahali pale ama zinapatikana pale. Kwa hiyo kwa kujitangaza haya mashirika itasaidia kukuza kipato chao na kuweza kutoa gawio kwa Serikali.

Pia niipongeze Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa jitihada zao walizofanya na wanazoendelea kufanya na kupelekea kupata gawio zuri kwa mwaka 2018/2019. Pia niombe Serikali iangalie yale yaliyoainishwa kama changamoto na Msajili wa Hazina ikiwemo mfumo hafifu wa TEHAMA, Sheria ya Msajili wa Hazina, ongezeko la mahitaji ya watumishi wenye utaalum na kukosekana kwa mfumo wa fedha za uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo pia ningekazia kwamba hii Ofisi ya Msajili wa Hazina iongezewe bajeti, kutokana na ukubwa wa kazi yake ili iweze kufanya kazi yake kwa ufanisi na tupate kile tunachokihitaji. Kwa upande kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina ningependa kushauri wafanye *Audit Management* za mara kwa mara kwa haya mashirika na taasisi ambazo Serikali inawezeza fedha zake. Kwa sababu tumeshuhudia hapa kuna mashirika yalikuwa yanasema kwamba hawawezi kutoa gawio, lakini baada ya kupewa siku 60 wameweza kupata, wengine wameanza kuleta gawio, kwa hiyo hii inaonesha kwamba wakati mwingine taarifa wanazotoa zinakuwa sio sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Sonia Magogo. Tuendeleo Mheshimiwa Halima James Mdee, baadaye Mheshimiwa Jitu Soni na Mheshimiwa Balozi Adadi ajiandae.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Nitaanzia kuchangia kamati ya PIC, ukurasa wa 25 ambao unazungumzia mashirika ambayo yanafanya matumizi kuliko uwezo wake wa kukusanya na vilevile uwezo ama faida ya shirika kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kwenye Shirika la Nyumba hasa ukizingatia kwamba mimi ni Mbunge wa Jimbo la Kawe na katika kipindi cha mwaka 2000 – 2015, kulikuwa kuna miradi mingi sana ya ujenzi ambayo ilikuwa inasimamiwa na Shirika la Nyumba la Taifa na kama miradi husika ingefanikiwa Serikali ingeweza kupata mapato mengi; mosi kwa kutumia *property tax*, lakini pili kwa kutumia uuzaji wa nyumba ama kupangisha nyumba na shughuli zozote za kijamii zilizokuwa zikiendelea ama ambazo zingendelea katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia taarifa ya PIC inaonesha kwamba Shirika la Nyumba la Taifa mwaka 2016/2017, mapato yalikuwa bilioni 154 matumizi 122; mwaka 2017/2018 mapato milioni 116, matumizi bilioni 83.2. Hata hivyo, ukiangalia taarifa ya Kamati inaonyesha kwamba ina dhamira ya kulaumu shirika zaidi pasipo kuangalia shirika limefikaje hapo. Sote tunajua kwamba mpango wa ujenzi wa nyumba *Regent*, ujenzi wa nyumba

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Morocco, ujenzi wa nyumba 711 (I) Kawe na ujenzi wa nyumba 711 (II) Kawe zimekwama kwa sababu Waziri wa Fedha amegoma kutoa kibali cha Shirika la Nyumba kuweza kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Waziri wa Fedha atujibu hili kwa sababu jana wakati Mwenyekiti wa PAC alipokuwa akizungumza na hili Bunge alisema, kutokana na miradi kukwama miradi yote mwaka 2017 Serikali inalazimika kumlipa mkandarasi kila siku ya Mungu shilingi milioni 20, kila siku ya Mungu. Hapa tunapozungumza *project* hizi nne tofauti kuna wakandarasi wanne tofauti. Sasa hii milioni 20 inalipwa kwa mkandarasi mmoja ambaye yupo kwenye *project* moja ama inalipwa kwa wakandarasi wanne, ama kila mkandarasi kati ya hawa wanne analipwa hiyo hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana huu mradi tunaeleza mimi ni jimboni kwangu 711(I) ulianza kufanyiwa kazi kwa 20% imewekezwa pale milioni 26.3, mradi ambao umekwama. Kwa hesabu ambazo Mwenyekiti ametuambia jana, kama kwa siku wanalipwa milioni 20 kwa *project* kwa mkandarasi. Tafsiri yake kwa mwaka wanaojua mahesabu zinakaribia bilioni saba kwa mwaka. Kwa miaka mitatu kuanzia mwaka 2017 mpaka sasa hivi tafsiri yake kuna bilioni karibu 21 ama 26, mimi nimesoma sheria mambo ya hesabu hesabu siyajui 21.6 nimeambiwa hapa na wachumi, zinadondoka chini kwa sababu tu kuna Waziri wa Fedha mmoja ambaye hata kama shirika limefikia ukomo lakini lilikuwa lina *business mind*, fedha ingeweza ikarudi zaidi ya kile ambacho kimekopwa na faida. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka mitatu mfululizo, mradi umekwama, juzi kama miezi kadhaa iliyopita niliuliza swali hapa Wizara ya Ardhi akajibu Naibu Waziri wa Ardhi, nikauliza ni kwa nini Mradi wa Kawe, Kawe 711 (I) 711 (II) Morocco na Regent imekwama; akaniambia eti ni kwa sababu Serikali imehamia Dodoma, kwa hiyo nguvu zote zilizokuwa zifanyike kwenye zile *project* zimehamia Dodoma. Serikali isiyokuwa na *vision*, Serikali isiyokuwa na mipango, anayeibuka anaibuka na jambo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni nini? Mradi wa *phase II* ambao ulikuwa unagharimu bilioni 103 na wenyewe, ile ni *phase I*, umefanywa kwa 30% tu, umetumia bilioni 34.8 mradi umelala. Kwa hiyo tafsiri nyingine na huyu mkandarasi wa pili na yeye analipwa milioni 20 yake kwa siku amekaa tu anakula bata halafu leo wanasema wana uchungu wa Watanzania, wana uchungu na matumizi ya fedha, *we can't allow this*. Nina ripoti ya CAG hapa, naomba ninukuu CAG amesema nini kuhusiana na hayo mamlaka ambayo Mheshimiwa Waziri anayo lakini ameamua kuyakalia. Anasema hivi

"Ikiwa NHC haitapata kibali cha kukopa na kushindwa kukamilisha miradi yake itapaswa iwalipe wakandarasi jumla ya shilingi bilioni 99.99 kutokana na uvunjaji wa mkataba." (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii fedha ni extra ya zile bilioni 21 ambazo tunazimwaga chini kwa sababu tu ya maamuzi ya kiseru ya kukurupuka. Pia anasema:

"Pia itawapasa kufanya marejesho ya shilingi bilioni 2.6 kwa wateja walioanza kulipia malipo ya awali ya ununuzi wa nyumba hizo."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kawe ama lile eneo ni *very strategic* yaani NHC walikuwa wanapata wateja kabla hata hawajamaliza ujenzi. Kwa hiyo kulikuwa kuna uhakika wa fedha upo hapa mkononi, kulikuwa kuna uhakika wa kodi za majengo, Mheshimiwa Mpango aliamua kutunyang'anya halmashauri *property tax* ili lile kapu lake linenepe. Kwa akili yangu iliniambia kama kweli yeye ni Mchumi maana sisi wengine ni Wanasheria makanjanja, uchumi hatujui, uchumi wake ungemwelekeza kwamba kuwekeza kwenye zile nyumba kungeweza kulisaidia hili Taifa. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba nipate majibu ya uhakika kutoka Serikalini *project* za Shirika la Nyumba, nimeamua nisimame nizungumze nyumbani kawe na nilizungumze shirika letu ambalo chini ya akina Mchechu tulikuwa tunaliangalia kama shirika la mfano. Halafu wanakuja watu wanasema, hatuwezi kukulipa milioni kadhaa. Lazima awalipe watu mamilioni kutokana na *brain*, kama *brain* yao inaleta *trillions* wawalipe kwa thamani hiyo. Wanakaa wanawaza kimaskini halafu wanataka *productivity*, hakuna vitu kama hivyo. Hata wenzetu waliotangulia huko *brain* yako ndio inaangalia kipimo chako cha mshahara. Kama wewe ni kilaza utapata hivi, kama Mungu amekujalia kuwa hivi utapata hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri tupate majibu ya haya mashirika na waache kusakizia ama kutupa mzigo kwa wetendaji wetu, wakati kinyumenyume wao ndio wanaovuruga na kuyanyonya mashirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nashukuru sana na natarajia Mwenyekiti anatanipa majibu. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati msilembelembe hizi taarifa. Nimeangalia jana taarifa ya PAC, ukiangalia CAG ana hoji mambo mengi ya muhimu, wanakuja hapa wanachagua vieneo vichache ili kuonyesha Serikali imefanya *wonders* kumbe kwenye hizi taarifa kuna mambo ya ajabu, mambo ya hovy ambayo Bunge tunatakiwa tusimamie kwa maslahi mapana ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, Mheshimiwa ndio nimerejea kama hivyo, msiyempenda amekuja. Ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee. Tunaendelea na Mheshimiwa Jitu Soni na baadaye Mheshimiwa Balozi Adadi na Mheshimiwa Richard Mbogo ajiandae. Mheshimiwa Jitu Soni.

MHE. JITU V. SONI: Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze Wenyeviti wote wawili kwa kutuletea taarifa nzuri, lakini pia na kamati kuchambua kazi walizofanya ndani ya mwaka mzima. Ni taarifa ambazo zinatupa dira lakini kuna maeneo ambayo tungependa kuchangia ili kuboresha zaidi ili na wao katika Kamati zao waendee kuishauri Serikali ili kufanya mabadiliko makubwa zaidi na tuweze kupata mafanikio makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitachangia Kamati zote mbili. Moja, naomba nichangia kwa upande wa Kamati ya Bajeti. Nishukuru kwamba taarifa yao kwa sehemu kubwa inaonesha kazi ambazo zilipangwa na ambazo wamefanya, lakini bado naomba niendeleo kuisitiza Kamati iendeleo kuifanyia kazi sekta nzima ya kilimo kwa mapana yake; kilimo, mifugo na uvuvi kwa sababu ndio inachangia kwa 27% kwenye pato la Taifa, lakini ukuaji wake bado ni 4.3%. Bado ni mdogo sana, tulitegemea sekta ya kilimo ukuaji wake ungekuwa angalau 20% au 30% kutokana na watu wengi kuwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo yote inatokana na kutokuwekeza kwenye Sekta ya Kilimo. Pia, siyo kuwekeza tu kwa Serikali au kuweka labda fedha ya kutosha na bajeti zilizopangwa, yaani *budget approval* na zile *disbursed* kuendana sawa kwenye fedha za maendeleo, lakini bado kuna changamoto nyingi ambapo Kamati hii ya Bajeti pamoja na Kamati ya Uwekezaji inaweza kutusaidia kwa kuhakikisha kwamba ile *blueprint for regulatory authorities* yaani *reforms* zile ziletwe haraka, kwasababu kwa mwendo tunaoenda, bado itatuchukua labda miaka mitano au kumi kufikia huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilimo hakiwezi kukua kwa sababu bado kuna kodi, tozo na ada nyingi sana ambazo zinazuia sekta hiyo kukua. Tunaondoa kitu kimoja kwa mwaka wakati ilitakiwa viondolewe vitu zaidi ya 50 au 60 ambavyo itafanya Sekta ya Kilimo kukua sana. Moja

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwa wale ambao ambao wamesajiliwa kwenye sekta ya kilimo ni kuwa rasmi (*formal sector*). Wale ambao wana kampuni wanalipa kodi, ada, tozo nyingi sana ambapo yule ambaye hajasajiliwa (*informal sector*) halipi chochote zaidi ya ushuru; kama ni ushuru, ni ushuru wa mazao. Hiyo inafanya wengi waondoke kwenye *formal sector* na kurudi kwenye *informal sector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye taarifa nzima utaona Sekta ya Kilimo, kwa mfano *horticulture* ambayo inaingiza zaidi ya dola milioni 680 kwa mwaka, hiyo bado hujajumuisha mboga mboga na matunda ambayo yanauzwa humu nchini ambayo ni zaidi ya mazao mengine yote au bidhaa yoyote nyingine yoyote inayozalishwa nchini, lakini sekta hiyo inachukuliwa kama ni sekta isiyokuwa rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili sekta hii iweze kuwa na nguvu zaidi, ni vizuri zile kodi, tozo, ada na ushuru mbalimbali ambazo ndiyo kikwazo zingeendelea kuondolewa. Nami napendekeza, ili tuendelee kuwa vizuri kwenye umwagiliaji, mitambo ile ya kuchimba mabwawa ya maji ingeondolewa kodi, kwa sababu bidhaa wanayozalisha huwezi kutoza kodi ya VAT. Kwa hiyo, wale wakileta hawapati ile *exemption* kutokana na mitaji (*Capital goods*). Kwa hiyo, bado kwa wao hiyo kodi inakuwa ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sekta nyingine, kwa mfano, ya madini au ya viwandani, akileta hiyo bidhaa wao hawajali. Wanalipa hiyo kodi kwa sababu au watapata hiyo *exemption on capital goods* kwa sababu bidhaa zao ziko *vatable* watasamehewa. Sasa kwenye Sekta ya Kilimo, hiyo haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumesamehe kwa mfano kwenye majokofu, kwenye *cold rooms* kwa ajili ya *horticulture*, lakini tungeenda mbali zaidi, hiyo hiyo gari ndiyo inatumika kwenye maziwa na samaki. Kwa hiyo, wangeangalia kwa mapana yake. Ni vizuri Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo, Wizara Mifugo zote zikae pamoja na kuangalia kwa mapana yake. Pia nyingine hazipo Wizara ya Fedha. Unakuta tozo na ada mbalimbali zipo katika taasisi mbalimbali kwa mfano OSHA iko sekta nyingine, *fire*, yote haya wanalipwa kwenye Sekta ya Kilimo. Ndiyo maana hata tukiondoa kodi yote kwa upande wa Wizara ya Fedha ikawa sifuri, bado hizi nyingine zikitozwa bidhaa ya nje bado itaendelea kuwa bei rahisi na hatutaweza kuendeleza kilimo hapa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni vizuri kwenye Sekta hii ya Kilimo na Mifugo Serikali ingekaa na Wizara nyingine zote wahakikishe kwamba ile *blueprint for regulatory authorities*, ile *reform* ifanyike haraka; na kwenye bajeti hii tunatarajia itakuja vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali iangalie kwamba watakuwa wanapata *indirect taxes*. Siyo lazima upate *direct tax*, tuangalie *indirect tax* ambayo itafanya Serikali ipate mapato makubwa zaidi na huduma kwa wananchi itaongezeka sana. Vile vile *coordination* baina ya Wizara moja na Wizara nyingine zote, jambo hilo pia lazima lifanywe vizuri na ninaamini Kamati hii ya PIC inaweza ikatusaidia kwa kuunganisha pamoja na Kamati zote ili chini ya Waziri wa Uwekezaji, jambo la uwekezaji wa ndani na wa nje yote iende sambamba

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukirudi pia kwa upande wa uwekezaji, nashauri kwa mfano kwenye shirika letu, kama tulivyopendekeza Serikali iwekeze, tunaipongeza kwamba TTCL sasa inafanya vizuri, lakini mngeiongezea mtaji wa kutosha. Kwa sababu leo kampuni binafsi ambayo wanachukua *data* kutoka TTCL na kuuza kwa wateja ambao ni raia wa kawaida, ni vizuri TTCL pia ingepata mtaji wa kutosha nao waendeleo kusambaza mawasiliano, *data* pamoja na *voice* ili iweze kuwa na nguvu kama tulivyosema kwa upande wa NIC.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria nyingi ambazo ziliunda haya mashirika zimepitwa na wakati. Ni vizuri zingeangaliwa upya ili zifanyiwe marekebisho ili mashirika haya pia yaweze kuwa na mchango mkubwa katika pato la Taifa lakini pia wananchi kuendelea kupata huduma vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbali na hiyo, kama nilivyosema kule kwenye Sekta ya Kilimo, ni vizuri tukaangalia bajeti ambayo imekuwa *approved* na bajeti ambayo inakuwa *disbursed* bado haijakaa vizuri. Ni muhimu wakaangalia nini kitapunguza gharama ili uzalishaji wa ndani uweze kukua na viwanda vya ndani viweze kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukiagiza viwanda vidogo vidogo ya vya thamani ya shilingi milioni 10, 20 au 30, vinatozwa kodi kama kawaida na wakati wa kuingiza hawapati ule msamaha wa *capital goods* ambayo ingesaidia viwanda hivi vidogo na Watanzania wengi wangeweza kuwekeza huko kwa sababu umeme umeenda katika maeneo mengi, pongezi kwa Serikali. Hiyo ingetusaidia kuwa na viwanda vidogo ambapo bidhaa zinazoenda viwandani zingekuwa zinatoka kwenye sekta ya kilimo, mifugo, uvuvi na ingetusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine muhimu ambalo Kamati inaishauri Serikali ni suala hili la *informal sector* na *formal sector*. Leo hii tumeona *informal sector* inaendelea kukua na hiyo ni kutokana na kwamba *formal sector* ndiyo wanakamuliwa, wanatozwa kodi, ada, tozo na ushuru mbalimbali ambayo inawafanya wengi sasa kukata tamaa na wengi sasa wanarudi kuwa *informal sector*. Lengo la Serikali ni kuwa na *formal sector* ambayo ni *strong*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuwaandikisha hawa walipa kodi kuongeza wigo ni muhimu sana kwa sababu wengi wakilipa, Serikali itaweza kupunguza kodi na ushuru mbalimbali ili jambo hili liweze kufanikiwa. Ombi langu ni kwamba Serikali ikubali kuunda taasisi moja, *Tanzania Regulatory Authority* ambayo taasisi zote hizi zitakuwa chini yake ili sasa mfanyabiashara alipe mara moja halafu sasa huko ndani wanagawana ili tuweze kudhibiti watu kwenda kudai fedha na kupiga faini za ajabu ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo, naomba nishukuru na kupongeza Kamati zote mbili kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Jitu Soni. Tunaendelea na Mheshimiwa Balizi Adadi, baadaye Mheshimiwa Richard Mbogo na Mheshimiwa Ester Mmasi wajiandae.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru sana kupata nafasi hii ya kuchangia hoja hizi za Wenyeviti wote wawili. Kabla sijaendelea, napenda kuungana na ndugu na Waheshimiwa Wabunge wote kumwomba ndugu yangu, rafiki yangu na jirani yangu ambaye alikuwa anakaa hapa ambaye ametangulia mbele ya haki. Tuzidi kumwomba ili roho yake iende peponi huko alikotangulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Rais na Mawaziri na Maofisa wote ambao wameshughulika kwenye mapatano ya mkataba wa Barrick ambao naamini kabisa kwamba utatuongezea pato la Taifa katika siku za hivi karibuni. Mkataba huo ni mzuri na ni vizuri mikataba kama hiyo basi ikafanyika kwenye sekta nyingine na siyo madini tu.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda kumpongeza Waziri na Maofisa wote kwa kuweza kugawa vizuri mapato na fedha ambazo wanazipata Wizaran, pamoja na kuwa hazitoshi, lakini wameweza kuzigawa katika mpango ambao ni mzuri na ambao unapaswa kupongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, tumpungeze pia Kamishna Mkuu wa TRA ambaye anafanya kazi nzuri, anaendelea kuleta mapato mazuri na siyo siri kwamba mwezi uliopita tu wa Desemba, tumeweza kupata karibu shilingi trilioni 1.9 ambazo hatujawahi kupata katika nchi hii. Ni vizuri Kamishna Mkuu akaendelea na moto huo huo ili kila mwezi basi atupe mrejesho na kuonekana kwamba mapato yanaendelea kupatikana kwa uzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, pia napenda tumpungeza Gavana wa Benki Kuu ambaye ameweza ku-stabilize dollar. Mtakumbuka dola ilikuwa inaporomoka kwa kasi kubwa sana, lakini governor na maofisa wake wameweza kukaa vizuri na kui-stabilize mpaka sasa hivi iko kwenye kiwango ambacho kinaridhisha kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nampongeza sana TR, Msajili wa Hazina kwa namna ambavyo ameweza kusimamia mashirika haya na kuweza kutoa dividends ambazo hazijawahi kupatikana katika nchi hii. Ni sifa kubwa sana, nanyi mmeona mabilioni ya fedha ambazo mashirika haya yameweza kuyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeshauri mambo mbalimbali katika Wizara ya Fedha. Mambo mengi yamechukuliwa na mengine hayakuchukuliwa. Mengi yaliyochukuliwa matunda yake yameonekana, lakini yapo mengine ambayo hayakuchukuliwa na ningependa kushauri Wizara ya Fedha iweze kuyaangalia vizuri ili kuhakikisha kwamba basi wanayachukua kwa lengo la kukuza uchumi wetu na kuongeza pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna miradi ambayo inabidi Serikali izidi kuifanyia kazi sana. Mradi wa Liganga na Mchuchuma, umekuwa ni kero. Siyo kero tu, Kamati tumejadili kwa kina na Mheshimiwa Waziri anajua kwamba viwanda vya chuma hapa nchini ambavyo viko 11 au 17 vyote vinachukua malighafi kutoka nje. Naamini kabisa mradi huu wa Liganga na Mchuchuma ungekuwa unafanya kazi, basi kusingekuwa na haja ya viwanda hivi kuagiza malighafi hizi kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana maamuzi ya mradi huu yafikie mwisho. Ni mradi mkubwa na utaona kwenye Mpango wa Maendeleo, Serikali ina mpango pia wa kujenga SGR ambayo itatoka bandarini Mtwara na kuweza kufika mpaka huko Liganga na Mchuchuma. Sasa ni vizuri Serikali ikaweka umuhimu na kuona kwamba mradi huu ni muhimu sana. Nimewahi kuona mradi wa makaa ya mawe kule Zimbabwe njia ya kwenda Victoria Falls, ni mradi mkubwa na unatoa ajira nyingi sana na uchumi wa nchi ya Zimbabwe unategemea sana mradi wa makaa ya mawe ambao uko kule Midlands.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri Serikali ilianganalie, tumelipigia kelele sana na tunaomba basi uamuzi ufikiwe. Isitoshe, kuna mradi kwa mfano wa kiwanda kile cha General Tyre Arusha, kila siku hapa Bungeni tumekuwa tukiongea suala hilo. Ni vizuri ikafikia mwisho, maana sioni kitu gani ambacho NDC wanafanya kwenye ule mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, tumekuwa tukipendekeza na hata kwenye bajeti iliyopita kuhusu ujenzi wa bandari ya uvuvi. Najua colleagues wangu wameongea hapa asubuhi na tukaambiwa kwenye bajeti kwamba iliyopita kwamba Serikali ina mpango wa kuanza kujenga bandari ya uvuvi, sasa sijui ni ujenzi huo umefikia wapi? Ni vizuri tukapewa ufafanuzi kutoka kwa Waziri mhusika.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kutembea kwenye baadhi ya nchi, tulikwenda Rwanda pamoja na Uganda ambapo kwenye hiyo *study tour* lengo lake ni kuangalia namna gani *Treasury Single Account (TSA)* inafanyakazi. Sisi tulikwenda Uganda na kwa kweli tuliona mpango huo unaendelea vizuri na unafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi hizo ambazo zinafanya, tulijiongeza na kwenda kutembea mjini na tuliona mambo ya ajabu ambapo tulikuta bidhaa nyingi sana ambazo zinapita hapa hapa kwetu, zinakwenda mpaka Kampala na Kampala kule unakuta Watanzania wengi na sio Watanzania tu, pamoja hata na wa nchi jirani wanakwenda Kampala kwa ajili ya kununua wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wa nchi jirani walikuwa wanakuja kwetu Kariakoo sasa hivi wamehamia kule Kampala. Sasa tuliiongea na Mheshimiwa Waziri na tuliona kwamba ni muhimu tuangalie tumekosea wapi? Ni kitu gani ambacho tunatakiwa tukifanye? Kwa nini bidhaa zitoke hapa, zipite hapa, ziende Kampala na watu wetu wa hapa watoke hapa waende kununua kule wazirudishe hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kwenye *transit* kuna ushuru ambao unatakiwa ufanyike na tumemshauri Mheshimiwa Waziri atengeneze Kamati ndogo iweze kukaa na kuona kwamba huu ushuru utafanya nini ili tuweze kuwa vizuri? Kwa hiyo, naamini kabisa Mheshimiwa Waziri atalichukua hilo na kuweza kuona kwamba tunafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti,...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Adadi. Kengele ya pili imelia.

MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naunga mkono hoja ya Mwenyekiti.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Richard Mbogo, baadaye Mheshimiwa Ester Mmasi na Mheshimiwa Esther Matiko ajiandae.

MHE. RICHARD P. MBOGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Kwanza namshukuru Mungu. Pia napenda niwapongeze Wenyeviti wote wa Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uwekezaji Mitaji ya Umma, kwa mawasilisho mazuri ambayo yanaenda kusaidia utendaji kazi wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, naomba niipongeze Serikali kwa ujumla nikianza na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, Waziri Mkuu, Makamu wa Rais na Watendaji wote kwa namna ambavyo juhudi zao zimeleta mabadiliko katika mashirika haya ya Umma ambayo yako chini ya *TR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niipongeze Kamati ya *PIC*, imekuwa na ushirikiano mkubwa sana, wanakamati wana ari na mori wa kufanya kazi na ushauri wao wametoa mzuri sana, wa kujituma katika kufanya kazi ya Kibunge kama ambavyo tumeagizwa na wananchi. Kwa uchache pia, naomba nimpongeze Athumani Mbuttuka na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri na kuchukua maoni ambayo Wabunge tunayatoa na wanayafanyia kazi. Tumeona mwaka jana 2019 wametoa ripoti nzuri sana ambayo itakuwa ni msaada kwa Serikali. *(Makofi)*

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na suala la uwekezaji kiujumla. Uwekezaji tunapata mapato ambayo hayatokani na kodi. Nami pia naungana na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuchukua hatua na kuweza kuanzisha Kampuni ya *Twiga Mineral Company* ambayo ni muunganiko wa *Barrick* na sisi na tunahisa 16% ambazo haziwezi kupunguzwa *and diluted*. Kwenye *economic benefit* ni 50 kwa 50. Hii ni hatua nzuri ambapo tutaongeza mapato yasiyotokana na kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa wito, tumsaidie Mheshimiwa Rais kwenye almasi kama alivyosema na kwenye *Tanzanite*. Kwa hiyo, nako tuweze kupata faida zaidi na kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuzungumzia suala la gawio. Ili tuweze kupata gawio zuri na nchi iweze kufaidika na mapato ambayo hayatokani na kodi lazima tufanye vitu viwili; kwanza, tudhibiti matumizi na pili, tuongeze mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge lilitunga Sheria ya Fedha Na. 16 ya mwaka 2015 ambapo inatakiwa gharama za uendeshaji zisizidi 60% lakini mashirika mengi yamekuwa yanazidi hii asilimia. Sasa tuombe TR pamoja na Serikali kwa ujumla kuendelea kusimamia ili kuweza kudhibiti mapato na mwisho wa siku itapatikana faida ambayo itakuwa inaongezeka kila mwaka na gawiwo litakuwa zuri kwa Serikali na kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa pili wa shilingi ni kuhusiana na mapato kiujumla kwenye kufanya biashara. Tutoe wito kwa mashirika yote kuwa wabunifu kwenye kuongeza aina za biashara ambazo zitaenda kuongeza mapato; na hii itapelekea faida pia kuweza kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala pia la ukusanyaji wa madeni. Kwenye ripoti na tumekuwa tukijadili kwenye Kamati kwamba taasisi nyingi hazikusanyi madeni ipasavyo. Tunajua kuna taratibu za kifedha ambazo deni likikaa muda mrefu inabidi uliripoti kwenye vitabu na matokeo yake linaenda kupunguza ile faida ambayo inaweza kupatikana. Kwa hiyo, tutoe wito kwa Watendaji wote wa Mashirika kuhakikisha kwamba wanakusanya madeni ili kuondoa hasara ambazo zitatokana na kutokokusanya madeni. (Makofi)

Pia kuna suala la kulipa madai mbalimbali na hasa ya kisheria kikodi. Kwa mfano, watu wamekatwa makato ya mifuko ya jamii kama *NSSF* lakini hayawasilishwi na ile inapelekea kisheria kuwa na *penalty*. Kwa hiyo, hili linatakiwa pia lizingatiwe kwa mashirika yetu ili kuondokana na hasara zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sera ya gawiwo, tuombe TR ahakikishe kwamba makampuni yote yanakuwa na sera ya gawiwo kwamba kwenye faida baada ya kodi ni kiasi gani kitaenda kwenye uwekezaji na kiasi gani kitaenda kugawiwa kama faida kwa ajili ya wanahisa wote kuweza kupata mgao wao tumeona baadhi ya mashirika hayana sera ya gawio matokeo yake kiasi gani kigawiwe maamuzi yanakuwa hayafanyiki na yanakuwa hayako *consistency*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Kamati yetu ilifanikiwa mwaka huu kukutana na kampuni ambazo tunahisa asilimia hamsini au chini ya hapo, kwa lugha nyingine tunaita *minority*. Hii imetia chachu kubwa sana kwa haya makampuni, tumeweza kutoa ushauri kwa sababu na sisi tuna hisa na wameweza kulisikiliza sana hili Bunge. Kwa hiyo tuombe kama kutakuwa na njia zaidi ya kuboresha na namna gani ya Bunge kuendelea kukutana na hizi kampuni ambazo tuna *minority* ziweze kuendelea.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la uwekezaji, kuna wakati sasa tunahitajika sisi wenye hisa tuwekeze zaidi kwenye hizi kampuni za *minority*. Kwa hiyo, mahali ambapo panaonekana kwamba panatija Serikali isisite kufanya *vetting* ya uhakika na kufanya uwekezaji ambapo mwisho wa siku tutakuwa na faida inayotokana na huo uwekezaji, *return on investment*. Kwa mfano, tulitembelea Kiwanda cha Sukari cha Kilombero, tumeona kwamba kikiongezeka uzalishaji utaongezeka, zaidi ya tani milioni moja na laki tano zitakuwa zinazalishwa na faida nyingine wakulima wetu wadogo wadogo wataenda pia na wenyewe kuongeza vipato kutokana na ongezeko. Sasa hivi wanatoa tani kama laki sita na sitini, kwa hiyo, uzalishaji ukiongezeka wataenda kutoa tani zaidi ya milioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iangalie na kuharakisha mazoezi yote ya ufuatiliaji, mahali ambapo panahitajika kutoa mtaji, basi wahakiki na watoe mtaji kwa wakati maana mwisho wa siku tunakuwa na gawio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni utekelezaji wa maagizo tuliyotoa mwaka jana, mojawapo ili kurahisisha Ofisi ya TR ni kwenda kwenye TEHAMA ambayo itamrahisishia kwenye kufuatilia mashirika na haya makampuni na tulishauri mwaka jana kwamba waingie kwenye mfumo, lakini kwenye ripoti ya TR, bado wako kwenye mazungumzo. Kwa hiyo tungeomba suala hili liharakishwe ili ufuatiliaji wa haya mashirika zaidi na makampuni zaidi ya 260 uwe unakuwa kwenye *finger tips*, kwa mfano tumeona makampuni mengi yako duniani lakini wanadhibiti dunia nzima kwa kupitia mifumo hii ya TEHAMA. Kwa hiyo, kwa upande huo itasaidia Ofisi ya TR na pia ikama iweze kuongezwa ili tija iweze kuongezeka kwenye hii Ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia pia niombe tuzingatie sana hii Sheria ya *Public Corporation Acts* ya 1993 ambayo ina mazingatio muhimu katika kudhibiti matumizi mbalimbali ndani ya Ofisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Richard Mbogo. Tunaendelea na Mheshimiwa Ester Mmasi, baadaye Mheshimiwa Ester Matiko na Mheshimiwa Mussa Mbarouk ajjandae.

MHE. ESTER M. MMASI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Kwanza kabisa napenda kuwapongeza Ofisi ya TR kwa kazi nzuri wanaoifanya pamoja na Kamati ya PIC lakini pia Ofisi ya Mheshimiwa Spika kwa sababu wamekuwa bega bega na sisi kuona kwamba tunapeleka ufanisi kwenye Mashirika yote ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zipo nyingi lakini kwa kwenda haraka ningependa kwenda moja kwa moja kwenye mada na nitapenda nichangie mashirika mawili, nitapenda nichangie shirika la TAWA ambalo linahusika na uhifadhi wa Wanyamapori lakini pia nitapenda nichangie Kampuni ya Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAWA ilianzishwa kupitia Sheria ya Uhifadhi wa Wanyamapori, Na.5 ya mwaka 2009, lakini pia katika kifungu cha 8 ilimpa mamlaka Mheshimiwa Waziri kuweza kuunda chombo chenye mamlaka kamili katika kusimamia na kuhifadhi wanyamapori. Hata hivyo, mpaka leo hapa ninapongeza takwa hili la kisheria halijaitimilika na Kamati yetu inasema kwamba kuna umuhimu kabisa wa kuona TAWA wanapatiwa sheria yake kwa maana ya kwamba tunaamini kabisa tutakapopata sheria yake TAWA itaenda kujijendesha kwa mapato tofauti na ilivyo sasa. Tunasema kwamba ni wakati mahususi TAWA iweze kujipatia sheria yake kwa sababu tumeona kazi kubwa TAWA inayofanya. Hapa ninapongeza ardhi tengefu zote zaidi ya asilimia sitini katika nchi yetu zinasimamiwa na TAWA.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haitoshi, ninapoongea hapa kwa mfano mapori tengefu yote yanasimamiwa na TAWA, lakini pia mapori ya akiba, *wetland*, *open areas* zinasimamiwa na TAWA, *Ramsar sites* zinasimamiwa na TAWA lakini pia utalii wa baharini unafanyika na TAWA na vitu kadha wa kadha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema sasa ni muda mahususi TAWA iweze kupatiwa sheria yake kwa sababu kwa muda mfupi toka ianze kufanya kazi mwaka 2016, TAWA ilipata mtaji kutoka Ngorongoro wa shilingi milioni mia tatu hamsini, lakini ninapoongea hapa leo TAWA imeweza kutengeneza faida ya shilingi ya bilioni 48 kwa mwaka. Kwa hiyo, hii ni *positive move* na tuna-*recommend* kwamba tunaomba sasa Serikali ione umuhimu wa kukipatia chombo hiki sheria yake mahususi ili kiweze kujiendesha chenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majukumu haya na *record* nzima walizoliweka TAWA pia kwa namna ambavyo walivyojanzisha wenyewe walikuwa na magari machache sana na Mkurugenzi kwa kipindi hicho alikuwa anatomia gari ya TANAPA kufanya *operations* za taasisi. Hadi sasa ninapoongea, TAWA ina magari *77 brand new zero kilometer*, kwa hiyo haya ni mafanikio makubwa kwa muda mfupi wa miaka mitatu. Kwa hiyo, tunasema kwamba ni muhimu sasa Serikali ikaamua kugatua madaraka pamoja na *operations* zote ziende TAWA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya tunaposema TAWA ipewe majukumu yake, tunafahamu kabisa, kwa mfano Sheria Na.5 kifungu cha 8 ambacho kinamtaka Waziri atoe mamlaka kamili ya chombo hiki ni kwamba kwa sasa katika sheria hii ilivyo, Mheshimiwa Waziri ndiye mwenye mamlaka ya kutoa vitalu vya kitalii vya uwindaji. Haya ni makosa, tutakapopata sheria hii mamlaka haya yataenda kwenye *Board of Directors*, lakini pia Kamishna wa TAWA atakuwa na mkono wa moja kwa moja kusimamia haya kwa sababu atakaposimamia na kuweza kutoa mwenyewe vitalu, tunaamini kabisa ataenda kuhifadhi *sustainable management* kwa taasisi hii ya TAWA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoongea hapa hata utalii wa picha Mheshimiwa Kamishna wa TAWA anakuwa hana mamlaka kamili, ingawaje jukumu hilo liko katika taasisi yake lakini hasimamii yeye, suala hili linasimamiwa na Mkurugenzi wa Wanyamapori.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba kabisa Wizara husika pamoja na Serikali ione kuna ulazima kabisa wa kuipa TAWA sheria yake ili iweze kushindana kama tunavyoona TANAPA inavyofanya vizuri, Ngorongoro inavyofanya vizuri, tukiipatia TAWA sheria yake na Meja Jenerali Semfuko alivyokuwa imara, tunaamini kabisa TAWA itaenda kufanya *wonders* katika hii dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nichangie suala la Kilombero. Ni dhahiri kama walivyosema wajumbe wenzangu, kwa sasa tuna umuhimu kabisa wa ku-*support* suala hili na tunaomba Serikali iwe makini na isimame na sisi katika kuona kwamba kibali kili walichoomba hawa watu toka miaka miwili iliyopita, basi kitolewe kwa sababu *domestic demand* ya sasa ya sukari ni tani 550, lakini kwa sasa tuna tani laki tatu na elfu hamsini katika viwanda vyetu vya ndani. Kwa hiyo, tunajua kabisa tuna *gap*, hivyo, ni vizuri sasa tukakubali kiwanda hiki kipanuliwe kwa sababu kitakapopanuliwa, sasa hivi Kilombero *Sugar* inachangia shilingi bilioni 350 katika uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *plan* hii ya *expansion* itaenda kuchangia bilioni 700, lakini pia wafanyakazi wataenda kuongezeka kutoka elfu nane mpaka elfu kumi na saba. Uchakataji wa malighafi katika taasisi ile unasema kwamba asilimia sitini ya *raw materials* ambayo ni miwa itazalishwa na *out growers* ambao ni mama zetu, dada zetu, vijana waliokuwa *disparate* walikosa ajira, wamezagaa kule Morogoro, ardhi ni nzuri, maji yapo, kwa hiyo,

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tunaomba kabisa Serikali itilie mkazo jambo hili kwa sababu sisi wabeba ilani tunayo ya kujibu, suala la ajira bado ni kizungumkuti, lakini ardhi tunayo, maporomoko ya maji tunayo na kiwanda kipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo nyuma mpaka Waziri alilazimika kwenda kiwandani pale kwa sababu kulikuwa na migomo mingi sana, wakulima wadogowadogo kila wakipeleka miwa wanaambiwa mara *sucrose* haipo, mara hivi, watapewa *terminologies* zote zile ili mradi tu kuonesha kwamba hawahitaji miwa mingi kwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaamini tutakapokwenda kupanua kiwanda kile malighafi tunayoambiwa asilimia 60 ya malighafi itatoka kwa wakulima wadogo wadogo, kiwanda kitachukua yote kwa sababu sasa hivi wakienda wanapewa *terminology* ngumu, lakini hii ni kuonesha kwamba kiwanda walichonacho kwa sasa hakiwezi ku-*accommodate* mazao yote ambayo yanapatikana katika muktadha huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mengi ya kuzungumza katika hili, lakini nafikiri kwamba ni vizuri sana Serikali ikaona umuhimu wa kupanua kiwanda hiki, kwa sababu hata kama tunataka tuipe Mkulazi ambayo ni taasisi ya Serikali pengine, na-*assume* hivyo, labda tukiisaidia Kilombero sisi tutakosa *stock* yetu. Hapana, leo ukienda Mkulazi tumewapa ardhi, tumetoa wafungwa magereza wamekwenda wamelima, wamesafisha, tumefanya kila kitu, lakini Mkulazi haina uwezo, leo miwa ya Mkulazi inaachwa kule porini, imetelekezwa kwa sababu hata kiwanda hakijanunuliwa, kinu hakipo, tuwape wawekezaji ambao wako tayari. Hakuna nchi ambayo inakataa au hakuna nchi ambayo haikubali uwekezaji wa watu binafsi na sisi pia naamini hatupo huko na kwa kuwa hatupo huko, naomba sasa Serikali ione umuhimu wa ku-*accommodate* hawa wenzetu, tuwape kibali ambacho wamekisotea kwa miaka miwili leo ili waweze kuanza kufanya upanuzi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache narudia tena, napenda kuipongeza Kamati yangu kwa kazi nzuri iliyofanya. Natambua kabisa katika mashirika tuliyoyahoji, kipaumbele chetu cha kwanza kilikuwa ni kuona kwamba Bodi za Wakurugenzi zinakuwepo, baadhi ya taasisi nyingi, asilimia 70 tulizokutana nazo ambazo zilikuwa hazina bodi sasa hivi zina bodi. Pia nafasi za kukaimu; asilimia 72 ya nafasi zote zilizokuwa zinakaimishwa, sasa hivi wameenda kupata *substantive post*, lakini, siyo hivyo tu, Kamati yetu pia ilisimama kikamilifu kuona kwamba na wanawake wanapewa nafasi katika mashirika haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo awali wakati tunaanza shughuli zetu za uendeshaji wa shughuli yetu tulikuja kubaini wanawake wengi wanaachwa kwenye ngazi za maamuzi, kwa hiyo kupitia Mheshimiwa Chegeni alikuwa imara sana kuweza kuona kwamba shirika linakuwa na namba nzuri ya wanawake wanaosimama katika ngazi za maamuzi. Kwa kweli katika hili naipongeza sana Kamati yangu, kwenye suala la *gender* tulisimama vizuri, Mheshimiwa Chegeni nampongeza mno pamoja na nafasi yake aliyonayo alisimama kikamilifu kuwatetea akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache nakushukuru sana na naomba kuunga mkono hoja taarifa zote za Kamati kama zilivyosomwa na kuwakilishwa. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Ester Mmasi. Tunaendelea na Mheshimiwa Esther Matiko baadaye Mheshimiwa Mussa Mbarouk na Mheshimiwa Zaynab Vullu ajiandae.

MHE. ESTER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami naenda kuchangia kwenye taarifa ya *PIC* na nikipata muda na Bajeti kidogo, lakini kwanza niwapongeze Wenyeviti wetu.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza na hoja ya kutokukamilika kwa miradi, tutaona kwenye Shirika la NSSF kuna Mradi wa *Holiday Inn* na ule wa Dege kule Kigamboni, mpaka leo haujakamilika hatujui hatima yake na zile fedha ni za wanachama ambazo zinatakiwa ziweze kuwekeza kwa tija zaidi ili ziweze kuzalisha na kuweza kuwalipa wanachama ambao wamechangia kwenye huo Mfuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nitagusia pia kwenye Shirika la Nyumba la Taifa, kwenye miradi mitatu kama ilivyoainishwa kwenye taarifa yetu ya *PIC*. Kwenye Mradi wa Mji wa Kawe tulitembelea pale Kamati yetu ya *PIC* mwaka juzi tukaelezwa na *by then* tukaambiwa kuna Watanzania ambao tayari walikuwa wameshatoa *deposit* kwa ajili ya kupanga na wengine kununua nyumba, kuanzia 2016 walikuwa wameshatoa *deposit*. Sasa tujjulize leo hao Watanzania ambao walitoa zile *deposit* zao, mradi haujakamilika *that means* hawajaweza kuhamia kwenye huo mradi. Sababu ambazo Serikali inatoa ni zile ambazo hazina tija kwa kweli na Serikali lazima iwe *responsible* kwa maamuzi ambayo imeyafanya ambayo yanaathiri miradi kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imesemwa hapa na jana imesemwa kweli, hivi kwa mtu gani ambaye anaweza akaona kwamba ni sawa kutoa bilioni 21 kuliko kutoa kibali kuweza kukamilishwa kwa ule mradi ambao tunajua kabisa Shirika la *NHC* ni shirika ambalo linajiendesha kibiashara, wala Serikali haitakiwi kutoa dhamana ila inatakiwa itoe kibali na benki ndiyo wanatakiwa ku-assess *business plan* ya shirika husika kuona kwamba ni *viable* apewe mkopo, wakitoa mkopo *for a certain period* inaweza ikarejesha na wala siyo Serikali kuendelea kukatalia kibali, *just* kutoa tu kibali shirika likakope, hiyo haikubaliki na sisi kama Wabunge lazima tuazime sasa Serikali iweze kutoa kibali ili *NHC* iweze kukopa, iweze kumalizia ule mradi na Watanzania ambao wamesha-*deposit* waweze kuhamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli tutaonekana wendawazimu sana, kwa yeyote yule ambaye anaweza kupata hata ile *view* tu ya ule Mji wa Kawe ulikuwa si tu unaenda kukuza uchumi wa Tanzania, lakini unaenda kubadilisha taswira ya Tanzania kabisa kwa Jiji la Dar es Salaam. Sasa ukisema umeutelekeza kwa sababu mnamahamia Dodoma, ni mambo ya ajabu sana, hata mwendawazimu hawezi kuyakubali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *Morocco square* ulikuwa umeshakamilika kwa asilimia 90 mwaka juzi, imebaki asilimia 10 nao umeachwa hizi asilimia kumi kwa miaka mitatu, unaachwa kukamilishwa. Hii siyo haki kabisa, mkandarasi anaendelea kulipwa asilimia 10 tu kukamilika kwa mradi, lazima Serikali iwajibike na ijue kabisa kwamba hii sekta ya ujenzi ndiyo sekta ya pili ambayo inachangia katika kutoa ajira Tanzania ukiacha ile ya kilimo, kwa hiyo ni lazima tujitoe zaidi kuhakikisha mambo yanasonga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni kupungua kwa mitaji kwenye mashirika yetu, taarifa imefafanua vizuri sana. Hapa nitaenda kugusia Shirika la *STAMICO*, shirika hili tumelitwisha jukumu kubwa sana la kusimamia miradi mikubwa na ya kimkakati, linasimamia *Stami Gold*, *Buhemba kule*, inasimamia *Kiwira*, inasimamia utafiti wa madini, ununuzi wa madini bati, lakini shirika hili limeendelea kujiendesha kwa hasara, mtaji unapungua kila mwaka, matumizi ya shirika hili tumeona na kwenye ripoti ni zaidi *on average 134 percent* ya pato ghafi, ina maana linajiendesha kahasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajuliza kama Serikali imeamua kuwekeza kwa baadhi ya mashirika kama ambavyo wamewekeza kununua ndege nyingi tena kwa mabilioni mengi ya fedha, wamewekeza kwenye *SGR trillions of money*. Shirika la *STAMICO* ambalo ni muhimu sana na miradi ambayo wameipa *Tanzanite One* ipo *STAMICO* kwa nini wasitenge mtaji wake mpaka juzi ilikuwa bilioni 33. Kwa nini hata tusi-*invest* pale hata bilioni 200 tu tuone ijiendeshe sasa hivi na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

iweze kuendeleza hiyo miradi ya kimkakati, *we have to start a balance*, huwezi kupeleka *materials* kwenye SGR, sijui wanataka *popularity* ili Watanzania waone, unaacha shirika ambalo ni la muhimu sana ambalo umelipa majukumu makubwa sana. Kwa hiyo, naomba sana Serikali ione umuhimu wa kuipa hela STAMICO ili iweze kuendesha vizuri hiyo miradi yote ambayo imeelekezwa STAMICO. Tunaona STAMICO imerithi madeni ambayo yametoka kwenye baadhi ya hayo mashirika mengine ambayo yamehamia STAMICO, lakini Serikali haionyeshi njia ya *ku-clear* hayo madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni ukosekanaji wa uwekezaji wa tija kutoka kwenye makampuni ya ubia tuliyonayo na hapa na-cite mfano wa TBC na Star Media, hii Star Media imekuwa ikijiendesha kwa hasara tangu ianze 2009 hapa Tanzania. Nakumbuka nilivyokuwa PIC Bunge la kumi tulihoji sana juu ya hii Star Media, lakini ukiangalia na ripoti yetu leo inaonyesha Star Media ilianza kwa mtaji wa milioni 238 ambayo ni takribani bilioni 547 za Kitanzania mwaka 2009. Walisema kwa *business plan* yao ikifika, ile *business plan* 2009 - 2014 wangeanza kutoa gawio kwa wanahisa lakini imekuwa kinyume ina-*operate under loss*, ripoti imeainisha kabisa, 2014 walipata *loss* ya bilioni 6.8; mwaka 2018 ilipata *loss* ya bilioni 19. Cha kushangaza mtaji mwaka 2009 ulikuwa bilioni 547, 2018 mtaji ni *half* wa bilioni 119, lakini bado tunaendelea kukumbatia Star Media kwamba ni shirika mbia na cha kushangaza hii Star Media ukitaka kuundwa hata Kamati Teule kufuatilia, unazuiliwa kwamba sijui kuna mambo nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliwaita Kamati ya PAC hawakutokeza, tunataka tujue kuna nini nyuma ya Star Media, fedha za Watanzania asilimia 35 tumewekeza pale kama wabia, tunataka kueleza Watanzania ni kwa nini huu mkataba hausitishwi ili tuweze kujua tuanze upya au tuachane nao? Huwezi kuwa na mbia ambaye ana-*operate under loss*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine na mbaya zaidi Star Media, CAG walifanya ukaguzi 2014/2015; 2015 walivyotaka kufanya ukaguzi wakakataa kutoa nyaraka, lakini CAG aliainisha madudu zaidi ya 34 kwenye Star Media. Kwa hiyo tunaiomba sana Serikali kama hamna kitu nyuma ya pazia ambacho mnakijua, tunaomba huu mkataba uwe *reviewed* na uvunjwe kwa sababu tayari wameshavunja makubaliano kwenye MoU kwa kutoweza kutoa hiyo faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni hoja ya kuhusiana na kukaimu tumeona na tumeshuhudia watendaji wanakosa mamlaka kamili ya kufanya *decision* kwa sababu unamkuta mtendaji anakaimu zaidi ya miezi 30, sheria inasema miezi sita kama umemkaimisha miezi 30 ina maana huyu mtendaji anafaa kuidhinishwa ili aweze kufanya maamuzi kamili akijua yeye ni CEO wa kampuni fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia kuna madeni mengi sana Serikali inadaiwa na hayo mashirika au taasisi. Kwa mfano tumeona ALAF wanadai bilioni 3.94 kutoka TBA kuanzia 2017, TRA wanadaiwa VAT fund na ALAF ambayo ni mbia mwenza wa Serikali bilioni 15. Sasa nyie mnadaiwa VAT fund bilioni 15 na siyo ALAF tu hawa ata ma *development partners* nao wengi wanadai kwamba wanadai *billions of money* kutoka Serikalini. Halafu mkija hapa mnasema makubwa, rudisheni kwanza hiyo VAT fund kwa wanaohusika halafu ndiyo mje mtupe tathmini halali ya makusanyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu anadai bilioni 15 mnategemea ata-*operate* vipi hii kampuni.

MHE. HALIMA MDEE: Wapigaji!

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, na hii ni kampuni moja tu, Serikali jamani tuache upigaji watu wanajua kwa sababu hamrudishi VAT funds.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. HALIMA MDEE: Wanapiga kwa staha.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tunayo AICC nayo inadai zaidi ya bilioni tatu kutoka Serikalini na mashirika lakini na taasisi nyingi sana zinadai wanapotoa huduma Serikalini hawalipwi. Msipowalipa hawa wanashindwa kujijendesha na kukosa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine napongeza kabisa mashirika yanapotoa gawio lakini nasikitika kwa mashirika ambayo yanakuta yanaomba mitaji lakini na yenyewe yanatoa gawio kama STAMICO. STAMICO anajiendesha kwa hasara lakini tulishughudia ikitoa bilioni moja Serikali. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther malizia.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile vyuo vikuu na wengine eti wanatoa michango kama UDSM, UDOM, UCLAS, VETA ni kama vile tunaweka kahela halafu baadae tunakazungusha kwa mgongo wa nyuma kanarudi tena. Siyo sahihi ni kama unakunywa uji wa mgonjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo pamoja na kwamba tuna-encourage watu watoe ile asilimia 15 ya michango na gawio lakini tuangalie zile ambazo zinatoa huduma *per se*. Kwa mfano UDSM au vyuo vikuu vingine ambavyo ndiyo vinatutolea, tunazalisha pale watu ambao wanakuja wataalam kwenye nchi yetu tena wenyewe wanataka tena waje pale watoe 15 percent na unajua Serikali ndiyo wanaleta hapa ndiyo tunawapitishia votes zao. Siyo haki ni kama vile tunacheza viini macho mbele ya macho ya watanzania, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Esther Matiko ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Mussa Mbarouk baadae Mheshimiwa Martha Umbulla na Mheshimiwa Shally Raymond ujijandae.

MHE. MUSSA B. MBAROUK: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, labda kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia afya njema na uhai tukaweza kukutana hapa tukaweza kuzungumza mambo mbalimbali yanayohusu Bunge letu na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze tu kwanza kwenye suala zima la bajeti, bajeti ni makadirio ya mapato na matumizi kwa Serikali au taasisi yoyote ile kwa mwaka au kwa mwezi au vyovyote vile viwavyo. Mara nyingi tumekuwa tunapitisha bajeti ambazo hazitekelezeki, tunapitisha bajeti lakini kwenye upelekaji wa fedha sasa inakuwa kiwango kilichohitajika katika bajeti hizo hakitekelezeki. Vilevile pia, kumekuwa na ucheleweshaji wa fedha katika miradi, kwa mfano miradi inayosimamiwa na halmashauri fedha unakuta inapelekwa katika robo ya mwisho ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake sasa zikifika katika halmashauri kwa sababu wanaogopa usije mwaka wa fedha ukaisha fedha ile ikarudi Hazina, matokeo yake inapitishwa miradi ya haraka haraka, miradi inakuwa iko chini ya kiwango, miradi haikaguliwi ipasavyo na matokeo yake sasa fedha zile zinakuwa kama tumekwenda kuzitupa. Nashauri Serikali ipeleke fedha mapema pale ambapo imekusudia kupeleka fedha za miradi katika halmashauri zetu na miradi yoyote ile ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni katika halmashauri kuzipora nazo vyanzo vya mapato. Kwa mtazamo wangu naona kama vile Serikali Kuu sasa imeamua kuziua Serikali za Mitaa kwa sababu hapa mwanzo tulichukua *property tax* ikapelekwa TRA lakini baadaye tena

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

ilipokuja TARURA tukaambiwa *parking*, mabango na *bus stands* na mapato mengine yote yanapelekwa TARURA. Ukipatazama hapa TARURA imepewa mamlaka ya kukusanya mapato lakini taa za barabarani, usafishaji wa mifereji bado uko kule kule kwenye halmashauri. Halmashauri watapata wapi fedha ya kununua luku au ya kulipia umeme wa taa za barabarani? Nasema hapa tunaziua Serikali za Mitaa (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nashauri, hebu tuziache vile vyanzo vilivyobaki navyo sasa tuache halmashauri iendeleo kukusanya mapato. Tumekuwa tukiwang'ang'ania kwamba nyingine zinakuwa zinakusanya chini ya kiwango na kwa mfano jana hapa wakati tulipokuwa tunapitisha taarifa za PAC na LAAC imefika mahali kwamba halmashauri zitakazoshindwa kukusanya mapato kwenye uvuvi inaambiwa waziri atazipoka mamlaka ya kukusanya mapato hayo. Sasa tujiulize halmashauri zitapelekwa vipi! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasemaji wengi waliozungumza wamesema mpaka madiwani sasa wanakaa vikao bila kulipwa posho zao za mwezi wala hizi *sitting* au posho zao za vikao. Nasema halmashauri kama tumeamua kuziua tuseme wazi, tuweke wazi yaani tusifichafiche kwa sababu hizi halmashauri ndiyo *Local Government*, ndiyo Serikali za wenyeji, ndiyo zinazofikia kero zaidi za wananchi kuliko Serikali Kuu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo zinazojenga madarasa, ndiyo zinazojenga barabara, ndiyo zilikuwa zinajenga labda shule, mifereji, maji taka na kadhalika lakini tunapora kila uchwao. Nina wasiwasi ipo siku tutakuja kuchukua vyanzo vyote tuwaambie wajitegemee watafute vyanzo vingine au wananchi tuwachangishe sasa kama vile kodi ya kichwa, hii itakuwa siyo sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri hapa halmashauri ikibidi tuzipelekee fedha kwa wakati lakini pia miradi ambayo wameikusudia kuitekeleza ipelekwe fedha ambayo inatosha tuzipeleke fedha pungufu. Tunapopeleka fedha pungufu miradi inakuwa imedumaa, utakuta majengo yamekaa muda mrefu hayaezekwi, zahanati zimekaa muda mrefu hazifanyi kazi, kwa hiyo, hapa nilikuwa nashauri fedha zipelekwe kwa mpango maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kusema ilikuwa ni kwenye suala zima hili la kodi kubwa kuwaua wafanyabiashara au kukimbiza wawekezaji. Nchi yetu tunasema tunataka Tanzania ya viwanda lakini ukitazama. Kwa maoni yangu naona kama tunasema hapa mdomoni tu. Hao wawekezaji wanapokuja katika nchi yetu adha wanayoipata wengine wamekuwa wanahama wanakimbilia nchi jirani. Ipo mifano mingi kwa mfano katika Jiji letu la Tanga tulikuwa na mwekezaji pale ana kiwanda cha kusaga unga wa ngano kinaitwa Pembe, *Pembe Wet Flower Mill Co. Ltd*. Ile iliajiri zaidi ya vijana 1000 pale Tanga lakini cha kushangaza sasa hivi imefungwa tangu mwaka jana mwezi wa tano kwa sababu ya kodi kubwa wanayotozwa na TRA. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, walikuwa na kiwanda tanzu cha kutengeneza vifungashio au visalfet inaitwa *Bajeber Packaging Co. Ltd*, nao pia wametozwa kodi kubwa wote kwa pamoja wamefunga viwanda, vijana wamekosa ajira sasa hivi ndiyo nasikia kama Tanga mmekuwa mkisikia kuna watoto wa ibilisi. Ni walewale vijana waliokuwa wakifanya kazi Pembe, wakifanya kazi CIC, wakifanya kazi viwanda vingine ambavyo vimefungwa hawana kipato, anategemewa na familia yake, anategemewa na wazazi wake, yeye mwenyewe anataka kutumia hana fedha matokeo yake wamejiita jina la ibilisi. Watoto wa ibilisi wamekuwa wanapora simu, wanawavizia akinamama wanapokwenda kwenye sherehe za harusi simu zinakwenda, cheni za dhahabu, viatu, fedha, vitu vyote wananyang'anya. (*Makofi*)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kama kweli tumekusudia kuwa Tanzania ya viwanda, wawekezaji wanapokuja tuwanyenyekkee, tuwape ushirikiano tuwapunguzie kodi ili waendeshe shughuli za kibiashara, walipe kodi ya Serikali lakini pia waajiri vijana wetu. Kama itakuwa mpango ni huu ni sawasawa na kumkamua ng'ombe maziwa bila ya kumpa malisho matokeo yake sasa maziwa yakiisha tutakuwa tunakamua damu. Tunajisifu tu kwamba TRA wamekusanya sasa hivi trilion 1.9 kwa mwezi, ni jambo zuri lakini tunajua hii *1.9 trillion* inavyopatikana. Leo Dar es Salaam katikati ya Jiji Kariakoo ukitaka fremu pia unapata kwa sababu kodi zimekuwa ni kubwa wafanya biashara wameshindwa wanakimbilia nchi jrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, hata wafanyabiashara wa malori sasa taarifa tulizonazo ni kwamba wengine malori yao wameyahamisha Tanzania wameyapeleka Kenya, wengine wamekwenda kuyasajili Zambia, wengine wamekwenda kusajili Burundi, wengine wamekenda kusajili Malawi kwa sababu kodi tunazowatoza ni kubwa na tuna utaratibu ambao haupo dunia nzima. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo dereva wa lori pia aambiwa awe *EFD mashine*, kwamba akipeleka mzigo wa *cement* labda Mwanza au Arusha akirudi akipakia hata magunia mawili au matenga kumi ya nyanya lazima alipe kwenye *EFD*. Wakati gari ikiharibika anatakiwa alizibe pancha, alipe njiani, alipe *ma-tan boy* na kadhalika, sasa wanaona imekuwa ni adha kubwa. Niseme baada ya kuhamisha usajili Tanzania wakapeleka nchi nyingine mapato yanaingia katika nchi hizo, naomba hapa Serikali ipaangalie upya, hebu tupunguze baadhi ya masharti kusudi tukaribishe kweli wawekezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalotaka kulisema, kuna matumizi mabaya ya fedha za Serikali na vilevile pia, hii inatokana na kutofata demokrasia ambayo ni ya vyama vingi kama ilivyokusudiwa. Labda hapo nitoe mfano, kwenye jiji letu la Tanga kuna madiwani wamerudi kwenye Chama Cha Mapinduzi, ninavyojua na ndiyo utaratibu, kanuni na sheria ilivyo kwamba kiongozi wa kisiasa akihama chama kimoja kwenda chama kingine amepoteza sifa ya kuwa na nafsi hiyo aliyoitumia. Sasa inakuwa madiwani hawa wameshahama kutoka CUF wamehamia CCM wanaingia kwenye vikao vya Kamati ya Fedha, wanaingia kwenye Baraza la Madiwani na wanalipwa posho za vikao na fedha ya mwisho wa mwezi. Haya ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbarouk ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ilianganalie jambo hili kwa makini kwa sababu huu mchezo ukiendelea itakuwa sasa kama sheria na kanuni tulizozitunga na kuapa kuziheshimu na kuzitekeleza hazina maana yoyote. Ahsante.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbarouk ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Martha Umbulla na baadae Mheshimiwa Shally Raymond ajiandae.

MHE. MARTHA J. UMBULLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi, kwanza naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia zawadi ya uzima na kuweza kuendelea na shughuli zetu hapa za kuwakilisha wananchi wetu. Kwanza kabisa naomba pia nichukue nafasi hii kuishukuru sana na kuipongeza Serikali ya Awamu Tano kwa kuwa taarifa zote tulizosomewa hapa zote zinaonesha ufanisi na hali chanya ya kuweza kuinua uchumi wa nchi yetu na hivyo tuna kila sababu ya kuipongeza Serikali kwa sababu mikakati yote ambayo tumeelezwa na kamati zote ni mikakati chanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, nitachangia maeneo mawili tu. Naomba nianze kwa kuchangia kwenye suala zima la mfumuko wa bei. Kunapokuwepo na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mfumuko wa bei hali hii inaondoa utulivu baina ya wananchi wetu na kwa hivyo hii hasa inatokana na upungufu wa chakula nchini. Kama kuna upungufu wa chakula ni wazi kwamba kutakuwa na mfumuko wa bei. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kipindi kilichopita cha 2017/2018 na 2018/2019 kwamba mfumuko wa bei ulipungua kutoka asilimia 5.3 hadi asilimia 3.5, kwa hivyo, ni hali nzuri. Kwa dalili tunazoziona tunamshukuru Mungu ni kudra zake pale ambapo mvua zinakuwa nyingi na hazileti madhara, lakini tunavyoangalia hali tunavyokwenda pamoja na mvua nyingi zinazonyesha lakini huenda ikaweza kuleta athari na kupunguza chakula hapa nchini. Hivyo Serikali isibweteke iweze kuona ni namna gani itajizatiti kuhakikisha kwamba hakutakuwa na mfumuko wa bei na hali ya chakula itakuwa nzuri nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali pia kwa kuunda chombo cha NFRA, NFRA ni chombo ambacho ni muhimu sana katika kuweka akiba ya chakula ili kuweza kuweza kutumia wakati wa uhitaji na hata pengine kuuza nje. Hivyo tunaiomba Serikali iweze kukijengea uwezo chombo hiki ili kutekeleza majukumu yake ya kununua chakula cha kutosha na hali hii ya kuwa mazao ya kutosha inaweza ikatusaidia katika masuala matatu. Kwanza, italeta utulivu kwa wananchi watakuwa na chakula cha kutosha; lakini vilevile inaweza ikasaidia kuhamisha wananchi kuwa na soko la uhakika mahali ambapo watauza mazao yao. Chombo hiki kitakaponunua mazao ya kutosha na huko tunakoelekea kwenye Serikali yetu ya viwanda tunaweza tukatumia mazao haya haya reserve ambayo itakuwa ziada ili kutumia katika kusindika mazao ya kilimo katika kuanzisha viwanda vya ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii si ya kubweteke kama ambavyo nilisema lakini Serikali itenge bajeti ya kutosha kuweza kuimarisha chombo hiki cha NFRA lakini vilevile na bodi ya mazao ya mchanganyiko. Naamini kwamba connection ya NFRA na mazao haya ni kuonesha ni jinsi gani kilimo ni muhimu katika kuinua uchumi wa nchi yetu. Kwa hivyo ni vizuri Serikali nayo ikatupia jicho suala zima la kilimo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo nilitaka kuchangia ni deni la Taifa. Tofauti na mfumuko wa bei ambapo umepungua kwa kipindi kilichopita, lakini deni la Taifa limepanda kidogo kwa asilimia 2.1. Hili tunaambiwa imesababishwa na masuala mbalimbali moja ikiwa mahitaji ya kugharamia miradi ya maendeleo na hasa pale ambapo inatumia mikopo vilevile ahadi ya misaada kutoka nje. Tunavyojua tunazo sheria mbalimbali zinazoenda sambamba na kutumia fedha za Serikali na hivyo nilikuwa naishauri Serikali pale ambapo tunahitaji kutumia fedha hizi kwa ajili kugharamia miradi mbalimbali sheria za fedha na kanuni na taratibu mbalimbali zitakapozingatwa na Serikali nina imani kwamba suala hili la deni la Taifa litakwenda likipungua na hasa pale ambapo Serikali itazingatia matumizi haya ya fedha za Serikali ambapo hakutakuwa na ubadhilifu na itazingatia hata mikataba ya kimataifa pale ambapo tunaona kwamba tunakiuka taratibu zile za kutumia fedha za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kuchangia mwisho mwisho ni pale ambapo unarudia michango mingine ambayo wenzangu wamesemea. Niliandaa kuchangia maeneo haya mawili na naomba sana Serikali izingatie yale ambayo nimeshauri na ahsanteni sana kwa kunisikiliza. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Martha Umbulla ahsante sana, tunaendelea na Mheshimiwa Shally Raymond baadaye Mheshimiwa Charles Mwijage na Mheshimiwa Joseph Kakunda ajiandae.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kipekee namshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai kutuweka wote hapa tuweze kuisemea nchi yetu mambo ya maendeleo na pia tuweze kuishauri Serikali. Awali ya yote naomba niwapongeze sana wenyeviti wote wawili kwa wasilisho lao na pia naomba nichukue nafasi hii rasmi kabisa

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji ambao ni wachumi waliobobea na mnaona mabadiliko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Katibu Mkuu Dotto James kwa kubana matumizi, mengine yamesemwa kwenye ripoti na sasa niende tu moja kwa moja kuzungumzia ile sekta ya benki. Kwenye kamati tumekesha na hawa watu, kamati ya bajeti tunatoka saa nne hawali, hawanywi hawachoki, Mheshimiwa Waziri anakuwa Dar es Salaam asubuhi jioni yuko na sisi na tumezungumza mambo mengi. Kuna mambo ambayo tumemshauri na naomba nichukue tena nafasi hii kuweka msisitizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya benki imekaa kibiashara na kweli ni biashara huria lakini Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kila leo anataka kumtetea mtu wa chini. Watu wa chini hawa wanaokota fedha zao kidogo kidogo, wanakuwa kwenye vikoba, wanataka kwenda kuweka fedha salama wanapeleka benki na benki wanaweka kwenye *savings account* wanapata asilimia moja tu (1 percent). 1 percent ikikatwa *service fee* inakata mpaka ile fedha yao waliyowekeza matokeo yake vikoba wameamua kufanya nini! Wameamua kuvunja vikoba ndani na kugawanya ule mtaji halafu wanaanza upya. Hapa nasimama nazungumzia wale wanawake walionituma hapa Bungeni, wanawake wa Kilimanjaro. Nawashukuru sana kunileta hapa na sitawaangusha nitalizungumzia jambo hili kila siku mpaka benki ziweze kulihuisha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiingii akilini, haiingii akili fedha zinavyokusanywa na benki zinakwenda kuwekwa kwenye *treasury bonds* lakini kwa miaka miwili ni asilimia 8.17, miaka mitano asilimia 10.22, miaka kumi wanalipwa wao asilimia 13, miaka 15 asilimia 15.19 na miaka 20 asilimia 16.71. Shida inatoka wapi! Kweli kuweka ni gharama na pia wanapokuja kulipa hujui yule aliyeweka fedha yake benki ataichukua saa ngapi atetemeshe, lakini kuna wale wazee ambao wanaweka fedha benki na wanaweka tu mpaka itakaposomwa siku ya mauti, fedha ile unakuta imekwisha. Hivi inakuwaje, tunakubalianaje na jambo hilo, nazidi kumuomba Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa vile alivyo msikivu hili jambo alizungumzie. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili naomba niwazungumzie watumishi wanaokopa benki. Mtumishi anakwenda kukopa benki, yeye amekaa ofisini mshahara ukija unakatwa deni linalipwa lakini asilimia yake ya kulipia lile deni (*interest rate*) inalingana na asilimia ya mtu ambaye anafanya biashara. Kuna *risk* gani hapo? Kuna *rate* ya *ku-default* ni ndogo sana mshahara tu ukiingia tu tayari imelipwa hata hapa Bungeni kwa wale tuliochukua mkopo mshahara ukiingia hujauona umeshalipa deni. Kwa nini sasa hayo mabenki yasiona kwamba wale wanaokuja kukopa ambao ni wafanyakazi hao ndio wale wanaolipa *pay as you earn* kubwa na yenyewe pia inakatwa bila kusumbua, wakashushiwa *interest rate* kutoka kwenye *two digits* kwenda kwenye *single digit*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana jambo hili lizidi kuangaliwa na linazungumzika. Mimi hainingii akilini tuna mabenki yetu mazuri kama CRDB, tuna mabenki yetu ya hapa nyumbani kama Posta, tuna benki kama NMB lakini mabenki ya nje yaje hapa yafanye *rough* ya kutafuta hela halafu na sisi tunajirusha tunataka kulingana nayo mnamsaidiaje huyu mwananchi wa chini anayezungumziwa siku zote na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hili jambo likakae kitaalamu zaidi hata kama hiyo hela wanakopeshana wenyewe kwa wenyewe waangalie basi jinsi gani *interest rate* itashuka na huyu mfanyakazi anayekesha ofisini anakopa kagari kake mnaziita sijui Vitz aone raha ya kufanya kazi ametulia ajue kwamba analipa kwa ustahi.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi kwamba tumelizungumza na narudia tena na ninaamini linafikirika na linazungumzika. Lakini niombe pia hii Wizara ya Fedha iweze kuangalia jinsi gani wale watu wa SACCOS watalipwa asilimia moja zaidi ya *interest* isilipwe moja kwa sababu wao wanakusanya kule nje wanaleta hela huku benki. Hiyo nayo wangetosha wapewe elimu na hayo mabanki na pia wapewe asilimia moja zaidi na iliwahi kutokea huko nyuma sijui inashindikana wapi ili waweze ku-run ofisi zao vizuri. Matokeo yake tutakuwa tu tunalaumu SACCOS hawafanyi lakini SACCOS pia hawapati elimu ya kutosha, SACCOS hawana motisha, SACCOS hizo ndio maana wanaanza kula wanakuwa mchwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya yalifanyika na yakawezekana naamini kwamba bado yatawezekana, tukiweza kuwapa motisha hawa wanaokwenda kutuokotea hela na nitawakumbusha tu. Mwaka jana Serikali ilichukua hela zake ambayo ilikuwa inawaachia mashirika yakae nazo waweke kwenye benki zao za *commercial* wamepeleka kwenye akaunti BOT lakini mashirika yale Benki zile zinaenda kutafuta hela na sasa hivi kuna benki ambazo zilikuwa na *deposit* kidogo zime-trip na benki hizo zinaendelea kumbe bado huku nje kuna hela, watu waliamua kuzishikilia lakini wale wakandarasi wanaolipwa pia na BOT zikisharejeshwa hela kwenye akaunti za wale makandarasi kwenye *commercial banks* wameenda kwenye zile benki ambazo zinaaminika na mnazijua benki zinazoaminika na sisi pia tuna-save huko kama CRDB. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine niwaombe sana watu sasa waende wanunue hisa, hisa zipo chini unaambiwa kwenye hisa *buy low, sell high* huu ndio wakati wote na mimi nawaambia wanunue hisa na wananchi wetu wapewe elimu ya hisa. Lakini nimwombe Mheshimiwa Dkt. Mpango leo tumezikia lugha ngumu sana huku ndani kwamba uchumi umeendaje wape hawa Wabunge wako semina, kuna mataasisi mengi tunatakiwa kuelimishwa tukuone tujue, Wabunge wanataka elimu ili waweze kufikiri *sharp* kama wewe. Dkt, please PHD yako ni ya ukweli sio *Honarally* umesoma vitabu mpaka vikasema *enough* wape watu semina hapa ndani tuongee lugha zinazofanana. Bahati nzuri nao wamekiri ni makanjanja lakini sio mmoja wengi hapa uchumi hatuujui. Tunaomba utupe semina kila Bunge likianza tupe semina tuongee lugha ambazo zinafanana na wewe baada ya kuzungumzia bajeti nakushukuru kwa yote uliyotufanyia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niipongeze sana Kamati ya PIC Kamati hii imefanya kazi kubwa na ya weledi chini ya Mheshimiwa Dkt Raphael Chegeni na niseme kwa mara ya kwanza tumeona *dividend* zikilipwa hadharani, kuna ambao walikuwa wana hisa lakini walikuwa hawalipwi hivi imekuaje *overnight* wakajua ni baada ya nyie Kamati kufanya na kwenda kuwaelimisha walipe. Wanapolipa inakuwaje, hela hizo zinaingia kwenye mfuko mkubwa wa Serikali tunapata vifaa ambavyo tunastahili kupata, tunapata dawa, tunapata hela za kununuliwa vitu ambavyo visingenunulika kama hizo hela zisingeokotwa. Kwa hiyo, nawapongeza sana hii Kamati ya PIC na nasema kwa kweli uzi ni huo huo Spika hakukosea, nampongeza sana Spika kwa sababu ni Kamati mpya ilikuwa haipo na naona tukienda tukirudi mambo yatafanyika makubwa zaidi. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Asante sana Mheshimiwa Shally Raymond tunaendelea sasa na Mheshimiwa Joseph Kakunda.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana ahsante sana kwa nafasi hii kwanza nianze kwa kusema kwamba naunga mkono hoja ya Kamati zote mbili, niipongeze sana Serikali kwa kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato pale TRA, mifumo ya *disbursement* ya fedha na mifumo ya ripoti ya fedha kweli imekaa vizuri sana kwa sasa hivi. Isipokuwa tatizo ambalo bado naliona ni mfumo wa uwajibikaji au *accountability framework* bado kidogo inahitaji kuboreshwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, si vizuri sana kusubiri mpaka CAG akague atoe ripoti ndio Watanzania wajue *status* ya thamani ya fedha kwenye miradi. Ingekuwa vizuri sana kama thamani ya fedha kwenye miradi ingekuwa inafatiliwa tangu fedha zinapopelekwa kwenye utekelezaji hadi utekelezaji unapofanyika mpaka miradi kukamilika. Kwa hiyo, nashauri tuboreshe mfumo mzima wa ufuatiliaji na tathmini ili tuweze kuboresha utekelezaji wetu. Taarifa ya utekelezaji wa bajeti nikiangalia ni nzuri sana lakini kipengele hiki cha ufatiliaji na tathmini kinachelewa kuboreshwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mawili la kwanza ni muhimu sana tuwe na sera ya ufatiliaji na tathmini ya nchi, pili mikakati ya ufatiliaji na tathmini ambayo itaboresha mpaka idara zote ambazo zinahusika na mambo ya mipango, ununuzi, uhasibu, ukaguzi wa ndani na mambo yote yanahusiana na suala hilo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani ushauri wa kuanzisha Ofisi ya Kamishna wa Mipango wa ufatiliaji na tathmini katika Wizara ya Fedha ni muhimu sana Serikali iutekeleze. Hapo mwanzo tulikuwa tunalalamikia wakandarasi sijui bei kubwa wakandarasi baadaye tukaagiza kwamba itumike *force account* lakini hata kwenye *force account* kumeanza kujitokeza matatizo ambayo yanapunguza ile thamani ya pesa kwenye mradi. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri tukiboresha eneo hili la ufatiliaji na tathmini tutakuwa tumeboresha sana matokeo bora ya miradi kwa wananchi wetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili fedha za mfuko wa jimbo kwa mfano mwaka jana zimetoka mwezi wa nane. Kamati za mfuko wa jimbo zimekaa kupanga matumizi ya hizo fedha lakini mpaka leo hii miradi mingi ya fedha hizi za mfuko wa jimbo haijatekelezwa kwa sababu tu fedha zilipokuja hazikuwa kwenye *activity* bajeti, kwa hiyo miradi yake ile mpaka iombewe kibali aidha kwa Wizara ya Fedha au TAMISEMI aidha *reallocation*. Nilikuwa nashauri ili kuondoa matatizo hayo Kamati za mfuko wa jimbo ziwe zinakaa mwezi Januari au Februari ili miradi ambayo imepangiwa matumizi iingie moja kwa moja kwenye *activity budget* wakati fedha zile zikitoka ziende kwenye utekelezaji na wakati ule Kamati za mfuko wa jimbo zifanye tu ufatiliaji na tathmini ya mradi unatekelezwa, hiyo itakuwa imeboresha kwa kiasi kikubwa sana utekelezaji. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho napenda kutoa pongezi kubwa kwa Serikali utekelezaji wa bajeti 2018/2019, 2019/2020 kwa kweli unaondelea ni mzuri na kazi kubwa sana zimefanyika hongera sana Serikali hasa kwenye miradi ya miundombinu, miradi ya afya, miradi ya elimu na kwa kweli naomba ndani ya Bunge hili nizungumze masikitiko yangu dhidi ya barua ambayo mwenzetu mmoja ameandika kutaka kuzuia fedha za miradi ya elimu. Ni kituko na ni aibu sana kwetu sisi Wabunge kuona mwenzetu ameandika barua ile wangukuwa wameandika watu wa NGO huko nje mimi nisingeshtuka sana lakini mwenzetu kaandika barua ile katika jimbo lake Serikali imepeleka shilingi bilioni moja kwa ajili ya kukarabati Sekondari ya Kigoma na sasa hivi sekondari ya Kigoma ni kama mpya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile wamepeleka zaidi ya shilingi bilioni 4 kwa ajili ya kuboresha elimu, sasa anazuia dola milioni 500 zisije kwa haraka kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa kitanzania. Nadhani hilo kwa kweli nieleze masikitiko yangu makubwa sana, na nimuombe

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

huko aliko amesoma vizuri tena amesoma hapa ndani akasoma nan je Ujerumani basi tuitumie elimu yetu kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa Tanzania hiyo ndio rai yangu badala ya kuwacheleweshea maendeleo. Unazuia shule 1000 zingeguswa na hizo fedha watoto zaidi ya 600,000 wangepaidika na zile fedha. Nadhani kwa kweli hilo mimi nasikitika sana sana na kama ananisikia huko aliko nilitamani nipaze sauti asikie huko aliko lakini kwa sababu yupo mbali basi naachia hapo lakini ataisikia kutoka kwenye *Hansard*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi hii asante sana, naunga mkono hoja. (Makofi)

MWENYEKITI: Asante sana Mheshimiwa Joseph Kakunda sasa Waheshimiwa Wabunge nampa nafasi Mheshimiwa William Lukuvi halafu baadaye nitampa Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango. Karibu Mheshimiwa William Lukuvi.

WAZIRI WA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwako kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hizi za leo na katika kuchangia kwangu nilitaka nitoe baadhi ya fafanuzi ya mambo yaliyozungumzwa hasa kuhusiana na Shirika la Nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nataka niseme kwamba huko kunakoitwa kudorora kwa miradi ya *National Housing* hakuna uhusiano wowote na maamuzi ya Serikali kuhamia Dodoma. Kwa sababu uamuzi wa kufanyia Dodoma umefanywa katika Awamu ya Kwanza, sisi Awamu ya Tano tungepozwa tu kwamba tumetekeleza mambo ambayo yameshindwa kutekelezwa kwa zaidi ya miaka 40. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hakukuwa na uhusiano na siamini kwamba Naibu Wangu Waziri alizungumza haya kwamba tunashindwa kutekeleza miradi ya *National Housing* kwa sababu tume-*divert fund* kuja Dodoma kwa sababu miradi ya Dodoma ya *National Housing* ilikuwepo na ilikuwa na fedha zake. Kwa hiyo, nilitaka niseme kwamba uamuzi huu hauna uhusiano na ile miradi lakini najua ni kweli kulikuwa na matatizo katika utekelezaji wa baadhi ya miradi ya Shirika la Nyumba hasa miradi mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Nyumba lilikuwa limejiingiza katika miradi mingi sana ya gharama nafuu ambayo ndio yalikuwa maelekezo ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi lakini pia ilijingiza kwenye miradi mikubwa sana ya kibiashara. Sasa ndani ya miradi hiyo kulikuwa na matatizo ya usimamizi, uongozi wa bodi lakini na utekelezaji. Kwa hiyo, kabla hatujafikiria kuingiza Shirika la Nyumba kwenda kukopa hizo fedha wanazotaka zikopwe, nimetoa maagizo kwa bodi mpya ambayo tumeiunda hivi karibuni ambayo naipongeza sana imegundua na imeanza kazi kwa kasi sana. Mambo ambayo tumeyafanya ambayo tumeagiza yafanyike ni kama ifuatavyo:-

(i) Tumeagiza kufanya *restructuring* ya mikopo, ile mikopo yote iliyokuwa imechukuliwa na kujenga hii miradi mbalimbali mnayoona tumeamua tufanye *restructuring* ya ile mikopo kwanza tuchunguze na tufanye *restructuring* na huo utaratibu umeshaanza kuzaa matunda tangu tumeagiza mpaka sasa tumeanza na mkopo mkubwa kwa mfano wa Shelta Afrika peke yake tulikuwa tunakopa kwa dola 17% baada ya kukaa tumezungumza sasa tumefikia asilimia 14 kwa shilingi. Kwa hiyo, tunapitia mikopo yote tunafanya *restructuring* itatupa nafuu zaidi kuliko hata hiyo kupoteza hizo mnazosema shilingi bilioni 20 kwa mwaka;

(ii) Tunapitia mikataba ndani ya mikataba ya ujenzi ile kuna baadhi ya vifungu ambavyo vilikuwa vinaongeza gharama ambavyo havina msingi na *contractors* tumewa-engage bahati nzuri ule mradi wa Morocco na huo 711 wa Kawe ni *contractor* mmoja. Tunapitia ile mikataba ili

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kuondoa mambo ambayo yalikuwa yanaweza kutekelezwa bila kuwepo na gharama hizi na kupunguza gharama na tukipunguza gharama hizi zitatusaidia wote, zitasaidia Serikali kupunguza gharama ya ujenzi lakini itawasaidia hata walaji, ununuzi wa zile *unit* tunafikiri hata ununuzi wa zile *units* zile *apartment* ulikuwa mkubwa kwa sababu ya baadhi ya mikataba iliyoingwiwa, kwa hiyo, tunafanya hili la pili.

Pia mjue ndani ya Shirika la Nyumba kuna *joint ventures* 194 mikataba yake ina mashaka sana kwa hiyo na yenyewe hii tumeikabidhi tunaipitia upya ili kuona hizi *joint ventures* hazikuingiwa sasa zipo *joint ventures* muda mrefu lakini baada ya kuchunguza baadhi ya *joint ventures* tunafikiri tulipigwa nazo zitatusaidia kupunguza gharama za uendeshaji la shirika.

(iii) Tumeamua hivi sasa kuanzisha na kuendeleza kampuni tanzu ya *National Housing* ya ujenzi. Tunayo daraja la kwanza ya ujenzi kampuni yetu ambayo kwa sasa peke yake kwa kipindi cha mwaka huu mmoja tumeingia na tunajenga miradi mikubwa 35 ikiwepo ni pamoja na Hospitali ya Rufaa ya Mara, na Hospitali ya Mkoa wa Mtwara tunakwenda vizuri sana. Miradi hii 35 peke yake itatuongezea faida ambayo itawezesha kukamilisha baadhi ya miradi hii;

(iv) Tumeamua kwamba katika maamuzi ya bodi zilizopita na *management* waliweza kununuanunua mali nyingi ambazo kwa kweli tunafikiri haikuwa msingi tulikopa pesa lakini wakanunua baadhi ya ardhi kwa mfano Arusha kule na sehemu nyingine. Mali kama zile tunafikiri hazikuwa na sababu kununuliwa kwa fedha za mikopo kwa hiyo bodi inaangalia uwezekano. Bodi ya sasa ina wataalam waliobobea inaangalia uwezekano wa kuuza baadhi ya *asset* ambazo zilinunuliwa bila kufanya utafiti wa kutosha ili fedha hizi zirudi ndani ya shirika ziweze kutekeleza miradi hii, na kazi inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini zile kazi za msingi za ujenzi wa nyumba za gharama nafuu hapa makao makuu hazitaathirika na ndio maana nimesema haina uhusiano wa kuhamia hapa kwa sababu ipo *program* ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu tulishajenga pale 150 na hivi sasa tunamalizia Iyumbu 68 na mwezi ujao tunaanza *apartment* 100 hapa Dodoma. Kwa hiyo, hii ni miradi tofauti na hii yote inatekelezwa kwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge, kwamba shirika lisipimwe kwa sababu ya ile miradi miwili, kazi za shirika zinakwenda vizuri kuliko wakati mwingine wowote. Hivi sasa miradi mingi sana iliyoko mikoani imekamilishwa na mingi ambayo nyumba nyingi ambazo tulikuwa tunatarajia tuuze tumebadilisha utaratibu, sasa tunataka tuuze kwa gharama nafuu zaidi kwa *tenant purchase* yaani mwananchi akiingia akipanga kodi yake ile tutaihesabu kama sehemu ya mauzo baada ya muda itakuwa mali yake badala ya kumlazimisha mwananchi aende benki kukopa mapesa mengi alipe *interest* huku alipe kodi, kwa hiyo kodi yake peke yake itamwezesha kununua nyumba. Nyumba nyingi tunafanya tumefanya Kahama, tunafanya sehemu zote ambapo tunajenga hivi sasa, huo ni ubunifu mpya wa bodi mpya na Serikali ya Awamu ya Tano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilitaka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba tukishamaliza kazi hii ya *restructuring* ya mikopo tukikamilisha kupitia hii mikataba mipya ya ujenzi najua tutapata nafuu kubwa sana. Kwanza hata Waziri wa Fedha sijamwambia tunasubiri tupate *return* ya *restructuring* hii na upitiaji wa mikopo hii ndio tujue *exactly* kiasi gani tunataka kukopa kumaliza na wapi tutakopa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaweza tukachukua hela ya Serikali kwa sababu Serikali ina pesa sio lazima twende benki, lakini tunazo Taasisi hivi sasa tuna Taasisi ya *TMRC* ambayo inawezesha mabenki kukopesha kama *push money* kwa ajili ya wajenzi wa nyumba za gharama nafuu tunaweza tukakopa hata huko. Kwa hiyo vyanzo vya kukopa vingi lakini lazima

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

tujikite katika ukopaji wenye tija na ukopaji wa gharama nafuu ambao utatuwezesha kushusha gharama ya ujenzi lakini kushusha gharama za wanunuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mmezungumzia habari ya gharama ya ujenzi lakini hamkwenda zaidi kwenye gharama za wanunuzi wa hizi nyumba, hizi nyumba ni ghali sana. Sasa kwa nini ilikuwa ghali tunafikiri ni kwa sababu yahii mikataba ambayo wajenzi wenyewe wamekubali kukaa na sisi ili kupunguza hizi gharama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mwenyekiti wa Kamati na Waheshimiwa Wabunge bahati mbaya kwenye hizi Kamati za Bunge sisi mawaziri huwa hatuingii lakini haya ndio maelekezo niliyotoa. Nimetoa maelekezo kwa bodi mpya na inafanya kazi nimeridhika kwamba wameanza vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la mwisho pia nimeagiza bodi ifanye *re-structuring* ya muundo wa Shirika la Nyumba. Muundo wa Shirika la Nyumba vilevile ulikuwa hauna haki sawa ndani ya watumishi, kwa hiyo, hata utendaji wa kazi ulidorora kidogo. Wako watu wachache walikuwa wanapata zaidi kuliko walio wengi. Kwa hiyo, sasa hivi wamepitia nashukuru kwamba juzi wamekaa Baraza la Wafanyakazi Nashukuru kwamba juzi wamekaa Baraza la Wafanyakazi, tunataka tujenge *morale* mpya ya watumishi wote wa Shirika la Nyumba ili kasi ya uendelezaji wa Shirika la Nyumba tuanze vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kuwahakikishia kwamba Serikali ya Awamu ya Tano inasimamia vizuri kazi ya Shirika la Nyumba. Mapato ya Shirika la Nyumba hayajateeraka na sasa Bodi hii ambayo tumeiunda inasimamia vizuri. Leo tumeanza kuona uwezo wa shirika lenyewe kuendeleza hii miradi kwa fedha za ndani. Wamebana matumizi na wanaendelea kubana matumizi lakini kuangalia upya hii miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge wa Kawe asiwe na wasiwasi. Tutamaliza ule mradi wa Morocco *Square* mwaka huu 2020, lakini pia tutamaliza na ule wa *seven eleven*. Ila tupe nafasi kidogo tuondoe ile hewa. Ni ngumu sana watu kujua, lakini mwenzenu niko ndani kidogo, nakiri kwamba nafikiri kuna hewa kidogo. Kwa sababu kama *re-structuring* ya mkopo mmoja umeweza kupunguza, kwanza kuondoa uwezekano wa kulipa kwa dola lakini kupunguza *interest* kwa 4% kutoka *seventeen* mpaka *fourteen*, huo mkopo mmoja tu, tunafikiri tunaweza. Kwa hiyo, tupeni nafasi, tuna uwezo na tutatekeleza hii miradi kwa gharama nafuu inayolipika na tutawapunguzia wanunuzi wa hizi nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa William Lukuvi. Kabla sijampa Mheshimiwa Dkt. Mpango, naomba nimpe Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe dakika tatu na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini dakika tatu, halafu baadaye atamalizia Mheshimiwa Dkt. Mpango.

WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa nami nichangie kwenye hoja iliyotolewa leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimelisikia suala la *Star Times* likiongelewa hapa nikaona ni muhimu sana nilitolee ufafanuzi angalau kwa kifupi kwa sababu tutakuja na ufafanuzi wa kina katika Bunge hili na kwa kutumia njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *Star Media* ambayo ni kampuni ya ubia kati ya *Star Times* ya China na Shirika letu la Utangazaji la *TBC* ni suala ambalo lilibuliwa ndani ya Serikali na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano mwenyewe, baada ya kuhoji kwa nini ubia uliodumu zaidi ya miaka saba usioneshe faida?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kauli ya Mheshimiwa Rais, Bodi ya Wakurugenzi ya TBC ikamwomba CAG afanye *special audit*, lakini nami vile vile kwa nafasi yangu ya Uwaziri nikaunda Kamati Maalum ambayo iliongozwa na Msemaji Mkuu wa Serikali, Mkurugenzi wa Maelezo, Dkt. Abbass pamoja na Mtendaji kutoka *Star Times* nao wafanye uchunguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliogopa kwamba pengine uchunguzi wa CAG ungechukua muda mrefu sana. Taarifa zote mbili zimetoka na tumeweza kubaini madudu mengi sana katika ubia huo. Madudu yale yenye mwelekeo wa kijinai, tumeyawasilisha kwenye vyombo husika vya Serikali vya masuala hayo. Yale ya kiutendaji tumeyafanyia marekebisho. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulitaarifu Bunge hili, kwa mara ya kwanza hata sisi wenyewe tumeanza kuona vitu vimeanza kuonekana *positive*. Mwaka huu *Star Media* imeweza kuchangia shilingi milioni 500 Hazina kwa mara ya kwanza. Siyo hivyo tu, mimi nina barua hapa sasa, *Star Media* imekubali kwa ule upungufu uliojitokeza uliosababishwa na baadhi ya watendaji wake, kulipa TBC shilingi bilioni tatu kuanzia mwezi wa tatu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mambo yanaenda vizuri na tumeyafanyia kazi na taarifa ndefu itatolewa katika Bunge hili na kwa kutumia njia nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana kwa ufafanuzi huo Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe. Tunaendelea na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini.

NAIBU WAZIRI WA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa, napongeza Kamati zote mbili kwa uwasilishaji mzuri na ushauri mzuri uliotolewa. Sisi kwa upande wa Sekta hii ya Madini kuna hoja kama mbili au tatu ambazo zimejitokeza, nazo ningependa kuchangia kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, Kamati zimeelezea namna ya kuimarisha utendaji wa Shirika la STAMICO. Napenda tu kukueleza kwamba Serikali imeendelea kuimarisha utendaji wa STAMICO kwa kuteua Bodi mpya na Menejimenti mpya ili ifanye kazi kwa ufanisi zaidi ya ilivyokuwa inafanya awali. Tumechagua watu wenye weledi na Mheshimiwa Rais alituteulia Mwenyekiti wa Kamati ya STAMICO, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, anafanya kazi vizuri na kwa kweli Bodi inatoa ushauri mzuri na kwa kweli kazi inaenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile limeongelewa suala la ukosefu wa mtaji. napenda kueleza kwamba Serikali pia imeendelea kuliwezesha Shirika la Madini la Taifa kadri fedha zinavyopatikana. Aidha, STAMICO imekuwa inatumia *assets* zake na hasa leseni ilizonazo kuzibadilisha kuwa sehemu ya mtaji. Kwa hiyo, ukiangalia maeneo mengi ni kwamba leseni ambazo zinamilikiwa na STAMICO, tunapokuwa tunaingia katika *joint venture* na makampuni mengine katika miradi hiyo, basi zile leseni za STAMICO zimekuwa ndiyo sehemu ya mtaji. Kwa hiyo, badala ya kutegemea mtaji sana kutoka Serikalini, tumeamua kutumia leseni zetu kuwa kama ni mchango wa mtaji katika miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile limezungumzwa sana suala la kupunguza gharama za uendeshaji. Tumepunguza muundo wa Shirika kutoka Kurugenzi zilizokuwa tano, sasa hivi tuna kurugenzi tatu. Hivyo, tumepunguza gharama ambapo zilikuwa zinatumiwa fedha nyingi kulipa au kuendesha zile kurugenzi kutoka Kurugenzi tano kuwa Kurugenzi tatu.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumepunguza gharama za uzalishaji wa madini hasa katika mradi wa *STAMIGOLD*. Tulikuwa tunazalisha wakia moja kwa dola za Kimarekani 1,800 ambapo hata katika mauzo katika Soko la Dunia unakuta wakia moja kwa mfano sasa hivi ni dola 1,400 kwa wakia moja. Kwa hiyo, tulikuwa tuna-*produce* kwa gharama kubwa, tunapokwenda kuuza tunauza kwa gharama ndogo. Tumeona kwamba Shirika lilikuwa linapata hasara na linatengeneza madeni makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumepunguza gharama za uzalishaji ya wakia moja kutoka dola 1,800 kuwa dola 940. Hata tunapopeleka katika soko tunakuta wakia moja inauzwa labda dola za Kimarekani, sasavi tumepambana hadi kufikia dola 1,500. Kwa hiyo, tunatengeneza faida. Ile *difference* ya 1,500 na 940, ile *difference* tunayoipata, ndiyo faida kwa Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Shirika limeanza kuuza madini yake. Badala ya kupeleka nje, kwa sababu kupeleka nje kuna gharama na ilikuwa inatugharimu kwa *trip* moja kupeleka dhahabu nje ya nchi, ilikuwa inatugharimu mpaka shilingi milioni 38, sasa hivi tumeshaanzisha masoko ya madini nchini na tumeamua sasa hivi katika mgodi ule wa *STAMIGOLD*, badala ya kupeleka nje na kwa sababu bei inajulikana, tunauza katika masoko yetu ya ndani. Hii inatuondolea ile gharama ya kusafirisha madini yao kupeleka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ni moja ya hatua ambazo tumechukua na tumeweza kupunguza gharama za uendeshaji. Hatua hizo zimesababisha shirika letu, kama mlivyosikia hapo majuzi, tumeweza kutengeneza faida na tumeweza hadi kutoa gawio kwa mchango wa Serikali, tumetoa kiasi cha shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini. Tunaendelea sasa na Mheshimiwa Dkt. Phillip Mpango na baadaye tutamalizia na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Naomba nitumie fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia nawapongeza sana Wenyeviti wawili wote wa Kamati kwa hoja nzuri sana ambazo wamezifanyia kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichangie baadhi ya hoja ambazo zimejitokeza humu ndani. Kwanza, kulikuwa na suala la Bajeti ya Fungu Na. 7 - Msajili wa Hazina kwamba ni kidogo, wamepata asilimia 16, hivyo wawezeshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka huu peke yake ambao tunaendelea kutekeleza, mpaka mwezi Desemba kwa upande wa kuwawezesha Ofisi ya Msajili wa Hazina ili waweze kufanya kazi yao ya kufuatilia hizi Taasisi za Umma, walishapewa asilimi 92 ya OC. Nafikiri tatizo linalojitokeza ni kwa sababu kuna baadhi ya vipengele na hususan fedha kwa ajili ya mitaji ya Mashirika ya Umma, lakini pia fedha kwa ajili ya kulipia madeni ya mashirika, hizi kwa kawaida huwa tunaziweka kwenye kasma ya dharura na haionekani kule kwenye Fungu Na. 7 moja kwa moja. Ni pale tu ambapo zinahitajika ndiyo tunazitoa na zinalipwa kutoka kwenye Fungu lile la dharura.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri ni kwamba tunaenda sasa kuanza mchakato wa bajeti, nafikiri kama ni macho ya ziada kwa ajili ya changamoto zile nyingine ambazo zilisemwa juu ya Ofisi hii muhimu sana, ni kipindi chake cha kuangaliwa.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu kampuni za simu kujiorodhesha kwenye soko letu la hisa la Dar es Salaam. Ilitolewa hoja kwamba mpaka sasa ni Vodacom peke yake ambayo imeorodheshwa wakati tulishakubaliana na sheria inataka mashirika yote ya simu yajiorodheshe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda tu niliarifu Bunge lako kwamba tuko katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa sheria. Kwa mfano, tunatarajia kwamba tigo watawasilisha *documents* zile zinazohitajika kwa ajili ya kujiorodhesha kwenye Soko la Hisa itakapofika mwezi ujao Februari, 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *Halotel* kama mnavyofahamu Waheshimiwa ni kwamba hii kule kwao ni kampuni ya jeshi. Kwa hiyo, panahitajika uamuzi wa wamiliki ili kuihamisha sasa ile kampuni kuwa *public company* ndiyo iweze kujiorodhesha kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam. Kwa hiyo, hilo linafanyika hivi sasa, tunatarajia kwamba hatua itafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Airtel, imechelewa kuorodheshwa kwenye Soko la Hisa kwa sababu kama mnavyokumbuka tulikuwa na ule mzozo wa umiliki wa hisa na sasa baada ya kutatuliwa lile, ndiyo tutaanza sasa mchakato wa kwenda sokoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuiwezesha *TTCL* kifedha, ni kweli kabisa shirika letu hili ni muhimu, tunahitaji kuboresha miundombinu yake. Utaratibu wa kwenda kununua nguzo za mitumba, hili hapana, haliruhusiwi na sheria ambayo ilitungwa na hili Bunge. Kwa aina ya teknolojia, aina ya kazi ambayo inafanywa na shirika letu hili ni muhimu sana tukahakikisha kwamba ile *infrastructure* inakuwa ni ya kisasa kabisa kutupeleka kwenye uchumi wa kidigitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tumeanza kuchukua hatua, mwezi Desemba Serikali ilitoa ridhaa kwa *TTCL* ambapo tuliwaruhusu waweze kukopa dola milioni 15 ambazo ni kama shilingi bilioni 34.2 hivi waweze kukopa kutoka kwenye benki za ndani kwa ajili ya kuweza kupanua miundombinu ya taasisi hii na kadri mahitaji yatakavyojitokeza, basi Serikali itayatazama kwa jicho hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la marekebisho ya VAT tena kwamba yaje kwa hafi ya dharura, *particularly* ili Serikali isidai kodi ya ongezeko la thamani kwenye miradi kama ile ya Halmashauri inayogharamiwa na fedha za Benki ya Dunia. Niseme tu tunalifanyia kazi, kwa hiyo Bunge litaarifiwa hapo baadaye, maamuzi ya Serikali kuhusu jambo hili ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa pia na mapendekezo ambayo yalishawahi kutolewa. Bunge hili huko nyuma liliwahi kueleza kwamba ni muhimu tunapofanya mabadiliko ya sheria zile zinazohusu ushirikiano kule Afrika Mashariki yapite kwenye Kamati ya Bajeti. Nafikiri nilishawahi kuliambia hili Bunge Tukufu kwamba sioni tatizo la kimsingi kutekeleza hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto moja iliyopo ni ya muda. Kwa mfano, mwaka uliopita mchakato wa kuchakata yale mapendekezo ambayo tulikuwa tumeyapata kutoka kwa wadau, yalipopita kwenye *task force on tax reforms* na baadaye kwenye *think tank*, siku ile ya mwisho tunafanya kikao ndiyo siku pia Kikao cha Jumuiya ya Afrika Mashariki kilikuwa kinaanza. Kwa hiyo, inakuwa ni *timing disconnect* kwamba tunafanyaje ili huu mchakato uwe umekamilika ili tuweze kuupitisha kwenye Kamati ya Bunge ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna changamoto ya pili kwamba Serikali kwa ujumla wake hata Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wanakuwa hawajaona hayo mapendekezo. Kwa hiyo, inakuwa ni vigumu kuyaleta kwenye Kamati kabla Serikali haijaji-*pronounce*.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nilitaarifu tena Bunge lako Tukufu kwamba tunapoleta yale mapendekezo kupitia *Finance Bill*, bado Bunge linayo nafasi ya kushauri juu ya yale ambayo tulikubaliana kule Afrika Mashariki. Kama Bunge au Mamlaka nyingine za Serikali haziridhiki na kile ambacho tulikubaliana kule, sisi tunachofanya ni kwamba huwa tunaandika barua kwa Sekretarieti ya Afrika Mashariki, tunasitisha utekelezaji wa hicho ambacho kilipeleka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niseme kulikuwa na hoja kwamba uchumi wetu uko vizuri lakini siyo kwa mtu mmoja mmoja. Nirudie tena kusisitiza kwamba mwenendo wa vigezo kuhusu viashiria vya uchumi jumla, tunakwenda vizuri sana. Yaani katika Afrika ni ukweli kabisa tunazidiwa na ncjhi chache sana, lakini ukuaji wa uchumi wa asilimia 6.9 ni ukuaji wa kasi kubwa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili la mmoja mmoja naomba tu nisisitize tu vitu vitatu hivi. Kwanza, ongezeko la ukuaji wa uchumi huwa linaongezeka kwanza kwenye mchango wa kila Sekta kwenye Pato la Taifa na unaona kabisa kwamba baadhi ya Sekta mchango wake kila mwaka unaongezeka, unakua kwa kasi. La muhimu kuzingatia ni kwamba wanaonufaika na ule ukuaji ni wale wanaoshiriki kwenye zile sekta ambazo zinakua haraka. Ndiyo maana msisitizo umekuwa ni kwamba ni lazima Watanzania tufanye kazi. Hilo ni la msingi sana kwa sababu vinginevyo huwezi kufaidika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, wananchi wanafaidika na ukuaji wa uchumi kupitia kwenye huduma za jamii zinazotolewa na Serikali. Kwa hiyo, ndiyo maana tunapoboresha elimu, afya, barabara na kadhalika, ndiyo njia ya pili ya kuwafaidisha wananchi kutokana na ukuaji wa uchumi. Mwananchi mmoja mmoja, lakini pia Taifa kwa ujumla. Kwa hiyo, ni muhimu sana kufanya uchambuzi vizuri kwamba hiki kinachosema mtu mmoja mmoja haonekani kufaidika ni nini hasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa kuwezesha Sekta ya Kilimo kama tulivyofanya kwenye Sekta ya Madini, nafikiri hoja inaweza kuwa ni ya kutafakari vizuri. Kwa sababu kilicho kikubwa kwa Serikali, kwanza kwa upande wa kilimo ni lazima tuhakikishe kwamba Sera zetu za Kilimo ni nzuri na hususan kwa sababu kilimo ni *private sector activity*. Kwa hiyo, lazima tuhakikishe kwamba sera zile ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la muhimu tujielekeze sasa kwenye miundombinu ambayo inawezesha kilimo na ndiyo hilo ambalo Serikali imekuwa inafanya tena kwa kasi. Miundombinu ya usafirishaji, maghala, umeme na *irrigation*, hapo ndiyo tutaweza kunyanyua kilimo. Lazima pia tujielekeze kuboresha huduma za fedha kwa wakulima, lazima tujielekeze kwenye huduma za ugani na utafiti kwenye kilimo. Huo ndiyo mwelekeo wa Serikali. Ukisoma *ASDP II*, huko hasa ndiyo tunapolenga. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia lazima tujielekeze kwenye *inputs* muhimu; mbolea, dawa na mbegu bora. Huo ndiyo mwelekeo na msukumo wa Serikali katika kuboresha na kukiwezesha kilimo. Nafikiri hiyo ndiyo njia sahihi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja nyingine, nafikiri ni tahadhari muhimu juu ya mwenendo wa mfumuko wa bei. Ni kweli mwenendo wa mfumuko wa bei kwa nchi yetu hivi sasa ni mzuri kabisa, isipokuwa tunazona hizi changamoto zinazooneshwa kwa upande wa chakula na vile vile upande wa nishati. Hili nalo ni muhimu na hasa ukizingatia wakubwa hao ambao wanatunishiana misuli, kwa hiyo, inaelekea kuleta shida kwenye bei ya mafuta.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachukua tahadhari kama Serikali kwa maana ya kusisitiza nishati mbadala, lakini pia kuhakikisha kwamba tuna akiba ya kutosha ya chakula. Hilo ni muhimu sana ili tuhakikishe kwamba mfumuko wa bei unaendelea kubakia kwenye kiwango ambacho hakiharibu mwenendo wa uchumi wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilitolewa pia hoja kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inahangaika na maafa haikuwekewa fedha yoyote kwenye bajeti. Naomba tu nikitaarifu kikao chako kwamba kwa kawaida *constitution* ya nchi yetu inataka asilimia moja ya bajeti yote ya Serikali itengwe kama *contingency*. Kwa hiyo, endapo itatokea dharura, hatutasita kutumia *contingency fund* kwa ajili ya kukabiliana na maafa kama yatajitokeza, lakini Mwenyezi Mungu anatupenda, naamini atatuepusha na madhara japo yameanza kutokea kwa wananchi kwa mfano kule Lindi na unaona Serikali ya Mkoa tayari imeingia kazini na pia Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Serikali ya Mkoa. (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri naomba umalizie maana nimekupa mrefu.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kumaliza jambo la mwisho tu, kwa upande wa kodi ya majengo, tunapokea ushauri, tutaufanyia kazi kwamba kodi ya majengo pengine ilipiwe kupitia ankara za umeme na maji. Kuna tahadhari pia, kwa sababu siyo ankara zote za umeme ni za matumizi ya nyumba, hilo lazima lifahamike. Vile vile, hata ankara za maji, nyumba nyingi hazina ankara za maji. Kwa hiyo, tuna changamoto kubwa. Ni jambo la kuchakata vizuri tuone kama linaweza likatupa *mileage*. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Mpango kwa ufafanuzi huo mzuri kabisa kupitia Wizara ya Fedha. Sasa tunamalizia na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Jenista Mhagama, karibu.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwa kuwapongeza sana Wenyeviti wa Kamati zote mbili kwa ripoti nzuri. Nawapongeza sana Wajumbe ambao ni washiriki wa Kamati hizo kwa ripoti ambazo wametuletea. Nami naomba nikiri kwamba ndani ya Serikali tunawashukuru kwa sababu wanaendelea kutushauri mambo mema na ninaomba kuwahakikishia kwamba tupo pamoja na tutaendelea kuyazingatia ili kujenga ustawi wa Taifa na wa Tanzania kwa ujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kabla sijaendelea nichukue nafasi hii pia kumpongeza sana Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli. Ni ukweli usiopingika, Rais wetu toka ameingia kwenye Serikali hii ya Awamu ya Tano amefanya kazi kubwa za utekelezaji wa Ilani lakini utekelezaji huo unaowagusa Watanzania wengi. Kwa sasa maendeleo ya Taifa letu yamekuwa ni mtambuka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia miradi ya maendeleo ambayo imetekelezwa ndani ya Serikali ya Awamu ya Tano unaiona kabisa mgawanyo wake unawagusa Watanzania kwenye mikoa yote kwa kuzingatia mahitaji na vipaumbele walivyonavyo. Ukisema masuala ya elimu bure, miundombinu ya maji, miundombinu ya barabara, ujenzi wa hospitali mpya, ujenzi wa vituo vya afya, ukarabati wa shule, kabisa Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana name kwamba Rais wetu na Serikali wamefanya kazi kubwa. (Makofi)

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo basi, kama tunatekeleza Ilani ya Uchaguzi, Rais wetu na Serikali wanatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Hata kuhamia hapa Dodoma haikuwa kukurupuka, ilikuwa ni utekelezaji wa Ilani. Kuhamia hapa Dodoma wote tumekuwa ni mashahidi, hakuna mji wowote ama nchi yoyote ambayo inaweza kukua kiuchumi kama haipanui shughuli za kiuchumi katika maeneo mbalimbali ya nchi hiyo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wala isingetusaidia, ukiachia mbali kurithi mawazo mazuri ya Baba wa Taifa hili, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere ambaye ni mwasisi wa Serikali kuhamia Dodoma, lakini Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na maamuzi dhahiri ya Rais wetu ya kuhamishia Serikali Dodoma yamekuwa na *effect* ambayo ni *positive* kwenye kukua kwa uchumi wa nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa nini? Baada ya Serikali kuhamia hapa Dodoma, tumeona kabisa miji inayozunguka hapa Dodoma imeanza kukua. Ukienda Singida inakua, Manyara - Babati kunakua, Iringa inakua na Morogoro inaendelea kukua. Kwa hiyo, kwa kuhamia tu hapa Dodoma unaona ile *multiplier effect* ya kuhamia Dodoma imeambukiza na Miji mingine ambayo ipo karibu na hapa Dodoma. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini maana yake? Mwisho wa siku tutakuwa tumekuza uchumi katika maeneo mengi ya nchi ya Tanzania, tutaongeza mapato, tutaboresha huduma za jamii, vile vile ukuaji wa uchumi huo utatatua na matatizo mengine ambatanishi kama matatizo ya ajira na mambo mengine kama miundombinu na huduma za jamii. Hapa Dodoma sasa hivi tuna hospitali kubwa ya Benjamin Mkapa, ukiacha mbali ile ya Muhimbili ambayo ilikuwa Dar es Salaam kwa muda mrefu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema tumehamia Dodoma, hatujaiacha Dar es Salaam. Dar es Salaam nayo imeendelea kufanyiwa mambo makubwa. Waheshimiwa Wabunge nyie ni mashahidi, katika historia ya nchi hii, miundombinu ya barabara inayojengwa kwa sasa kwenye Jiji la Dar es Salaam ni miundombinu ya hali ya juu. Huo ni ushahidi kabisa. Miundombinu inayowekezwa pale Dar es Salaam itafanya Jiji la Dar es Salaam kuwa ni Jiji la kibiashara na likiwa Jiji la kibiashara litasaidia sana kukuza uchumi wa Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niseme Waheshimiwa Wabunge, ninadhani sisi kama Wabunge tukihesabu yale yanayofanyika Dar es Salaam na katika Mikoa mingine yote Tanzania, hakika tunayo kila sababu ya kumpongeza sana Rais wetu kwa maamuzi aliyoyafanya katika kipindi chake pamoja na Serikali yake. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba nimtoe hofu dada yangu Mheshimiwa Halima, Mwenyekiti mpya wa Wanawake wa CHADEMA na kumwomba tu aunge mkono juhudi za Rais wetu na hasa pale Dar es Salaam katika kuleta maendeleo. Namwomba afikishe salamu hizi za upendo wa kazi znuri ya Rais wetu kwa wanawake wa CHADEMA nchi nzima na hasa pale Dar es Salaam. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumzwa hapa suala la Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF). Ninaomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge, nakubali NSSF huko nyuma baada ya Serikali yetu kuingia, tumegundua kulikuwa na matatizo makubwa. Sasa tulichokifanya ni kuendelea kuhangaika kuona kwamba ule uwekezaji ambao ulifanyika huko nyuma usiokuwa na tija unarekebishwa haraka ili kuwe na manufaa na tija kwa wanachama na Watanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi juzi tu, tunayo majengo ya muda mrefu Mtoni Kijichi, nimeyakabidhi wa Waziri wa Elimu yatumike kama hosteli za wanafunzi wa elimu ya juu,

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wanaosoma katika Vyuo Vikuu pale Dar es Salaam. Tumekabidhi hosteli zile mpaka kufika mwezi wa Tatu wanafunzi wasiopungua 4,000 na kitu watapata makazi kwenye zile hosteli mpya. Tutakwenda mpaka nafasi zisizopungua 8,000 na kitu. Kwa hiyo, hiyo ni kazi kubwa, ni lazima muone Serikali inafanya kazi na inajaribu kurekebisha kila ambapo hapakuwa na tija. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa imetolewa hoja kwamba hili shirika linakufa. Ninachokwenda kufanya sasa hivi ni utathmini wa mfuko (*actuarial*), hii ndio itatuambia. Hatuwezi kusema kitu kingine chochote, mfuko unakufa bila *actuarial*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua *facts* za kawaida kwa sasa, makusanyo ya shirika mwaka 2018 kwa mwezi yalikuwa shilingi bilioni 60 tu. Kufika mwaka 2019 yameongezeka mpaka shilingi bilioni 96 kwa mwezi. Hilo ni ongezeko na tunaona kumbe shirika linakufa. Uwekezaji kwenye dhamana za Serikali ilikuwa ni *negative* mwaka 2018, lakini baadaye ikaja kuongezeka mpaka 8%. Leo ninaposimama hapa, imefika asilimia 20 kwenye dhamana za Serikali. Kwa hiyo, hilo ni ongezeko. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na malimbikizo ya wastaafu yenye thamani ya fedha za Kitanzania shilingi bilioni 109, mpaka kufika 2019 toka hiyo 2018 fedha hizo za malimbikizo na malipo mengine tumeshalipa shilingi bilioni 409. Kwa hiyo, unaona kwamba shirika linaendelea kufanya vizuri. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, daraja la Kigamboni ambalo ndiyo mradi umesemwa hapa, ni kweli una matatizo na tunaufanyia kazi kuyaondoa. Tumeweza kuongeza makusanyo kwenye Daraja la Kigamboni kutoka shilingi bilioni 697 mwaka 2018 mpaka shilingi bilioni 950 mwaka 2019. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge, Serikali imejipanga, tunajua miradi hii ya uwekezaji kwenye Mashirika yetu ya Hifadhi ya Jamii ni fedha za wanachama. Tunachokifanya sasa hivi ni kutembelea mradi mmoja baada ya mwingine, kutafuta namna ya kuhakikisha uwekezaji huo unakuwa na tija kwa wanachama na Watanzania kwa ujumla.

Kwa hiyo, nakubaliana na ushauri walioutoa Waheshimiwa Wabunge, pale ambapo hapajafanyika vizuri, tutafanya vizuri, lakini kama shirika linafanya vizuri, tutaendelea kuwapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ahsante sana kwa hoja zilizotolewa. (Makofi)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ufafanuzi mzuri kuhusu jitihada zinazochukuliwa na Serikali. Sasa naomba niwaite Wenyeviti. Naanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aje kuhitimisha au ku-*windup* kwa yale ambayo yamechangiwa. Karibu sana Mheshimiwa Mashimba Ndaki kwa dakika 20.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa tena nafasi ili niweze kuhitimisha hoja yangu ambayo iliwekwa Mezani kwako asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Kamati ya Bajeti imechangiwa na Wabunge tisa; Mheshimiwa Dkt. Sware Semesi, Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mheshimiwa Jitu, Mheshimiwa Adadi Rajabu, Mheshimiwa Mussa Mbarouk, Mheshimiwa Martha Umbulla, Mheshimiwa Shally Raymond, Mheshimiwa Joseph Kakunda na Waziri wa Fedha na Mipango - Mheshimiwa Dkt. Mpango.

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye hoja zilizosemwa na Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu muda wangu ni kidogo sana hapa. Mheshimiwa Dkt. Sware aliongelea kuhusu VAT kwenye miradi ya *World Bank*, kuiwezesha *NFRA*, uwekezaji kwenye Sekta ya Kilimo na uwekezaji kwenye Shirika la *TTCL*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala yote hayo tumeyazungumza kwenye Kamati na pia kwenye taarifa yetu tumeyaonesha. Kwa mfano, kipengele cha 12 - Mapendekezo ya Kamati; 12:3, 12:5 *NFRA* ukurasa ule wa saba kipengele cha 3:2 na Sekta ya Kilimo tumeizungumza sana hasa ukurasa ule wa saba kipengele cha 3:1.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kuwa ukuaji wa uchumi ungechochewa zaidi na Sekta ya Kilimo, lakini pia sekta ambazo Serikali imewezeza zaidi zinachangia kwa sehemu kubwa sana kwenye kilimo. Kwa mfano, Sekta ya Ujenzi inachangia kwa sehemu kubwa sana kwa sababu mimi naamini sekta hizi huwezi kuziweka peke yake zikawa na faida kwenye uchumi, lakini zina faida kilimo pia kwa sababu ya namna ya mwingiliano wa kilimo pamoja na sekta ambazo Serikali iliwezeza sana. Hata hivyo, bado kuna umuhimu kwa Serikali kuwezeza zaidi kwenye suala hili la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbaraka Dau aliongelea masuala ya *TRA* kufikia shilingi trilioni 1.9, nami naungana naye kuipongeza *TRA* kwa sababu kwa kweli wamefika kiwango ambacho ni kikubwa na kwa kweli ni cha kupigiwa mfano. Huwezi kudharau jambo hili. Shilingi trilioni 1.9 ni kiwango kikubwa, ingawa kweli bado jitihada zinatakiwa kufanyika, lakini ni kiwango kikubwa kabisa ambacho tunahitaji kutambua. Nasi kama Kamati tumetambua hilo na kwa kweli wamefanya jitihada mno. Kwa muda wa nusu mwaka makusanyo ya nchi kwa ujumla ni asilimia 95 nukta, sikumbuki sawa sawa lakini ni asilimia 95. Sasa makusanyo ya namna hii kwa mtu yeyote kwa kweli lazima apongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Dau amezungumzia upotevu wa mapato yasiyo ya kodi, lakini bado Kamati inaendelea kuisitiza pia kwamba kuhusiana na suala hili na tunatambua kwamba mapato kweli yanapotea hasa kwenye bandari zinazoitwa bubu; sasa kwenye Kamati pia tulisisitiza sana kwamba suala hili liangaliwe vizuri kwa sababu ni muhimu sana kuziangalia hizi bandari bubu. Bahati nzuri mwaka 2019 tulipitisha bajeti ya kumruhusu Waziri anayehusika na Wizara hii kuweza kuzitambua bandari bubu. Kwa hiyo, ni suala tu la Serikali sasa kuona ni kwa namna gani wanaweza wakazitambua baadhi ya bandari bubu ili kuweza kupunguza upotevu wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dau alizungumzia pia ukusanyaji wa kodi ya majengo, naye alisema hakuwa ameona kwenye taarifa yetu, lakini kwa kweli kwenye taarifa yetu suala hili tulizungumza na kwenye mapendekezo kipengele kile cha 12:9 tulilitaja vizuri na naamini Mheshimiwa Dau atakuwa ameona pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia alizungumza juu ya mfumo wa *stamps* za kieletroniki (*ETS*). Kamati inaipongeza Serikali sana kwa kuja na mfumo huu madhubuti ambao tunaweza kusema umetoa *real time data*, yaani kwa makusanyo yanayokusanywa kwa wakati ule ule na lakini pia kuziba mianya ya upotevu wa mapato. Mfumo huu umeonyesha matokeo chanya na hivyo Serikali haina budi kuangalia sehemu nyingine pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza na mfumo huu mwanzoni kabisa, Kamati ilitaarifiwa kwamba Serikali wanaanza na vinywaji vile vikali, lakini wanaendelea kuweka *ETS* kwenye viwanda vile vinavyozalisha vinywaji baridi; maji, soda na kadhalika. Nadhani pia Serikali wataangalia ili kwenda kwenye bidhaa zaidi ya hizo za vinywaji peke yake kwa sababu katika Kamati tuliona pia pengine labda wanaweza wakaenda mpaka kwenye *cement* na

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

bidhaa nyingine ili mradi tu kuhakikisha kwamba kodi inayotokana na bidhaa hizo ambazo tunaweza kuweka *ETS*, basi kodi hiyo ipatikane kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia alizungumza juu ya mchango wa hisani ya jamii (*social responsibility*). Mheshimiwa Dau alisema kule kwake kuna mtu mmoja anachangia shilingi milioni mbili nadhani kwa mwaka na alikuwa anaona pengine hicho ni kiwango kidogo. Sasa ipo Sheria ya Mapato Na. 332 ambayo inazungumza juu ya suala hilo. Kwa hiyo, ni muhimu sheria hii ikafuatwa ili kwamba wananchi wanaozunguka eneo hilo ambalo mwekezaji yupo na wenyewe waweze kufaidika na kitu hiki kwa sababu kipo kwenye sheria zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji mwingine ni Mheshimiwa Jitu Soni, yeye aliongelea kuhusu masuala ya Sekta ya Kilimo na *Blue Print*. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyochukua hasa katika kuondoa tozo mbalimbali ikiwa ni pamoja na zile alizokuwa akizitaja Mheshimiwa Jitu. Bado tunasisitiza *Blue Print* kwa sababu bado ipo kwenye mchakato wa kufanyiwa kazi, basi Serikali iharakishe kufanyia kazi suala hili ili wananchi na wafanyabiashara kweli wawe na mazingira mazuri ya kufanyia biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia alizungumzia kuhusiana na Serikali ione umuhimu wa kusimamia Sekta ya Kilimo na kuondoa vikwazo vya kikodi katika sekta hii. Suala hilo limezungumzwa pia na Wabunge wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la *TTCL* ambalo Mheshimiwa Waziri pia amelizungumzia. Tunashukuru kwamba Serikali imekubali kwamba *TTCL* inahitaji kuwezesha. Kwa kweli inahitaji kuwezesha hasa katika suala la minara. Tunashukuru kwamba Serikali inakubaliana na pendekezo tuliloliweka kwa sababu tayari wameshakutoa ruhusa ili waweze kukopa kama Mheshimiwa Waziri alivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi pia tulikubaliana kwamba *TTCL* hawapaswi kununua minara mitumba, baada ya maelezo yanayohusiana na sheria tuliyoiweka sisi wenyewe. Kwa hiyo, hatukubaliani na suala hilo, lakini bado tunasisitiza kwamba Serikali ione umuhimu wa kuiwezesha *TTCL* ili iweze kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab ameongelea masuala ya miradi ya Liganga na Mchuchuma na pia mradi wa *General Tyre*. Tumesisitiza kwenye taarifa yetu kuhusiana na miradi hii ya kimkakati ambayo ipo kwenye Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano kwamba miradi hii basi Serikali iharakishe namna ya kuitekeleza kwa haraka iwezekanavyo kwa sababu ina tija na ina faida kwa nchi yetu. Kwa hiyo, Serikali iangalie tu ni kwa namna gani inaweza ikaharakisha uanzishwaji wa miradi hii ili iweze kuwasaidia wananchi na kulisaidia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tu na *reservations* zetu kwenye mradi wa *General Tyre* ule wa Arusha kwa sababu tuliona ni kama mipango yake haiendi sawa sawa na pengine wawekezaji waliokuwa wameshapatikana tayari, Kamati ilikuwa inaona kama wawekezaji hao hawajawa *serious* kiasi cha kutosha kuweza kuanzisha au kufufua kiwanda hiki cha *General Tyre*. Kwa hiyo, tulitoa tahadhari kwa Serikali kwamba iwe makini inapokaribisha hawa wawekezaji ili kuona kama wanaweza wakafanya kazi hiyo au watashindwa kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbarouk aliongelea masuala ya mapato na vyanzo vya Halmashauri kwa mazingira ya biashara. Ni kweli tumekubaliana, lakini mapato na vyanzo vya Halmashauri amezungumzia; lakini ukijaribu kuangalia kuhusu mapato ya Halmashauri kwenye taarifa ambayo tumewasilisha mbele yako, mapato ya Halmashauri yamepanda. Sasa sijaelewa Mheshimiwa Mbarouk anapozungumza mapato au vyanzo vya

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

mapato ya Halmashauri alikuwa anamaanisha mapato ya aina gani? Kuhusu suala la mazingira ya biashara tunakubaliana naye kwa sababu pia tumelizungumza kwenye taarifa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Martha Umbulla aliongelea masuala ya Deni la Taifa, mfumuko wa bei na NFRA. Mimi nakubaliana naye na sisi tumezungumza kwenye taarifa yetu kwamba suala la Deni la Taifa inabidi liangaliwe kwa sababu ukuaji wake ni ule wa nje. Ni wale wakopeshaji wa nje, sio wakopeshaji wa ndani. Sasa wakopeshaji wa nje wana mambo yao. Sasa ni vizuri kuliangalia kwa makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mfumuko wa bei tulizungumza pia tukashauri Serikali iangalie mfumuko wa bei pamoja na riba zinazotolewa na mabenki yetu ili kuona uwiano wa hivi vitu viwili kama tunaweza kubadilisha au kusahihisha riba zinazotolewa na mabenki yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la NFRA Mheshimiwa Mama Umbulla tunakubaliana kabisa kwamba NFRA lazima iwezeshe kifedha na kimtaji kwa sababu hivyo ilivyo sasa hivi inakua ni ngumu sana wao kununua chakula au mahindi hasa wakati mahindi yamekuwa kwa wingi kwa wakulima wetu, hasa ukizingatia kwamba suala la chakula ndiyo linalosaidia kupunguza mfumuko wa bei zaidi linapokuwa ni zuri. Sasa likiachwa linaelea, siyo vizuri sana kwa sababu italeta shida kwenye mfumuko wa bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Shally Raymond aliongelea mwenendo wa riba pamoja na gharama za mabenki. Mheshimiwa Joseph Kakunda, aliongelea mfumo wa uwajibikaji wa watumishi Serikalini uangaliwe namna ya kuwa na huo mfumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Kakunda alizungumzia juu ya utokaji wa fedha za mfuko wa jimbo zipangiwe mwezi Januari. Yaani kazi zake zipangwe mwezi Januari, zikija tu ziende kwenye miradi moja kwa moja. Suala hili nadhani linahitaji mjadala mkubwa, kwa sababu ni kweli zikija zinaweza zikaenda kwenye miradi, lakini nadhani mfuko wa Jimbo kazi yake ni kuchochea au kuhamasisha maendeleo, sio kumaliza miradi iliyoanzishwa na Halmashauri husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kmahitaji ya Jimbo yanabadilika mara kwa mara, sasa yakipangwa moja kwa moja kuanzia Januari halafu yaje yatekelezwe mwezi wa Kumi au wa Kumi na Moja pesa zinapokuja, inaweza kabisa wakati huo ikawa mahitaji yamebadilika yamekuwa mengine na kwa hiyo utekelezaji wake ukawa ni mgumu. Kwa sababu mfuko huu uko chini ya Waheshimiwa Wabunge, nadhani wanaelewa maana yake, pesa zake hizi zinapokuja kwenye Majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kakunda ndio alikuwa wa mwisho kuchangia. Labda suala la VAT kwenye miradi linafanyiwa kazi na Serikali na Serikali imekubali...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Malizia Mheshimiwa.

MHE. MASHIMBA M. NDAKI – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi kumaliza hoja yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Ahsante sana. *(Makofi)*

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

MHE. PAULINE P. GEKUL: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa. Naona hoja yako imeungwa mkono na sasa nitawahoji Wabunge moja kwa moja.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati hiyo katika kipindi cha mwezi Januari, 2019 hadi Januari, 2020 ilipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Haya. Hoja, taarifa, mapendekezo na maoni ya Kamati yamekubaliwa na sasa ni Maazimio ya Bunge. *(Makofi)*

Tumalizie na Kamati ya PIC, Mwenyekiti karibu kwa ajili ya ku-*wind up*, Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni.

MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UWEKEZAJI NA MITAJI YA UMMA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kukamilisha hoja ambayo iko hapa Mezani. Kwanza napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa maandishi na kwa kuzungumza hapa Bungeni. Nikianza na Mheshimiwa Augustine Vuma, Mheshimiwa Sonia Magogo, Mheshimiwa Halima Mdee, Mheshimiwa Jitu Soni, Mheshimiwa Richard Mbogo, Mheshimiwa Ester Mmasi, Mheshimiwa Esther Matiko, Mheshimiwa Shally Raymond, Waheshimiwa Mawaziri ambao kwa kweli wamechangia na kutoa ufafanuzi mkubwa sana; Mheshimiwa William Lukuvi (Waziri wa Ardhi), Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe (Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo), Mheshimiwa Stanlaus Nyongo (Naibu Waziri wa Madini), Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango (Waziri wa Fedha na Mipango) na Mheshimiwa Jenista Mhagama (Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, sitapenda sana kusema kila mmoja alivyosema, nita-*wrap up* kwa pamoja. Kwanza napenda niseme kwamba Waheshimiwa Wabunge naomba tuelewe tafsiri ya gawio. Ukisema gawio hatuzungumzii ile *dividend per se*. Tumesema neno gawio kwa maana tumejumuisha vitu vitano humo ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mashirika ambayo yanafanya biashara (*commercial entities*) wanalipa gawio na hii inakotolewa baada ya kuwa umeshapata faida na baada ya faida sasa ndiyo unapata gawio lake. Vilevile kuna mchango wa asilimia 15 wa *growth turnover* ya kila taasisi ambayo inatoa huduma pamoja na wakala. Vilevile tuna fedha asilimia 70 ya *redemption excess capital*, rejesho la mtaji uliozidi kwa hizi taasisi za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapata asilimia 28 kutokana na mapato ya TTMS, mfumo wa mawasiliano ya simu na vilevile Serikali inapata mapato kutokana na riba ambayo inakopesha kwenye hizi taasisi. Kwa hiyo, kwa ujumla wake ndiyo gawio. Hata Waheshimiwa waliokuwa wanazungumza hapa ni kwa sababu wanajua *dividend*; wanasema kwa nini tunapata hasara? Wanatoa *dividend*, hapana. Hoja ni kwamba kila taasisi ya Serikali ambapo Serikali ina hisa pale ndani, imewekeza, kama siyo gawio, itoe mchango kwa Serikali. Ndiyo maana yake hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema maneno hayo, naomba sasa niwashukuru wale wote waliochangia kwa kuzungumza na kwa maandishi. Pia hoja za Taasisi za Umma kutoa gawio kwa Serikali zimezungumzwa na Wabunge wengi humu ndani. Naendelea kusisitiza

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

kwamba Serikali ihakikishe taasisi zote zinazotakiwa kutoa gawio zinafanya hivyo na mashirika yanayotakiwa kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali yanatimiza takwa hilo. Kamati inaamini kuwa bajeti ya Serikali inaweza kuendeshwa kwa kutumia mapato yatokanayo na kodi na mapato yasiyotokana na kodi ambayo ndiyo Kamati yangu imekuwa ikisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la marekebisho ya sheria na kuhusu suala zima la kufanya kazi kwa taasisi ambazo zinakiuka matakwa ya Sheria ya Fedha Na. 16 ya mwaka 2015, viongozi wake waweze kuchukuliwa hatua. Wakikiuka matakwa ya sheria hii, lazima Serikali iwachukulie hatua kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kuhusu watumishi kukaimu nafasi. Hili limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Kwa kweli tungependa kuona kwamba nafasi ambazo zinakaimiwa, Serikali inachukua hatua za makusudi ili kuweza kupata watendaji ambao ni *substantive*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la michango, kwa mfano suala la miradi ambayo haijakamilishwa ya *National Housing*, Mheshimiwa Lukuvi ameelezea vizuri sana, sina haja ya kurudia tena. Nafikiri hata Mheshimiwa Mdee amemwelewa vizuri, kwamba Serikali imeangalia baadhi ya mikataba ambayo ilikuwa na matatizo, ndiyo maana inafanyia utafiti mzuri ili kupata *solution* ya kudumu ili mashirika yetu yaweze ku-*perform* inavyotakiwa. Nakushukuru sana Mheshimiwa Lukuvi kwa kutoa ufafanuzi ambao kwa kweli ni wa kina na ninajua kila mmoja ameweza kuelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la *TTCL* na hili Mheshimiwa Dkt. Mpango amelizungumzia vizuri; na suala la *STAMICO* Mheshimiwa Nyongo amelizungumzia vizuri, sina haja ya kurudia tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la sheria kupitwa na wakati, ni kweli sheria nyingi za taasisi hizi toka kuanzishwa kwake zimepitwa na wakati. Kwa hiyo, kuna haja kubwa ya kuanza kupitia mchakato wa sheria hizi ili kuwezesha mazingira yaliyopo yaendane na hitaji la kisheria la sasa hivi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la madeni, inasikitisha kuona kwamba baadhi ya taasisi za Serikali zinashindwa kulipa madeni yake, na hata ku-*collect* madeni ambayo inada. Kwa hiyo, tunatoa msisitizo kwa Serikali ihakikishe kwamba tatizo hili linaondolewa haraka iwezekanavyo ili taasisi zinazotoa huduma ziweze kuendelea na majukumu yake na kuwa na ukwasi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwepo wa Sera ya Gawio, limezungumzwa hapa na Serikali imeshasikia, tumeshatoa maelekezo kwamba lazima kila taasisi inayofanya biashara lazima iwe na Sera za Gawio. Hiyo imeshakuwa *concluded*. Hatuna shaka kwamba Serikali itafuatailia na *TR* ana maelekezo mahususi ya Kamati yangu kwamba lazima kila shirika na taasisi ya Serikali inayopaswa kutoa gawio iwe na Sera ya Gawio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwekezaji katika taasisi ambazo Serikali ina hisa chache; Serikali inatakiwa kufanya tathmini ya kina na kuona namna bora ya kuwekeza katika taasisi ambazo ina umiliki wa hisa chache kwa kuwa uwekezaji huo utaongeza faida kwa Serikali na njia ya gawio na pia njia ya mafanikio mbalimbali wanayopata wananchi wa Tanzania walio katika maeneo ya uzalishaji wa taasisi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ni kuhusu suala la Ofisi ya *TR*. Mheshimiwa Dkt. Mpango amefafanua vizuri zaidi, sina haja ya kuirudia, kwamba iwezeshe kwa maana ya

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

rasilimali fedha na rasilimali watu iweze kufanya kazi yake vizuri pamoja na kuboresha suala zima la TEHAMA katika ofisi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la *Star Media* Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe amelieleza vizuri sana. Ilikuwa inasikitisha, baada ya Kamati kushindwa kupata taarifa na kuzungumza na hawa watu, lakini baada ya Serikali kuingilia kati, tumeona mafanikio, mpaka wametoa na gawio la shilingi milioni 500, hiyo ni hatua moja wapo. Naamini kabisa kwamba Serikali itaendelea kulifanyia kazi kwa umakini zaidi na kuhakikisha kwamba suala la *Star Media* na *TBC* linapatiwa ufumbuzi unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ambayo tunaomba Serikali iichukue kwa nguvu zote ni kurejesha fedha za madai ya VAT. Makampuni na taasisi nyingi zinalalamika, Serikali hamrejeshi. Tunaomba sana hili kama Serikali, tuweke mkazo ili tusizidi kuyaumiza mashirika na kampuni ambazo yame-tie up capital katika suala zima la VAT refund.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa nafasi ya pekee, nafikiri hata Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla mtaungana nami kabisa. Licha ya Mheshimiwa Jenista Mhagama kuzungumza kwamba *NSSF* imefanya kazi vizuri zaidi; na kwa kweli kama alivyosema shirika limebadilika, mfuko umebadilika sana. Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri Jenista Mhagama kwa jitihada ambazo amezifanya katika Mfuko huu wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumaliza, yote haya ni tisa, kumi tumpongeze sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli. Toka ameingia madarakani umeona kwamba gawio kwa taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma zilikuwa haziji. Leo hii tumeweza kukusanya zaidi ya shilingi trilioni 1.05, ni historia. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kama inawezekana tuwe na Azimio la Bunge la Kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua hiyo. Fedha hizi ni kwa Watanzania, ndiyo maana miradi inaendelea, inafanyika kwa sababu tuna fedha ambayo ilikuwa haipatikani lakini sasa inapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa maelezo hayo, naomba kutoa hoja ya Kamati. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MHE. ZAYNABU M. VULU: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Raphael Chegeni, Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (*PIC*). Hoja yako imeungwa mkono, sasa nami nawahoji Wabunge moja kwa moja.

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma kuhusu shughuli zilizotekelezwa na Kamati hiyo katika kipindi cha mwezi Februari, 2019 hadi Januari, 2020 ilipitishwa na Bunge)

MWENYEKITI: Kwa hiyo, naamini ambao wamekubaliana na mapendekezo, maoni na taarifa nzima hii kama ilivyo kuwa maazimio ya Bunge wameafiki na wamekubali Wabunge

NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)

wote. Kwa hiyo, sasa nasema rasmi kwamba taarifa za Kamati zote mbili, maoni na mapendekezo yake yote sasa ni maazimio ya Bunge.

Namalizia kwa kutumia fursa hii kuwapongeza Kamati zote mbili; Kamati ya Bajeti na Kamati ya PIC pamoja na Wenyekiti wake wote wawili kwa kazi kubwa mliyoifanya kwa mwaka mzima na hatimaye mkawasilisha taarifa zenu hizi mbele ya Bunge leo na hatimaye zikawa maazimio ya Bunge. Nawapongeza sana na nawatakieni kila la heri katika utekelezaji wa mwaka huu unaofuata. *(Makofi)*

Pia ni matumaini yangu sana kwamba Serikali wameskia yote na taarifa hii wataitumia kama ni Azimio la Bunge katika kutekeleza yale ambayo Bunge limeona kwamba yafanyiwe kazi. Nao nawataki kila la heri katika utekelezaji wa hayo ambayo wameyaona.

Baada ya kusema hayo, sasa naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho, tarehe 31, Januari, 2020, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 1.38 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa,
Tarehe 31 Januari, 2020 Saa Tatu Asubuhi)*